# SHUHUDA KWA KANISA

2026 Edition

1 · 2 · 3 · 4 · 5 · 6 · 7 · 8 · 9



Uhamisho Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

MaarifaMtandaoni.com

RohoYaUnabii.Org

SAMARITAN LAYMEN MINISTRIES



SHUHUDA KWA KANISA
Gombo la 8
2026 Edition
New Jersey, Marekani
RohoYaUnabii. Org / RohoYaUnabii.Africa
MaarifaMtandaoni.Com
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

UHAMISHONI UGHAIBUNI MTANDAONI MAJUMBANI
2026 EDITION, JERSEY, MAREKANI

# SHUHUDA KWA KANISA
# GOMBO LA 8

ENENDENI MITANDAONI KOTE

**KARIBUNI katika safari ya KUSIKILIZA NA KUSOMA SHUHUDA PAMOJA**

**MaarifaMtandaoni.Com ROHOyaUNABII.Org RohoYaUnabii.Africa**

**SHUHUDA KATIKA SAUTI- SIKILIZA SHUHUDA**
**Shuhuda ni magombo tisa, yenye kurasa 4738 yaliyoanza kuandikwa mwaka 1855**
Madhumuni, ushauri wa kiroho na ushauri wa kivitendo katika nyanja mbali mbali kama vile (Soma kurasa za 5TShuhuda 663-667)
**2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.**

## Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4Tsw 472)
## Madhumuni, ushauri wa kiroho na ushauri wa kivitendo katika nyanja mbali mbali kama vile (Soma kurasa za 5TShuhuda 663-667)

Miaka 10 iliyopita tulikutana na watu wanaosoma Shuhuda kwa Kingereza kule Dallas, Texas, Marekani, kwenye mkutano wa Vijana wa Marekani uitwao Generation of Youth for Christ -GYC (Testimonies for the Church-Revivalplan.com). Walitueleza umuhimu wa kuyasoma magombo haya na kutuhamasisha kuyasoma, hapo ndipo tulipoanza kuyasoma, tulikuwa tumesikia sura zake chache ila siyo sura zote. Tuling'amua kuwa hayakuwa na tafsiri ya Kiswahili. Nasi Tunashauri kila mtu asome magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua wiki 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com). Ukisoma au kusikiliza nusu saa kwa siku, itakuchukua miezi mine kumaliza magombo yote tisa. Tulianza kuyatafsiri kama marafiki miaka sita iliyopita, na ilituchukua muda wa mwaka, kisha tukaingia uhariri, na uhakiki.
Magombo ya Shuhuda tisa, ni kurasa 4738, ambazo zimetafsiriwa kwa ajili ya kila mwanadamu, na hasa wale watu wanaompenda Mungu na kutamani mabadiliko ya tabia. Habari hizi ni muhimu sana hivyo wewe uko huru kunakili na kusambaza kwa wengine kama zilivyo. Kwa nakala ya kidijitali ya vitabu hivi, tafadhali tembelea R*ohoYaUnabii.Org, RohoYaUnabii.Africa MaarifaMtandaoni.Com, MaarifaMtandaoni.Africa* au kwa Kingereza ***WhiteEstate.org***. Kugushi Maandishi ya namna hii au kuyakaba koo yasinene, ni kujiletea taabu kubwa. Yeremia 36:27 na Ufunuo 22:18,19 na Kumbukumbu la Torati 4:9.Enendeni Mtandaoni Kote duniani.

**Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo na kufanya tabia zetu zifae.**

Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu, na kuishi mtindo wa maisha anayotaka Bwana. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua 'Google App' ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

-Mkakati wa uamsho au Tumaini linalotiririka ni msaada mkubwa kwetu leo ambao hatuelewi vyema tufanye nini ili Maisha yetu yampendeze MUNGU na watu, katika muda ambao maadili yanayomomonyoka na ulimwengu hauna mafundisho mema au haufundishi kabisa. Mafundisho haya ni mazuri kwa kila binadamu anayeelewa Kiswahili! Mpango huu kwa Kingereza utaupata katika Revivalplan.Com

Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)

'Maelfu ya watu wataoongoka kwenye ile Kweli, katika saa ya kumi na moja, AMBAO wataupata

na kuukubali Ukweli wa injili na Neno la Mungu na KUHUISHWA KWA harakati za Roho wa Mungu.—EGW'88 755 (1890). – {LDE 212.2}.' Unabii huu unatimia, Maelfu ya watu duniani kote wanamwamini Mwenyezi Mungu na kubatizwa kwa siku moja, kwa wazi au kwa faragha. Tafsiri zetu ni kama Wikipedia, ukitaka kuongeza ladha bila kupoteza maana, wewe boresha tu, ila usipoteze kabisa ujumbe na maana iliyokusudiwa. Kila Shuhuda imehaririwa mara tano, binafsi nimepitia mara tatu. Tumeweka Pointers (2Tsw 45.5) na kadhalika ili ujihakikishie mwenyewe na kutafsiri kwa ubora zaidi unapotaka. Sw inawakilisha, Kiswahili ambacho kinazidi kupanuka na kuwa moja za lugha za Wakristo wengi duniani. Niliona Machapisho ya Nuru kwa Kanisa ambayo sasa tukiyaona tunashangaa, ila enzi hizo yalikuwa yenyewe kabisa kwa uzuri, japo yalichuja kurasa 4738 na kuwa 80 tu!

Asante kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Washauri, Wahakiki, Waombezi, Wanaufundi na wote ambao wanasaidia hii kazi ya Machapisho duniani kote. Tuna idadi ya vitabu 130 sasa. Kama umeshiriki hii kazi na jina lako halikuweka, tafadhali tujulishe, Asante

## MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni ROHO MTAKATIFU, ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika Mashariki wanahitaji pia kusoma Maandishi ya kalamu iliyovuviwa, kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la MUNGU limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 7000 kati ya 14,000, ambayo bado kufikiwa, angalia Joshuaproject.org na habari za '1040 window'

'Sambaza Biblia kote,' ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la MUNGU kote.

Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lolote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe chochote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga ufalme wa Mungu, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandao ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu Afrika, basi tunabidishwa pia kuwa waandishi, Watunzi wa nyimbo, na watu wa kuhifadhi kumbukumbu zetu kwa miaka mingi, kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya Ya jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa umakini, nyimbo zilizoimbwa miaka kama 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu vya tenzi na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabuni, nasi hapa tuna nyimbo nzuri, ambazo zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu ya Biblia takatifu, na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo nyimbo za watoto? Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission'-misheni iliyogeuka na kuwa kinyume cha kawaida. Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa, Kireno, Kihispania na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu. Watoto wetu na sisi mara zingine tunaona pengine tuwe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au tuwe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni ule waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je, viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila maandalizi hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba sio utamaduni wetu kuandika, ila sio utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Sio kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii, kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa muktadha wa Maandiko kwa Waamini ni vizuri tupatie watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti na asili ya kabila la mtu, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili, kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali, nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

## UTANGULIZI

Wapendwa vitabu hivi ni vyetu sote! Maana kila mtu anahitaji Mashauri. Shuhuda ni vitabu vya mashauri na maonyo. Kwenye wingi wa Ushauri hapaanguki jambo, na kuna usalama. Masihi Yu karibu kuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya na yatuchome sana, na kutuvutia tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na ROHO MTAKATIFU kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Hivi ndivyo vitu pekee ambavyo tutaenda navyo mbinguni.

Shuhuda zimejaa mashauri, Makaripio na maonyo ya maisha ya kila siku kwa undani zaidi. Tumeambiwa kwenye maagizo kwamba shuhuda zina kila namna ya kukamilisha tabia zetu. Tulisikia kuhusu kuwepo kwa Shuhuda kwa Kanisa ila hatukujua sana kwamba zinahusiana na nini! Ila baada ya kuanza kusoma kila siku katika mpango wa kusoma Shuhuda Revivalplan.com kwa lugha ya Kiingereza tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili maana waamini wengu wanaishi chini ya Sahara, ambao kuna wengi wanaozungumza Kiswahili. Kwa sasa, takwimu zinaonesha kuwa Afrika ina asilimia 50% ya waamini wanaotarajia marejeo ya YESU (Waadventista). Miaka kama 10 iliyopita, ni asilimia 3% tu ya Maandishi ya Roho ya Unabii ilikuwa imetafsiriwa Kiswahili.

Wana Marejeo wanaozungumza Kiswahili duniani sasa ni 11%. Kutokana na Google wale wanaozungumza Kingereza ‘fluently’ katika nchi za Kiswahilii ni asilimia ndogo sana kuliko tunavyofikiria! Tumepewa ulimwengu wa Kiswahili tuufikie. Hivyo Kutafsiri mambo haya ni jambo la dharura. Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

1. Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."
2. Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha Neno la MUNGU
3. Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania
4. Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa.

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua ‘Google App’ ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

Google imesaidia mambo kadhaa mfano Kujua zama hizo kulikuwa na mambo gani, mfano

mitindo na mavazi ya sketi za hoops miaka ya 1800BK zilizozungumziwa; zitakupa maoni waliyokuwa nayo wakati ule utakapoingia katika tovuti. Japo hekima haiongezeki kwa urahisi, maarifa yameongezeka, hivyo angalia mambo haya kwa kichujio cha Biblia zaidi ya teknolojia. Usiogope kurejelea kamusi, ndio kujifunza. Muumini daima ni mwanafunzi na anasaidiwa zaidi kukumbuka mambo mengi anapotumia machapisho zaidi ya njia zingine. Mengine ya Kingereza imebidi tuweke maana tunayatumia na hivyo utapata utambuzi wa jambo haraka, mfano mara nyingi hatusemi Jimbo, ila Konferensi/conference, majina ya magonjwa au mitindo n.k Tunashauri kila mtu magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua miezi 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com)

Wenu wadhamini, watafsiri, wahariri, washauri, wahakiki, marafiki, wajoli na ndugu katika safari ya kwenda mbinguni.

Zifuatazo ni sentensi za Kalamu ya matumain, kalamu iliyovuviwa kwa wamaani, ya Ellen White kuhusu umuhim u wa kuzisoma Shuhuda.

*1."Niliichukua Biblia ya thamani na kuizingira kwa Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa, zilizotolewa kwa ajili ya watu wa MUNGU. Hapa, nilisema, kesi za karibu zote zinapatikana. Dhambi wanazopaswa kuacha zimeianishwa. Shauri wanalotaka linaweza kupatikana hapa, likitolewa kwa kesi zingine zinazofanana na Zao wenyewe. MUNGU ameridhika kuwapatia kanuni juu ya kanuni na amri juu ya amri. Lakini si wengi wenu ambao wanajua kwa hakika kile kilichomo katika Shuhuda. Hamyafahamu Maandiko. Laiti mngelifanya Neno la MUNGU kuwa funzo kwenu, kwa shauku ya kufikia kiwango cha Biblia na kufikia ukamilifu wa Kikristo, msingehitaji Shuhuda. Ni kwa sababu mmepuuza kujifunza Kitabu cha MUNGU kilichovuviwa ndio maana Yeye ametaka kuwafikia kwa shuhuda rahisi na za moja kwa moja, akiita usikivu wenu kwenye maneno ya uvuvio ambayo mlikuwa mmepuuza kuyatii, na kuwahimiza kuyatengeneza/kuyaumba maisha yenu kulingana na mafundisho Yake safi na yaliyotukuka. {5T 664.3}*

2.“Mashaka na hata kutokuamini shuhuda za ROHO WA MUNGU, kunayachachua makanisa yetu kila mahali. Shetani angependa iwe hivi. Wachungaji wanaohubiri ubinafsi badala ya Kristo wangependa iwe hivi. Shuhuda hazisomwi na wala hazithaminiwi. MUNGU amezungumza na wewe. Nuru imekuwa ikiangaza kutoka kwa Neno Lake na Kutoka kwa Shuhuda, na haya yote yamechukuliwa kwa urahisi na kupuuzwa”. 5T 217.2

3.“Mwokozi wangu alinitangazia kwa mjumbe WAKE. "Kazi yako," Alinielekeza “Ni kubeba Neno Langu... kuchukua Neno Langu mbele ya wale wasioamini, na kwa kalamu na sauti kemea kutokana na Neno, matendo ambayo sio sawa ....… Kwa ushawishi thabiti wa unyenyekevu, kwa sauti na kalamu, ujumbe nitakaoutoa utasikika kutoka kwa mtu ambaye hajawahi kujifunza shuleni… “Usimwogope mwanadamu, Sio wewe unayezungumza: ni Bwana Anayetoa jumbe kwa siku hizi za mwisho; nazo zitaandikwa katika vitabu, na zitasimama milele zote, ili kushuhudia dhidi ya wale ambao wameongozwa kuziacha kwa sababu ya ushawishi wa udanganyifu wa uovu.” RH, Julai 26, 1906

4.Niliona kwamba wote wanapaswa kuchunguza mioyo na Maisha yao kwa ukaribu na kuona ikiwa hawakuwa wamefanya makosa yaleyale ambayo wengine walisahihishwa, na ikiwa maonyo yaliyotolewa kwa wengine hayakuhusu kesi zao wenyewe. Ikiwa ndivyo, wanapaswa kuhisi kwamba ushauri na maonyo yalitolewa haswa kwao na wanapaswa kufanya matumizi hayo kwao, kana kwamba walikuwa wanaambiwa wao wenyewe. {2T 687.2}

5.“Zamani MUNGU alinena na wanadamu kwa kinywa cha manabii na mitume. Katika siku hizi Anazungumza na wanadamu kUPITIA Shuhuda za Roho WAKE. Hakukuwa na wakati ambapo MUNGU aliwafundisha watu WAKE kwa bidii zaidi ya vile anavyowafundisha sasa juu ya mapenzi Yake na njia ambayo angewataka wafuate…… Acha shuhuda Ipimwe kwa matunda yake .... kwamba kazi hii ni ya MUNGU, au sio ya MUNGU. MUNGU hafanyi chochote kwa kushirikiana na Shetani…… Hakuna kazi ambayo ni nusu ya Shetani au nusu ya MUNGU katika jambo hilo. Ushuhuda ni wa ROHO WA MUNGU, au wa Shetani. Udanganyifu wa mwisho kabisa wa Shetani utakuwa ni kuzifanya Shuhuda za ROHO WA MUNGU zisiwe na ushawishi. "Mahali ambapo hakuna maono, watu huangamia." Mithali 29:18. Shetani atafanya kazi kwa ustadi na kwa njia tofauti na kupitia wakala tofauti kutia mashaka imani ya watu wa MUNGU wa masalio katika Ushuhuda wa Kweli…. FLB: 296 "Jambo moja ni hakika: Wale Waadventista Wa Sabato ambao wanachukua msimamo wao chini ya bendera ya Shetani kwanza wataacha imani yao katika maonyo na makaripio yaliyomo katika Shuhuda za ROHO WA MUNGU. Lt156-1903

6.“Ukikosa Imani katika Shuhuda utaondoka kwenye Ukweli wa Biblia. 5T: 674

7.“Nimejawa na huzuni ninapofikiria hali ya watu wetu. BWANA hajatufungia mbingu, lakini njia yetu wenyewe ya kurudi nyuma imetutenga na MUNGU … Na bado cha kushangaza ni kuwa maoni ya jumla ya wengi ni kwamba wanafikiri kanisa linastawi na kwamba amani na ustawi wa kiroho uko katika mipaka yake yote. "Kanisa limeacha kumfuata Kristo Kiongozi Wake na linarudi nyuma kuelekea Misri. Walakini ni wachache wanaochukua tahadhari dhidi ya uhitaji wao wa nguvu za kiroho… 5T: 217

8.“Nimeonyeshwa kuwa kutokuamini Shuhuda kumekuwa kukiongezeka kadiri watu wanavyorudi nyuma kutoka kwa MUNGU. Hali hii ipo katika safu zetu zote, na katika nyanja zote. Lakini ni wachache wanaojua ni uzoefu gani kanisa linaenda kupitia. Niliona kwamba kwa sasa tuko chini ya uvumilivu wa BWANA; lakini hakuna anayejua ukubwa wa rehema ambayo imetolewa kwetu. Lakini ni wachache waliojitoa kwa MUNGU kwa moyo wote. Kuna wachache tu ambao, ni kama nyota katika usiku wenye dhoruba kali, ambazo, huangaza hapa na pale kati ya wingu… RH, Agosti 30,1906

9.“Wakati Shuhuda, ambazo ziliaminiwa wakati mmoja, zinapotiliwa shaka na kuachwa, Shetani anajua waliodanganywa hawataachia hapo; na huongeza juhudi zake maradufu hadi atakapowaingiza kwenye uasi wa wazi, uasi ambao huwa hauwezi kupona na huishia katika uharibifu. "Shuhuda haipaswi kuhafifisha Neno la MUNGU, bali kuliinua na kuzivutia akili Kwake, ili Ukweli mzuri wa kunyenyekesha uweze kuwavutia wote... Ikiwa ungefanya Neno la MUNGU

kuwa Somo lako, na hamu ya kufikia Kiwango cha Biblia na kufikia kwa ukamilifu wa Kikristo, usingehitaji Shuhuda….. Ukweli wa ziada haujatolewa: lakini MUNGU kupitia shuhuda amerahisisha Kweli kuu ambazo tayari zimetolewa, na kwa njia Yake Mwenyewe aliyochagua amezileta mbele ya watu ili zituamshe na kuvutia akili zetu. Ili sote tusiwe na udhuru FLB: 295

10.“Wengi sasa wanadharau maonyo ya uaminifu yaliyotolewa na MUNGU katika Shuhuda…. Lakini Upinzani dhidi ya vitisho vya MUNGU hautazuia utekelezaji wake. Kukataa Maneno ya Bwana, yaliyonenwa kupitia chombo CHAKE alichokichagua, itasababisha hasira Yake tu na mwishowe italeta uharibifu kwa mkosaji. 5T: 678

11."Uelewa wa wale wanaodharau Shuhuda zilizo wazi za Neno la MUNGU, na kukataa kuamini kwa sababu ni jambo linalowabugudhi au lisilovutia wengi kufanya, utatiwa giza; Ukweli utaonekana kwao kama uongo, na uongo utakubaliwa kama Ukweli…. Lakini upendo kwa Kristo na kwa roho ambazo alizifia kwa ajili Yake, zitamwongoza mtumishi wa MUNGU kutoa maonyo na wito kwa uaminifu. SW, Juni 23, 1908

12."Kupuuza Nuru ni Kuikataa." 13 Agizo nilipewa na Mwokozi, "Sio wewe ambaye wamekukataa, lakini Mimi, Mwokozi wao …… Wale ambao wamepuuza Jumbe ambazo nimempa mjumbe wangu kubeba wamemtukana YULE aliyetoa jumbe hizo. …….Watunze Watu, HAO kundi la malisho Yangu, wasifundishwe na matabibu au walimu wanaokataa maonyo ambayo nimetoa kupitia mjumbe wangu.’ SpM: 384

13."Wengi wanaenda kinyume kabisa na nuru ambayo MUNGU amewapa watu WAKE, kwa sababu hawasomi vitabu ambavyo vina nuru na maarifa yenye kutoa tahadhari, makaripio, na maonyo……. Nuru ya thamani sana, inayotoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, imefichwa chini ya pishi. MUNGU atawafanya watu WAKE wawajibike kwa uzembe huu. Hesabu lazima itolewe KWAKE kwa kila mwale wa nuru ambao umeangazia njia yetu, ikiwa nuru hii imeboreshwa kwa maendeleo yetu katika mambo ya mbingu au imekataliwa kwa sababu ilikubalika kwao kufuata mwelekeo wa mambo.” 5T: 681

14.“Ushuhuda huu, ukipokelewa utaamsha utendaji, na kusababisha kujishusha, na kukiri dhambi. Shahidi wa Kweli anasema, "Nazijua kazi zako, ya kuwa hu baridi wala hu moto." Na tena, " Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." Halafu inakuja ahadi, “Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.…. “Makosa na dhambi hizi, ambazo zimewaleta watu wa MUNGU katika hali yao ya unyonge, upofu, na umasikini, lazima yaonekane, na kuamsha toba ya bidii, na kuondoa dhambi hizi ambazo zimewaleta watu katika hali mbaya sana, hali ya upofu na udanganyifu wa kutisha. Ushuhuda ulio wazi lazima uishi kanisani. Na hii peke yake itajibu ujumbe kwa Watu Wa laodikia…. RH, Septemba 16, 1873

15."Hatupaswi kuogopa na kuuomba msamaha ulimwengu kwasababu ya kuwaambia Ukweli: Tunapaswa kudharau kuficha mambo. Dhihirisha rangi zako halisi ili kukidhi mahitaji ya

wanadamu na malaika (1Wakor 4:9) kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu). Wacha ieleweke kwamba Waadventista Wa Sabato hawawezi kufanya mapatano yoyote udunia. Kwa maoni yako na imani yako lazima kusiwe na kuonekana kidogo kwa kutetereka: ulimwengu una haki ya kujua nini cha kutarajia kutoka kwetu. - Sisi ni wamoja katika imani katika Kweli za msingi za Neno la MUNGU … Tuna ujumbe kwaajili ya ulimwengu wote, Amri za MUNGU na Shuhuda za YESU KRISTO ni mzigo wa kazi yetu Ev: 16 na 179

16."Bwana anakusudia kuwaonya, kuwakaripia, kuwashauri wanadamu, kupitia shuhuda zinazotolewa, na kuzivutia akili zenu kwa umuhimu wa Ukweli wa Neno Lake. Shuhuda zilizoandikwa siyo za kutoa nuru mpya, bali kusisitiza kwa uwazi kwenye moyo, Ukweli wa uvuvio ambao tayari umefunuliwa. Wajibu wa mwanadamu kwa MUNGU na kwa wanadamu wenzake umebainishwa waziwazi katika Neno la MUNGU, lakini ni wachache miongoni mwenu wanaotii nuru iliyotolewa. Ukweli wa ziada haujatolewa; bali MUNGU kupitia Shuhuda amerahisisha zile Kweli kuu zilizokwisha kutolewa, na kwa njia Yake aliyoichagua Mwenyewe kuzileta mbele ya watu ili kuziamsha na kuzivutia akili, ili wote waachwe bila kisingizio. {5T 665.1}

17. “Kiburi, kujipenda, ubinafsi, uchoyo, chuki, husuda na wivu vimefunika kwa ukungu, nguvu za ufahamu, na ile Kweli, ambayo ingewafanya muwe na hekima ili kufikia wokovu. Ile Kweli Imepoteza uwezo Wake-Bwana wa kuchangamsha moyo, na kudhibiti akili. Kanuni muhimu sana za ucha Mungu na ibada, hazieleweki kwa sababu hakuna njaa na kiu ya ujuzi wa Biblia, usafi wa moyo, na utakatifu wa maisha. Shuhuda hazijaletwa ili kulipuuzia Neno la MUNGU, bali kuliinua juu na kuvutia akili, kwamba usahili mzuri wa Ukweli unaweza kugusa mioyo ya watu wote. {5T 665.2}

18,"Nilisema zaidi: Kama vile Neno la MUNGU linavyozingirwa ndani ya vitabu hivi na vipeperushi, ndivyo ambavyo MUNGU amewawekea hizi kuta kwa ajili ya maonyo, mashauri, makemeo na kutia moyo. Hapa mlipo mnalia mbele za MUNGU, katika uchungu wa nafsi zenu, kwa ajili ya nuru zaidi. Nimeidhinishwa kutoka kwa MUNGU kuwaambia kwamba hakuna mwale mwingine wa nuru kupitia Shuhuda utakaoangaza katika njia yenu mpaka muitumie kwa vitendo ile nuru ambayo imekwishakutolewa. Bwana amewazingira kwa nuru; lakini ninyi hamjaithamini, mmeikanyaga, na wengine wameidharau nuru, wengine wameipuuza au kuifuata lakini kwa kutojali, ni wachache wameweka mioyo yao kuitii nuru ambayo MUNGU ameridhika kuwapatia. {5T 666.1}

Shuhuda zina Kila HALI NA mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake, tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kuziona uso kwa Uso, Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

1. Alex Ngamije -PreciousPresentTruth.org Rwanda
2. Stephen Letta-Masasi, Tanzania
3. Samuel Mhololo -Kigoma, Tanzania
4. Musa Budodi -Shinyanga Tanzania
5 Isack Msusu-Kigoma, Tanzania
6. Mr and Mrs Kumbuka Mlazi Misibo -Kigoma, Tanzania
7. Aimo Abayo –Morogoro, Tanzania
8. Zablon Mgonja -Arusha, Tanzania
9. Mwalimu Peter Marwa -Mwanza, Tanzania
10. Faustine Momadi Mkama -Dar Es Salaam,Tanzania
11. Paul Masaka -Oklahoma, Marekani
12. Ibrahimu Makamba-Tarime, Tanzania
13. Geoffrey Herman -Manyara, Tanzania
14. Pendo Makori -Visiga,Tanzania
15. Judi Mmari Mugane -Siha, Tanzania
16. Kikundi cha Mbaki/Ngulu Maombi -TAUS—USA
17. Women Prayer Warriors WPM -California, Marekani
18. Ezekiel Ojwang -Kiterere,Tanzania
19. John Mugane -Nakuru, Kenya
20. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
21. Eliphas Sambeke -Arusha, Tanzania
22. Stefano Kasiri -Kibaha, Tanzania
23.Gideon Christian - Ukerewe, Tanzania
24.Musa Muneja -Bariadi, Tanzania
25. Victoria Swai Mhololo -Arusha, Tanzania
26. Julius Letta -Morogoro, Tanzania
27. John Chilala Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
28. Milinje Bariki Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
29. Mbaraka Hamisi -Kilimanjaro, Tanzania
30. Rachel Akinyi Atandi-Nairobi, Kenya
32. Mbusi Mpagalushu -Bariadi, Tanzania
33. James Ongoro- Mara, Tanzania
34. Basanthi Thavamani-Lazar -Madras, India
35. Ndege Aruya-Rorya, Tanzania
36. Kwandu Kasiri -Pwani,Tanzania
37. Elinath Elisante Kukome -Kilimanjaro, Tanzania
38. Sharifa Athuman Seleman -Dar-es-Salaam, Tanzania
39. Jackson Musa Singano -Dar-es-Salaam, Tanzania
40. Daniel Masaka -Kisii, Kenya

41. Ellen Nyangoye- Nyagori-Rorya, Tanzania
42.Fares Ogilo-Rorya, Tanzania
43. Walter Nehemia -Dar Es Salaam, Tanzania
44. Gerard Nyafanga -Mara, Tanzania
45. Bilionea Wayoga-Rorya, Tanzania
46. Bettie Magesa Muasya-Machakos, Kenya
47. Kilango Makala -Kilimanjaro, Tanzania
48. Loyce Pima -Bunda, Tanzania
49. Niwaeli Mburuja -Hedaru, Tanzania
50. Cindy Tustch -Washington, Marekani
51. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
52. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
53. John Ngasa -Mwanza, Tanzania
54. Methusela Mahumbi-Bariadi, Tanzania
55. Elmad Daudi Ndonga-Mombasa, Kenya
56. Luck Rahim Datoo -Arusha, Tanzania
57. Ruth Lilian Bango -Arusha, Tanzania
58. Mohammed Mboi -Kisii, Kenya
59. William Kalokaza-Rukwa, Tanzania
60. Eline Mrema-Kilimanjaro, Tanzania
61.Obed Lissi-Baraton, Kenya
62. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
63. Emmanuel Oola-Rorya, Tanzania
64.Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania
65. Mr and Mrs Weber- Alaska, Marekani
66. Eliakim Mabula-Bariadi, Tanzania
67. Ngusa Mayunga-Rukwa, Tanzania
68. Evans Mobegi-Kisii, Kenya
69. Debbie Bisheli-Nairobi, Kenya
70. Yunus Tiras-Tarime, Tanzania
71.Sharon Ondieki-Nairobi, Kenya
72. Ibrahimu Ibare-Tarime, Tanzania
73. Ghati Matiko-Tarime, Tanzania
74. Haron Wamboa-Machakos, Kenya
75. Timothy Misungwi-Michigan, Marekani
76. Enoc Omosa-North Carolina, Tanzania
77. Filipo Lubua-Pittsburg, Marekani
78. Gibson Mujuni-Kagera, Tanzania
79. Mickey Marr-Scranton, Marekani
80. Lisa Lothian-New York, Marekani
81. Azizi Jacob-Niassa, Mozambique
82. Robert Ndinayo-Goma, Congo
83. Eduardo Punda-Beira, Mozambique

84. Kasereka Mbilika-Goma, Congo
85. Mmaliro Congo-Goma, Congo
86. Yunus Tiras Magira-Tarime, Tanzania
87.Nasra Idrissa Oola-Lushoto, Tanzania
88.Daudi Jabez Masaka-Pennslvyania, Marekani

Wenu katika huduma ya ***MaarifaMtandaoni.Com***, ***MaarifaMtandaoni.Africa*** ***RohoYaUnabii.Org***, ***RohoYaUnabii.Net***, ***RevivalPlan.Com*** na ***Tumaini Ughaibuni Youtube***

Shuhuda zina Kila hali au mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kumwona Mwokozi uso kwa Uso, na kuziona Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

Waanzilishi wa Huduma Grace Momadi Masaka, Daniel Masaka, Paul Masaka na Daudi Masaka-New Jersey, Marekani

Uhamishoni.Ughaibuni.Mtandaoni.Majumbani

**2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.**

Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)

Wenu katika huduma ya ***MaarifaMtandaoni.Com***, ***MaarifaMtandaoni.Africa*** ***RohoYaUnabii.Org*** ***RohoYaUnabii.Net***, ***RevivalPlan.Com*** na ***Tumaini Ughaibuni Youtube***
Daniel Masaka and Grace Momadi Masaka -New Jersey, Marekani

# YALIYOMO


MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI... 1

UTANGULIZI 3

Nyakati Za Gombo La Nane 10

SEHEMU YA 1—FURSA ZILIZOPO 13

SURA YA 1

KAZI YETU 14

SURA YA 2

UTUME WETU 17

SURA YA 3

UWEZO ULIOAHIDIWA 21

SURA YA 4

WAJIBU WETU 25

SURA YA 5

KAZI NYUMBANI NA UGHAIBUNI 30

SURA YA 6

KAZI HUKO ULAYA 35

SURA YA 7

MANDHARI YA VITA 37

SEHEMU YA 2—USHAURI UNAORUDIWA MARA KWA MARA 42

SURA YA 8

MAONYO NA MASHAURI YALIYOTOLEWA KWA KANISA LA BATTLE CREEK 43

SURA YA 9

WAJIBU WETU KWA ULIMWENGU 47

SURA YA 10

KAZI YA UMISIONARI NYUMBANI NA UGHAIBUNI 49

SURA YA 11

ROHO MTAKATIFU KATIKA SHULE ZETU 53

SURA YA 12

KUONDOKA KUTOKA KWENYE UNYOFU 58

SURA YA 13

MTAFUTE MUNGU KWA AJILI YA MSAADA 60

SURA YA 14

OMBI KWA NDUGU WALIOKO BATTLE CREEK 65

SURA YA 15

ONYO LILILOPUUZWA 69

SURA YA 16

MATOKEO YA MATENGENEZO 73

SURA YA 17

ONYO MAKINI (MAZITO) 75
SURA YA 18
MOTO WA REVIEW AND HERALD 80
SURA YA 19
KILE AMBACHO KINGEWEZA KUWAPO 85
SURA YA 20
USAHAULIFU 87
SEHEMU YA 3—BARUA KWA MATABIBU 100
SURA YA 21
THAMANI YA JARIBIO 101
SURA YA 22
KUWEKEZA KILA KITU BATTLE CREEK) 108
SURA YA 23
ENENDENI KATIKA MAENEO MENGI 117
SURA YA 24
KUSUDI LA MUNGU KWA AJILI YA TAASISI ZAKE 123
SURA YA 25
KUSUDI LA MUNGU KATIKA KAZI YA UMISIONARI WA TIBA 127
SURA YA 26
ONYO 131
SURA YA 27
SHIKILIA/ IINUE KAZI YA TIBA 133
SURA YA 28
UMOJA WA JUHUDI 137
SURA YA 29
KRISTO NDIYE NJIA YA MAOMBI NA BARAKA 141
SURA YA 30
MANENO YA KUTIA MOYO 143
SURA YA 31
THAMANI YA NENO LA MUNGU 152
SURA YA 32
KAZI KWA AJILI YA WAKATI HUU 154
SURA YA 33
MTAZAMO MPANA ZAIDI 158
SURA YA 34
KRISTO MFANO WETU 162
SEHEMU YA 4—JIHADHARINI 168
SURA YA 35
MASOMO KUTOKA WAKATI ULIOPITA 169

SURA YA 36
VIJANA WETU WATAFUNDISHWAJE? 174
SURA YA 37
UONGOZI 183
SURA YA 38
WAMOJA NA KRISTO KATIKA MUNGU 185
SURA YA 39
WASHIRIKI WALEI WASONGE MBELE 189
SURA YA 40
JE! TUTAKUTWA TUMEPUNGUA? 191
SURA YA 41
KWENDA NYUMBANI 194
SEHEMU YA 5—MAARIFA YA MUHIMU 196
SURA YA 42
MUNGU KATIKA ASILI 197
SURA YA 43
MUNGU MWENYE NAFSI 203
SURA YA 44
MAARIFA YA UONGO NA YA KWELI KUHUSU MUNGU 216
SURA YA 45
HATARI KATIKA MAARIFA YA KUKISIA 225
SURA YA 46
UONGO NA UKWELI KATIKA ELIMU 236
SURA YA 47
UMUHIMU WA KUTAFUTA MAARIFA YA KWELI 241
Sura ya 48
MAARIFA YANAYOPOKELEWA KUPITIA KWA NENO LA MUNGU 246
SURA YA 49
HITAJI LETU KUU 254

MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu, ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika wanahitaji pia kusoma kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window'

'Sambaza Biblia popote,' ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la Mungu kote.

Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lo lote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe cho chote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandano ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabu, nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo nyimbo za watoto?. Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu, na wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni, waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza,  Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi?  Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa Waumini ni vizuri tupate watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1 -908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

Back of the BOOK cover -Mkakati wa uamsho au  Tumaini linalotiririka ni msaada

mkubwa kwetu leo ambao hatuelewi vyema tufanye nini ili Maisha yetu yampendeze Mungu na watu, katika muda ambao maadili yanamomonyoka na ulimwengu hauna mafundisho mema au haufundishi kabisa. Mafundisho haya ni mazuri kwa kila binadamu anayeelewa Kiswahili!

“Nilichukua Biblia ya thamani, na kuizingira kwa “Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa,” zilizotolewa kwa ajili ya watu wa Mungu ili kusahihisha tabia zao. na "Hapa," nilisema na kuona kwamba, "karibu kesi za watu wote zinawakilishwa na maonyo haya waliyopewa watu hawa. Dhambi wanazopaswa kuepuka zimeonyeshwa. Shauri ambalo wangetamani linaweza kupatikana kuhusiana na jambo fulani la maisha yao, lipo hapa kwenye hizi shuhuda, limetolewa tayari, kwani kuna kesi zingine zinazofanana na zao wenyewe kabisa, na ambazo zitatatua tatizo lao wakifuata ushauri wake. Mungu amependezwa kukupa amri juu ya amri na kanuni juu ya kanuni Lakini wengi wenu hamyajui mashauri yaliyomo ndani ya Shuhuda, hamyafahamu Maandiko jinsi mnavyopaswa. Endapo mngelifanya Neno la Mungu kuwa Ndiyo mada kuu ya elimu/mafunzo kwenu, mkiwa na shauku ya kufikia vigezo vya Biblia na ukamilifu wa Kikristo, basi msingezihitaji Shuhuda. Ila ni kwa sababu mmepuuzia kujielimisha na Kitabu cha Mungu kilichovuviwa, yaani Biblia na ndio maana Yeye ametafuta kuwafikia kwa Shuhuda rahisi na nyofu, zinazolenga moja kwa moja mada, akivutia usikivu wenu/wako kwa Maneno yaliyovuviwa. ambayo mlikuwa mmepuuzia kuyatii, na kuwasihi mtengeneze maisha yenu kulingana na mafundisho Yake safi na yaliyotukuka." 5T 664.3

## UTANGULIZI

Wapendwa vitabu hivi ni vyetu sote! Maana kila mtu anahitaji Mashauri. Kwenye wingi wa Ushauri hapaanguki jambo, na kuna usalama. Masihi Yu karibu kuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya na yatuchome sana, na kutuvutia tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na Roho Mtakatifu kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Hivi ndivyo vitu pekee ambavyo tutaenda navyo mbinguni.

Shuhuda zimejaa mashauri, Makaripio na maonyo ya maisha ya kila siku kwa undani zaidi. Tumeambiwa kwenye maagizo kwamba shuhuda zina kila namna ya kukamilisha tabia zetu. Tulisikia kuhusu kuwepo kwa Shuhuda kwa Kanisa ila hatukujua sana kwamba zinahusiana na nini! Ila baada ya kuanza kusoma kila siku katika mpango wa kusoma Shuhuda Revivalplan.com kwa lugha ya Kingereza tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili maana Divisheni yetu ambayo ina watu wengi wanaozungumza lugha ya Kiswahili, ndiyo Divisheni

iliyo na watu wengi duniani (East-Central Africa Division of Seventh-day Adventists) kwa sasa, na takwimu zinaonesha kuwa Afrika sasa ina asilimia 50% ya waumini wanaotarajia marejeo ya YESU (Waadventista). Asilimia 3% ya Maandishi ya Roho ya Unabii yametafsiriwa Kiswahili.

Wana Marejeo wanaozungumza Kiswahili duniani sasa ni 11%. Kutokana na Google wale wanaozungumza Kingereza 'fluently' katika nchi za Kiswahilii ni asilimia ndogo sana kuliko tunavyofikiria! Tumepewa ulimwengu wa Kiswahili tuufikie. Hivyo Kutafsiri mambo haya ni jambo la dharura. Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

1. Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."

2. Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha Neno la Mungu

3. Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania

4. Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa.

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni Roho Mtakatifu, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua 'Google App' ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

Google imesaidia mambo kadhaa mfano Kujua mitindo na mavazi ya sketi za hoops miaka ya 1800BK; itakupa maoni waliyokuwa nayo wakati ule. Japo hekima haiongezeki kwa urahisi, maarifa yameongezeka, hivyo angalia mambo haya kwa kichujio cha Biblia zaidi ya teknolojia. Usiogope kurejelea kamusi, ndio kujifunza. Muumini daima ni mwanafunzi na anasaidiwa zaidi kukumbuka mambo mengi anapotumia machapisho zaidi ya njia zingine. Mengine ya Kingereza imebidi tuweke maana tunayatumia na hivyo utapata utambuzi wa jambo haraka, mfano mara nyingi hatusemi Jimbo, ila Konferensi/conference, majina ya magonjwa au mitindo n.k Tunashauri kila kanisa liwe na magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua miezi 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com)

Wenu wadhamini, watafsiri, wahariri, washauri, wahakiki, marafiki, wajoli na ndugu

katika safari ya kwenda mbinguni.

“Mashaka na hata kutokuamini shuhuda za Roho wa MUNGU, kunayachachua makanisa yetu kila mahali. Shetani angependa iwe hivi. Wachungaji wanaohubiri ubinafsi badala ya Kristo wangependa iwe hivi. Shuhuda hazisomwi na wala hazithaminiwi. MUNGU amezungumza na wewe. Nuru imekuwa ikiangaza kutoka kwa Neno Lake na Kutoka kwa Shuhuda, na zote zimechukuliwa kwa urahisi na kupuuzwa”. 5T 217.2

“Mwokozi wangu alinitangazia kwa mjumbe Wake. "Kazi yako," Alinielekeza “Ni kubeba Neno langu ... kuchukua Neno langu mbele ya wale wasioamini, na kwa kalamu na sauti kukemea kutokana na Neno matendo ambayo sio sawa ... Kwa ushawishi thabiti wa unyenyekevu, kwa sauti na kalamu, ujumbe nitakaoutoa utasikika kutoka kwa mtu ambaye hajawahi kujifunza shuleni… “Usimwogope mwanadamu, Sio wewe unayezungumza: ni Bwana Anayetoa jumbe kwa siku hizi za mwisho; nazo zitaandikwa katika vitabu, na zitasimama milele zote, ili kushuhudia dhidi ya wale ambao wameongozwa kuziacha kwa sababu ya ushawishi wa udanganyifu wa uovu.” RH, Julai 26, 1906

Niliona kwamba wote wanapaswa kuchunguza mioyo na Maisha yao kwa ukaribu na kuona ikiwa hawakuwa wamefanya makosa yaleyale ambayo wengine walisahihishwa, na ikiwa maonyo yaliyotolewa kwa wengine hayakuhusu kesi zao wenyewe. Ikiwa ndivyo, wanapaswa kuhisi kwamba ushauri na maonyo yalitolewa haswa kwao na wanapaswa kufanya matumizi hayo kwao kana kwamba walikuwa wanaambiwa wao wenyewe. {2T 687.2}

“Zamani MUNGU alinena na wanadamu kwa kinywa cha manabii na mitume. Katika siku hizi Anazungumza na wanadamu kwa Shuhuda za Roho Wake. Hakukuwa na wakati ambapo MUNGU aliwafundisha watu Wake kwa bidii zaidi ya vile anavyowafundisha sasa juu ya mapenzi Yake na njia ambayo angewataka wafuate…. Acha Ushuhuda upimwe kwa matunda yake .... kwamba kazi hii ni ya MUNGU, au sio ya MUNGU. MUNGU hafanyi chochote kwa kushirikiana na Shetani… Hakuna kazi nusu ya 12 Shetani au nusu ya MUNGU katika jambo hilo. Ushuhuda ni wa Roho wa MUNGU, au wa shetani. Udanganyifu wa mwisho kabisa wa Shetani utakuwa ni kuzifanya Shuhuda za Roho wa MUNGU zisiwe na ushawishi. "Mahali ambapo hakuna maono, watu huangamia." Mithali 29:18. Shetani atafanya kazi kwa ustadi na kwa njia tofauti na kupitia wakala tofauti kutia mashaka imani ya watu wa MUNGU wa masalio katika Ushuhuda wa kweli…. FLB: 296 "Jambo moja ni hakika: Wale Waadventista Wasabato ambao wanachukua msimamo wao chini ya bendera ya Shetani kwanza wataacha imani yao katika maonyo na makaripio yaliyomo katika Shuhuda za Roho wa Mungu. Lt156-1903

“Ukikosa Imani katika Shuhuda utaondoka kwenye Ukweli wa Biblia. 5T: 674

“Nimejawa na huzuni ninapofikiria hali ya watu wetu. BWANA hajatufungia mbingu, lakini njia yetu wenyewe ya kurudi nyuma imetutenga na MUNGU… Na bado cha kushangaza ni kuwa maoni ya jumla ni kwamba kanisa linastawi na kwamba amani na ustawi wa kiroho uko katika mipaka yake yote. "Kanisa limeacha kumfuata Kristo Kiongozi Wake na linarudi nyuma kuelekea Misri. Walakini ni wachache wanaochukua tahadhari dhidi ya uhitaji wao wa nguvu za kiroho… 5T: 217

“Nimeonyeshwa kuwa kutokuamini Shuhuda kumekuwa kukiongezeka kadiri watu wanavyorudi nyuma kutoka kwa MUNGU. Hali hii ipo katika safu zetu zote, katika nyanja zote. Lakini ni wachache wanaojua ni uzoefu gani kanisa linaenda kupitia. Niliona kwamba kwa sasa tuko chini ya uvumilivu wa BWANA; lakini hakuna anayejua ukubwa wa rehema ambayo imetolewa kwetu. Lakini ni wachache waliojitoa kwa MUNGU kwa moyo wote. Kuna wachache tu ambao, ni kama nyota katika usiku wenye dhoruba kali, huangaza hapa na pale kati ya wingu… RH, Agosti 30,1906

“Wakati Shuhuda, ambazo ziliaminiwa wakati mmoja, zinapotiliwa shaka na kuachwa, Shetani anajua waliodanganywa hawataachia hapo; na huongeza juhudi zake mara dufu hadi atakapowaingiza kwenye uasi wa wazi, ambao huwa hauwezi kupona na huishia katika uharibifu. "Ushuhuda haupaswi kuhafifisha Neno la MUNGU, bali kuliinua na kuzivutia akili kwake, ili Ukweli mzuri wa unyenyekevu uweze kuwavutia wote ... Ikiwa ungefanya Neno la MUNGU kuwa Somo lako, na hamu ya kufikia Kiwango cha Biblia na kufikia kwa ukamilifu wa Kikristo, usingehitaji Shuhuda… Ukweli wa ziada haujatolewa: lakini MUNGU kupitia Ushuhuda amerahisisha Kweli kuu ambazo tayari zimetolewa na kwa njia Yake Mwenyewe aliyochagua amezileta mbele ya watu ili ziamshe na zivutie akili. ili wote wasiwe na udhuru FLB: 295

“Wengi sasa wanadharau maonyo ya uaminifu yaliyotolewa na MUNGU katika ushuhuda…. Lakini Upinzani dhidi ya vitisho vya MUNGU hautazuia utekelezaji wake. Kukataa Maneno ya Bwana, yaliyosemwa kupitia chombo Chake alichokichagua, itasababisha hasira Yake tu na mwishowe italeta uharibifu kwa mkosaji. 5T: 678

"Uelewa wa wale wanaodharau Shuhuda zilizo wazi za Neno la MUNGU, na kukataa kuamini kwa sababu ni jambo linawabugudhi au lisilovutia wengi kufanya, utatiwa giza; Ukweli utaonekana kwao kama uongo, na uongo utakubaliwa kama Ukweli…. Lakini upendo kwa Kristo na kwa roho ambazo alizifia kwa ajili yake, zitamwongoza mtumishi wa MUNGU kutoa maonyo na wito kwa uaminifu. SW, Juni 23, 1908

"Kupuuza Nuru ni Kuikataa." 13 Agizo nilipewa na Mwokozi, "Sio wewe ambaye wamekukataa, lakini Mimi, Mwokozi wao …… Wale ambao wamepuuza Jumbe ambazo nimempa mjumbe wangu kubeba wamemtukana YULE aliyetoa jumbe hizo. …Watunze Watu, kundi la malisho yangu, wasifundishwe na matabibu au walimu wanaokataa maonyo ambayo nimetoa kupitia mjumbe wangu.' SpM: 384

"Wengi wanaenda kinyume kabisa na nuru ambayo MUNGU amewapa watu wake, kwa sababu hawasomi vitabu ambavyo vina nuru na maarifa yenye tahadhari, makaripio, na maonyo…. Nuru ya thamani sana, inayotoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, imefichwa chini ya pishi. MUNGU atawafanya watu Wake wawajibike kwa uzembe huu. Hesabu lazima itolewe Kwake kwa kila mwale wa nuru ambayo imeangazia njia yetu, ikiwa imeboreshwa kwa maendeleo yetu katika mambo ya mbingu au imekataliwa kwa sababu ilikubalika kwao kufuata mwelekeo wa mambo." 5T: 681

"Ushuhuda huu, ukipokelewa utaamsha utendaji, na kusababisha kujishusha, na kukiri dhambi. Shahidi wa Kweli anasema, "Najua kazi zako, ya kuwa hu baridi wala hu moto." Na tena, " Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." Halafu inakuja ahadi, "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.…. "Makosa na dhambi hizi, ambazo zimewaleta watu wa MUNGU katika hali yao ya unyonge, upofu, na umasikini, lazima zionekane, na zinaamsha toba ya bidii, na kuondoa dhambi hizi ambazo zimewaleta katika hali mbaya sana. hali ya upofu na udanganyifu wa kutisha. Ushuhuda ulio wazi lazima uishi kanisani. Na hii peke yake itajibu ujumbe kwa Walaodikia…. RH, Septemba 16, 1873

"Hatupaswi kuogopa na kuomba msamaha ulimwengu kwa kuwaambia Ukweli: Tunapaswa kudharau kuficha mambo.Dhihirisha rangi zako halisi ili kukidhi mahitaji ya wanadamu na malaika (1Wakor 4:9 kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu). Wacha ieleweke kwamba Waadventista Wasabato hawawezi kufanya mapatano yoyote. Kwa maoni yako na imani yako lazima kusiwe na kuonekana kidogo kwa kutetereka: ulimwengu una haki ya kujua nini cha kutarajia kutoka kwetu. - Sisi ni wamoja katika imani katika Ukweli wa kimsingi wa Neno la MUNGU… Tuna ujumbe kwaajili ya ulimwengu wote, Amri za MUNGU na Shuhuda za YESU KRISTO ni mzigo wa kazi yetu Ev: 16 na 179

"Niliichukua Biblia ya thamani na kuizingira kwa Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa, zilizotolewa kwa ajili ya watu wa Mungu. Hapa, nilisema, kesi za karibu zote zinapatikana. Dhambi wanazopaswa kuacha zimeianishwa. Shauri wanalotaka

linaweza kupatikana hapa, likitolewa kwa kesi zingine zinazofanana na wao wenyewe. Mungu ameridhika kuwapatia kanuni juu ya kanuni na amri juu ya amri. Lakini si wengi wenu ambao wanajua kwa hakika kile kilichomo katika Shuhuda. Hamyafahamu Maandiko. Laiti mngelifanya Neno la Mungu kuwa funzo kwenu, kwa shauku ya kufikia kiwango cha Biblia na kufikia ukamilifu wa Kikristo, msingehitaji Shuhuda. Ni kwa sababu mmepuuza kujifunza Kitabu cha Mungu kilichovuviwa ndio maana Yeye ametaka kuwafikia kwa ushuhuda rahisi na wa moja kwa moja, akiita usikivu wenu kwenye maneno ya uvuvio ambayo mlikuwa mmepuuza kuyatii, na kuwahimiza kuyatengeneza/kuyaumba maisha yenu kulingana na mafundisho yake safi na yaliyotukuka. {5T 664.3}

"Bwana anakusudia kuwaonya, kuwakaripia, kuwashauri, kupitia shuhuda zinazotolewa, na kuzivutia akili zenu kwa umuhimu wa ukweli wa Neno Lake. Shuhuda zilizoandikwa siyo kutoa nuru mpya, bali kusisitiza kwa uwazi kwenye moyo ukweli wa uvuvio ambao tayari umefunuliwa.Wajibu wa mwanadamu kwa Mungu na kwa wanadamu wenzake umebainishwa waziwazi katika Neno la Mungu, lakini ni wachache miongoni mwenu wanaotii nuru iliyotolewa. Ukweli wa ziada haujatolewa; bali Mungu kupitia Shuhuda amerahisisha zile Kweli kuu zilizokwisha kutolewa na kwa njia Yake aliyoichagua Mwenyewe kuzileta mbele ya watu ili kuziamsha na kuzivutia akili, ili wote waachwe bila kisingizio. {5T 665.1}

“Kiburi, kujipenda, ubinafsi, chuki, husuda na wivu vimefunika nguvu za ufahamu, na Ukweli, ambao ungewafanya muwe na hekima ili kufikia wokovu, mmepoteza uwezo Wake wa kuvutia na kutawala akili. Kanuni muhimu sana za utauwa hazieleweki kwa sababu hakuna njaa na kiu ya ujuzi wa Biblia, usafi wa moyo, na utakatifu wa maisha. Shuhuda si kwa ajili ya kulidharau Neno la Mungu, bali kuliinua na kuvutia akili, kwamba usahili mzuri wa Ukweli unaweza kuwavutia wote. {5T 665.2}

"Nilisema zaidi: Kama vile Neno la Mungu linavyozingirwa ndani ya vitabu hivi na vipeperushi, ndivyo ambavyo Mungu amewawekea ukuta kwa ajili ya maonyo, mashauri, makemeo na kutia moyo. Hapa mlipo mnalia mbele za Mungu, katika uchungu wa nafsi zenu, kwa ajili ya nuru zaidi. Nimeidhinishwa kutoka kwa Mungu kuwaambia kwamba hakuna mwale mwingine wa nuru kupitia Shuhuda utakaoangaza katika njia yenu mpaka muitumie kwa vitendo nuru iliyokwishatolewa. Bwana amewazingira kwa nuru; lakini hamjaithamini, mmeikanyaga, na wengine wameidharau nuru, wengine wameipuuza au kuifuata lakini kwa kutojali, wachache wameweka mioyo yao kuitii nuru ambayo Mungu ameridhika kuwapatia. {5T 666.1}

Shuhuda zina Kila mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kuziona uso kwa Uso, Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

## NYAKATI ZA GOMBO LA NANE

GOMBO LA 8 LILICHAPISHWA ILI KUKABILIANA NA MGOGORO - MGOGORO MKUBWA KABISA AMBAO KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO LIMEWAHI KUKUTANA NAO. UMUHIMU NA DHARURA YA JAMBO HILI UNATHIBITISHWA KWA VILE KITABU HICHO KILITOKA KATIKA KIWANDA CHA KUPIGA CHAPA MNAMO MWEZI MARCH, 1904, MIEZI KUMI NA TANO BAADA YA GOMBO LA 7 KUCHAPISHWA. KWA WAKATI WA UTOAJI WAKE, HAIKUJULIKANA JINSI AMBAVYO WIMBI LINGEGEUKA. LEO TUNAWEZA KUANGALIA NYUMA NA KUONA KWAMBA MAFUNDISHO YAKE YENYE KUTEGEMEZA YALIKUWA NI KIPENGELE KIKUBWA KATIKA KUZUIA JANGA LILILOTISHIA.

WAKATI KAZI YA MADHEHEBU ILIPOKUWA INAENEA ILI KUUZUNGUKA ULIMWENGU, NA WAKATI KULIKUWA NA UPANGAJI UPYA WA KONFERENSI KUU AMBAO ULIOFANYA UWEZEKANO WA UKUAJI WA MAANA WA HARAKA, MAENDELEO KATIKA MJI WA MAKAO MAKUU YETU YA ZAMANI BATTLE CREEK, MICHIGAN, YALIONEKANA AMBAYO, KAMA YASINGELIZUIWA YANGEONGOZA, KATIKA UHARIBIFU WA MISINGI HASA YA IMANI YA WAADVENTISTA WA SABATO. YOTE YALITUKIA KWA NAMNA YA WEREVU KIASI KWAMBA HATARI ZAKE HAZIKUGUNDULIWA MWANZONI, KWANI KOSA LILIKUWA LINAJIONESHA LENYEWE CHINI YA VAZI LA "NURU MPYA."

KARIBU NA MWISHO WA KARNE, BAADHI YA WAFANYAKAZI WA MADHEHEBU, NA HASA KIONGOZI KATIKA MASLAHI YA UMISHENARI WA TIBA/UTABIBU, ALIUNGA MKONO MAFUNDISHO FULANI KUHUSU NAFSI YA MUNGU AMBAYO HAYAKUPATANA KABISA NA MAFUNDISHO YA WAZI YA NENO LA MUNGU NA YA KANISA. BADO MAFUNDISHO HAYA PANTHEISMU YALITANGAZWA KUWA NI MAENDELEO KATIKA UELEWA WA UJUMBE HUO, AMBAO UKUBALI WAKE WA UJUMLA, ILIDAIWA, HULETA UZOEFU WA KUFURAHISHA KWA WATU WA MUNGU NAO UNGEHARAKISHA UMALIZAJI WA KAZI. MAONI HAYA YA KUABUDU MIUNGU, YAANI PATHEISMu, YALIMWONESHA MUNGU SIO KAMA NAFSI KUU YENYE MWILI ANAYETAWALA ULIMWENGU, BALI KAMA UWEZO, NGUVU, INAYOONEKANA NA KUHISIWA NDANI YA ASILI NA KUENEA KATIKA ANGAHEWA YENYEWE. WAKICHANGANYA NGUVU ZA MUNGU NA NAFSI YAKE, WALIMWONA MUNGU NDANI YA JUA, KATIKA MAUA, KATIKA NYASI, NDANI MTI, NA NDANI YA WANADAMU WENZAO. MITAZAMO HII YA AJABU NA MIGENI< LAKINI YA KUPENDEZA SANA ILIWASILISHWA HADHARANI KATIKA MKUTANO MKUU MMOJA WA KONFERENSI KUU, YALIKUWA YAKITETEWA KWA UHURU KATIKA CHUO CHA BATTLE CREEK, NA YALIWASILISHWA TENA NA TENA KATIKA HOSPITALI YA BATTLE CREEK. KWA MUDA MREFU HII "NURU MPYA" ILIKUWA MADA YA MAZUNGUMZO WAKATI WAFANYAKAZI WADVENTISTA

WA SABATO WALIPOKUSANYIKA ISIVYO RASMI AU KWA AJILI YA NYAKATI ZA USHAURI. WAKATI AMBAPO LILIKUWA NI JAMBO LA KUSHUGHULISHA SANA KWA VIONGOZI WA KANISA, JUHUDI ZAO ZA KUZUIA MAFUNZO HAYA YA IBADA YA MIUNGU ILIONEKANA KUTOKUFAA KABISA.

HADI MWISHO WA MAJIRA YA BARIDI YA 1902-03 VUGUVUGU HII ILIPATA NGUVU. NDIPO TATIZO LIKAWA KALI KUTOKANA NA UCHAPISHAJI WA KITABU JUU YA FIZIOLOJIA NA ELIMUSIHA KILICHOANDIKWA MTINDO WANAOPENDA, AMBACHO NDANI YAKE MGANGA KIONGOZI WA KANISA ALIWEKA MAONI HAYA KWA WEREVU. KITABU HICHO KILITOLEWA ILI KIPATE KUUZWA KWA WINGI NA WAADVENTISTA WA SABATO ILI KUSAIDIA KUPATA FEDHA ZA KUJENGA UPYA HOSPITALI YA BATTLE CREEK. ILIONEKANA KWA VIONGOZI WA KANISA KWAMBA MGOGORO UNGEWEZA KUFIKIKIWA KWA HAKIKA KATIKA KIKAO CHA MKUTANO MKUU WA KONFERENSI KUU KILICHOFANYIKA WAKATI WA MAJIRA YA KUCHIPUA YA 1903, WALIPOTUMAINI KWAMBA MAMA WHITE ANGESHUGHULIKA KWA DHAHIRI NA JAMBO HILO. LAKINI KILA MARA ALIPOSEMA ALIONEKANA KUZUIWA NA ALIWASILISHA UJUMBE WENYE WITO WA UMOJA KATIKA KAZI NA HITAJI LA KUUNGANA NA KUSONGA MBELE PAMOJA KWA BIDII. KIKAO CHA MKUTANO MKUU WAKONFERENSI KUU KILIPOFUNGWA, SUALA HILI BADO HALIKUWA LIMEGUSWA.

MIEZI CHACHE BAADAYE, KATIKA MAJIRA YA KUPUKUTISHA YA 1903, MAMA WHITE ALIAGIZWA KATIKA NJOZI KUKABILIANA BILA KUSITA NA MOJA KWA MOJA NA MAFUNDISHO YA IBADA YA MIUNGU NA KUONYESHA HATARI ZA MAFUNDISHO YANAYOAMBATANA NAYO YA KUKISIA NA UMIZIMU. TAARIFA ILIYOTUMWA NAYE KUTOKA CALIFORNIA ILIWAFIKIA NDUGU KATIKA KIKAO CHA BARAZA LA MAJIRA YA KUPUKUTISHA KULE WASHINGTON, DC, WAKATI WA KILELE CHA MGOGORO HUU WOTE SASA WANGEWEZA KUONA KUWA MUNGU ALIKUWA AKIONGOZA NA KUILINDA KAZI YAKE, NA KATIKA NURU YA UJUMBE WA ROHO YA UNABII KARIBU WOTE WALICHUKUA MSIMAMO WAO KUWA UPANDE WA UKWELI. UWANJANI, HATA HIVYO, KULIKUWAPO NA MKANGANYIKO, MASHAKA, NA GHASIA. SHUHUDA KWA KANISA, GOMBO LA 8, ILIBEBA UJUMBE JUU YA JAMBO HILI AMBAO KWA MANENO YA HAKIKA YALIFAFANUA UKWELI NA HIVYO KULIACHA KOSA KUJITOKEZA KWA TOFAUTI YA WAZIWAZI. MGOGORO ULIKABILIWA, NA KANISA LILIOKOLEWA. HAKUNA UWEZO WA MWANADAMU PEKE YAKE AMBAO UNGEWEZA KULIHIFADHI KANISA KATIKA MGOGORO HUU.

ZAIDI YA MAJADILIANO HAYA MAKUU KUHUSU MAFUNDISHO,YENYE UTATA, KULIKUWAKO NA MASUALA MENGINE YA KANISA KATIKA NYAKATI ZA GOMBO LA 8. WIKI CHACHE TU MARA BAADA YA GOMBO LA 7 KUTOKA KATIKA KIWANDA CHA KUPIGA CHAPA, LIKIWA NA UJUMBE WAKE WA USHAURI KUHUSU KAZI INAYOFANYIKA KATIKA NYUMBA ZETU ZA UCHAPISHAJI, KIWANDA CHA SHIRIKA LA UCHAPISHAJI CHA REVIEW AND HERALD KILIANGAMIZWA NA MOTO. HUU

ULIKUWA NI MSIBA MKUU WA PILI KULE BATTLE CREEK NA UKAFUATIA MOTO WA HOSPITALI KATIKA MUDA CHINI YA MIEZI KUMI NA MOJA.

KULIKUWA NA MATATIZO AMBAYO NI YA KAWAIDA KATIKA HASARA HII AMBAYO NI MAKUBWA ZAIDI YA KURUDISHIA MALI ILIYOHARIBIKA. KWA MIAKA MINGI MASHAURI YA ROHO YA UNABII YALIDAI KUTAWANYIKA KWA WAUMINI KUTOKA KATIKA BATTLE CREEK NA KUANZISHWA KWA HOSPITALI, MASHIRIKA YA ELIMU, NA UCHAPISHAJI KATIKA SEHEMU NYINGINE. WATU WETU WALIOMBWA KUTOKUJIKUSANYA KWA WINGI KATIKA MAKAO MAKUU YA KAZI NA KUJENGA MAKAZI YAO HAPO. ILIKUWA NI KATIKA KUITIKIA MASHAURI HAYA NDIPO CHUO KIKUU CHA ZAMANI CHA BATTLE CREEK KILIHAMISHIWA ENEO LA SHAMBANI KULE BERRIEN SPRINGS, MICHIGAN. SASA MTAMBO WA UZALISHAJI WA REVIEW AND HERALD UKIWA UMEHARIBIWA NA MOTO, ILIONEKANA KWA VIONGOZI KUWA NI WAKATI WA HERI KUHAMISHA KAZI YA NYUMBA YA UCHAPISHAJI KWENDA SEHEMU NYINGINE, NA HATUA ZINAZOFAA ZILICHUKULIWA KATIKA MWELEKEO HUO.

TANGU MWANZO MAKAO MAKUU YA KONFERENSI KUU YALIWEKWA KARIBU NA OFISI YA REVIEW AND HERALD. TAASISI MBILI HIZI ZILIONEKANA KAMA VILE HAZIWEZI KUTENGANISHWA. MPANGO WOWOTE WA KUHAMISHA MOJA UNGEHUSISHA NYINGINE. KATIKA KUITIKIA MWONGOZO KUPITIA ROHO YA UNABII, MAENEO YANAYOFAA YALITAFUTWA, NA HATIMAYE, KATIKA VIUNGA VYA WASHINGTON, DC, MJI MKUU WA TAIFA MAJENGO YANAYOKUBALIKA YALIPATIKANA, NA KAZI YA NYUMBA YA UCHAPISHAJI NA OFISI ZA KONFERENSI KUU ZILIHAMISHIWA KATIKA KITUO HICHO MNAMO AGOSTI, 1903.

ILI KUWASAIDIA WAADVENTISTA WA SABATO KUELEWA USULI WA CHANZO CHA MAAFA YALIYOITEKETEZA KABISA NYUMBA YA UCHAPISHAJI, NA HITAJI LA KUANZISHA UPYA KAZI KATIKA MSINGI MPYA NA KATIKA ENEO JIPYA, "MASHAURI YALIRUDIA MARA KWA MARA" YALIWEKWA KATIKA GOMBO LA 8.

MASUALA HAYA, YANAHUSU KAZI YETU YA UTABIBU/TIBA, KAZI YETU YA UCHAPISHAJI, NA MAFUNDISHO HASA YA KANISA, YALIKUWA NI MAKUBWA NA YANGEWEZA KUVUTA KWA URAHISI USIKIVU WA WATU WETU KOTE ULIMWENGUNI KUTOKA KWENYE KAZI KUU ILIYO MBELE YETU –ILE YA KUPELEKA INJILI YA MILELE KWA ULIMWENGU WOTE. INGAWA GOMBO LA 8 LILITOLEWA KIMSINGI KUKABILIANA NA MIGOGORO HIYO, NA KUTENGENEZA NJIA SAHIHI ILIYO DHAHIRI DAIMA KWA WAADVENTISTA WA SABATO, ELLEN WHITE ALITUMIA NJIA CHANYA. KITABU KINAANZA, SIYO KWA PICHA YA MATATIZO YANAYOTUKABILI, BALI NA SEHEMU YENYE KICHWA "FURSA ZILIZOPO" AMBAZO KWA HIZO "KAZI YETU" INAANZISHWA KWA NAMNA YA KUVUTIA. SURA ZINAZOFUATIA JUU YA "UTUME," "NGUVU ILIYOAHIDIWA," NA MAONI YA WAJIBU WETU NYUMBANI NA UGHAIBUNI, KWA MTAJO WA PEKEE JUU YA "KAZI. HUKO ULAYA." JINSI AMBAVYO INGEMPENDEZA ADUI MKUU WA UKWELI IKIWA AKILI NA MAWAZO YA WATU WA MUNGU YANGEWEZA KUGEUZWA KUTOKA KATIKA KAZI KUBWA AMBAYO ILIKUWA HAIJAMALIZWA. NA HABARI ZA KUBAHATISHA KUHUSU UUNGU, NA USHUPAVU WA DINI, AU NA MAWAZO YA YALIYOCHANGANYIKA YA MFUMO. BALI WATU WA

MUNGU HAWAKUTAKIWA KUVUTWA KWINGINE KUTOKA KATIKA KAZI YAO YA KUUELIMISHA ULIMWENGU. WAKIKAZA MACHO YAO KWENYE KAZI, HATUA ZA MAENDELEO ZILIFANYIKA.

KWELI, BAADHI WALIPOTEZA WELEKEO WAO KATIKA MGOGORO ULE WA 1902-03. MALI FULANI ZA SHIRIKA ZILIPOTEZWA NA MADHEHEBU; LAKINI, BADALA YA KURUDISHA KAZI NYUMA, MGOGORO HUU ULIASHIRIA MWANZO WA VUGUVUGU KUU YA KUTAKA MAENDELEO. MAONYO YA SEHEMU HII "JIHADHARI" NA UFAFANUZI DHAHIRI WA UKWELI ULIOMO KWENYE KUNDI LA SURA KUHUSU "MAARIFA MUHIMU"  DAIMA UTASAIDIA KULILINDA KANISA KUTOKANA NA MAFUNDISHO YA KUPOTOSHA, NA MASHAURI MENGINE YA GOMBO LA 8 YATAKUWA NA FAIDA HADI MWISHO WA WAKATI.

Wadhamini Wa Machapisho Ya Ellen G. White.

## SEHEMU YA 1—FURSA ZILIZOPO

Israeli atatoa maua na kuchipuka;     Nao watajaza uso wa ulimwengu matunda." Isaya 27: 6.

## SURA YA 1
## KAZI YETU

Kazi yetu ni nini? Je ni sawa na ile aliyopewa Yohana Mbatizaji, ambaye tunasoma juu yake: "Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito Yake." Mathayo 3: 1-3. {8T 9.1}

Wote ambao wanahusika kweli kweli katika kazi ya Bwana katika siku hizi za mwisho watakuwa na ujumbe thabiti wa kuubeba. Soma Aya chache za kwanza za sura ya arubaini ya Isaya: {8T 9.2}

"Sikiliza, ni sauti ya mtu aliaye, Itengenezeni nyikani njia ya Bwana; Nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu. Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa; 5 Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja; Kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya." Isaya 40: 3-5. {8T 9.3}

"Sikiliza, ni sauti ya mtu asemaye, Lia! Nikasema, Nilie nini? Wote wenye mwili ni majani, Na wema Wake wote ni kama ua la kondeni; Majani yakauka, ua lanyauka; Kwa sababu pumzi ya Bwana yapita juu yake. Yakini watu hawa ni majani. Majani yakauka, ua lanyauka; Bali Neno la Mungu wetu litasimama milele." Aya ya 6-8. {8T 9.4}

Sura hii imejazwa na mafundisho yanayofaa kwetu kwa wakati huu. Neno la Bwana kwetu ni: "Tubuni, tengenezeni njia ya kuifufua kazi Yangu." {8T 10.1}

Kuhamishwa kwa kazi kwenda Washington kazi ambayo mpaka sasa inaendelea kule Battle Creek ni hatua katika mwelekeo sahihi. Tunapaswa kuendelea kusonga mbele kwenda katika maeneo ya ng'ambo, ambapo watu wako katika giza la kiroho. Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa." Aya ya 4. Kila kikwazo kwa ajili ya ukombozi wa watu wa Mungu kinapaswa kuondolewa kwa ufunguzi wa Neno Lake na uwasilishaji wa uwanda "Bwana asema." Nuru ya Kweli inapaswa kuangaza; kwa maana giza limeifunika dunia, na giza kuu hufunika watu. Ukweli wa Mungu aliye hai inapaswa kutokea kinyume na makosa. Tangaza habari njema. Tunaye Mwokozi ambaye ameyatoa maisha Yake ili wale wanaomwamini wasipotee, bali wawe na uzima wa milele. {8T 10.2}

Vizuizi kwa ajili ya maendeleo ya kazi ya Mungu vitajitokeza; lakini wewe usiogope. Katika nguvu za Mfalme wa wafalme, Mungu wetu anayeshikilia agano anaunganisha upole na utunzaji wa mchungaji mpole. Hakuna kitu kinachoweza kusimama katika njia Yake. Nguvu Zake ni kamili, na ni ahadi ya utimilifu wa hakika wa ahadi Zake kwa watu Wake. Anaweza kuondoa vizuizi vyote vinavyopinga maendeleo ya kazi Yake. Ana njia ya kuondoa kila shida, ili wale wanaomtumikia na kuheshimu njia Anazotumia wapate kuokolewa. Wema na upendo Wake havina kikomo, na agano Lake haliwezi kubadilika. {8T 10.3}

Mipango ya maadui wa kazi Yake inaweza kuonekana kuwa thabiti na imara sana, lakini Yeye Anaweza kupindua mpango wenye nguvu kuliko yote miongoni mwa mipango hii, na kwa wakati Wake na njia Yake atafanya hivi, atakapoona kuwa imani yetu imejaribiwa vya kutosha na kwamba tunamkaribia Yeye na kumfanya kuwa mshauri wetu. {8T 10.4}

Katika siku zenye giza kabisa, wakati ambapo inaonekana kuwa za kuogofya sana, usiogope. Mwamini Mungu. Yeye Anatenda mapenzi Yake, akifanya mambo yote vyema kwa niaba ya watu Wake. Nguvu za wale wanaompenda na kumtumikia zitafanywa upya siku kwa siku. Ufahamu Wake utawekwa kuwa msaada kwao, ili wasipotee katika kutekeleza makusudi Yake. {8T 10.5}

Haipaswi kukata tamaa katika utumishi wa Mungu. Imani yetu inabidi istahimili shinikizo linaloletwa kuiathiri. Mungu ana uwezo na Yuko tayari kuwapa watumishi Wake nguvu zote wanazohitaji. Atafanya zaidi kutimiza matarajio ya juu kabisa ya wale wanaomtumaini. Yeye Atawapa hekima inayohitajika kwa ajili ya haja zao anuwai. {8T 11.1}

Mtume Paulo aliyejaribiwa alisema: "Naye akaniambia, Neema Yangu yakutosha; maana uweza Wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa

furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu." 2 Wakorintho 12: 9, 10. {8T 11.2}

Jamani ndugu zangu, shikilia imara mwanzo wa ujasiri wenu imara mwisho. Nuru ya ukweli wa Mungu haipaswi kupunguzwa. Inabidi iangaze katikati ya giza la makosa ambalo linaifunika ulimwengu wetu. Neno la Mungu inabidi lifunguliwe kwa wale walio katika vyeo vya juu vya duniani, na vile vile kwa wale walio katika hali ya chini zaidi. {8T 11.3}

Kanisa la Kristo ni wakala wa Mungu wa kuutangaza Ukweli; limepewa mamlaka na Yeye kufanya kazi maalumu; na ikiwa litakuwa aminifu kwa Mungu, kwa kuzitii amri Zake, ndani yake kutakuwamo ubora wa uweza wa Kiungu. Ikiwa litamheshimu Bwana Mungu wa Israeli, hakuna nguvu inaweza kusimama dhidi yake. Ikiwa atakuwa mkweli kwa utii wake, nguvu za adui hazitaweza kumshinda kama vile ambavyo makapi yasivyoweza kuipinga kimbunga. {8T 11.4}

Mbele ya kanisa kuna pambazuko la siku angavu, yenye utukufu, ikiwa litavaa vazi la haki ya Kristo, likijiondoa kutoka kwa utii wote kwa ulimwengu. {8T 11.5}

Washiriki wa kanisa sasa wanahitajika kuungama kurudi nyuma kwao na kusonga mbele pamoja. Ndugu zangu, msiruhusu chochote kingie kati kitakachowatenganisha mtu mmoja na mwingine au na Mungu. Msiongelee tofauti za maoni, bali unganeni katika upendo kwa Ukweli kama ulivyo katika Yesu. Njoo mbele za Mungu, na uombe damu iliyomwagika ya Mwokozi kama sababu kwa nini unapaswa kupokea msaada katika vita dhidi ya uovu. Wewe hutaomba bure. Kadiri unavyomkaribia Mungu, kwa toba ya moyoni na kwa uhakika kamili wa imani, adui anayejaribu kukuangamiza wewe atashindwa. {8T 11.6}

Mgeukie Bwana, enyi wafungwa wa tumaini (Zek 9:12,13). Tafuta nguvu kutoka kwa Mungu, Mungu aliye hai. Onesha imani, nyenyekevu isiyoyumba katika uweza Wake na utayari Wake kuokoa. Kutoka kwa Kristo kunatiririka kijito hai cha wokovu. Yeye Ndiye Chemchemi ya uzima, Chanzo cha nguvu zote. Iwapo kwa imani tutashikilia nguvu Zake, Yeye Atabadilisha, atabadilisha kwa jinsi ya kustaajabisha, mwonekano mbaya kabisa, wa kukatisha tamaa. Atalifanya hili kwa ajili ya utukufu wa Jina Lake. {8T 12.1}

Mungu huwataka wale walio waaminifu Kwake, ambao wanamwamini, kuwatia moyo wale wasioamini na wasio na matumaini. Hebu Bwana na atusaidie kusaidiana na kumthibitisha kwa imani hai. {8T 12.2}

"Mwimbieni Mungu, nguvu zetu, nyimbo za furaha, Mshangilieni Mungu wa Yakobo. Pazeni Zaburi, pigeni matari, Kinubi chenye sauti nzuri, na kinanda." Zaburi 81: 1, 2. {8T 12.3}

"Ni neno jema kumshukuru Bwana, Na kuliimbia Jina Lako, Ee Uliye juu. Kuzitangaza rehema Zako asubuhi, Na uaminifu Yako wakati wa usiku. Kwa chombo chenye

nyuzi kumi, Na kwa kinanda, Na kwa mlio wa kinubi. 4 Kwa kuwa umenifurahisha, Bwana, Kwa kazi yako; nitashangilia Kwa ajili ya matendo ya mikono Yako." Zaburi 92: 1-4. {8T 12.4}

"Njoni, tumwimbie Bwana, Tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu. Tuje mbele Zake kwa shukrani, Tumfanyie shangwe kwa Zaburi. Kwa kuwa Bwana ni Mungu mkuu, Na Mfalme mkuu juu ya miungu yote. Mkononi Mwake zimo bonde za dunia, Hata vilele vya milima ni Vyake. Bahari ni Yake, Ndiye aliyeifanya, Na mikono Yake iliumba nchi kavu. 6 Njoni, tuabudu, tusujudu, Tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba." Zaburi 95: 1-6. {8T 13.1}

"Mwimbieni Bwana wimbo mpya, Mwimbieni Bwana, nchi yote. Mwimbieni Bwana, libarikini Jina Lake, Tangazeni wokovu Wake siku kwa siku. Wahubirini mataifa habari za utukufu Wake, Na watu wote habari za maajabu Yake. Kwa kuwa Bwana ni mkuu Mwenye kusifiwa sana. Na wa kuhofiwa kuliko miungu yote.” Zaburi 96:1-4. {8T 13.2}

"Mfanyieni Bwana shangwe, dunia yote; Mtumikieni Bwana kwa furaha; Njoni mbeleZzake kwa kuimba; Jueni kwamba Bwana Ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu Wake; Tu watuWake, na kondoo wa malisho Yake. Ingieni malangoni Mwake kwa kushukuru; Nyuani Mwake kwa kusifu; Mshukuruni, lihimidini Jina Lake; Kwa kuwa Bwana Ndiye mwema; Rehema Zake ni za milele; Na uaminifu Wake vizazi na vizazi." Zaburi 100. {8T 13.3}

## SURA YA 2

## UTUME WETU

Ni kusudi la Mungu kwamba watu Wake watakuwa watu waliotakaswa, waliosafishwa, watakatifu, wanaowasilisha nuru kwa wote walio karibu nao. Ni kusudi Lake kwamba, kwa maisha yao kuwa mfano wa Ukweli, watakuwa sifa katika dunia. Neema ya Kristo inatosha kufanya hili litokee. Lakini hebu watu wa Mungu wakumbuke kwamba ni pale tu wanapoamini na kuzitenda kanuni za injili ndipo Yeye anapoweza kuwafanya kuwa sifa duniani. Ni pale tu wanapotumia vipaji vyao walivyopewa na Mungu katika utumishi Wake ndipo watakapofurahia utimilifu na nguvu ya ahadi ambayo kanisa limeitwa kusimama juu yake. Ikiwa wale wanaokiri kumwamini Kristo kama Mwokozi wao, watafikia kiwango cha chini tu cha kipimo cha dunia, kanisa litashindwa kuzaa mavuno mengi ambayo Mungu anayatarajia. "Umeonekana kuwa umepunguka" huandikwa kwenye rekodi yake. {8T 14.1}

Agizo lile ambalo Kristo aliwapa wanafunzi Wake mara tu kabla ya kupaa Kwake ndio hati ya umishenari wa ufalme Wake. Katika kuitoa kwa wanafunzi, Mwokozi

aliwafanya kuwa mabalozi Wake na kuwapa hati zao za utambulisho. Ikiwa, baadaye, wangetakiwa kuthibitisha na kuulizwa ni kwa mamlaka gani, wao wavuvi wasio na elimu, walisonga mbele kama walimu na waponyaji, wangeweza kujibu: "Yeye Yule ambaye Wayahudi walimsulubisha, lakini akafufuka kutoka kwa wafu, ametuteua katika utumishi wa Neno Lake, akitangaza, 'Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani." {8T 14.2}

Kristo alitoa agizo hili kwa wanafunzi Wake kama wahudumu Wake wakuu, wasanifu ambao walipaswa kuweka msingi wa kanisa Lake. Yeye Aliweka juu yao, na juu ya wote ambao wangefuatia kama wahudumu Wake, wajibu wa kupeleka injili Yake kutoka kizazi hadi kizazi, kutoka zama hadi zama. {8T 14.3}

Wanafunzi wale hawakupaswa kuwangojea watu waje kwao. Walipaswa kwenda kwa watu, kuwatafuta wenye dhambi kama mchungaji anavyowatafuta kondoo waliopotea. Kristo aliufungua ulimwengu mbele yao kama uwanja wao wa kazi. Walipaswa kwenda "ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Marko 16: 15. Walipaswa kuhubiri juu ya Mwokozi, kuhusu maisha Yake ya huduma isiyo na ubinafsi, Kifo Chake cha aibu, Upendo Wake usio na kifani, usiobadilika. Jina lake lilipaswa kuwa neno lao kuu, kiunganishi chao cha umoja. Kwa Jina Lake walipaswa kuzishinda ngome za dhambi. Imani katika Jina Lake ilipaswa kuwaonesha kuwa ni Wakristo. {8T 14.4} Akiwapa wanafunzi maelekezo zaidi, Kristo alisema: "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." "Lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu." Matendo 1: 8; Luka 24:49. {8T 15.1}

Kwa kulitii Neno la Bwana wao wanafunzi walikusanyika huko Yerusalemu kusubiri kutimizwa kwa ahadi ya Mungu. Hapa walikaa siku kumi, siku za kujichunguza moyo kwa kina. Waliweka mbali tofauti zote na wakakaribiana pamoja katika ushirika wa Kikristo. {8T 15.2}

Mwishoni mwa siku kumi Bwana alitimiza ahadi Yake kwa umwagwaji wa ajabu wa Roho Wake. “Kukaja ghafula, toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyika, kama ndimi za moto, uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.” "Na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu." Matendo 2: 2-4, 41. {8T 15.3}

“Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na

kulithibitisha lile Neno kwa ishara zilizofuatana nalo. (Marko 16:20). Licha ya upinzani mkali ambao wanafunzi walikutana nao, kwa muda mfupi injili ya ufalme ilikuwa imetangazwa katika sehemu zote za dunia zilizokaliwa. {8T 15.4}

Agizo walilopewa wanafunzi limetolewa kwetu pia. Leo, kama wakati ule, Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka anapaswa kuinuliwa mbele za wale wasiomjua Mungu na wasio na tumaini ulimwenguni. Bwana anawaita wachungaji, walimu, na wainjilisti. Kutoka nyumba hadi nyumba, watumishi Wake wanapaswa kutangaza ujumbe wa wokovu. Kwa kila taifa, kabila, lugha, na jamaa habari za msamaha kupitia kwa Kristo zinapaswa kupelekwa. {8T 15.5}

Ujumbe haupasi kutolewa kwa maneno ya woga na kuzungumza bila ari kana kwamba huna uhai, au bila roho, bali kwa maneno dhahiri, thabiti, yenye kusisimua. Mamia wanasubiri onyo ili wakimbie na kuponya nafsi zao. Ulimwengu unahitaji kuona ndani ya Wakristo ushahidi wa nguvu ya Ukristo. Sio tu katika maeneo machache, lakini ulimwenguni kote, wajumbe wa rehema wanahitajika. Kutoka katika kila nchi kunasikika kilio: "Vuka uje,... utusaidie." Tajiri na maskini, wa juu na wa chini, wanaita kwa ajili ya nuru. Wanaume na wanawake wana njaa ya Ukweli kama ulivyo katika Yesu. Watu wanaposikia injili ikihubiriwa kwa nguvu kutoka juu, watajua kwamba karamu imeandaliwa kwa ajili yao, nao wataitikia wito: "Njoni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari." Luka 14:17. {8T 16.1}

Maneno "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe" (Marko 16:15) husemwa kwa kila mmoja wa wafuasi wa Kristo. Wote ambao wameitwa katika maisha ya Kristo wameitwa kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa wanadamu wenzao. Shauku ile ile ya roho ambayo (Yeye Kristo) alihisi kwa ajili ya kuwaokoa waliopotea inapaswa kudhihirika ndani yao. Sio wote wanaweza kujaza nafasi moja, lakini kwa wote kuna mahali na kazi. Wote ambao baraka za Mungu zimetolewa kwao wanapaswa kuitikia kwa huduma halisi; kila kipawa kinapaswa kutumika kwa ajili ya maendeleo ya ufalme Wake. {8T 16.2}

### Ahadi Isiyobadilika

Kristo alifanya mpango kamili kwa ajili ya kuendelezwa kwa kazi waliyopewa wanafunzi, na kuweka juu Yake Yeye mMenyewe jukumu la mafanikio yake. Maadamu walitii Neno Lake, na kufanya kazi pamoja Naye, kamwe wasingeshindwa. Enendeni ulimwenguni mwote, aliwaamuru, nendeni katika sehemu za mbali kabisa za ulimwengu kunakokaliwa na watu, lakini mjue ya kuwa uwapo Wangu utakuwa pale. Fanya kazi kwa imani na ujasiri, kwani hautakuja kamwe wakati ambapo nitawaacha. {8T 16.3}

Kwetu sisi pia ahadi ya uwapo wa kudumu wa Kristo imetolewa. Kupita kwa wakati hakujafanya badiliko lolote katika ahadi Yake wakati wa kuagana. Yuko pamoja nasi leo, kwa hakika kama alivyokuwa na wanafunzi, Naye atakuwa pamoja nasi "hata ukamilifu wa dahari." {8T 17.1}

"Songa mbele ukiihubiri injili kwa mataifa yote," Mwokozi anatuambia, "ili wapate kuwa watoto wa Mungu. Niko pamoja nanyi katika kazi hii, nikiwafundisha, nikiwaongoza, nikiwafariji, nikiwaimarisha, Ili nikiwapa mafanikio katika kazi yenu ya kujikana nafsi na ya kujitoa. Nitaigusa mioyo, nikiwathibitisha kuhusu dhambi, na kuigeuza kutoka gizani kwenda kwenye nuru, kutoka kutotii kwenda kuwa wenye haki. Katika nuru yangu wataona mwanga. Mtakutana na upinzani wa mawakala wa kishetani, lakini wekeni imani yenu Kwangu. Mimi sitawaangusha kamwe." {8T 17.2}

Je! hamdhani kwamba Kristo anawathamini wale wanaoishi kikamilifu kwa ajili Yake? Je! hamdhani kwamba Yeye huwatembelea wale ambao, kama Yohana mpendwa, kwa ajili Yake wako katika maeneo magumu yenye majaribio na mitihani? Yeye Anawatafuta waaminifu Wake, na hufanya ushirika nao, akiwatia moyo na kuwaimarisha. Na malaika wa Mungu, wenye nguvu zaidi, hutumwa na Mungu kuwahudumia watendakazi Wake wa kibinadamu ambao wanausema Ukweli kwa wale wasioujua. {8T 17.3}

Kwa mhudumu wa injili, Mungu ametoa kazi ya kuwaongoza kwa Kristo wale ambao wametanga kutoka kwenye njia nyembamba. Anapaswa kuwa na busara na bidii katika juhudi zake. Mwishoni mwa kila mwaka anapaswa kuwa na uwezo wa kuangalia nyuma na kuona roho zilizookolewa kama matokeo ya kazi yake. Wengine itabidi awaokoe kwa hofu, "kwa kuwanyakua katika moto; mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili," "akilishika lile Neno la imani vile vile kama alivyofundishwa." Yuda 23; Tito 1: 9. Agizo la Paulo kwa Timotheo linawajia wachungaji wa leo: "Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa Kwake na kwa ufalme Wake; lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. 2 Timotheo 4: 1, 2. {8T 17.4}

Lakini sio tu kwa wale wanaolihubiri Neno Mungu ameweka jukumu la kutafuta kuokoa wenye dhambi. Yeye Ametoa kazi hii kwa wote. Mioyo yetu inapaswa kujazwa na upendo wa Kristo kiasi kwamba maneno yetu ya shukrani yatachangamsha mioyo mingine. Hii ni huduma ambayo wote wanaweza kuifanya, na Bwana anaikubali kama ambayo imetolewa Kwake Yeye Mwenyewe. Yeye Anaifanikisha, akimpatia mfanyakazi mwaminifu neema inayompatanisha mwanadamu na Mungu. {8T 18.1}

Bwana na awasaidie watu wake kutambua kwamba kuna kazi ya dhati na bidii inayopaswa kufanywa. Na awasaidie kukumbuka kuwa nyumbani, kanisani, na ulimwenguni wanapaswa kufanya kazi za Kristo. Hawaachwi kufanya kazi peke yao. Malaika ni wasaidizi wao. Na Kristo ni msaidizi wao. Basi hebu na wafanye kazi kwa uaminifu na bila kuchoka. Katika wakati unaofaa watavuna ikiwa hawatazimia. {8T 18.2}

Mkristo aliye msafiri hatasalimu amri kwa shauku yake ya kutaka kupumzika. Anasonga mbele bila kusita kwa mwendo thabito, akisema: "Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia." Hii ndiyo kauli mbiu yake: "Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu … Bali nakaza mwendo …… sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu." Wafilipi 3: 12-14. (19) {8T 18.3}

## SURA YA 3
## UWEZO ULIOAHIDIWA

Mungu hatuagizi kufanya kwa nguvu zetu wenyewe kazi ile iliyo mbele yetu. Ametoa msaada wa Kiungu kwa dharura zote ambazo rasilimali zetu za kibinadamu haziwezi kumudu. Yeye Anamtoa Roho Mtakatifu kusaidia katika kila shida, kuimarisha tumaini na imani yetu, kuangazia akili zetu na kuisafisha mioyo yetu. {8T 19.1}

Mara tu kabla ya kusulubiwa Kwake Mwokozi aliwaambia wanafunzi Wake: "Mimi sitawaacha ninyi yatima." "Nitamwomba Baba, Naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele." Lakini atakapokuja huyo Roho wa Kweli atawaongoza awatie kwenye Kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri Lake Mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake."

“Atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia." Yohana 14:18, 16; 16:13; Yohana 14:26. {8T 19.2}

Kristo ameandaa kwamba kanisa Lake litakuwa mwili uliobadilishwa, ulioangazwa na nuru ya mbinguni, ulio na utukufu wa Imanueli. Ni kusudi Lake kwamba kila Mkristo atazungukwa na angahewa ya kiroho ya nuru na amani. Hakuna kikomo kwa manufaa/kufaa kwa yule ambaye, akiweka nafsi kando, anatoa nafasi kwa ajili ya utendaji wa Roho Mtakatifu juu ya moyo wake na anaishi maisha yaliyowekwa wakfu kabisa kwa Mungu. {8T 19.3}

Matokeo ya kumwagwa kwa Roho katika siku ya Pentekoste yalikuwa nini? Habari njema za Mwokozi aliyefufuka zilipelekwa katika mipaka ya mwisho kabisa ya ulimwengu uliokaliwa. Mioyo ya wanafunzi ilichajiwa kwa nguvu na ukarimu ulioshehenii, wa kina, na ulioenea, kiasi kwamba uliwasukuma kwenda katika miisho ya dunia wakishuhudia: “Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo. (Wagalatia 6:14). Walipotangaza Ukweli kama ulivyo katika Yesu, mioyo ilijitoa kwa nguvu ya ujumbe. Kanisa liliwaona waongofu wakimiminika kwake kutoka pande zote. Watu waliorudi nyuma waliongolewa upya. Wenye dhambi waliungana na Wakristo katika kuitafuta ile lulu ya thamani kubwa. Wale ambao walikuwa ni wapinzani wakubwa na wachungu kabisa wa injili wakawa watetezi wake. Unabii ulitimizwa: “Wanyonge watakuwa "kama Daudi," na nyumba ya Daudi "kama malaika wa Bwana." Kila Mkristo aliona kwa ndugu yake mfano wa Kiungu wa upendo na ukarimu. Shauku moja ilishinda. Mada moja ya kuigwa ilimeza mengine yote. Tamaa/Shauku moja tu ya waumini ilikuwa ni kudhihirisha mfano wa tabia ya Kristo na kufanya kazi kwa ajili ya kuukuza ufalme Wake. {8T 19.4}

"Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka Kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote." Matendo 4:33. Chini ya kazi zao waliongezwa kanisani watu wateule, ambao, walipopokea Neno la uzima, walitoa wakfu maisha yao kwa kazi ya kuwapa wengine tumaini ambalo lilikuwa limejaza mioyo yao amani na furaha. Mamia walitangaza ujumbe huu: "Ufalme wa Mungu umekaribia." Hawakuweza kuzuiliwa au kuogopeshwa na vitisho. Bwana alisema kupitia kwao; na, kokote walikoenda, wagonjwa waliponywa, na maskini walihubiriwa injili. {8T 20.1}

Mungu anaweza kufanya kazi kwa nguvu sana pale wanadamu wanapojitoa kwa utawala wa Roho Wake. {8T 20.2}

Kwetu sisi leo, kama ilivyokuwa kweli kwa wanafunzi wa kwanza, ahadi ya Roho ni yetu. Mungu leo atawapa wanaume na wanawake uwezo kutoka juu, kama alivyowapa wale ambao katika Siku ya Pentekoste walilisikia Neno la wokovu. Sasa hivi, Roho Wake na neema Yake ni kwa ajili ya wote wanaozihitaji na

watakaomwamini na kumchukua kwa Neno Lake. {8T 20.3}

Weka umakini hapa, tilia maanani kwamba ilikuwa ni baada ya wanafunzi kufikia umoja kamili, wakati hawakuwa wanashindana kwa ajili ya nafasi ya juu zaidi, ndipo Roho alimwagwa. Walikuwa wamepatana. Tofauti zote zilikuwa zimewekwa mbali. Na ushuhuda uliochukuliwa na wao baada ya kupewa Roho ni ule ule. Zingatia Neno: "Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja." Matendo 4:32. Roho wa Yeye aliyekufa ili watenda dhambi wapate kuishi alihuisha/aliisisimua kusanyiko lote la waumini. {8T 20.4}

Wanafunzi hawakuomba baraka kwa ajili yao wenyewe. Walielemewa na mzigo wa roho. Injili ilipaswa kupelekwa hadi miisho ya dunia, nao walidai majaliwa ya uwezo ule ambao Kristo alikuwa ameahidi. Ndipo ilikuwa kwamba Roho Mtakatifu alimwagwa, na maelfu waliongolewa kwa siku moja. {8T 21.1}

Hivyo ndivyo inavyoweza kuwa sasa. Hebu Wakristo na waondoe mifarakano yote na wajitoe kwa Mungu kwa ajili ya kuwaokoa watu waliopotea. Hebu na waombe kwa imani baraka iliyoahidiwa, nayo itakuja. Kumwagwa kwa Roho katika siku za mitume ilikuwa ni "mvua ya vuli," na matokeo yalikuwa ni ya kupendeza na utukufu. Lakini mvua ya masika itakuwa nyingi zaidi. Ni ahadi gani imetolewa kwa wale wanaoishi katika siku hizi za mwisho? "Irudieni ngome, enyi wafungwa wa tumaini; hata hivi leo nasema ya kwamba nitakurudishia maradufu." "Mwombeni Bwana mvua wakati wa masika, naam, Bwana afanyaye umeme, Naye atawapa manyunyu ya mvua, kila mtu atapewa nyasi kondeni." Zekaria 9:12; 10: 1. {8T 21.2}

Kristo alitangaza kwamba mvuto wa Kiungu wa Roho ulikuwa uwe na wafuasi Wake hadi mwisho. Lakini ahadi hiyo haijatathaminiwa ipasavyokama inavyopaswa kuwa; na kwa hivyo kutimizwa Kwake hakuonekani kama ambavyo ingekuwa. Ahadi ya Roho ni jambo linalofikiriwa kidogo; na matokeo yake ni kile tu kinachoweza kutarajiwa - ukame wa kiroho, giza la kiroho, uchakavu wa kiroho, na kifo. Mambo madogo-madogo hushughulisha umakini wa akili, na nguvu ya Kiungu ambayo ni muhimu kwa ajili ya ukuaji na ustawi wa kanisa, na ambayo ingeleta baraka zingine zote katika msafara wake, inakosekana, ingawa hutolewa kwa ukamilifu wake. {8T 21.3}

Ni kukosekana kwa Roho ndiko kunakofanya huduma ya injili kukosa nguvu kiasi kile. Kujifunza, kipaji, ufasaha, kila zawadi ya asili au inayopatikana kwa kujifunza, inaweza kumilikiwa; lakini, bila uwapo wa Roho wa Mungu, hakuna moyo utakaoguswa, hakuna mwenye dhambi atakayeletwa kwa Kristo. Kwa upande mwingine, ikiwa wameunganishwa pamoja na Kristo, na ikiwa wanazo karama za Roho, Wale walio maskini na wajinga kabisa katika wanafunzi  Wake watakuwa na

uwezo ambao utaathiri mioyo ya watu. Mungu huwafanya kuwa mifereji kwa ajili ya mbubujiko wa mvuto wa hali ya juu ulimwenguni. {8T 21.4}

Kwa nini hatuoni njaa na kiu kwa ajili ya karama ya Roho, kwani hii ndiyo njia ambayo kwayo tunapaswa kupokea uwezo? Kwa nini hatuizungumzii, hatuiombi, hatuhubiri kuhusu hiyo? Bwana Yupo tayari sana kumtoa Roho Mtakatifu kwetu kuliko wazazi walivyo tayari kutoa zawadi zilizo nzuri kwa watoto wao. Kila mtendakazi anapaswa kumsihi Mungu kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Makundi yanapaswa kukusanyika pamoja kuomba msaada wa pekee, wa hekima ya kimbingu, ili waweze kujua jinsi ya kupanga na kutekeleza mipango kwa hekima. Hasa watu wanapaswa kumwomba Mungu ili awabatize wamishenari kwa Roho Mtakatifu. {8T 22.1}

Uwepo wa Roho pamoja na watendakazi wa Mungu utaupa uwasilishaji wa Ukweli uwezo ule ambao hakuna heshima wala utukufu wowote wa ulimwengu ungeweza kutoa. Roho hutoa nguvu ile ambayo inazihimili roho zile zinazopambana, zinazopigana mweleka katika kila dharura, katikati ya ukatili wa jamaa, chuki ya ulimwengu, na utambuzi wa kutokukamilika kwao na makosa. {8T 22.2}

Ari kwa ajili ya Mungu iliwasukuma wanafunzi kushuhudia Ukweli kwa nguvu kubwa. Je! ari hii haipaswi kuichochea mioyo yetu na hamu ya kusimulia kisa cha upendo unaokomboa, wa Kristo na Yeye aliyesulubiwa? Je! Roho wa Mungu hapaswi kuja leo kama jibu kwa maombi ya bidii, yasiyochoka, na kuwajaza watu uwezo kwa ajili ya huduma? Kwa nini basi kanisa ni dhaifu kiasi hicho na kukosa kuwa na Roho Mtakatifu? {8T 22.3}

Ni fursa ya kila Mkristo, sio kutazamia tu, bali kuharakisha ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo. Kama wale wote wanaolikiri jina Lake wangelikuwa wanazaa matunda kwa ajili ya utukufu Wake, ni kwa haraka kiasi gani ulimwengu wote ungepandwa mbegu ya injili. Haraka mavuno ya mwisho yangepevuka, na Kristo angekuja kukusanya nafaka ya thamani. {8T 22.4}  23

Ndugu na dada zangu, ombeni kwa ajili ya Roho Mtakatifu, Mungu yuko nyuma ya kila ahadi aliyoitoa. Mkiwa na Biblia zenu mikononi mwenu, sema: "Nimefanya kama ulivyosema, nawasilisha ahadi Yako, 'Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa.'" Kristo anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." “Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mathayo 7: 7; Marko 11:24; Yohana 14:13. {8T 23.1}

Upinde wa mvua kuzunguka kiti cha enzi ni uhakikisho kwamba Mungu ni mkweli;

kwamba ndani Yake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka. Tumetenda dhambi dhidi Yake na hatustahili fadhila Zake lakini bado ni Yeye Mwenyewe aliyeweka katika midomo yetu lile ombi la ajabu kabisa miongoni mwa maombi: "Usituchukie, kwa ajili ya Jina Lako, usikifedheheshe kiti cha enzi cha utukufu Wako, kumbuka, usilivunje agano ulilofanya nasi." Yeremia 14:21. Yeye Ameahidi Mwenyewe kusikiliza kilio chetu tunapokuja Kwake tukikiri kutokustahili kwetu na dhambi. Heshima ya kiti chake cha enzi iko hatarini Neno Lake kwetu lisipotimizwa. {8T 23.2}

Kristo huwatuma wajumbe Wake katika kila sehemu ya utawala wake kuwasilisha mapenzi Yake kwa watumishi Wake. Anatembea katikati ya Makanisa Yake. Anataka sana kuwatakasa, kuwainua, na kuwaadilisha wafuasi Wake. Mvuto wa wale wanaomwamini utakuwa katika ulimwengu harufu ya maisha kwa uzima. Kristo anashikilia nyota katika mkono Wake wa kuume, na ni kusudi Lake kuiruhusu nuru Yake iangaze kupitia kwao kwenda kwa ulimwengu. Hivyo anatamani kuwaandaa watu Wake kwa ajili ya huduma ya juu zaidi katika kanisa la mbinguni. Ametupatia kazi kubwa ya kufanya. Hebu na tuifanye kwa uaminifu. Hebu na tuoneshe katika maisha yetu kile ambacho neema ya Bwana inaweza kufanya kwa wanadamu. {8T 23.3}

## SURA YA 4
## WAJIBU WETU

Kuna nyakati ambapo maono dhahiri yanawasilishwa kwangu juu ya hali ya kanisa la masalio, hali ya kutokujali kwa kutisha kwa mahitaji ya ulimwengu unaoangamia kwa kukosa maarifa ya Ukweli kwa ajili ya wakati huu. Halafu nina saa kadhaa, na wakati mwingine siku kadhaa, za uchungu mkali. Wengi ambao wamepewa Ukweli wa kuokoa wa ujumbe wa malaika wa tatu wanashindwa kutambua kwamba wokovu wa roho unategemea kujitoa na shughuli ya kanisa la Mungu. Wengi

wanatumia baraka zao katika huduma kwa nafsi. Lo, moyo wangu unaumia kiasi gani kwa sababu Kristo anaaibishwa na tabia yao isiyofanana na ya Kristo! Lakini, baada ya uchungu kupita, ninajisikia kufanya kazi kwa bidii zaidi kuliko hapo awali ili nipate kuwaamsha waweke bidii isiyo na ubinafsi kwa ajili ya wokovu wa wanadamu wenzao. {8T 24.1}

Mungu amewafanya watu Wake kuwa mawakili wa neema na kweli Yake, na ni jinsi gani anachukulia kupuuza kwao kutoa baraka hizi kwa wanadamu wenzao? Hebu tufikirie kuwa koloni fulani la mbali la Uingereza lina shida kubwa kwa sababu ya njaa na vita vinavyotishia kuja. Watu wengi wanakufa kwa njaa, na adui mwenye nguvu anajikusanya mpakani, akitishia kuiharakisha kazi ya mauti. Serikali kule nyumbani inafungua maghala yake; fadhila za umma zinamwagika; misaada inamiminika kupitia mifereji mingi. Meli husafirishwa ikiwa na bidhaa za thamani kwa ajili ya maisha na hupelekwa kwenye eneo la mateso, ikifuatana na maombi ya wale ambao mioyo yao imehamasishwa kusaidia. Na kwa muda fulani meli husafiri moja kwa moja kufikia mwisho wa safari yake. Lakini, baada ya kuwa mbali na nchi kavu, shauku ya wale waliopewa dhamana ya kubeba chakula kwa wanaoteseka na njaa hupungua. Ijapokuwa wanafanya kazi inayowafanya kuwa washirika pamoja na malaika, wanapoteza mawazo ya yale mema waliyoanza nayo. Kupitia kwa washauri wabaya, jaribu linaingia. {8T 24.2}

Kundi la visiwa liko katika njia yao, na, ingawa ni mbali na wanapokwenda, wanaamua kupiga simu. Jaribu ambalo tayari limeingia linakua na nguvu zaidi. Roho ya ubinafsi inachukua umiliki wa akili zao. Manufaa ya kibiashara yanajitokeza. Wale wanaosimamia meli hiyo wanashawishika kubaki visiwani. Kusudi lao la mwanzo la rehema linapotea kutoka katika upeo wa macho yao. Wanawasahau watu wale wenye njaa ambao walitumwa kwao. Akiba waliyokabidhiwa hutumika kwa faida yao wenyewe. Mali kwa ajili ya ukarimu zinageuzwa kuwa mali za ubinafsi. Wanabadilisha njia ya maisha kwa faida ya ubinafsi, na huwaacha wanadamu wenzao wakifa. Kilio cha wanaoangamia kinapanda kwenda mbinguni, na Bwana anaandika katika rekodi Yake kisa cha unyang'anyi. {8T 24.3}

Fikiri kuhusu kitisho cha wanadamu kufa kwa sababu wale waliowekwa katika usimamizi wa njia za msaada walithibitika kuwa si waaminifu kwa dhamana yao. Ni vigumu kwetu kutambua kwamba mwanadamu anaweza kuwa na hatia ya dhambi mbaya kama hiyo. Lakini bado nimeagizwa kukuambia wewe, ndugu yangu, dada yangu, kwamba Wakristo wanairudia dhambi hii kila siku. {8T 25.1}

Katika Edeni, mwanadamu alianguka kutoka katika hali yake ya juu na kupitia katika dhambi akawa ni mwenye kupatwa na kifo. Ilionekana mbinguni kwamba wanadamu walikuwa wakiangamia, na huruma ya Mungu iliamshwa. Kwa gharama kubwa sana Alipanga njia za msaada. Mungu "aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

Yohana 3:16. Hakukuwa na tumaini lolote kwa mkosaji isipokuwa kupitia kwa Kristo. Mungu aliona kwamba "hapana mtu, akastaajabu kwa kuwa hapana mwombezi; basi, mkono Wake Mwenyewe ndio ulimletea wokovu; na haki Yake ndiyo iliyomsaidia." Isaya 59:16. {8T 25.2}

Bwana alichagua watu na kuwafanya kuwa hazina za Ukweli Wake. Ilikuwa kusudi Lake kwamba kwa kufunuliwa kwa tabia Yake kupitia kwa Israeli, watu wangevutwa kuja Kwake. Kwa ulimwengu wote mwaliko wa injili ulipaswa kutolewa. Kupitia kwa fundisho la huduma ya kafara, Kristo alipaswa kuinuliwa mbele ya mataifa, na wote wale ambao wangemwangalia wangeishi. {8T 25.3}

Lakini Israeli hawakulitimiza kusudi la Mungu. Walimsahau Mungu na kuacha kuona heshima yao ya juu kama wawakilishi Wake. Baraka walizozipokea hazikuleta baraka kwa ulimwengu. Manufaa yao yote yalitengwa kwa ajili ya utukufu wao wenyewe. Walimnyima Mungu huduma aliyoitaka kutoka kwao, na kuwanyima wanadamu wenzao uongozi wa kidini na mfano mtakatifu. {8T 26.1}

Hatimaye Mungu alimtuma Mwanawe kuwadhihirishia wanadamu tabia Yake Yeye Asiyeonekana. Kristo alikuja na kuishi hapa duniani maisha ya utii wa sheria ya Mungu. Yeye Aliyatoa maisha Yake ya thamani apate kuiokoa dunia na kuwafanya watumishi Wake kuwa mawakili Wake. Kwa kumtoa Kristo kuwa zawadi, hazina zote za mbinguni zilitolewa kwa mwanadamu. Kanisa lilipewa shehena ya chakula cha mbinguni kwa ajili ya roho zenye njaa. Hii Ndiyo hazina ambayo watu wa Mungu walikuwa wameagizwa kuibeba kwa ulimwengu-Yeye Ndiyo Hazina. Walipaswa kutekeleza wajibu wao kwa uaminifu, wakiendelea na kazi yao hadi pale ambapo ujumbe wa rehema umeuzunguka ulimwengu. {8T 26.2}

Kristo alipaa kwenda na kumtuma Roho Wake Mtakatifu kutoa uwezo kwa ajili ya kazi ya wanafunzi wake. Maelfu waliongolewa katika siku moja. Katika kizazi kimoja injili ilipelekwa kwa kila taifa chini ya mbingu. Lakini kidogo kidogo badiliko lilikuja. Kanisa lilipoteza upendo wake wa kwanza. Likawa mchoyo/mbinafsi na mpenda raha. Roho ya ulimwengu ilipendwa sana. Adui alitupa uchawi wake kwa wale ambao Mungu alikuwa amewapa nuru kwa ajili ya ulimwengu uliomo gizani, nuru ambayo ilipaswa kuangaza kwa matendo mema. Ulimwengu uliporwa baraka ambazo Mungu alitaka watu wazipate. {8T 26.3}

Je! jambo lilo hilo halirudiwi katika kizazi hiki? Wengi katika siku zetu wanazuia kile ambacho Bwana amewakabidhi kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu ambao haujaonywa, wala kuokolewa. Katika Neno la Mungu malaika anaoneshwa akiruka katikati ya mbingu, "mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14: 6-7 {8T 26.4}

Ujumbe wa Ufunuo 14 ni ujumbe ambao tunapaswa kuupeleka kwa ulimwengu. Ndio mkate wa uzima kwa ajili ya siku hizi za mwisho. Mamilioni ya wanadamu wanaangamia katika ujinga na uovu. Lakini wengi wa wale ambao Mungu amewakabidhi ghala ya uzima wanaziangalia roho hizi bila kuzijali. Wengi husahau kwamba kwao umekabidhiwa mkate wa uzima kwa ajili ya wale walio na njaa ya wokovu. {8T 27.1}

Oo, kwa ajili ya Wakristo waliojiweka wakfu, kwa ajili ya msimamo thabiti kama wa Kristo, kwa ajili ya imani inayofanya kazi kwa upendo na kuitakasa roho! Mungu na atusaidie kutubu na kubadilisha matendo yetu ya uvivu kuwa shughuli iliyowekwa wakfu kwa kwa ajili ya Mungu. Na atusaidie kuonesha kwa maneno na matendo yetu kwamba tunafanya mzigo wa roho zile zinazongamia kuwa yetu wenyewe. {8T 27.2}

Hebu na tushukuru kila wakati kwa sababu ya uvumilivu wa Mungu na harakati na matendo yetu ya kukawia, yasiyo na imani. Badala ya kujidanganya kwa mawazo ya kile ambacho tumekifanya, baada ya kufanya kidogo tu, tunapaswa kufanya kazi kwa dhati na bidii zaidi. Hatupaswi kukomesha juhudi zetu au kulegeza umakini wetu katika kukesha. Kamwe ari yetu isipungue. Maisha yetu ya kiroho inabidi yahuishwe kila siku na kijito kile kinachofurahisha mji wa Mungu wetu. Inabidi daima tuzitazamie fursa za kutumia kwa ajili ya Mungu talanta zile ambazo ametupa. {8T 27.3}

Ulimwengu ni ukumbi wa maonesho ya mchezo wa kuigiza (theatre); wahusika, wakazi wake, wanajiandaa kuigiza sehemu zao katika drama kuu ya mwisho. Miongoni mwa umati mkubwa wa wanadamu hakuna umoja, isipokuwa pale watu wanapoungana pamoja ili kutimiliza makusudi yao ya ubinafsi. Mungu anaangalia. Makusudi Yake kuhusu raia Wake waasi yatatimizwa. Ulimwengu haujatiwa mikononi mwa wanadamu bado, ingawa Mungu anaruhusu vipengele vya mkanganyiko na machafuko yatawale kwa muda fulani. Nguvu kutoka chini isiyoonekana inafanya kazi kuleta matukio makuu ya mwisho kwenye drama hii - Shetani akija kama Kristo, na kufanya kazi kwa udanganyifu wote wa udhalimu ndani ya wale ambao wanajifunga pamoja katika mashirika ya siri. Wale ambao wanaosalimu amri kwa mapenzi makali kwa ajili ya shirikisho wanatekeleza mipango ya adui. Sababu itafuatiwa na athari. {8T 27.4}

Uovu karibu unafikia kikomo chake. Mkanganyiko umeujaza ulimwengu, na ogofyo kuu hivi karibuni litakuja juu ya wanadamu. Mwisho umekaribia sana. Sisi ambao tunaujua Ukweli tunapaswa kujiandaa kwa ajili ya kile kitakachopasuka/kitakachotokea ulimwenguni kama mshangao mkubwa. {8T 28.1}

Yohana anaandika: “Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na Yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso Wake, na mahali pao

hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.” Ufunuo 20:11, 12. {8T 28.2}

Je! Sisi kama kanisa tumelala? Laiti, kama vijana wa kiume na wa kike katika taasisi zetu ambao kwa sasa hawako tayari kwa ajili ya kutokea kwa Bwana, hawajajiandaa kuwa ajili ya kuwa washiriki wa familia ya Bwana, wangeweza tu kutambua ishara za nyakati, ni mabadiliko ya jinsi gani yangelionekana ndani yao! Bwana Yesu anatoa wito kwa wafanyakazi wenye kujikana nafsi kufuata nyayo Zake, kutembea na kufanya kazi kwa ajili yake, kuuinua msalaba, na kufuata anakoongoza njia. {8T 28.3}

Wengi wanaridhika kwa urahisi na kumpa Bwana matendo hafifu ya huduma. Ukristo wao ni dhaifu. Kristo alijitoa Mwenyewe kwa ajili ya wenye dhambi. Ni kwa shauku iliyoje kwa ajili ya wokovu wa roho tunapaswa kujazwa tunapowaona wanadamu wakiangamia katika dhambi! Nafsi hizi zimenunuliwa kwa bei kubwa mno. Kifo cha Mwana wa Mungu juu ya msalaba wa Kalvari ndicho kipimo cha thamani yao. Kila siku wanaamua iwapo watapata uzima wa milele au mauti ya milele. Na bado wanaume na wanawake wanaokiri kumtumikia Bwana wanaridhika kujaza muda na usikivu wao kwa mambo yenye umuhimu mdogo. Wanaridhika na kutofautiana mtu na mwenzake. Kama wangelijitoa wakfu kwa kazi ya Bwana, wasingekuwa wanapambana na kushindana kama familia ya watoto watukutu. Kila mkono ungehusishwa katika huduma. Kila mtu angekuwa amesimama katika kituo chake cha kazi, akifanya kazi kwa moyo na roho kama mmisionari wa msalaba wa Kristo.

Roho ya Mkombozi ingekaa ndani ya mioyo ya watenda kazi, na kazi za haki zingetekelezwa. Wafanyakazi katika huduma yao wangebeba pamoja nao sala na huruma ya kanisa lililoamshwa. Wangepokea maelekezo yao kutoka kwa Kristo na wasingelipata muda wa ugomvi na mashindano. {8T 28.4}

Ujumbe ungetoka katika midomo iliyoguswa na makaa yaliyo hai kutoka katika madhabahu ya Mungu. Maneno ya dhati, yaliyotakaswa yangelinenwa. Maombi ya unyenyekevu, ya moyo uliovunjika kwa ajili ya watu wengine yangepanda kwenda mbinguni. Kwa mkono mmoja wafanyakazi wangemshikilia Kristo, na kwa mkono mwingine wangewashika wenye dhambi na kuwavuta kuja kwa Mwokozi. {8T 29.1}

“Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.” Mathayo 24:14. {8T 29.2}

"Uwaokoe wanaochukuliwa ili wauawe; Nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe. Ukisema, Sisi hatukujua hayo; Je! Yeye aipimaye mioyo siye afahamuye? Naye ailindaye nafsi yako siye ajuaye? Je! Hatamlipa kila mtu sawasawa na kazi yake? 13”

Mithali 24:11, 12. (30) {8T 29.3}

## SURA YA 5
## KAZI NYUMBANI NA UGHAIBUNI

St. Helena, California, Agosti 7, 1902.

"Hamsemi ninyi, Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, Mimi nawaambieni, Inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno. Naye avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda kwa uzima wa milele, ili yeye apandaye na yeye avunaye wapate kufurahi pamoja. Kwa maana hapo Neno hilo huwa kweli, Mmoja hupanda akavuna mwingine." Yohana 4: 35-37. {8T 30.1}

Baada ya kupanda mbegu, mkulima analazimika kungojea kwa miezi kadhaa ili ichipuke na kukua na kuwa nafaka tayari kwa kuvunwa. Lakini katika kuipanda anatiwa moyo na matarajio ya matunda katika siku zijazo. Kazi yake inafanywa kuwa nyepesi na tumaini la matokeo mema katika wakati wa kuvuna. {8T 30.2}

Sivyo ilivyo zile mbegu za Ukweli zilizopandwa na Kristo akilini mwa mwanamke Msamaria wakati wa mazungumzo Yake pamoja naye pale kisimani. Mavuno ya kupanda kwake mbegu hayakuwa mbali, bali papo hapo. Hata kabla ya Maneno Yake kutamkwa, mbegu iliyopandwa kwa jinsi hiyo ilichipuka na kuzaa matunda, ikiamsha ufahamu wake, na kumwezesha kujua kwamba alikuwa akiongea na Bwana Yesu Kristo. Aliruhusu miale ya nuru ya Bwana iangaze ndani ya moyo wake. Akisahau mtungi wake wa maji, alifanya haraka kwenda kuwajulisha ndugu zake Wasamaria habari njema. "Njoni," alisema, "mtazame Mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Je! Haimkini huyu kuwa Ndiye Kristo? " Aya ya 29. Nao wakatoka mara moja kuja kumwona. Hapo ndipo alipofananisha roho za Wasamaria hawa na shamba la nafaka. "Inueni macho yenu," aliwaambia wanafunzi Wake, myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno." {8T 30.3}

"Basi wale Wasamaria walipomwendea, walimsihi akae kwao; naye akakaa huko

siku mbili." Na hizi zilikuwa siku zenye shughuli nyingi kiasi gani! Je, kumbukumbu ya matokeo ikoje? "Watu wengi zaidi wakaamini kwa sababu ya Neno Lake. 4.42 Wakamwambia yule mwanamke, Sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya maneno yako tu; maana sisi tumesikia wenyewe, tena twajua ya kuwa hakika huyu Ndiye Mwokozi wa ulimwengu." Aya ya 40-42. {8T 30.4}

Kristo, kwa kufungua akilini mwa Wasamaria Neno la uzima, alipanda mbegu nyingi za Ukweli na kuwaonesha watu jinsi ambavyo wao, pia, wangeweza kupanda mbegu za Ukweli katika akili za wengine. Je! Ni wema wa kiasi gani ungeweza kutimizwa ikiwa wote wanaoujua Ukweli wangefanya kazi kwa ajili ya wenye dhambi, kwa wale ambao wanahitaji sana kujua na kuelewa Ukweli wa Biblia na ambao watauitikia mara moja kama Wasamaria walivyoitikia Maneno ya Kristo! Je! Ni kwa udogo kiasi gani, sisi tunaingia katika utume wa Mungu wa kuwaonea watu huruma juu ya suala lile ambalo linapaswa kuwa kifungo chenye nguvu kabisa cha muungano kati yetu na Yeye Mwenyezi Mungu-huruma kwa roho zilizopotoka, zenye hatia, zinazoteseka, zilizokufa katika makosa na dhambi! Ikiwa watu wangeshiriki huruma za Kristo, daima wangekuwa na sikitiko moyoni mara kwa mara juu ya hali ya maeneo mengi maskini, yaliyokosa kabisa watendakazi. {8T 31.1}

Kazi katika maeneo ya kigeni inapaswa kuendelezwa kwa bidii na kwa akili. Na kazi katika kivuli/eneo la nyumbani haifai kupuuzwa kwa namna yoyote. Hebu maeneo yale yaliyo karibu na nyumbani kwetu, kama vile miji mikubwa katika nchi yetu, yasipitwe na kupuuzwa. Maeneo haya ni muhimu kabisa kama eneo lolote lile la kigeni. {8T 31.2}

Ujumbe wa huruma wa Mungu wenye kutia moyo unapaswa kutangazwa katika miji ya Marekani. Wanaume na wanawake wanaoishi katika miji hii wanajisokota zaidi na zaidi katika mahusiano yao ya biashara. Wanashughulika na ujenzi wa majengo ambayo minara yake inafika juu angani kama wendawazimu. Akili zao zimejazwa na mipango yenye njama na matamanio ya  makuu. Mungu anamwambia kila mmoja wa watumishi Wake wanaohudumu: Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu Wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao, Isaya 58: 1. {8T 31.3}

Hebu na tumshukuru Bwana kwamba kuna watendakazi wachache wanaofanya kila liwezekanalo kuinua kumbukizi kwa ajili ya Mungu katika miji yetu iliyopuuzwa. Hebu tukumbuke kuwa ni jukumu letu kuwatia moyo wafanyakazi hawa. Mungu huchukizwa wakati ambapo watu hawawathamini, hawawatii moyo na kuwaunga watendakazi wetu waaminifu katika miji yetu mikubwa katika nchi yetu wenyewe hapa. Kazi katika eneo/fildi ya nyumbani ni tatizo kuu sasa hivi. Wakati wa sasa ndio

fursa nzuri mno tutakayokuwa nayo ya kufanya kazi katika maeneo haya. Kitambo kidogo hali itakuwa ngumu zaidi. {8T 32.1}

Yesu aliulilia Yerusalemu kwa sababu ya hatia na ukaidi wa watu Wake wateule. Yeye Analia pia kuhusiana na ugumu wa mioyo ya wale ambao, wakidai kuwa wafanyakazi pamoja naye, wanaridhika kwa kutokufanya chochote. Je! Wale ambao wanapaswa kuthamini thamani ya roho za watu wanaobeba, pamoja na Kristo, mzigo mzito na huzuni ya daima, iliyochanganyika na machozi, kwa ajili ya miji ya dunia? Uharibifu wa miji hii, ambayo karibu kabisa imejitoa kwa ibada ya sanamu, unakaribia. Katika siku ile kuu ya kutoa hesabu ya mwisho ni jibu gani linaweza kutolewa kwa kupuuza kuingia katika miji hii sasa? {8T 32.2}

Huku tukiendelea na kazi ndani ya Marekani, Bwana na atusaidie kuzipa nchi zingine umuhimu wanaopaswa kuwa nao, ili watendakazi katika maeneo haya wasifungwe, hata wasiweze kuacha kumbukizi za Mungu katika maeneo mengi. Hebu tusiruhusu manufaa na neema nyingi sana kumezwa zote katika nchi hii. Hebu tusiendelee kupuuza wajibu wetu kwa mamilioni ya watu wanaoishi katika nchi zingine. Hebu tupate uelewa mzuri wa hali hii na tufidie wakati uliopita. {8T 32.3}

Ndugu na dada zangu mlioko Marekani, inaweza kuwa kwamba kwa kuinua macho yenu ili mpate kuona mashamba ya mbali yakiwa meupe tayari kwa mavuno, mtapokea mioyoni mwenu wenyewe neema tele ya Mungu. Ninyi ambao kwa sababu ya kutokuamini kwenu mmekuwa maskini kiroho, kupitia kwa kazi ya mtu binafsi, mtakuwa matajiri katika matendo mema. Hamtazishindisha njaa tena roho zenu katikati ya chakula tele, bali mtajitwalia vitu vile vizuri ambavyo Mungu amewawekea akiba. Pale unapoanza kutambua jinsi ambavyo wafanyakazi katika maeneo ya kigeni wanapaswa kuendeleza kazi wakiwa na ukata wa kipato, utafanya kila uwezalo ili kusaidia, na roho zenu zitaanza kupata uhai, hamu yenu ya kiroho itapata afya, na akili zenu zitahuishwa na kuburudishwa na Neno la Mungu, ambalo ni jani kutoka katika mti wa uzima ulio kwa ajili ya uponyaji wa mataifa. {8T 32.4}

Kwa kujibu swali la Bwana, "Nimtume nani?" Isaya alijibu, "Mimi hapa; nitume mimi." Isaya 6: 8. Wewe, ndugu yangu, dada yangu, inawezekana usiweze kuingia katika shamba la Bwana la mizabibu mwenyewe, lakini unaweza kutoa mali ya kuwapeleka wengine. Hivyo mtakuwa mnaweka pesa zenu kwa wabadilishanaji/wachuuzi; na Bwana atakapokuja, mtaweza kumrudishia Yeye iliyo yake pamoja na riba. Mali zenu zinaweza kutumika katika kuwapeleka na kuwategemeza wajumbe wa Mungu, ambao kwa sauti na kwa mvuto watatoa ujumbe: "Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito Yake." Mathayo 3:3. Mipango inafanywa kwa ajili ya maendeleo ya kusudi hilo, na sasa ndio wakati wako wa kufanya kazi. {8T 33.1}

Ikiwa mtafanya kazi kwa kujikana nafsi, mkifanya kila mnachoweza ili kusaidia maendeleo ya kusudi hili katika maeneo mapya, Bwana atawasaidia na

kuwaimarisha na kuwabariki. Weka tumaini lako katika uhakika wa uwapo Wake, ambao unakuhimili, na ambao ni nuru na uzima. Tenda yote kwa kwa ajili ya upendo kwa Yesu na kwa ajili ya roho za thamani ambazo amewafia. Fanya kazi ukiwa na kusudi safi, lililopambwa na mbingu ili kumtukuza Mungu. Bwana anaona na kufahamu, Naye atakutumia, licha ya udhaifu wako, ikiwa tu utatoa talanta yako kama zawadi iliyowekwa wakfu kwa ajili ya huduma Yake; kwa kuwa katika huduma hai, isiyo na ubinafsi, wale walio dhaifu wanapata nguvu na hufurahia sifa Yake ya thamani kuu. Furaha ya Bwana ni ishara ya nguvu. Ikiwa wewe ni mwaminifu, basi amani ile ipitayo ufahamu wote itakuwa ni thawabu yako katika maisha haya, na katika maisha ya baadaye utaingia katika raha ya Bwana wako. {8T 33.2}

**Januari 23, 1903**.

Inabidi niandike kitu kuhusiana na jinsi ambavyo miji yetu huko Marekani imepitwa na kupuuzwa, miji ile ambayo Ukweli haujatangazwa ndani yake. Ujumbe lazima upelekwe kwa maelfu ya wageni wanaoishi ndani ya miji hii katika eneo la nyumbani. {8T 34.1}

Siwezi kuelewa ni kwa nini watu wetu wana mzigo mdogo kiasi hicho wa kuchukua kazi ile ambayo Bwana ameiweka mbele yangu kwa miaka mingi, kazi ya kutoa ujumbe wa Ukweli wa sasa katika Majimbo ya Kusini. Wachache wamejisikia kuwa juu yao kulikuwa na jukumu la kushikilia kazi hii. Watu wetu wameshindwa kuingia katika eneo jipya na kufanya kazi katika miji ya Kusini. Mara kwa mara Bwana amewasilisha mahitaji ya eneo hili, bila matokeo yoyote maalumu. Wakati mwingine nimehisi kana kwamba siwezi tena kubeba mzigo wa kazi hii. Nilifikiri kwamba, ikiwa watu wangeendelea kuipuuza kazi hii, ningeacha mambo yafuate upepo na kwenda na kuomba kwamba Bwana awe na rehema juu ya wajinga wasiojua injili na wale ambao wako nje ya njia. {8T 34.2}

Lakini Bwana ana majadiliano na wachungaji wetu na washiriki, na lazima niongee, nikiweka juu yao mzigo wa kazi ya Kusini na ya miji ya nchi yetu. Ni nani anahisi kuwa na mzigo mzito kuona ujumbe ule uliotangazwa huko Greater New York na katika miji mingine mingi bado haujafanyiwa kazi hadi sasa? Si fedha zote ambazo zinaweza kukusanywa zinapaswa kutumwa kutoka Marekani kwenda katika nchi za mbali, wakati ambapo katika uwanja wa nyumbani kuna fursa za kufaa kama hizi za kutoa Ukweli kwa mamilioni ambao hawajawahi kuusikia. Miongoni mwa mamilioni haya kuna wawakilishi wa mataifa mengi, ambao wengi wao wako tayari kuupokea ujumbe. Kuna mengi bado yanapaswa kufanywa karibu na vivuli vya nyumbani mwetu - katika miji ya California, New York, na majimbo mengine mengi. {8T 34.3}

Mungu anawaambia watu Wake: "Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia." Isaya 60: 1. Kwa nini, basi, wanahisi mzigo mdogo kiasi hicho kusimamisha bendera ya Ukweli katika maeneo mapya? Kwa nini hawatii Neno hili: "Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia

mwivi, wala nondo haharibu?" Luka 12:33. Kwa nini hawarudishi kwa Bwana kilicho Chake Mwenyewe, ili apate kukiwekeza kwenye biashara ya mbinguni? Kwa nini hakuna wito wa dhati na bidii zaidi kwa ajili ya watu wanaojitolea kuingia kwenye shamba la mavuno yanayokuwa meupe? Isipokuwa zaidi imefanywa kuliko ambavyo imefanywa katika miji ya Marekani, wachungaji pamoja na washiriki watakuwa na hesabu kubwa ya kupatana na Yule ambaye amempangia kila mtu kazi yake. {8T 35.1}

Tunarudia maombi: "Ufalme Wako uje, Mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Mathayo 6: 10 Je! Tunafanya sehemu yetu katika kuyajibu maombi haya? Tunakiri kuamini kwamba agizo ambalo Kristo aliwapa wanafunzi Wake limetolewa kwetu pia. Je! Sisi Tunalitimiza? Mungu na asamehe kutokujali kwetu kunakotisha katika kutokufanya kazi ambayo hadi sasa bado hatujaigusa na ncha za vidole vyetu. Je! Kazi hii itafanywa lini? Inafanya moyo wangu kuugua na kupata uchungu kuona upofu kama huo kwa upande wa watu wa Mungu. {8T 35.2}

Wapo maelfu katika Marekani wanaoangamia kwa ujinga, kutokujua na dhambi. Na kwa kuangalia mbali katika eneo fulani la mbali, wale ambao wanaujua Ukweli huyapita bila kujali maeneo haya yenye uhitaji yaliyo karibu nao. Kristo anasema: "Leo nenda kafanye kazi katika shamba la mizabibu." "Hamsemi ninyi, Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, Mimi nawaambieni, Inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno." Mathayo 21:28; Yohana 4:35. {8T 35.3}

Amkeni, amkeni, ndugu na dada zangu, na muingie katika yale maeneo huko Marekani ambayo hayajawahi kufanyiwa kazi. Baada ya kutoa kitu kwa ajili ya maeneo ya ugenini, usifikiri kuwa wajibu wako umekwisha. Kuna kazi ya kufanywa katika maeneo ya ugenini, lakini kuna kazi ya kufanywa ndani ya Marekani ambayo pia ni muhimu sana kama huko nchi za nje. Katika miji ya Marekani kuna watu karibu wa kila lugha. Hawa wanahitaji nuru ambayo Mungu ameitoa kwa kanisa Lake. {8T 36.1}

Bwana anaishi na kutawala. Punde atainuka katika utukufu na kuitikisa sana dunia. Ujumbe wa pekee sasa unapaswa kutolewa, ujumbe ambao utaipenya giza la kiroho na kusadikisha na kuongoa roho za watu. "Jiponye nafsi yako," ni wito unaopaswa kutolewa kwa wale wanaokaa katika dhambi. Lazima sasa tuwe wenye wanyofu na wenye bidii sana. Hatuna muda hata kidogo wa kutumia katika ukosoaji, shutuma na lawama. Hebu wale ambao wamefanya haya huko nyuma waanguke magotini mwao kwa maombi, na hebu wajihadhari jinsi wanavyoweka maneno na mipango yao mahali pa maneno na mipango ya Mungu. {8T 36.2}

Hatuna muda wa kufikiri sana juu ya mambo ambayo hayana umuhimu wowote. Muda wetu unapaswa kutolewa kwa ajili ya kutangaza ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu wenye hatia. Watu wanahitajika ambao wanasonga mbele chini ya msukumo wa Roho wa Mungu. Mahubiri yatakayohubiriwa na baadhi ya wachungaji wetu itabidi yawe ni yenye nguvu zaidi kuliko ilivyo sasa, la sivyo, watu wengi waliorudi nyuma watabeba ujumbe usio na nguvu kwa woga, na usio na

maana, ambao huwabembeleza watu kulala. Kila hotuba inabidi itolewe katika dhana ya hukumu mbaya ambazo zitaushukia ulimwengu hivi karibuni. Ujumbe wa Ukweli unapaswa kutangazwa na midomo iliyoguswa kwa kaa la moto kutoka kwenye madhabau ya kiungu. {8T 36.3}

Moyo wangu unajawa na uchungu pale ninapofikiri juu ya ujumbe usio na nguvu, unaotolewa kwa woga, na unaosambazwa na baadhi ya wachungaji wetu, wakati wanao ujumbe unaohusu uzima na mauti wa kuutoa. Wachungaji wamelala; washiriki walei wamelala; na ulimwengu unaangamia katika dhambi. Mungu na awasaidie watu Wake kuamka na kutembea na kufanya kazi kama wanaume na wanawake walio katika mipaka ya ulimwengu wa milele. Hivi karibuni mshangao wa kuogofya utakuja juu ya wakazi wa ulimwengu. Ghafla, kwa uweza na utukufu mwingi, Kristo atakuja. Ndipo wakati huo hakutakuwa na muda wa kujiandaa kukutana Naye. Sasa ndio wakati wetu wa kuutoa ujumbe wa onyo. {8T 37.1}

Sisi ni mawakili, tuliokabidhiwa na Bwana wetu ambaye hayupo, utunzaji wa nyumba Yake na masilahi Yake, ambayo alikuja ulimwenguni humu kuitumikia. Amerudi mbinguni, akituacha kuwa wasimamizi, na anatarajia kuwa tutakesha na kungoja kwa ajili ya kutokea Kwake. Hebu na tuwe waaminifu kwa dhamana yetu, asije ghafla na kutukuta tumesinzia. (38) {8T 37.2}

## SURA YA 6
## KAZI HUKO ULAYA

St. Helena, California, Desemba 7, 1902.

Kwa Ndugu Zangu mlioko Ulaya--

Nina maneno ya kusema nanyi. Muda umefika wa mengi kutimizwa huko Ulaya. Kazi kubwa, kama ambayo imefanyika Marekani, inaweza kufanywa huko Ulaya. Hebu vituo vya Sanitarium vya afya na tiba rahisi vianzishwe, hebu migahawa yenye kuleta Usafi na Afya ianzishwe. Hebu nuru ya Ukweli wa sasa uangaze kutoka katika mitambo ya uchapaji. Hebu kazi ya kutafsiri vitabu vyetu isonge mbele. Nimeoneshwa kuwa katika nchi za Ulaya, taa zitawashwa katika maeneo mengi. {8T 38.1}

Kuna maeneo mengi ambapo kazi ya Bwana haijaonekana inavyostahili. Msaada

unahitajika nchini Italia, Ufaransa, Scotland, na katika nchi nyingine nyingi. Kazi kubwa inapaswa kufanywa katika maeneo haya. Wafanyakazi wanahitajika. Kuna vipawa miongoni mwa watu wa Mungu huko Ulaya, na Bwana anatamani vipawa hivi vitumike katika kuanzisha kote katika Uingereza na bara hili, vituo ambavyo kutoka humo nuru ya Ukweli Wake inaweza kuangaza. {8T 38.2}

Kuna kazi ya kufanywa huko Scandinavia. Mungu Yuko tayari kufanya kazi kupitia kwa waumini wa Scandinavia kama vile kwa waumini wa Marekani. {8T 38.3}

Ndugu zangu, fungamaneni na Bwana Mungu wa majeshi. Mruhusu awe hofu yako, Naye umruhusu awe utisho wako. Wakati umefika wa kazi Yake kupanuliwa. Nyakati za taabu ziko mbele yetu, lakini ikiwa tutasimama pamoja katika ushirika wa Kikristo, bila kuwa na mtu anayepambana kwa ajili ya kupata ukuu, Mungu atafanya kazi kwa nguvu kwa ajili yetu. {8T 38.4}

Hebu tuwe na matumaini na ujasiri. Kukata tamaa katika utumishi wa Mungu ni dhambi na kukosa busara. Yeye Anajua kila hitaji letu. Yeye Ana nguvu zote. Yeye Anaweza kuwapa watumishi wake kiasi cha ufanisi kulingana na mahitaji yao. Upendo Wake Usio na huruma Zake zisizo na kikomo hazichoshwi kamwe. Kwa ukuu wa uweza Yeye Anaunganisha pamoja upole na uangalizi wa mchungaji mwema. Hatuna haja ya kuwa na hofu kwamba hatatimiza ahadi Zake. Yeye ni Ukweli wa milele. Kamwe hatabadilisha agano ambalo ameliweka na wale wampendao. Ahadi Zake kwa kanisa Lake zinasimama imara milele. Yeye Atalifanya Kanisa Lake kuwa bora milele, furaha ya vizazi vingi. {8T 38.5}

Jifunze sura ya arubaini na moja ya Isaya (41), na ujitahidi kuielewa katika umuhimu wake wote. Mungu anatangaza: " Nitafunua vijito vya maji juu ya vilima, na chemchemi katikati ya mabonde; nitageuza jangwa kuwa ziwa la maji, na mahali pakavu kuwa vijito vya maji. Nitapanda katika jangwa mwerezi, mshita, mhadasi, na mbono; nitatia katika nyika mberoshi, mtidhari, na mteashuri pamoja; ili waone, na kujua, wakafikiri, na kufahamu pamoja, ya kuwa mkono wa Bwana ndio uliofanya jambo hilo. Mtakatifu wa Israeli Ndiye aliyeliumba." Isaya 41:18-20. {8T 39.1}

Yeye aliyemchagua Kristo amejiunga na uwezo ambao hakuna safu ya hekima ya kibinadamu au nguvu inaweza kuupindua. "Usiogope, kwa maana Mimi ni pamoja nawe," anatangaza; " usifadhaike, kwa maana Mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu" "Kwa maana Mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; Mimi nitakusaidia." Aya ya 10, 13. {8T 39.2}

"Mtanifananisha na nani, basi, nipate kuwa sawa Naye? Asema Yeye aliye Mtakatifu.

Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi; aletaye nje jeshi lao kwa hesabu; Yeye aziita zote kwa majina; kwa ukuu wa uweza Wake, na kwa kuwa Yeye ni hodari kwa nguvu Zake; hapana moja isiyokuwapo mahali Pake. Mbona unasema, Ee Yakobo, mbona unanena, Ee Israeli, Njia yangu imefichwa, Bwana asiione, na hukumu yangu imempita Mungu wangu asiiangalie? Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; akili Zake hazichunguziki. Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo. Hata vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka; bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia." Isaya 40: 25-31. {8T 39.3}

Nuru ya Ukweli inapaswa kuangaza hadi miisho ya dunia. Nuru kubwa na kubwa zaidi inaangaza kwa uangavu wa kimbingu kutoka katika uso wa Mkombozi juu ya wawakilishi Wake, ili ipate kutawanywa kupita katika giza la ulimwengu wa kishenzi/kikafiri. Kama watenda kazi pamoja Naye, hebu na tuombe kwa ajili ya utakaso wa Roho Wake, ili tuweze kuangaza zaidi na zaidi. {8T 40.1}

Nuru ya Ukweli wa sasa wakati huu inaangaza katika mabaraza ya wafalme. Usikivu wa viongozi wa serikali unaelekezwa kwa Biblia, - kitabu cha sheria cha mataifa, - nao wanalinganisha sheria zao za kitaifa na sheria Zake. Kama wawakilishi wa Kristo, sisi hatuna muda wa kupoteza. Jitihada zetu hazipaswi kuwekewa mipaka katika maeneo machache ambapo nuru imekuwa nyingi kiasi kwamba haifurahiwi. Ujumbe wa injili unapaswa kutangazwa kwa mataifa yote na kabila na lugha na jamaa. {8T 40.2}

## SURA YA 7
## MANDHARI YA VITA

Katika maono niliona majeshi mawili yakiwa katika pambano la kutisha. Jeshi moja liliongozwa na bendera zenye nembo za ulimwengu; lingine liliongozwa na bendera yenye damu ya Mfalme Imanueli. Bendera moja baada ya nyingine iliachwa kuburura mavumbini wakati kundi baada ya kundi kutoka katika jeshi la Bwana lilijiunga na adui na kabila baada ya kabila kutoka safu ya adui liliungana na watu wa Mungu wanaozitunza amri. Malaika anayeruka katikati ya mbingu anaweka bendera ya Imanueli mikononi mwa watu wengi, wakati jemadari hodari alitangaza kwa sauti kuu: "Njooni. Hebu wale ambao ni waaminifu kwa amri za Mungu na ushuhuda wa Kristo sasa wachukue msimamo wao. Tokeni kati yao, mkatengwe, msiguse kitu

kilicho najisi, Nami nitawakaribisha, Nami nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa wana na binti Zangu. Hebu wote wale Wanaopenda watokee ili kumsaidia Bwana, kumsaidia Bwana dhidi ya shujaa. {8T 41.1}

Vita viliendelea. Ushindi ulibadilishana kutoka upande huu kwenda upande ule. Sasa askari wa msalaba walirudi nyuma, "kama vile afapo mtu mgonjwa." Isaya 10:18. Lakini kilichoonekana kama kukimbia kwao na kurudi nyuma kulikuwa ni kwa ajili ya kupata nafasi nzuri zaidi. Kelele za shangwe zilisikika. Wimbo wa kumsifu Mungu ulipanda juu, na sauti za malaika ziliungana katika wimbo huo, pale askari wa Kristo waliposimamisha bendera Yake kwenye kuta za ngome ambazo hadi kufikia wakati huo zilikuwa zikishikiliwa na adui. Jemadari wa wokovu wetu alikuwa akiweka mpango wa vita na kutuma msaada kwa askari Wake. Uweza Wake ulioneshwa kwa nguvu, ukiwatia moyo kuendeleza vita hadi malangoni. Yeye Aliwafundisha mambo ya ajabu kuhusu haki kadiri alivyowaongoza hatua kwa hatua, wakishinda na kushinda. {8T 41.2}

Hatimaye ushindi ulipatikana. Jeshi lililofuata bendera iliyo na maandishi, "Amri za Mungu, na imani ya Yesu," lilikuwa na ushindi mkuu. Askari wa Kristo walikuwa karibu na malango ya jiji, na kwa furaha mji ulimpokea Mfalme Wake. Ufalme wa amani na furaha na haki ya milele ulianzishwa. {8T 41.3}

Sasa kanisa liko katika mapambano. Sasa tunakabiliwa na ulimwengu ulio katika giza la usiku wa manane, ambao karibu umejitoa kabisa katika ibada ya sanamu. Lakini siku inakuja ambapo vita vitakuwa vimepiganwa, ushindi umepatikana. Mapenzi ya Mungu yanapaswa kutimizwa hapa duniani, kama huko mbinguni. Ndipo mataifa hayatakuwa na sheria nyingine yoyote isipokuwa sheria ya mbinguni. Wote watakuwa familia yenye furaha, umoja, wakiwa wamevaa mavazi ya sifa na shukrani - vazi la haki ya Kristo. Asili yote, katika uzuri wake wa kupita kiasi, daima itatoa kwa Mungu zawadi ya sifa na ibada. Ulimwengu utasafishwa na nuru ya mbinguni. Miaka itasonga mbele kwa furaha. Nuru ya mwezi itakuwa kama nuru ya jua, na nuru ya jua itakuwa kubwa mara saba kuliko ilivyo sasa. Katika mandhari hii nyota za asubuhi wataimba pamoja, na wana wa Mungu watapiga kelele kwa furaha, wakati ambapo Mungu pamoja na Kristo wataungana katika kutangaza: "Dhambi haitakuwapo tena, wala mauti hayatakuwapo tena." {8T 42.1}

Hii ndio mandhari ambayo iliyowasilishwa kwangu. Lakini kanisa ni lazima nalo litapambana na maadui wanaoonekana na wasioonekana. Mawakala wa Shetani katika umbo la wanadamu wako uwanjani. Watu wameungana ili kumpinga Bwana wa majeshi. Mashirikisho haya yataendelea hadi Kristo atakapoondoka katika mahali Pake pa maombi kwa ajili ya watu Wake mbele ya kiti cha rehema na kuvaa mavazi ya kisasi. Mawakala wa kishetani wako katika kila mji, wanashughulika

kupanga na kuwaandaa katika makundi wale ambao wako kinyume na sheria ya Mungu. Walioweka nadhiri kuwa watakatifu na wale wanaokiri kutokuamini wanachukua upande wao katika makundi haya. Huu sio wakati wa watu wa Mungu kuwa wanyonge. Hatutathubutu kuchukuta tahadhari, na kuweka ulinzi hata kwa wakati mmoja. {8T 42.2}

“Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu Zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama;  bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga Kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu.” Waefeso 6: 10-17. {8T 42.3}

"Na hii ndiyo dua yangu, kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote; mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo; hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu." Wafilipi 1: 9-11. {8T 43.1}

"Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, … kama mnasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili; wala hamwaogopi adui zenu, katika neno lo lote; kwao hao ni ishara mathubuti ya kupotea, bali kwenu ninyi ni ishara ya wokovu, huo utokao kwa Mungu. Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili Yake." Aya ya 27-29. {8T 43.2}

Katika siku hizi za mwisho maono yanadhihirishwa utukufu wa baadaye, matukio yanayooneshwa na mkono wa Mungu, na haya yanapaswa kuwa ya kupendeza kwa kanisa Lake. Ni nini kilichomhimili Mwana wa Mungu katika usaliti na jaribu Lake? Aliiona taabu ya roho Yake Naye akaridhika. Alitazama kwa kitambo kidogo anga la umilele na kuona furaha ya wale ambao kupitia kwa unyenyekevu Wake wangepokea msamaha na uzima wa milele. Yeye Alijeruhiwa kwa makosa yao, alichubuliwa kwa maovu yao. Adhabu ya amani yao ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa kwake walipona. Sikio lake lilisikia kelele za waliokombolewa. Aliwasikia waliokombolewa wakiimba wimbo wa Musa na Mwana-Kondoo. {8T 43.3}

Lazima tuwe na maono ya siku za usoni na heri ya mbinguni. Simama kwenye lango la umilele, na hapa usikie ukaribisho wa neema unaotolewa kwa wale ambao katika

maisha haya wameshirikiana na Kristo, wakiona kuwa ni fursa na heshima kuteseka kwa ajili Yake. Wakiungana na malaika, walitupa taji zao miguuni pa Mkombozi, wakisema: "Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka. … Heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na Yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele." Ufunuo 5:12, 13. {8T 44.1}

Hapo waliokombolewa huwasalimu wale ambao waliwaelekeza kwa Mwokozi aliyeinuliwa. Wanaungana katika kumsifu Yeye aliyekufa ili wanadamu wapate maisha yanayolingana na maisha ya Mungu (milele). Pambano limekwisha. Dhiki zote na vita vimekwisha. Nyimbo za ushindi zinaijaza mbingu yote waliokombolewa wanaposimama kuuzunguka kiti cha enzi cha Mungu. Wote wanauinua wimbo wa furaha kwa vinubi vyao: "Anastahili, anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, Naye anaishi tena, mshindi." {8T 44.2}

"Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo, Ufunuo 7: 9, 10. {8T 44.3}

"Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu Lake, na Yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, Naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao. "Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." Aya ya 14-17; 21: 4. {8T 44.4}

Je! utaupata uvuvio wa maono haya? Je! utaruhusu akili yako kufikiri sana juu ya maono hayo? Je! hutaongolewa kweli kweli, na kisha usonge mbele kufanya kazi kwa roho tofauti kabisa na roho ambayo kwayo umefanya kazi katika siku zilizopita, ukimwondoa adui kutoka mahali pake, ukivunja kila kizuizi kipingacho maendeleo ya injili, ukiijaza mioyo na nuru na amani na furaha ya Bwana? Je! roho duni ya kutafuta makosa na manung'uniko haitazikwa, na kamwe isipate ufufuo? Je! uvumba wa sifa na shukrani hautapanda kutoka katika mioyo iliyosafishwa na kutakaswa na kutukuzwa na kuwapo Kwake Kristo? Je! kwa imani hatuwashika wenye dhambi na kuwaleta msalabani? {8T 45.1}

Ni akina nani sasa watakaojitoa kwa ajili ya utumishi wa Bwana? Ni akina nani sasa watakaotoa kiapo/ahadi ya kutokushirikiana na ulimwengu, bali kutoka katika ulimwengu na kujitenga, wakikataa kuichafua roho na mipango na mazoea ya kidunia ambayo yamekuwa yakiliweka kanisa chini ya uwezo wa adui? {8T 45.2}

Tuko katika ulimwengu huu kwa ajili ya kuinua msalaba wa kujikana nafsi. Tunapouinua msalaba huu tutagundua kuwa unatuinua sisi. Hebu kila Mkristo asimame mahali pake, akipata msukumo na uvuvio wa kazi ambayo Kristo alifanya kwa ajili ya roho za watu alipokuwa katika ulimwengu huu. Tunahitaji shauku ya shujaa wa Kikristo, ambaye anaweza kustahamili kumwona Yeye asiyeonekana. Imani yetu inapaswa kufufuliwa. Askari wa msalaba wanapaswa kuweka mvuto chanya kwa ajili ya wema. "Mtu asiye pamoja Nami Yu kinyume changu; na mtu asiyekusanya pamoja Mami hutapanya." Mathayo 12:30. Kutokujali katika maisha ya Mkristo ni kumkana kwa wazi Mwokozi. {8T 45.3}

Je! hatupaswi kuona katika ulimwengu leo Wakristo ambao katika sifa zote za kazi zao wanastahili jina wanalolibeba? Ambao wanatamani kufanya matendo yanayomstahili askari shujaa wa msalaba? Tunaishi karibu na mwisho wa pambano kuu, wakati roho nyingi zinapaswa kuokolewa kutoka katika utumwa wa dhambi. Tunaishi katika wakati ambapo kwa wafuasi wa Kristo ahadi ya pekee ni: "Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28: 16-20 Yeye aliyeamuru nuru iangaze kutoka gizani, Yeye ambaye ametuita kutoka gizani na kuingia katika nuru Yake ya ajabu, anatuamuru tuangaze nuru yetu mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yetu mema na kumtukuza Baba yetu aliye mbinguni. Nuru imetolewa kwa watu wa Mungu kwa kipimo kikubwa kiasi kwamba Kristo anathibitishwa kuwa na haki ya kuwaambia kwamba wao wanapaswa kuwa nuru ya ulimwengu. {8T 45.4}

Kwa matabibu na wachungaji wetu ninatuma ujumbe huu: Shikilia kazi ya Bwana kana kwamba umeamini Ukweli huu kwa wakati huu. Watendakati wa umishenari wa tiba/matibabu na watendakazi katika huduma ya injili wanapaswa kufungwa pamoja kwa vifungo visivyoweza kuvunjika. Kazi yao inapaswa kufanywa kwa namna ya kupendeza na ya nguvu. Katika makanisa yetu yote kunapaswa kuwapo na uongofu mpya na kujitoa upya wakfu kwa ajili ya huduma. Je! Hatupaswi, katika kazi yetu katika siku za usoni na katika mikusanyiko ambayo tunafanya, kuwa wa umoja? Je! Hatupaswi kupigana mieleka sana kwa maombi kwa Mungu, tukimwomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu kuingia katika kila moyo? Uwapo wa Kristo, unadhihirika miongoni mwetu, ungetibu ukoma wa kutokuamini ambao umefanya huduma yetu kuwa dhaifu na isiyofaa kiasi hicho. Tunahitaji pumzi ya uhai wa Mwenyezi Mungu kupulizwa ndani yetu. Tunapaswa kuwa mifereji ambayo ndani

yake Bwana anaweza kutuma nuru na neema kwa ulimwengu. Wale waliorudi nyuma inabidi warejeshwe. Tunapaswa kuweka mbali dhambi zetu, kwa kukiri na kutubu tukinyenyekesha mioyo yetu yenye kiburi mbele za Mungu. Mafuriko ya nguvu za kiroho yanapaswa kumiminwa juu ya wale walio tayari kuyapokea. {8T 46.1}

Iwapo tu tungetambua jinsi Yesu alivyofanya kazi kwa dhati na bidii katika kupanda mbegu ya injili ulimwenguni, sisi, tunaoishi mwishoni kabisa mwa hukumu ya upelelezi, na kufungwa kwa mlango wa rehema, tungefanya kazi bila kuchoka kutoa mkate wa uzima kwa roho zinazoangamia. Kwa nini sisi tuna ubaridi na tu watu wazembe wasiojali? Kwa nini mioyo yetu haivutiwi kiasi hicho? Kwa nini hatuko tayari kiasi hicho kujitoa  sisi wenyewe kwa ajili ya kazi ambayo kwayo Kristo aliweka wakfu maisha Yake? Lazima kitu fulani kifanyike kuponya kutokujali kwa kutisha kulikotushikilia. Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa aibu tunapoona ni kiasi gani kidogo tumefanya kwa kulinganisha na ambavyo tungeweza kufanya katika kupanda mbegu za Ukweli. {8T 46.2}

Ndugu na dada zangu wapendwa, ninazungumza nanyi kwa maneno ya upendo na upole/laini. Harakisheni na jiwekeni wakfu kabisa kwa kazi ya kutoa nuru ya Ukweli kwa ajili ya wakati huu kwa wale waliomo gizani. Dakeni roho ile ya Mfanyakazi Mkuu. Jifunze kutoka kwa Rafiki wa wenye dhambi jinsi ya kuhudumia roho zenye ugonjwa wa dhambi. Kumbuka kwamba katika maisha ya wafuasi Wake lazima kuonekane kujitoa kule kule, utii ule ule kwa kazi ya Mungu, kwa kila dai la kijamii, kila mapenzi ya kidunia, ambayo yalionekana katika maisha Yake. Madai ya Mungu lazima yafanywe kuwa ya kwanza kila wakati. Mfano wa Kristo unapaswa kutuhuisha kuweka bidii bila kukoma kwa ajili ya faida ya wengine. {8T 47.1}

Mungu anatoa wito kwa kila mshiriki wa kanisa kuingia katika huduma Yake. Ukweli ambao haujawekwa katika mtindo wa maisha, ambao haujatolewa kwa wengine, hupoteza uwezo wake wa kuhuisha,  uhai unaotoa nguvu, na nguvu yake ya uponyaji. Kila mtu inabidi ajifunze kufanya kazi na kusimama katika nafasi yake kama mbeba mzigo. Kila ongezeko kwa kanisa linapaswa kuwa wakala mmoja zaidi wa kutekeleza mpango mkuu wa ukombozi. Kanisa lote, likifanya kazi kama mmoja, likichanganyika katika umoja mkamilifu, linapaswa kuwa wakala hai wa umishenari, likisonga mbele kwa bidii za kimishenari, na kuongozwa na Roho Mtakatifu. {8T 47.2}

Kazi hii ambayo itaufanya ulimwengu kujazwa na nuru kama maji yanavyoifunika bahari, haipaswi kufanywa na watu wenye vyeo vya juu peke yao, wala watu wenye nafasi katika mabaraza, bodi, kamati na halmashauri peke yao, wala mameneja wa vituo vyetu vya Sanitarium vinavyoshugulikia afya na tiba rahisi peke yao na watu wa

nyumba za uchapaji peke yao. Kazi hii inaweza kutimizwa tu na kanisa lote likifanya sehemu yake chini ya uongozi na kwa uweza wa Kristo. {8T 47.3}

•

## SEHEMU YA 2—USHAURI UNAORUDIWA MARA KWA MARA

"Naye Bwana, Mungu wa baba zao, akatuma kwao kwa mikono ya wajumbe Wake, akiondoka mapema, na kutuma; kwa sababu aliwahurumia watu Wake, na makao Yake." 2 Mambo ya Nyakati 36:15.

## SURA YA 8
## MAONYO NA MASHAURI YALIYOTOLEWA KWA KANISA LA BATTLE CREEK

*[Makala Zilizojumuishwa Katika Sura Hii Zimetolewa Katika Shuhuda Iliyochapishwa Kwanza Kwa Jinsi Ya Kipeperushi Na Kugawanywa Kwa Washiriki Wa Kanisa La Battle Creek Mnamo Miaka Ya 1894, 1895, Na 1898.]*

Granville, NSW, Julai 20, 1894.

Ninapenda kuwakumbusha ndugu zangu juu ya tahadhari na maonyo ambayo nimepewa kuhusu kuwekeza fedha siku zote katika Battle Creek ili kutengeneza chumba au nafasi moja zaidi au kufanya mambo yawe rahisi zaidi. Maeneo mapya yanapaswa kuingiwa; Ukweli unapaswa kutangazwa kuwa ushuhuda kwa mataifa yote. Kazi hii inarudishwa nyuma ili bendera ya Ukweli isiweze kuinuliwa, kama inavyopaswa kuwa, katika maeneo haya mapya. Wakati ambapo ndugu zetu huko Marekani wanajisikia kuwa huru kuwekeza fedha katika majengo ambayo muda utadhihirisha kwamba wangeweza kufanikiwa hata vyema zaidi na kutenda haki bila ya kuwa na hayo, maelfu ya dola zinatumika hivyo ambazo Bwana alitaka zitumike katika "maeneo ya ng'ambo." Nimewasilisha maonyo na tahadhari hizi, kama Neno la Bwana; lakini moyo wangu umesikitishwa kuona kwamba, licha ya haya yote, fedha zimepotezwa ili kutosheleza mahitaji haya ya kudhaniwa; jengo liliongezwa

kwenye jengo kiasi kwamba fedha hazikuweza kutumika katika sehemu ambazo hawana hali zinazofaa, hawana jengo kwa ajili ibada ya pamoja kwa Mungu au kutoa tabia kwa kazi hiyo, hakuna mahali ambapo bendera ya Ukweli ingeweza kuinuliwa. Mambo haya nimeyaweka mbele yako; na bado umeendelea kutenda vile vile, kumeza/kutumia fedha yote, fedha ya Mungu, katika eneo moja, wakati Bwana amesema kuwa kiasi kingi tayari kilikuwa kimekwishawekezwa katika sehemu moja, ambayo ilimaanisha kuwa hakukuwa na kitu chochote katika sehemu zingine, ambapo kulipaswa kuwa miundombinu na majengo na vifaa, hata vya kuanzia. {8T 48.1}

Ni wito gani mlikuwa nao wa kuwekeza maelfu ya dola katika majengo ya ziada ya shule? Mlidhani kuwa matumizi haya yalihitajika, lakini je! maombi hayakuja kwenu kuwakataza kuwekeza fedha jinsi hiyo? {8T 49.1}

## Wakati wa Mwisho

Nilioneshwa kuwa hali mbaya ya mambo ipo katika ulimwengu wetu. Malaika wa rehema anakunja mbawa zake, tayari kuondoka. Tayari uweza wa kuzuia wa Bwana unaondolewa kutoka duniani, Shetani anatafuta kuchochea vipengele mbalimbali katika ulimwengu wa kidini, akiwaongoza watu kujiweka wenyewe chini ya mafunzo ya yule mdanganyifu mkuu, ambaye anafanya kazi kwa madanganyo yote ya udhalimu kwa wana wa kuasi. Tayari wakazi wa dunia wanakunyika chini ya uongozi wa mkuu wa giza, na huu ni mwanzo tu wa mwisho. {8T 49.2}

Sheria ya Mungu imefanywa batili. Tunaona na kusikia kuhusu machafuko na mfadhaiko, uhitaji na njaa, matetemeko ya ardhi na mafuriko; matendo maovu ya ukatili wa kuogofya yatafanywa na wanadamu; hamaki, tamaa na wala si akili, hutawala. Ghadhabu ya Mungu iko juu ya wakazi wa ulimwengu, ambao kwa haraka wanaharibika kama walivyokuwa wakazi wa Sodoma na Gomora. Tayari moto na mafuriko vinaharibu maelfu ya maisha na mali ambazo zimekusanywa kwa ubinafsi kwa kuwadhulumu maskini. Bwana hivi karibuni atafupisha kazi Yake na kuikomesha dhambi. Oo, kwamba matukio ambayo yamekuja mbele yangu ya maovu yanayotendwa katika siku hizi za mwisho, na yaweze kuleta mguso na fikra za kina katika akili za watu wale wanaoungama kuwa wa Mungu. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa. Bwana anaondoa vizuio Vyake duniani, na hivi karibuni kutakuwa na kifo na uharibifu, uhalifu unaongezeka, na matendo maovu, ya kikatili dhidi ya matajiri waliojiinua dhidi ya maskini. Wale ambao hawana ulinzi wa Mungu

hawatapata usalama mahali popote au katika nafasi yoyote. Mawakala wa kibinadamu wanapewa mafunzo na wanatumia uwezo wao wa ubunifu kuweka katika utendaaji vyombo vyenye uwezo mkubwa kabisa wa kuharibu, kujeruhi na kuua. {8T 49.3}

Badala ya kupanua na kujenga majengo ya ziada katika Battle Creek au maeneo mengine ambayo taasisi zetu tayari zimeanzishwa, inabidi kuweko na kuweka mipaka ya mahitaji. Hebu fedha na wafanyakazi watawanyike ili kuwakilisha Ukweli na kutoa ujumbe wa onyo katika "sehemu za mbali." {8T 50.1}

### Msaada Wakati wa Shida

Wana wa Israeli walipokuwa wanasafiri katika jangwa, Bwana aliwalinda dhidi ya nyoka wenye sumu; lakini wakati ulifika wakati ambapo, kwa sababu ya dhambi ya Israeli, ugumu wa moyo, na ukaidi, Bwana aliondoa nguvu yake ya kuzuia kutoka kwa hawa wanyama watambaao, na watu wengi waliumwa na kufa. Ndipo nyoka yule wa shaba aliinuliwa, ili kwamba wote waliotubu na kumtazama kwa imani wapate kuishi. {8T 50.2}

Wakati wa mchafuko na taabu ulio mbele yetu, wakati wa shida kama ambayo haijawahi kutokea tangu kuwapo kwa taifa, Mwokozi aliyeinuliwa atawasilishwa kwa watu katika nchi zote, ili wote wanaomtazama Yeye kwa imani wapate kuishi. {8T 50.3}

### Kushindwa Kumheshimu Mungu

Kwa kuzingatia hali ya hatari iliyoko mbele yetu je ni kitu gani wanafanya wale wanaokiri kuamini Ukweli? Niliitwa na Mwongozi wangu, ambaye alisema, "Nifuate," nami nilioneshwa mambo miongoni mwa watu wetu ambayo hayakulingana na imani yao. Ilionekana kuwapo na wazimu wa baiskeli. Pesa zilitumika kukidhi shauku katika mwelekeo huu ambazo ingeweza kuwa bora, bora zaidi, kama zingewekezwa katika kujenga nyumba za ibada, kwa kuwa kuna mahali ambapo zinahitajika mno. Yaliwasilishwa mbele yangu mambo ya kushangaza sana huko Battle Creek. Mvuto wa kuduwaza ambao ulikuwa kama uchawi ulionekana kupita kama wimbi juu ya watu wetu huko, na nikaona kwamba huu ungelifuatiwa na majaribu mengine. Shetani hufanya kazi kwa nguvu ya kusudi kuwashawishi watu wetu kuwekeza wakati na pesa zao katika kukidhi mahitaji ya kudhaniwa. Hii ni aina ya ibada ya sanamu. Mfano huu utafuatwa, na wakati mamia wanakufa kwa njaa ya mkate, wakati njaa na tauni vinaonekana na kuhisiwa, kwa sababu Mungu hawezi, kulingana na utukufu wa Jina Lake mwenyewe, kuwalinda wale wanaofanya kazi kinyume na mapenzi Yake, je! wale wanaokiri kumpenda na kumtumikia Mungu

watende kama watu wa siku za Nuhu, wakifuata fikra za mioyo yao? (Baiskeli zilikuwa ghali na watu walitumia kurandaranda nazo mijini, ili kujionyesha na siyo kubeba mizigo au mazoezi, hizi ni enzi kabla ya magari kuvumbuliwa mwaka 1884) {8T 50.4}

Wakati ambapo umekuwa ukikidhi matakwa yako katika matumizi ya fedha-fedha ya Mungu-ambayo lazima utatoa hesabu juu yake, kazi ya umishenari imezuiliwa na kufungwa kwa sababu ya uhitaji wa fedha na wafanyakazi wa kusimamisha bendera ya Ukweli sehemu zile ambapo watu kamwe hawajasikia ujumbe wa onyo. Je! Mungu atawaambia wale ambao kwa ubinafsi wanapendeza mawazo yao wenyewe na kukidhi tamaa zao wenyewe: " Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya Bwana wako."? Mathayo 25:23. {8T 51.1}

Ndugu na dada zangu mlioko Battle Creek, ni ushuhuda wa aina gani mnautoa kwa ulimwengu usioamini? Nimeoneshwa kuwa Bwana hauangalii mwenendo wenu kwa upendeleo au ukubali, kwa kuwa utendaji wenu unapingana na ungamo lenu. Ninyi si watendaji wa Maneno ya Kristo. {8T 51.2}

Niliambiwa na mwongozi wangu: "Angalia, na uone ibada ya sanamu ya watu Wangu, ambao nimekuwa nikiongea nao, nikiamka mapema, na kuwaonyesha hatari zao. Nilitarajia kwamba watazaa matunda." Kulikuwa na wengine ambao walikuwa wakipania umahiri na ukuu, kila mmoja akijaribu kumshinda mwenzake katika kukimbiza baiskeli zao kwa kasi zaidi. Kulikuwa na roho ya ugomvi na mashindano kati yao ni nani anapaswa kuwa mkubwa zaidi. Roho hii ilikuwa sawa na ile iliyooneshwa katika michezo ya besiboli kwenye uwanja wa chuo. Mwongozi wangu alisema: "Mambo haya ni dhambi kwa Mungu. Kote karibu na mbali roho zinaangamia kwa kukosa mkate wa uzima na maji ya wokovu." Shetani anaposhindwa katika mwelekeo mmoja, atakuwa tayari kabisa na hila na mipango mingine ambayo itaonekana kuwa ya kupendeza na ya kuhitajika, na ambayo itachukua pesa na mawazo yote, na kuhimiza ubinafsi, ili aweze kuwashinda wale ambao wanaongozwa kwa urahisi katika starehe bandia na ya ubinafsi. {8T 52.1}

Swali linatokea: Je! Watu hawa wanabeba mzigo gani kwa ajili ya maendeleo ya kazi ya Mungu? Ni katika nini wanapata umuhimu wa kazi iliyo kwa ajili ya wakati huu? Kristo aliwaambia wanafunzi Wake: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu. … nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni." Mathayo 5:16 Je! uwekezaji huu wa fedha na huku kuzungusha baiskeli katika mitaa ya Battle Creek kunatoa ushahidi wa Ukweli wa imani yenu katika onyo zito la mwisho linalopasa kutolewa kwa wanadamu ambao wamesimama kwenye mpaka wa ulimwengu wa milele? {8T 52.2}

Ndugu na dada zangu mlioko Marekani, ninatoa wito wangu kwenu. “Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna.” Wagalatia 6: 7. Maisha ya wengi ni teketeke na laini. Hakuna kitu wanachojua kuhusu kubeba shida kama askari wema wa Kristo. Wao ni vizuizi kwa kazi ya kuokoa roho. Wana mahitaji mengi; kila kitu lazima kiwe kile kitakachowapunguzia usumbufu na kuishi maisha rahisi, ili kupendeza ladha na tamaa yao. Wao wenyewe hawatafanya chochote, na wale ambao wangefanya kitu wanawazuia kwa dhana zao na matakwa ya kufikirika, na upendo wao wa sanamu. Wanajiona kuwa ni Wakristo, lakini hawajui maisha halisi ya Mkristo yanamaanisha nini. Kunamaanisha nini kuwa Mkristo? Kunamaanisha kuwa kama Kristo. {8T 52.3}

Bwana anapowaona watu Wake wakiwekea mipaka matakwa yao ya kufikirika na kuwa na desturi ya kujikana nafsi, si kwa roho ya huzuni, ya majuto, kama mke wa Lutu alivyotoka Sodoma, bali kwa furaha, kwa ajili ya Kristo, na kwa sababu ni jambo sahihi kufanya, kazi itasonga mbele kwa nguvu. Usiruhusu chochote, hata kiwe ni cha thamani kiasi gani, hata kiwe kinapendwa kiasi gani, kumeza/kuteka akili na mapenzi yako, kukuvuta kutoka katika kusoma Neno la Mungu au kutoka katika maombi ya dhati na bidii. Kesheni mkiomba. Ishi kulingana na maombi yako mwenyewe. Shirikiana na Mungu kwa kufanya kazi kwa upatanifu pamoja Naye. Fukuza kutoka katika hekalu la roho kila kitu ambacho kinachukua sura ya sanamu. Sasa ni muda wa Mungu, na muda Wake ni muda wako. Piga vita vizuri vya imani, ukikataa kufikiri au kuzungumza kutokuamini. Ulimwengu unapaswa kusikia ujumbe wa mwisho wa onyo. {8T 53.1}

(Kwa muhtasari, anachosema Ellen White kuhusu fasheni y abaiskeli ya Battle Creek ni ukweli dhabiti wa kiroho hata leo. Haijapitwa na wakati. Hakika hii sio siri. Na kwa vile tunapenda vitu zaidi, tuna mwelekeo zaidi wa kujitahidi kwa umahiri kununua vitu ambavyo hatuhitaji, hata hatuna mwelekeo wa kujinyima kwa ajili ya misheni, kile alichoandika kuhusu baiskeli ni cha wakati huu zaidi, kuliko wakati aliandika. Wengine tunachukia kuwekea vizuizi katika bajeti zetu kwa vitu visivyo vya lazima, yale aliyoandika pia ni magumu sana kukumbuka._

## SURA YA 9
## WAJIBU WETU KWA ULIMWENGU

Granville, NSW, Julai 20, 1894.

Inabidi pawepo na mabadiliko thabiti katika kusudi na moyo wa kazi katika sehemu zile ambapo wanaume na wanawake wamepokea nuru kubwa zaidi. Je, Wanafanya nini kuwaonya wale ambao hawaelewi kwamba Bwana anakuja hivi karibuni? "Tazama, Bwana anakuja kutoka mahali Pake, ili kuwaadhibu wakaao duniani, kwa

sababu ya uovu wao; ardhi nayo itafunua damu Yake, wala haitawafunika tena watu wake waliouawa." Isaya 26:21. Ni nani, ninauliza, anachukua mzigo kwa ajili ya roho ambazo zinaangamia nje ya Kristo? Ni nani atatoka nje ya kambi, achukua shutumu na aibu yake? Ni nani atakayeacha nyumba zenye kufurahisha na vifungo vya thamani vya uhusiano, na kubeba nuru ya thamani kuu ya Ukweli kwenda katika nchi za mbali? Kila siku, kila wakati, huja kwa wale ambao wamekabidhiwa nuru ya Ukweli, waliolemewa na umuhimu mkubwa sana kwamba wanaume na wanawake katika kila nchi wanajiandaa kwa neema au kwa ole, wakiamua hatima yao kwa ajili ya umilele. {8T 53.2}

Mungu ametoa kafara za kushangaza kwa wanadamu. Yeye Ametumia nguvu kubwa kumrudisha mwanadamu kutoka katika makosa na dhambi kufikia uaminifu na utii, lakini nimeoneshwa kwamba Yeye hafanyi chochote pasipo ushirikiano wa mawakala wa kibinadamu. Kila kipaji cha neema na uwezo na ufanisi kimetolewa kwa ukarimu Naye. Nia zenye nguvu kabisa zimetolewa ili kuamsha na kudumisha kuwa hai katika moyo wa mwanadamu roho ile ya umishenari, ili juhudi za mawakala wa Kiungu na wa kibinadamu ziweze kuunganishwa. Lakini watu wetu wamefanya nini kuhusiana na kutoka katika Battle Creek, kubeba nuru kwenda katika maeneo yale ambapo bendera ya Bwana haijasimamishwa bado? Je! Bwana katika Mkutano wa hivi karibuni hakufungua madirisha ya mbinguni na kuwamwagia baraka? Je, mmetumiaje karama ya Mungu? Yeye Amewapatia nguvu ya nia ya utendaji, ili kwa uvumilivu na tumaini na uangalifu wa kudumu mpate kumtangaza Kristo na Yeye aliyesulubiwa, mkiwaita watu kutubu dhambi zao, mkitangaza onyo kwamba Kristo anakuja hivi karibuni kwa uweza na utukufu mkuu. {8T 54.1}

Ikiwa washiriki wa kanisa la Battle Creek hawataamka sasa na kwenda kufanya kazi katika maeneo ya umishenari, basi watarudi kwenye usingizi kama wa kufa. Je! Roho Mtakatifu alifanyaje kazi katika mioyo yenu? …… Je! Hamkuhamasishwa kutumia vipaji ambavyo Mungu amewapa, ili kila mwanamme na mwanamke na vijana wapate kuvitumia kutangaza Ukweli wa wakati huu, kila mtu akiweka mtu binafsi kwenda katika miji ambamo ndani yake Ukweli haujawahi kutangazwa, na kuiinua bendera? {8T 54.2}

Je! Nguvu zenu hazijahuishwa na baraka ambayo Mungu amewapa? Je! Ukweli haujagusa kwa kina zaidi katika roho zenu na kuleta ushawishi mioyoni mwenu? Je! hamtaona kwa uwazi umuhimu wake kwa wale wanaopotea nje ya Kristo? Tangu kufunuliwa dhahiri kwa baraka za Mungu, je! mnamshuhudia Kristo wazi zaidi na kwa uthabiti kuliko hapo awali? {8T 55.1}

Roho Mtakatifu ameleta katika akili zenu Kweli muhimu, za lazima kwa ajili ya uzima za wakati huu. Je! Maarifa haya yanapaswa kufungwa kwenye leso na kufichwa ardhini? Hapana, hapana. Yanapaswa kutolewa kwa watoa riba (Mathayo 25:27). Kadiri mtu anapotumia vipaji vyake kwa uaminifu, hata viwe vidogo kiasi gani, Roho Mtakatifu huchukua vitu vya Mungu, na kuviwasilisha upya akilini. Kupitia kwa Roho Wake Mungu anafanya Neno Lake kuwa nguvu ya kuhuisha. Ni ya haraka na ya nguvu, yenye mvuto mkubwa akilini, sio kwa sababu ya kujifunza au akili ya wakala wa kibinadamu, bali ni kwa sababu uweza a Kiungu unafanya kazi pamoja na uwezo

wa kibinadamu. Na ni kwa uweza wa Kiungu ndiko sifa zote zinapaswa kutolewa. {8T
55.2}

Je! Ubinafsi na maisha rahisi ya wale ambao wana starehe na faraja za kidunia na nyumba za kupendeza zitatutamanishe? Je! Tutakoma kama wakala wa maadili kutumia nguvu zetu kwa ajili ya kuokoa roho? Je! Sauti zetu zikose kuwa dhahiri? Ndipo Mungu ataweka laana yake juu yetu sisi ambao tumekuwa na nuru kubwa kiasi hicho, na kuandika kwenye kuta za nyumba zetu: "Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu." 2 Timotheo 3: 4. Yeye Atatia ulimi katika mawe, nayo yatasema; lakini Mungu anawaamuru ninyi mlioko Battle Creek kusonga mbele. {8T 55.3}

### Jinsi ya Kupata Mafanikio

Azimu, si kwa nguvu zako mwenyewe, bali kwa nguvu na neema uliyopewa na Mungu, kwamba utaweka wakfu Kwake sasa, sasa hivi, kila nguvu, kila uwezo. Kisha utamfuata Yesu kwa sababu Yeye anakuamuru, nawe hautauliza ni wapi, au ni thawabu gani itatolewa. Itakuwa heri kwako pale utakapolitii Neno: "Nifuate Mimi." Sehemu yako ni kuwaongoza wengine kwenye nuru kwa juhudi za busara, za uaminifu. Chini ya ulinzi wa Kiongozi wa Kiungu, utafanya, azimu kuchukua hatua, bila kusita hata kidogo. {8T 55.4}

Unapokufa kwa ajili ya nafsi, unapojisalimisha kwa Mungu, kufanya kazi Yake, kuiruhusu nuru ambayo amekupa Yeye iangaze katika matendo mema, hutafanya kazi peke yako. Neema ya Mungu inasimama kushirikiana na kila juhudi kuwaangazia wajinga na wale ambao hawajui kuwa mwisho wa vitu vyote umekaribia. Lakini Mungu hatafanya kazi yako. Nuru inaweza kuangaza kwa wingi, lakini neema iliyotolewa itaongoa roho yako pale tu inapokuamsha kushirikiana na wakala wa Kiungu. Wewe unaitwa kuvaa silaha za Kikristo na kuingia katika utumishi wa Bwana kama askari wenye bidii. Uweza wa Mungu utashirikiana na juhudi za kibinadamu kuvunja uchawi wa maliwazo ya ulimwengu ambayo adui ametia juu ya roho za watu. {8T 56.1}

Tena naomba msaada ambao tulipaswa kuwa nao, fedha ambazo tunapaswa kuwa nao, iwapo kitu chochote kimetimizwa katika nchi hii. Hebu mioyo yenu na ivutwe kwa upendo kwa ajili ya roho zinazoangamia. Tii msukumo ule unaotolewa na Mbingu ya Juu. Usimhuzunishe Roho Mtakatifu kwa kuchelewa. Usipinge njia za Mungu za kujipatia tena roho kutoka katika utumwa wa dhambi. Kwa kila mtu, kulingana na vipaji vyake kadhaa, amepewa kazi yake. Jitahidi, na Mungu atakubali juhudi zako. {8T 56.2}

## SURA YA 10
## KAZI YA UMISIONARI NYUMBANI NA UGHAIBUNI

Granville, NSW, Julai 24, 1895.

Shamba la Mungu ni ulimwengu. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake: "mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." Na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa Jina Lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. Matendo 1:8; Luka 24:47. Petro aliwaambia waumini: "ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Matendo 2:39. {8T 56.3}

Mungu anatangaza: "Nami nitampanda katika nchi kwa ajili yangu mwenyewe; Nami nitamrehemu yeye asiyepewa rehema; Nami nitawaambia wale wasiokuwa watu Wangu, Ninyi ndinyi watu Wangu; nao watasema, Wewe Ndiwe Mungu wangu." Hosea 2:23. "Asema hivi, Ni neno dogo sana wewe kuwa mtumishi Wangu ili kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejeza watu wa Israeli waliohifadhiwa; zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa, upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia" Isaya 49: 6. {8T 57.1}

Mungu amemwaga kwa wingi Roho Wake Mtakatifu juu ya waumini katika Battle Creek. Mmetumiaje baraka hizi? Je! Mmefanya kama walivyofanya wale watu ambao Roho Mtakatifu alikuja juu yao katika Siku ya Pentekoste? Ndipo "wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri Neno." Matendo 8: 4. Je! tunda hli limeonekana katika Battle Creek? Je! Kanisa limefundishwa na Mungu kujua wajibu wao, na kuiakisi ile nuru ambayo wameipokea? {8T 57.2}

### Kielelezo cha Kazi Tunayopaswa Kuifanya

“Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali Neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana.” Aya ya 14. Roho wa Mungu alikuwa akisubiri kuziangazia roho na kuzigeuza kuelekea katika Ukweli. {8T 57.3}

Angalia ni juhudi kiasi gani ilitumika kwa ajili ya mtu mmoja tu, Mkushi. "Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa. Naye akaondoka, akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, towashi, mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea, ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. {8T 57.4}

“Roho akamwambia Filipo, Sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, Je! Yamekuelea haya unayosoma? Yerusalemu hata Gaza, ambao ni jangwa. Akaondoka, akaenda; na tazama, mtu mmoja Mkushi, towashi mwenye mamlaka kuu chini ya Kandake, malkia wa Waethiopia, ambaye alikuwa msimamizi wa hazina yake yote, naye alikuwa akija Yerusalemu kuabudu, alikuwa anarudi, ameketi katika gari lake soma nabii Isaya. {8T 57.4}

Basi, Roho Mtakatifu akamwambia Filipo, "Sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, Je! Yamekuelea haya unayosoma? Akasema, Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye…… {8T 58.1}

"Filipo … akianza kwa Andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. 8.36 Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, Tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu, akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo Ndiye Mwana wa Mungu. {8T 58.2}

“Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza. {8T 58.3}

“Kisha, walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi. Lakini Filipo akaonekana katika Azoto, na alipokuwa akipita akahubiri Injili katika miji yote, hata akafika Kaisaria.” Matendo 8: 26-40. {8T
58.4}

Katika uzoefu wa Filipo na Mkushi imewasilishwa kazi ambayo kwayo Bwana anawaita watu Wake. Mkushi anawakilisha tabaka kubwa ambalo linahitaji wamishenari kama Filipo, wamishenari ambao wataisikia sauti ya Mungu na kwenda kule anakowatuma. Wapo wale ulimwenguni ambao wanasoma Maandiko, lakini hawawezi kuelewa maana yake. Wanaume na wanawake ambao wana maarifa juu ya Mungu wanahitajika kulielezea Neno kwa roho hizi. {8T 58.5}

### Kazi Iliyopuuzwa

Katika mfano wa Msamaria mwema kuhani na Mlawi walimtazama mtu yule mnyonge ambaye alikuwa ameporwa na kujeruhiwa, lakini haikuonekana kwao kufaa kumsaidia yule ambaye, kwa sababu alikuwa hajiwezi na kutelekezwa, alihitaji

mno msaada. Kuhani na Mlawi wanawawakilisha wengi, wengi katika Battle Creek. {8T 59.1}

Roho nyingi zinaweza kuokolewa ikiwa eneo la Kusini linaweza kupata sehemu japo ndogo tu ya fedha zilizotumika kwa wingi kupita kiasi katika Battle Creek ili kufanya mambo yawe ya kufaa zaidi, na bila usumbufu. {8T 59.2}

Urithi wa Bwana umepuuzwa ajabu, na Mungu atawahukumu watu wake kwa sababu ya jambo hili. Kiburi na kupenda kujionyesha huridhishwa na mafao yaliyolimbikizwa, wakati maeneo mapya yameachwa bila kuguswa. Karipio la Mungu liko juu ya wasimamizi kwa sababu ya ubaguzi/upendeleo wao na ugawaji wa mali Yake kwa ubinafsi. {8T 59.3}

Kitu kimefanywa katika misheni za kigeni, na kitu fulani katika misheni za nyumbani; lakini kwa jumla, eneo kubwa sana limeachwa bila kufanyiwa kazi. Kazi imewekwa mahali pamoja tu, kila kitu kipo katika makao makuu. Maslahi ya kazi ya Mungu hapo Battle Creek yamekuwa mengi mno, na hii inamaanisha kuwa sehemu zingine za shamba la Bwana zinanyimwa vifaa na miundombinu ambayo ilipaswa kuwa nayo. Maandalizi makubwa na makubwa zaidi, katika ujenzi na upanuzi wa majengo, ambayo yamekusanywa mahali pamoja na kushikilia idadi kubwa huko Battle Creek, haukubaliani na mpango wa Mungu, bali unapingana moja kwa moja na mpango Wake. {8T 59.4}

Imesisitizwa kwamba kulikuwa na faida kubwa kuwa na taasisi nyingi zilizowekwa mahali pamoja karibu-karibu, kwamba zingetiana nguvu kila moja na nyenzake nazo zingeweza kutoa msaada kwa wale ambao wanaotafuta elimu na ajira. Hii ni kulingana na hekima na fikra za kibinadamu; itakubalika kuwa, kwa mtazamo wa wanadamu, kunufaika kwingi hupatikana kwa kulundika majukumu mengi huko Battle Creek; lakini njozi inabidi kupanuliwa. {8T 59.5}

Taasisi hizi inabidi zigawanywe katika sehemu nyingi ili kazi ipate kuanza katika miji ambamo itakuwa muhimu kutengeneza vituo vya mvuto, vinavyovutia. Majengo yanapaswa kujengwa na majukumu kuwa na vituo mahalia katika maeneo mengi ambayo kwa sasa yamenyimwa masilahi muhimu, ya kiroho ili kutunisha kupita kiasi ziada ambayo tayari iko huko Battle Creek. Bwana hatukuzwi na usimamizi huu kwa upande wa wale ambao wako katika nafasi zenye madaraka. "Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari." "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma." Habakuki 2:14; Yohana 17: 3. {8T 60.1}

Wokovu wa wapagani kwa muda mrefu umechukuliwa kuwa jambo ambalo linapaswa kushirikisha maslahi ya Wakristo, na ni haki kabisa kuleta nuru kwenye mipaka yao yenye giza. Lakini kazi ya umishenari nyumbani pia inahitajika. Wapagani wanaletwa malangoni mwetu hasa. Ujinga wa ibada ya sanamu uko karibu kabisa na nyumba zetu. Jambo fulani linafanyika kwa ajili ya watu ambao si weupe-yaani watu weusi, lakini ni kidogo sana ikilinganishwa na wale ambao tayari wana ujuzi wa Ukweli, ambao wamepata fursa zisizo na idadi, lakini ambao hawajathamini sana faida zake. Kwa wale ambao hawaujui Ukweli, hebu upendo wa Yesu uwasilishwe, nao utafanya kazi kama chachu kwa ajili ya mabadiliko ya tabia. {8T 60.2}

Tunafanya nini kwa shamba la Bwana la Kusini mwa Marekani? Nimeangalia kwa wasiwasi mno kuona iwapo mpango fulani usingelifaa kuwekwa katika utendaji kwa ajili ya kufidia upuuziaji wa dhambi kwa eneo hilo, lakini sioni pendekezo au azimio la kufanya chochote. Huenda kuna kitu kimepangwa ambacho sijakiona. Ninatumahi hivyo, na Bwana asifiwe ikiwa ni hivyo. Lakini ingawa kwa miaka kadhaa wajibu wetu umepangwa kwa jinsi iliyo thabiti kabisa, lakini bado eneo la Kusini limeguswa tu na ncha za vidole vyetu. Sasa ninahisi kwa kina kusema kwa dhati na ari katika kulileta tena mbele yenu eneo hili lililopuuzwa la shamba la Bwana la mizabibu. Jambo hili linaletwa mbele yangu tena na tena. Nimeamshwa wakati wa usiku, na amri imekuja: Andika mambo hayo ambayo nimeyafungua mbele yako, kwamba watu watasikia au kwamba wataepuka. {8T 60.3}

## SURA YA 11
## ROHO MTAKATIFU KATIKA SHULE ZETU

Cooranbong, NSW, Mei 10, 1896.

Ninawauliza ninyi ambao mnaishi katikati kabisa ya kazi kupitia upya uzoefu wa miaka mingi na muone iwapo kwa kweli "vema mtumishi mwema" inaweza kutamkwa kwenu. Ninawaomba walimu katika shule zetu kufikiria kwa makini, kwa maombi: Je! Mimi binafsi nimekesha kwa ajili ya roho yangu kama mtu anayeshirikiana na Mungu kwa ajili ya usafi wake kutokana na dhambi zote na utakaso wake wote? Je! Unaweza kwa kanuni na mfano kuwafundisha vijana utakaso, kupitia Ukweli, hadi wafikie utakatifu? {8T 61.1}

Je! mmekuwa mkimwogopa Roho Mtakatifu? Wakati mwingine Roho huyu amekuja na mvuto unaoenea kabisa katika shule huko Battle Creek na kwenye shule katika maeneo mengine. Je! mlitambua uwepo Wake? Je! mlimpa heshima inayomstahili mjumbe wa mbinguni? Wakati Roho alipoonekana kuwa anapambana na vijana, je! mlisema: "Hebu tuweke kando masomo yote, kwa maana ni dhahiri kwamba tunaye mgeni wa kimbingu miongoni mwetu? Hebu tumpe Mungu sifa na heshima." Je! ninyi, kwa mioyo iliyovunjika, mliinama katika maombi pamoja na wanafunzi wenu, mkisihi kwamba mpate kupokea baraka ile ambayo Bwana alikuwa anaiwasilisha kwenu? {8T 61.2}

Mwalimu Aliye Mkuu Mwenyewe alikuwa kati yenu. Je, Mlimheshimu? Je! Hakujulikana kabisa kwa baadhi ya walimu? Je! kulikuwa na haja ya kumwita mtu fulani mwenye kudhaniwa kuwa na mamlaka ya kuweza kumkaribisha au kumfukuza Mjumbe huyu kutoka mbinguni? Ingawa hakuonekana, uwapo Wake ulikuwa miongoni mwenu. Lakini je wazo halikuelezwa kuwa katika shule muda inabidi utolewe kwa ajili ya kusoma na kujifunza, na kwamba kila jambo na wakati wake, kana kwamba saa zilizotengwa kwa ajili ya masomo ya kawaida zilikuwa ni za thamani sana kuweza kutolewa kwa ajili ya utendaji wa mjumbe wa mbinguni? {8T 61.3}

Ikiwa kwa namna yoyote ile umemzuia au kumfukuza Roho Mtakatifu, ninakusihi utubu haraka iwezekanavyo. Ikiwa yeyote miongoni mwa walimu wetu hajaufungua mlango wa moyo wake kwa Roho wa Mungu, bali ameufunga na kuutia kufuli, ninawasihi wafungue mlango na kuomba kwa dhati na bidii: "Kaa nami." Wakati Roho Mtakatifu anapodhihirisha uwapo Wake katika chumba chako cha shule, waambie wanafunzi wako: "Bwana anaashiria kwamba leo ana somo kwetu lenye umuhimu wa mbinguni, lenye thamani kuliko masomo yetu ya kawaida. Hebu na tusikilize; hebu tuiname mbele za Mungu na kumtafuta kwa moyo wote." {8T 62.1}

Hebu niwaambie ninachojua kuhusu Mgeni huyu wa mbinguni. Roho Mtakatifu alikuwa akiwaza sana juu ya vijana wakati wa saa za shule; lakini baadhi ya mioyo ilikuwa baridi na yenye giza kiasi kwamba hawakuwa na hamu kwa ajili ya uwapo wa Roho, na nuru ya Mungu iliondolewa. Kwamba Mgeni huyu wa mbinguni angefungua ufahamu wote, angetoa hekima na maarifa katika mikondo yote ya masomo ambavyo vingeweza kutumika kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Mjumbe wa Bwana alikuja kusadikisha kuhusu dhambi na kulainisha mioyo iliyo migumu kwa sababu ya kujitenga na Mungu kwa muda mrefu. Yeye Alikuja kudhihirisha upendo mkuu ambao kwa huo Mungu amewapenda vijana hao. Wao ni urithi wa Mungu, na waelimishaji wanahitaji "elimu ya juu zaidi" kabla hawajastahili kuwa walimu na

washauri kwa vijana. {8T 62.2}

Mwalimu anaweza kuelewa mambo mengi kuhusu ulimwengu wa asili na sayari; anaweza kujua yote kuhusu muundo wa viumbe hai, ubunifu wa sanaa ya mitambo, ugunduzi wa sayansi ya asili; lakini hawezi kuitwa msomi isipokuwa ana maarifa ya kumjua Mungu wa pekee wa Kweli na Yesu Kristo, aliyemtuma. Kanuni yenye asili ya Mwenyezi Mungu lazima ienee na kutawala katika mwenendo wetu na kutufunga kwa Mungu. Hii kwa namna yoyote ile haitakuwa kizuizi cha kujifunza sayansi ya Kweli. Kumcha Bwana ni chanzo cha hekima, na mtu ambaye anakubali kufinyangwa na kufanyizwa katika mfano wa Kiungu ndiye kielelezo bora kabisa cha kazi ya Mungu. Wote wanaoishi katika ushirika na Muumbaji wetu watakuwa na uelewa wa kusudi Lake katika kuumbwa kwao, nao watatambua kuwa Mungu anawawajibisha kutumia vitivo vyao vyote kwa kusudi bora kabisa. Hawatatafuta kujitukuza wala kujidhalilisha. {8T 62.3}

## Mapenzi ya Mungu Juu Yetu

Maarifa ya Mungu hupatikana kutoka kwenye Neno Lake. Ujuzi wa majaribio ya utauwa wa Kweli, unaopatikana katika kujitoa kila siku wakfu na huduma, unahakikisha elimu ya hali ya juu kabisa ya mwili, akili, na roho. Kujitoa huku wakfu kwa nguvu zetu zote kwa Mungu kunazuia kujiinua mwenyewe. Ugawaji wa uweza wa Kiungu/Bwana huheshimu bidii yetu ya kutafuta hekima ambayo itatuwezesha kutumia wanadamu uwezo wa juu kabisa kwa namna ambayo itamheshimu Mungu na kuwabariki wenzetu. Kwa kuwa uwezo wa vitivo hivi unatokana na Mungu, na wala si kwa kujiumbia mwenyewe, vinapaswa kuthaminiwa kama kipaji kutoka kwa Mungu kwa ajili ya kutumika katika utumishi Wake. {8T 63.1}

Uwezo wa akili uliokabidhiwa na mbingu unapaswa kuchukuliwa kama uwezo wa juu, kutawala ufalme wa mwili. Tamaa za asili na shauku zinapaswa kuwekwa chini ya udhibiti wa dhamiri na nguvu za kiroho. {8T 63.2}

Dini ya Kristo kamwe haimdhalilishi mpokeaji wake; kamwe haimfanyi kuwa duni au kuwa mwenye ovyo, jeuri, rafu, kukosa staha/uungwana au kujiona, mwenye harara, mwenye kuonesha hisia kali au mwenye moyo mgumu. Kinyume chake, husafisha akili za kupambanua mazuri, huadilisha busara ya kuchagua mazuri, na kuboresha, kutakasa na kukuza fikira, na kuwafanya kuwa watumwa wa Kristo. Mfano bora ya Mungu kwa watoto ajili ya Wake uko juu kuliko ambavyo fikira ya juu kabisa ya mwanadamu inaweza kufikia. Ametoa katika sheria Yake takatifu nakala ya tabia Yake. {8T 63.3}

Kristo Ndiye Mwalimu mkuu kuliko waimu wote ambao ulimwengu umewahi kuwafahamu. Je! Ni kipimo gani anachoshikilia Yeye mbele ya wote wanaomwamini?

“Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.” Mathayo 5:48. Kama Mungu alivyo mkamilifu katika mazingira yake, ndivyo mwanadamu anavyoweza kuwa mkamilifu katika mazingira yake. {8T 64.1}

Kipimo cha tabia ya Mkristo ni kufanana na Kristo. Mbele yetu imefunguliwa njia ya maendeleo ya daima. Tunalo lengo tunalopaswa kulipata, kiwango cha kufikia, ambacho kinajumuisha kila kitu kizuri na safi na bora na kilichoinuliwa. Lazima kuwe na jitahada endelevu na kupiga hatua daima kwenda mbele na kwenda juu kuelekea katika ukamilifu wa tabia. {8T 64.2}

Paulo anasema: “Sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika: ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu." Wafilipi 3:13, 14. {8T 64.3}

Haya ndiyo mapenzi ya Mungu kuhusu wanadamu, kutakaswa kwao. Katika kusukumiza safari yetu kwenda juu, kuelekea mbinguni, kila uwezo wa akili ni lazima uwekwe katika hali bora kabisa ya afya, ukiwa tayari kufanya huduma ya uaminifu. Uwezo ambao Mungu amempa mwanadamu unapaswa kutumika kwa nguvu zote. Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako." Luka 10:27. Mwanadamu hawezi kulifanya hili mwenyewe; lazima awe na msaada wa Mwenyezi Mungu. Ni sehemu gani wakala wa kibinadamu atende? “Utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema." Wafilipi 2:12, 13. {8T 64.4}

Bila utendaji wa Mwenyezi Mungu, mwanadamu hangeweza kufanya jambo jema lolote. Mungu anamwita kila mtu apate kutubu, lakini bado mwanadamu hawezi hata kutubu mwenyewe isipokuwa Roho Mtakatifu amefanya kazi moyoni mwake. Lakini Bwana hataki mtu yeyote asubiri hadi amefikiri kwamba ametubu kabla ya kuchukua hatua kwenda kwa Yesu. Mwokozi Siku zote anaendelea kuwavuta watu wapate kufikia toba; wanahitajika tu kujisalimisha na kukubali kuvutwa, na mioyo yao itayeyushwa kwa toba. {8T 64.5}

Mwanadamu amepewa sehemu katika pambano hili kuu la uzima wa milele; ni lazima auitikie utendaji wa Roho Mtakatifu. Kutahitajika pambano kuweza kuvunja nguvu za giza, na Roho hufanya kazi ndani yake kulitimiza hili. Lakini mwanadamu si kiumbe kisichoonesha hisia, kilichotulia tu bila ya utendaji na kungoja kuokolewa katika uvivu. Anaitwa kuhenyesha kila misuli na kutumia kukizoeza kwa bidii kila kitivo katika mapambano ya kutokufa; lakini ni Mungu anayetoa ufanisi. Hakuna mwanadamu anayeweza kuokolewa katika uvivu. Bwana anatuambia: "Jitahidini kuingia katika mlango ulio mwembamba, kwa maana nawaambia ya kwamba wengi watataka kuingia, wasiweze.” “Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana

mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache." Luka 13:24; Mathayo 7:13, 14. {8T 65.1}

## Kufanya Kazi Kinyume na Roho Mtakatifu

Ninawasihi wanafunzi katika shule zetu kuwa watu wenye kiasi, hekima, msawaziko mzuri wa akili, bila ya kuwa na harara. Upuuzi wa vijana haumpendezi Mungu. Burudani zao na michezo hufungua mlango kwa mafuriko ya majaribu. Katika vitivo vyenu vya kiakili mnamiliki kipaji cha mbinguni toka kwa Mungu, na hampaswi kuruhusu mawazo yenu kuwa ya bei rahisi na ya chini (hovyo na maadili mabaya). Tabia iliyotengenezwa kulingana na kanuni za Neno la Mungu itadhihirisha kanuni thabiti, matamanio safi, adili. Roho Mtakatifu anaposhirikiana na uwezo wa akili za mwanadamu, matokeo ya hakika ni shauku juu, takatifu……. {8T 65.2}

Mungu huona yale ambayo macho yenye upofu ya walimu hayawezi kutambua, kwamba uovu wa kila aina na kiwango unapambana ili upate kutawala, ukifanya kazi dhidi ya maonesho ya wazi ya uweza wa Roho Mtakatifu. Mazungumzo ya kawaida mno, na mawazo duni yaendayo chini, yaliyopotoka, yanafumwa katika nyuzi za tabia. {8T 65.3}

Vyama kwa ajili ya anasa za kipuuzi za ulimwengu, mikusanyiko kwa ajili ya kula, kunywa, na kuimba, vinasukumwa na roho ambayo itokayo chini. Hivyo ni sadaka kwa Shetani. Maonesho ya wendawazimu wa kupenda baiskeli ni kosa kwa Mungu. Gadhabu yake imewaka dhidi ya wale wanaofanya mambo kama hayo. Katika kujifurahisha huku akili hupumbazwa, kama katika kunywa pombe. Mlango unafunguliwa kwa ajili ya ushirikiano usio na adabu, usiotakaswa, na uchafu. Mawazo, yakiwa yameruhusiwa kukimbia katika mkondo dhaifu wa chini, mapema hupotosha uwezo wote wa kiumbe huyo. Kama Israeli ya zamani, wapenda anasa hula na kunywa, na kuamka kucheza. Kuna raha na kufanya karamu za ulevi, kicheko na shangwe za sauti ya juu. Katika haya yote vijana hufuata mfano wa waandishi wa vitabu vilivyowekwa mikononi mwao kwa ajili ya kusoma. Uovu mkubwa kabisa wa haya yote ni athari ya kudumu ambayo mambo haya yanatia katika tabia. {8T 66.1}

Wale ambao wanaongoza katika mambo haya huleta juu ya kusudi la doa ambalo halifutiki kwa urahisi. Wanajeruhi roho zao wenyewe, na katika maisha yao yote watabeba makovu. Mtenda maovu anaweza kuona dhambi zake na kutubu; Mungu anaweza kumsamehe mwenye dhambi; lakini nguvu za utambuzi, ambazo daima zinapaswa kuwekwa kuwa kali na nyeti kuhisi tofauti kati ya yaliyo matakatifu na yale ya kawaida, zinaangamizwa kwa kiwango kikubwa. Mara nyingi sana mbinu na

ubunifu wa wanadamu hukubaliwa kama ya Bwana Mwenyewe. Baadhi ya roho zitatenda kwa upofu na kukosa hisia, zikiwa tayari kupokea kwa moyo mkunjufu hisia hafifu,za hovyo, za kawaida, na hata za kikafiri, huku zikigeuka dhidi ya uthibitisho wa Roho Mtakatifu. {8T 66.2}

## SURA YA 12
## KUONDOKA KUTOKA KWENYE UNYOFU

Cooranbong, NSW, Januari 12, 1898.

Nimefurahi kuwa Bwana kwa rehema analizuru tena kanisa. Moyo wangu unatetemeka ninapofikiri juu ya mara nyingi ambazo amekuja, na Roho Wake Mtakatifu ametenda kazi kanisani; lakini baada ya hisia za papo hapo kumalizika, utendaji wa rehema wa Mungu unasahaulika. Kiburi, kutokujali kiroho, ndio kumbukumbu iliyoandikwa mbinguni. Wale ambao walitembelewa na rehema na neema tele za Mungu walimfedhehesha Mkombozi wao kwa kutokuamini kwao…… {8T 66.3}

Mwokozi amewazuru mara nyingi huko Battle Creek. Kwa hakika kama vile alivyotembea katika mitaa ya Yerusalemu, akitamani kupumua pumzi ya uhai ya maisha ya kiroho ndani ya mioyo ya wale waliokata tamaa na walio karibu na kufa, Je, amekuja kwako wewe. Miji ambayo ilibarikiwa sana na uwapo Wake, msamaha Wake, karama Zake za uponyaji, ilimkataa; na ushahidi mkubwa kama huo, ndio, mkubwa zaidi, wa upendo usioweza kulipika ambao umetolewa Battle Creek na bila ya mwitikio. Je! Kristo hajajaza kanisa Lake kwa manufaa na baraka? Je, Yeye Hajatuma watumishi Wake na ujumbe wa msamaha na haki, kutolewa bure kwa wote watakaoupokea? {8T 67.1}

Yerusalemu ni kielelezo cha kile kanisa litakavyokuwa ikiwa litakataa kutembea katika nuru ambayo Mungu ameitoa kwake. Yerusalemu ilipendelewa na Mungu kama ghala ya amana takatifu. Lakini watu Wake walipotosha Ukweli, na wakadharau maombi na maonyo yote. Hawakuheshimu mashauri Yake. Nyua za hekalu zilichafuliwa na bidhaa na unyang’anyi. Ubinafsi na upendo wa mali, husuda na ugomvi, vilipendwa. Kila mtu alitafuta kupata faida kutoka upande wake. Kristo aligeuka kutoka kwao akisema: "Ee Yerusalemu, Yerusalemu," ninawezaje kukutoa? “Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!!"

Mathayo 23:37. {8T 67.2}

Hivyo ndivyo Kristo anavyohuzunika na kuyalilia makanisa yetu, taasisi zetu za elimu, ambazo zimeshindwa kutimiza matakwa ya Mungu. Huwa anakuja kuichunguza Battle Creek, ambayo imekuwa ikienda katika safari ile ile kama Yerusalemu. Nyumba ya uchapishaji imegeuzwa kuwa madhabahu iliyotiwa unajisi, na kuwa mahali pa Bidhaa na biashara isiyo takatifu. Imekuwa mahali ambapo udhalimu na ulaghai umefanyika, ambapo ubinafsi, kijicho, husuda, na shauku vimetawala. Lakini bado watu ambao wameongozwa katika utendaji huu ulio juu ya kanuni mbaya wanaonekana kutokujua kuhusu uelekeo wao mbaya wa utendaji. Maonyo na kusihi vinapowajia, wanasema: Je! Hasemi kwa mifano (parables)? Maneno ya onyo na karipio yametendewa kama visa visivyo na maana kabisa. {8T 67.3}

Kristo alipotazama chini kutoka katika kilele cha Mlima wa Mizeituni, Aliona hali hii ya mambo ikiwa katika kila kanisa. Maonyo yanawafikia wote wanaofuata nyayo za watu wa Yerusalemu, ambao walikuwa na nuru kubwa kiasi kile. Watu hawa wako mbele yetu kama onyo. Kwa kukataa maonyo ya Mungu katika siku zetu hizi, watu wanarudia dhambi ya Yerusalemu. Bwana huona kile ambacho wakala wa kibinadamu hakioni naye hatakiona - matokeo ya ubunifu wote wa wanadamu katika Battle Creek. Yeye Amefanya yote ambayo Mungu angeweza kufanya. Amemulika nuru mbele ya macho ya watu, ili dhambi zao zisije kufikia mpaka ambapo toba haiwezi kuhisiwa. Lakini kwa mchakato mrefu wa kutoka katika kanuni za haki na uadilifu, watu wamejiweka mahali ambapo nuru na Ukweli, haki na rehema, havitambuliwi. Mwelekeo huu umekuwa sehemu ya asili yao hasa. {8T 68.1}

Ninatoa wito kwa wote ambao wameungana katika mwelekeo wa utendaji ambao ni mbaya kimsingi, kufanya matengenezo thabiti na milele baada ya hapo kutembea kwa unyenyekevu pamoja na Mungu…. {8T 68.2}

Hivi si visa visivyokuwa na maana, au mambo madogomadogo, bali ni Ukweli. Tena ninauliza: Umesimama Je, wewe upande gani? "Bwana akiwa Ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! Mfuateni Yeye." 1 Wafalme 18:21. {8T 68.3}

## SURA YA 13
## MTAFUTE MUNGU KWA AJILI YA MSAADA

Cooranbong, NSW, Juni 8, 1898.

Kuna nyakati ambapo Ukweli lazima uzungumzwe, kwamba watu watasikia au kwamba watauvumilia. Bwana anafedheheshwa sana pale wale wanaokiri kuuamini Ukweli wanashindwa kupatana wao kwa wao, na kukata rufaa kwa wanasheria. Je! mtajifunza Neno la Mungu na kutii mafundisho yaliyotolewa juu ya jambo hili? Maslahi ya kusudi la Mungu hayapaswi kutolewa kwa watu ambao hawana uhusiano wowote na mbingu. {8T 69.1}

Mambo yamewasilishwa mbele yangu ambayo yameijaza roho yangu na uchungu mkali. Niliwaona watu wakiwa wameungana mkono kwa mkono na wanasheria, lakini Mungu hakuwa pamoja nao. Wakiwa na fikira nyingi juu ya kazi hiyo, wanaenda kwa wanasheria kwa ajili ya msaada wa kutekeleza mipango yao. Nimeagizwa kusema kwa watu kama hao kwamba hawaendi chini ya uvuvio/msukumo wa Roho wa Mungu. {8T 69.2}

"Je! Ni kwa sababu hapana Mungu katika Israeli, hata mnakwenda kuuliza kwa Baalzebubu, mungu wa Ekroni?" 2 Wafalme 1: 3. Watu walio katika nafasi zenye madaraka wanaungana na wale waliomo kanisani na nje ya kanisa, ambao ushauri wao unapotosha. Je! Ni muhimu kwa Bwana kuja kwako na fimbo ili kukuonesha kwamba wewe unahitaji uzoefu wa hali ya juu kabla ya kuandaliwa kwa ajili ya kuonana na familia ya juu? Je! Utaungana na watu ambao wana uwezo wa kushtaki, kusingizia kwa kufikiri na kunena mabaya juu ya mambo ambayo Mungu anayakubali? Kwa Jina la Bwana ninawaambia kuwa mnahitaji utambuzi wa wazi zaidi na uoni/macho safi zaidi ya kiroho. {8T 69.3}

Iwapo nuru ambayo Mungu amewapa tena na tena, kwamba vituo vya umisionari vinapaswa kuanzishwa katika miji mingi, na kwamba kazi na fedha zilizowekwa

chini ya makao makuu ya Battle Creek zinapaswa kugawanywa na kuwekwa katika maeneo mengi, ingelifuatwa, hali ya sasa ya machafuko na upungufu wa fedha isingelikuwapo kamwe. {8T 69.4}

Watu walioko Battle Creek wamepuuza mashauri ya Bwana kwa sababu ilikuwa inawafaa wao, kuwa na kazi hiyo kuwa na makao makuu yake pale. Mungu ameyaacha haya kuwa matokeo ya hekima yao ya kibinadamu, na matunda yake yanaonekana katika mfadhaiko wa sasa. {8T 70.1}

"Ni nani miongoni mwenu amchaye Bwana, aitiiye sauti ya mtumishi Wake? Yeye aendaye katika giza, wala hana nuru, naye alitumainie Jina la Bwana, na kumtegemea Mungu wake. Tazama, ninyi nyote mwashao moto, mjifungiao hiyo mienge; endeni ninyi katika mwali wa moto wenu, na katikati ya mienge mliyoiwasha. Mtayapata haya kwa mkono Wangu; mtalala kwa huzuni." Isaya 50:10, 11. {8T 70.2}

"Haya! Basi, ukawaambie watu wa Yuda, na wenyeji wa Yerusalemu, ukisema, Bwana asema hivi, Tazama, ninafinyanga mabaya juu yenu, na kuwaza mawazo juu yenu; rudini sasa, kila mmoja na aiache njia yake mbaya; zitengenezeni njia zenu, na matendo yenu. Lakini wao wasema, Hapana tumaini lolote; maana sisi tutafuata mawazo yetu wenyewe, nasi tutatenda kila mmoja wetu kwa kuufuata ushupavu wa moyo wake mbaya. Basi, kwa ajili ya hayo, Bwana asema hivi, Ulizeni sasa katika mataifa, ni nani aliyesikia habari za mambo kama hayo; bikira wa Israeli ametenda tendo lichukizalo sana. Theluji ya Lebanoni itakoma katika jabali la kondeni? Au je! Maji ya baridi yashukayo toka mbali yatakauka? Maana watu wangu wamenisahau, wameufukizia ubatili uvumba; nao wamewakaza katika njia zao, katika mapito ya zamani, ili wapite katika njia za kando, katika njia isiyotengenezwa.” Yeremia 18: 11-15. {8T 70.3}

## Kazi ya Umishenari wa Tiba

Tena na tena Bwana ameonesha kazi ambayo kanisa huko Battle Creek na mengine yote yalipo kote Marekani yanapaswa kufanya. Wanapaswa kufikia kiwango cha juu zaidi katika maendeleo ya kiroho kuliko vile walivyofikia. Wanapaswa kuamka kutoka kwa usingizi na kwenda nje ya kambi, wakifanya kazi kwa ajili ya roho zilizo karibu kuangamia. {8T 70.4}

Watendakazi wa umishenari wa tiba wanafanya kazi ambayo imepuuzwa kwa muda mrefu ambayo Mungu alitoa kwa kanisa huko Battle Creek - wanatoa wito wa mwisho kwa ajili ya karamu ambayo [Bwana] ameiandaa. {8T 71.1}

Ndugu zangu, kwa nini mnaweka vitu vingi na kuvifungia ndani ya Battle Creek? Kwa nini hamchukui vijuzuu na kazi ya umishenari katika miji mingine, ambako kuna kazi nyingi za umishenari zinazopaswa kufanywa? {8T 71.2}

Maslahi mengi ambayo yameweka kituo katika Battle Creek yanapaswa kugawanywa na kugawanywa tena, na kuwekwa katika miji mingine. Ninyi mnaodhani kuwa ni watu wenye busara mnaweza kusema: "Itagharimu sana. Tunaweza kufanya kazi hapa Battle Creek kwa gharama ndogo."Sawa, Je Bwana hajui haya yote? Je! Yeye si Mungu anayeelewa hoja zote zisizokuwa za imani ambazo zimeshikilia masilahi mengi huko Battle Creek? Amewafunulia kwamba vituo vinapaswa kuwekwa katika miji yote. Hii ingewataka watu wengi kutoka Battle Creek ili kufanya kazi katika maeneo mengine. {8T 71.3}

Ili kuendelezwa mbele kwa usahihi, kazi ya umishenari wa tiba inahitaji vipaji. Inahitaji mikono yenye nguvu, iliyo tayari, pamoja na usimamizi wa busara, wenye kupambanua. Lakini je hii inawezekana wakati wale walio katika nafasi za juu - wenyeviti wa makonferensi na wachungaji - wanazuia njia? {8T 71.4}

Bwana anawaambia kwa wenyeviti wa makonferensi/majimbo na kwa ndugu wengine walio maarufu: "Ondoeni vizuizi ambavyo vimewekwa mbele ya watu." {8T 71.5}

Watu wetu huko Battle Creek hawajatumia vipaji vyao katika kupanga na kubuni jinsi ya kusimamisha bendera ya Ukweli katika maeneo ambayo ujumbe haujatangazwa na ambapo juhudi thabiti zinapaswa kufanywa; na Bwana amewasukuma Dk. Kellogg na washirika wake kufanya kazi ambayo ni ya kanisa na ambayo walipewa, lakini ambayo walichagua kutokuikubali. Baadhi katika Battle Creek, badala ya kuichukua kazi waliyopewa na Mungu, kwa kufuata njia yao wenyewe ya ubinafsi, wamepofusha macho yao ya kiroho na macho ya kiroho ya wengine; naye Mungu ameweka kazi Yake ya thamani mikononi mwa wale ambao wataichukua na kuisogeza mbele. {8T 71.6}

Mungu Yuko katika mahali Pake Patakatifu, Naye anakaa pia pamoja na yule aliye na roho ya unyenyekevu na yenye toba, ili kuhuisha roho ya unyenyekevu na kuhuisha mioyo ya wale wenye moyo uliopondeka na wa kutubu. Wale ambao wanafanya kazi ya umishenari wa tiba wanapaswa kuwa na kibali kamili na ushirikiano wa kanisa. Ikiwa hawana hivi, wanazuiliwa. Hata hivyo, watasonga mbele. Sio mpango wa Mungu kwamba kuwepo na makanisa mawili katika Battle Creek kwa sababu ya kukosekana ushirikiano. Ni bora zaidi kiasi gani kutafuta umoja katika utendaji. Ikiwa wafanyakazi wa umishenari wa tiba watachukua mwelekeo huu wa bidii katika makanisa yaliyopo kila mahali, ikiwa watafanya kazi katika hofu ya Mungu, wataona milango mingi ikifunguliwa mbele yao, na malaika watafanya kazi pamoja nao. {8T 72.1}

Tafadhali soma mwaliko wa kuja katika karamu, na wito wa mwisho kutolewa. Chunguza na kujifunza kile kinachofanyika ili kutimiza amri ya Yesu. Siwezi kuelewa

ni kwa nini kutokujali kiasi kile kunaoneshwa, kwa nini unapaswa kusimama mbali na kukosoa na kwenda mbali. Wavu wa injili unapaswa kutupwa baharini, nao utavuta wema na wabaya. Lakini je kwa kuwa hivi ndivyo ilivyo, je, wanaume na wanawake wapuuze juhudi zilizofanywa kuwaokoa wale watakaoamini na ambao wataungana kufikia tabaka lile ambalo Kristo alisema juu yake akiwakemea Mafarisayo? Wenye dhambi na makahaba, Alisema, "wanatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu." Je! hamtaona kwamba hata kanisani kuna wale ambao hawana uhusiano wowote na Mungu? Lakini Kristo anasema: Viacheni vyote [magugu na ngano] vikue hata wakati wa mavuno: na wakati wa mavuno nitawaambia wale wavunao: Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome, bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu." {8T 72.2}

Bwana anapotembea katika makanisa, akiwapa maagizo wapate kufanya kazi fulani, nao wanakataa kufanya kazi hiyo; na pale ambapo wengine, juhudi zao za kibinadamu zikiunganishwa na za Kiungu, wanajaribu kufikia kina hasa cha huzuni na mateso ya mwanadamu, baraka ya Mungu itakaa kwa wingi juu yao. Ingawa ni wachache tu wanaokubali neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, kazi yao haitakuwa bure; kwa kuwa roho moja tu ni ya thamani, ya thamani sana, mbele za Mungu. Kristo angekufa kwa ajili tu ya roho moja ili mtu huyo apate kuishi katika zama za milele. {8T 72.3}

Hebu na tujifunze sura ya kumi na nane ya Mathayo. Sura hii inapaswa kuyatia nuru macho yetu. "Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni. [Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopotea.] Mwaonaje? Mtu akiwa na kondoo mia, mmoja akampotea, je! Hawaachi wale tisa na tisini, akaenda milimani, na kumtafuta yule aliyepotea? Hata akipata kumwona, amin, nawaambia, amfurahia huyo zaidi, kuliko wale tisa na tisini wasiopotea. Vivyo hivyo haipendezi mbele za Baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa wadogo hawa apotee" Mathayo 18: 10-14. {8T 73.1}

Roho nyingi zinaokolewa, kwa kunyanguliwa kwa ghafula kutoka mikononi mwa Shetani, na wafanyakazi waaminifu. Mtu fulani lazima awe na mzigo wa roho wa kuwapata wale waliopotea kutoka kwa Kristo. Uokoaji wa roho moja ambayo Shetani amekuwa na ushindi juu yake husababisha furaha kati ya malaika wa mbinguni. Wapo wale ambao wameharibu ndani yao ile sura ya kimaadili ya Mungu. Wavu wa injili inabidi iwakusanye na kuwaleta ndani maskini hawa waliotengwa. Malaika wa Mungu watashirikiana na wale wanaojihusisha na kazi hii, ambao wanafanya kila juhudi kuziokoa roho zinazoangamia, kuwapa fursa ambazo wengi hawajawahi kuwa nazo. Hakuna njia nyingine ya kuwafikia ila kwa njia ya Kristo. Daima Yeye alifanya kazi ili kupunguza mateso na kufundisha haki. Ni kwa jinsi hiyo tu wenye dhambi wanaweza kuinuliwa kutoka katika vina vya udhilifu na maanguko ya kutisha. {8T 73.2}

Wafanyakazi ni lazima wafanye kazi kwa upendo, wakiwalisha, kuwatakasa, na kuwavika wale wanaohitaji msaada wao. Kwa njia hii watu hawa waliotengwa wanaandaliwa kujua kwamba mtu anajali kuhusu roho zao. Bwana amenionesha kuwa wengi wa hawa maskini waliotengwa kutoka kwa jamii, kupitia utendaji wa mawakala wa kibinadamu, watashirikiana na uweza wa Mwenyezi Mungu na kujitahidi kurejesha sura ya kimaadili ya Mungu kwa wengine ambao kwa ajili yao Kristo amelipa bei ya damu Yake Mwenyewe. Wataitwa wateule wa Mungu, wenye thamani, nao watasimama karibu na kiti cha enzi cha Mungu. {8T 74.1}

## Tahadhari

“Ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika Zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule Wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu.” {8T 74.2}
“Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. Lakini fahamuni neno hili; kama mwenye nyumba angaliijua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha, wala asingaliiacha nyumba Yake kuvunjwa. Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu Yuaja. Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye Bwana wake alimweka juu ya nyumba Yake, awape watu chakula kwa wakati wake? Heri mtumwa yule, ambaye Bwana Wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amin, nawaambieni, atamweka juu ya vitu Vyake vyote. Lakini mtumwa yule mbaya akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia; akaanza kuwapiga wajoli wake, na kula na kunywa pamoja na walevi; Bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wanafiki; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.” Mathayo 24:30, 31, 42-51. {8T 74.3}

Ndugu zangu, muwe waangalifu, waangalifu sana. Kuna kazi inayofanywa na wamishenari wa tiba ambayo inaitikia kwa maelezo yaliyotolewa katika aya ya 48-51. Bwana anafanya kazi kuwafikia wale ambao wameharibikiwa tabia kabisa. Wengi watajua nini maana ya kuvutwa kwa Kristo, lakini hawatakuwa na ujasiri wa kimaadili wa kupambana dhidi ya hamu ya kula na uchu. Lakini wafanyakazi hawapaswi kuvunjika moyo kwa sababu ya hili; kwa maana imeandikwa, "Nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4: 1. Je! ni wale tu waliookolewa kutoka katika vina vya chini kabisa ndio wanaorudi nyuma? Wapo wale katika huduma ambao wamepata na nuru na maarifa ya Ukweli, ambao hawatakuwa washindi. Hawazuii hamu yao ya chakula na uchu, harara, au kujikana kwa ajili ya Kristo. Watu wengi wanyonge waliotengwa, watoza ushuru na wenye dhambi, watalishikilia

tumaini lililowekwa mbele yao katika injili na wataingia katika ufalme wa mbinguni mbele ya wale ambao wamepata fursa kubwa na nuru kuu, lakini wametembea gizani. Katika siku ile kuu ya mwisho wengi watasema: "Bwana, Bwana, tufungulie." Lakini mlango utafungwa, na kubisha kwao kutakuwa bure. {8T 75.1}

Tunapaswa kuyahisi mambo haya kwa kina, kwa kuwa ni ya kweli. Tunapaswa kuwa na makadirio ya juu ya Ukweli na ya thamani ya roho. Muda ni mfupi, na kuna kazi kubwa ya kufanywa. Ikiwa hujisikii shauku kwa ajili ya kazi inayoendelea mbele, ikiwa hutaunga mkono kazi ya umishenari wa tiba katika makanisa, itafanywa bila kibali chako; kwani ni kazi ya Mungu, na hivyo ni lazima ifanyike. Ndugu na dada zangu, chukueni msimamo wenu upande wa Bwana na mwe wafanyakazi wenye ari, wenye bidii, watenda kazi wenza dhati na jasiri pamoja na Kristo, mkifanya kazi pamoja Naye kutafuta na kuwaokoa waliopotea. {8T 75.2}

## SURA YA 14
## OMBI KWA NDUGU WALIOKO BATTLE CREEK

Cooranbong, N.S.W., Juni 8, 1898.

Kwa nini, ndugu, mnaendelea kuweka masilahi mengi yakiwa yamefungiwa katika Battle Creek? Kwa nini hamsikilizi mashauri na maonyo ambayo mmepewa kuhusu jambo hili? Kwa nini hamchukui hatua za kudhamiria na wazi za kuanzisha vituo vya mvuto katika miji mikubwa mingi? Je! Ni kwanini hamziungi mkono Michigan Tract Society na International Tract Society [Mashirika ya Vijitabu vya Dini] kuanzisha ofisi zao katika miji ambayo kuna kazi nyingi za umishenari za kufanya, na ambapo makatibu wao na wafanyakazi wengine wanaweza kushiriki kila mmoja katika kazi ya umishenari, wakifanya kama viongozi katika shughuli muhimu? Tokeni nje na kwenda kazini, ndugu, tokeni na kwenda kazini, na kuwaelimisha wafanyakazi wenu kufanya kazi kwa wale ajili ya wale walioko nje ya kambi. Kwa nini mnaficha taa yenu kwa kuendelea kubaki katika Battle Creek? Nendeni nje, ndugu, nendeni katika maeneo ya ng'ambo. {8T 76.1}

Kuna kazi nyingi za kufanywa, na wafanyakazi wetu wenye uzoefu wanapaswa kujitahidi kujiweka mahali ambapo watakutana moja kwa moja na wale wanaohitaji msaada. Kwa kulinganisha wataweza kufanya kidogo tu wakiwa katika Battle Creek. Je! ni sahihi, ndugu, kwa wewe kuweka taa yako ikiwa imefichwa chini ya pishi au chini ya kitanda? Je! Si vyema zaidi kwamba ufanye kile ambacho Bwana ameonesha wazi kwamba unapaswa kukifanya? Azimu sasa kwamba utaacha

kipaumbele chako, yale unayoyapenda, na njia yako, na kwamba utatii sauti Yake. Mtafute Bwana kwa bidii kabisa, kwa maombi ya unyenyekevu, ya hamasa kwa ajili ya hekima na mafanikio katika jitihada hili. Kisha ichukue taa kutoka chini ya pishi, mbali na mahali panapoonekana kupendeza zaidi kwa ajili ya masilahi yako ya kifedha, na kutoka chini ya kitanda, mbali na mahali panapofaa kabisa kwa ajili ya raha yako  (au mahali panapowezakuwa na usumbufu) na uiweke juu ya kinara, ili iweze kutoa mwanga kwa wote walioko nyumbani. {8T 76.2}

Hali ya hatari katika juhudi za umishenari iko juu yetu. Kuna kazi kubwa ya kufanywa, na ikiwa kazi hii inafanywa kwa dhati na bidii katika Battle Creek, ikiwa itafanywa kwa uaminifu katika makanisa yote ya Michigan, ikiwa itatekelezwa kwa nguvu katika makanisa yetu yote ya zamani na ngome za mvuto, tunaweza kutumaini kwamba mvuto wake utachachua makanisa katika majimbo yote, mengi ambayo kwa sasa yanasimama kama kana kwamba yamepooza. {8T 76.3}

Taasisi ambazo Mungu amezianzisha kama vituo vya mvuto kwa ajili ya usambazaji wa nuru haziunganishi masilahi yao na kufanya kazi pamoja kama vile Mungu anavyohitaji. Wasimamizi wa taasisi hizi wanapaswa kujua kwamba kazi yao ya kwanza kabisa ni kupatana na wafanyakazi wenzao. Wachungaji wetu lazima waamke ili kuielewa hali hiyo. Injili ni uwezo utakasao katika ulimwengu wetu. Mvuto wake katika mioyo utaleta maelewano. Bendera ya Ukweli inapaswa kuinuliwa na upatanisho wa Kristo kuwasilishwa kama mada kuu, na kiini cha kuzingatiwa. {8T 77.1}

Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuwa kwa kazi ya kanisa kama mkono wa kulia ulivyo kwa mwili. Malaika wa tatu anasonga mbele akitangaza amri za Mungu na imani ya Yesu. Kazi ya umishenari wa tiba ni injili katika utendaji-injili kwa viitendo. Mielekeo yote ya kazi inapaswa kuunganishwa kwa upatanifu katika kutoa mwaliko: "Njoni; kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari." {8T 77.2}

Kwa wale walio katika Battle Creek umetolewa ujumbe kwamba wengi wanapaswa kuhamia mahali ambapo wanaweza kushiriki katika kazi hii hii kwa kuhusiana na biashara zao za maisha. Laiti kama wangeondoka kwa imani, wakiwa tayari kuvumilia kazi ya kuchosha na ufukara kwa ajili ya kazi hii, wangepata uzoefu mwingi katika mambo ya Mungu. Lakini walidhani kwamba wangepata mambo kuwa rahisi zaidi katika Battle Creek, kwamba kazi huko ingekuwa na usumbufu kidogo pale kuliko mahali pengine, na kwa hivyo walibaki. Wengi ambao wamejazana katika Battle Creek hawapati faida humo kwa sababu hawatumii maarifa wanayopokea. Hawana faida yoyote katika Battle Creek, bali wanaongeza idadi ya watu wanaohitaji uongofu. Hawana roho ya kujitoa dhabihu. Wanayo mengi yahusuyo nafsi na kidogo yamhusuyo Kristo, imani kidogo na matendo machache

mema. Wanadhani kwamba wana dini, lakini jumla yake ni sifuri tu-bure. {8T 77.3}

Mungu anazungumza nanyi katika Neno Lake, akisema: "Kwa kuwa watu hawa hunikaribia na kuniheshimu kwa vinywa vyao, bali mioyo yao wamefarakana Nami, na kicho chao walicho nacho Kwangu ni maagizo ya wanadamu waliyofundishwa; kwa sababu hiyo Mimi nitafanya tena kazi ya ajabu kati ya watu hawa, kazi ya ajabu na mwujiza; na akili za watu wao wenye akili zitapotea, na ufahamu wa wenye busara wao utafichwa." {8T 78.1}

"Na katika siku hiyo viziwi watasikia maneno ya hicho chuo, na macho ya vipofu yataona katika upofu na katika giza. Wanyenyekevu nao wataongeza furaha yao katika Bwana, na maskini katika wanadamu watafurahi katika Mtakatifu wa Israeli." Isaya 29:13, 14, 18, 19. {8T 78.2}

Ndugu zangu, Bwana amewaita ninyi muweze kufanya kazi fulani, lakini wala hamjaifanya; na mahali ambapo ulipo kuna mfarakano na malumbano na mashindano. Lakini haipaswi kuwa hivi. Mungu hakusudii kwamba wafanyakazi Wake watakaa mbali mbali kama atomu zilizojitenga. Wote wana kazi kubwa na makini ya kufanya, na inabidi ifanywe chini ya usimamizi wa Mungu. {8T 78.3}

Mungu atafanya mambo makubwa kwa watu ajili ya Wake ikiwa watashirikiana Naye. Yeye Atafanya kazi katika akili za watu, ili kwamba ipate kuonekana katika maisha yao, hata katika ulimwengu huu, utimizwaji wa ahadi ya hali ya baadaye:
"Nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi;
Jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi.
Litachanua maua mengi, na kufurahi, naam, kwa shangwe na kuimba;
Litapewa uzuri wa Lebanoni, utukufu wa Karmeli na Sharoni:
Watauona utukufu wa Bwana, Ukuu wa Mungu wetu.
Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu.

Yafanyeni imara magoti yaliyolegea.
Waambieni walio na moyo wa hofu, Jipeni moyo, msiogope:
Tazama, Mungu wenu atakuja na kisasi,
Na malipo ya Mungu;
Atakuja na kuwaokoa ninyi.
Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa,
Na masikio ya viziwi yatazibuliwa.
Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu,
Na ulimi wake aliye bubu utaimba;
Maana katika nyika maji yatabubujika;
Na vijito jangwani.
Na mchanga ung'aao mfano wa maji utakuwa ziwa la maji,

Na nchi yenye kiu itakuwa chemchemi za maji:
Katika makao ya mbweha, walipokuwa wamelala,
Patakuwa na majani, pamoja na mianzi na manyasi.
Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia,
Nayo itaitwa, Njia ya utakatifu;
Wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao [waliokombolewa]; Wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo.
Hapo hapatakuwa na simba,
Wala mnyama mkali hatapanda juu yake;
Hawataonekana hapo;
Bali waliokombolewa watakwenda katika njia hiyo:
Na hao waliokombolewa na Bwana watarudi,
Watafika Sayuni wakiimba;
Na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao:
Nao watapata kicheko na furaha,
Huzuni na kuugua zitakimbia."  Isaya 35, ARV {8T 78.4}

Jangwa lenyewe halina utukufu wala ubora, na kwa Bwana itabidi kutolewa heshima yote kwa ajili ya mabadiliko yaliyofanywa. Kazi hii kubwa ni ya Mungu. Kwa hiyo msiwatukuze watu walio chini ya utendaji maalumu wa uweza Wake. Mtukuzeni Mungu, Naye ataendelea kutenda. {8T 79.1}

Bwana ana kazi maalumu kwa watu Wake kufanya katika wakati huu. Anasema: " Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu, yafanyeni imara magoti yaliyolegea." Hii ndio kazi yenyewe ambayo mtume Paulo anayakabidhi makanisa yapate kuifanya. "Inyosheni mikono iliyolegea na magoti yaliyopooza," anasema, "mkaifanyie miguu yenu njia za kunyoka, ili kitu kilicho kiwete kisipotoshwe, bali afadhali kiponywe. 12.14 Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao; 12.15 mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo." Waebrania 12: 12-15. {8T 79.2}

Ninaomba kwamba sasa kuliko ilivyowahi kuwa, wachungaji na washiriki wa kanisa wote waweze kuja kumsaidia Bwana, kumsaidia Bwana dhidi ya nguvu za giza. Jifunze kwa maombi sura ya kumi na saba ya Yohana. Sura hii haipaswi kusomwa tu tena na tena; Ukweli wake unapaswa kuliwa, kueleweka vyema na "Kwa ajili yao," Kristo aliomba: "Najiweka wakfu mwenyewe, ili na hao watakaswe katika kweli. Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami ndani Yako; hao nao wawe ndani Yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba Wewe Ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama Sisi

tulivyo umoja. Mimi ndani yao, Bawe ndani Yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa Ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda Mimi." Yohana 17: 19-23. {8T 80.1}

Je Maneno haya, yenye umuhimu wa ajabu kiasi hiki kwetu, yapuuzwe daima? Mungu anawataka wale wanakiri kuwa watoto Wake kuyachunguza Maneno haya, kuyala, kuyaishi. Yeye Anawataka kujitahidi kuwa na umoja na upendo, vinginevyo kinara cha taa kitaondolewa kutoka mahali pake. {8T 80.2}

## SURA YA 15
## ONYO LILILOPUUZWA

St. Helena, California, Novemba, 1901.

"Angalieni, nawawekea mbele yenu hivi leo baraka na laana; baraka ni hapo mtakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wenu, niwaagizayo leo; na laana ni hapo msiposikiza maagizo ya Bwana, Mungu wenu, mkikengeuka katika njia niwaagizayo leo, kwa kuandama miungu mingine msiyoijua." Kumbukumbu la Torati 11: 26-28. {8T 81.1}

"Tena itakuwa, mtakaposikiza kwa bidii maagizo Yangu niwaagizayo leo, kwa kumpenda Bwana, Mungu wenu, na kumtumikia kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote, ndipo nitakapowapa mvua ya nchi yenu kwa wakati wake, mvua ya masika, na mvua ya vuli, upate kuvuna nafaka yako, na divai yako, na mafuta yako. Nami nitakupa nyasi katika mavue yako kulisha wanyama wako wa mifugo, nawe utakula na kushiba. Jitunzeni nafsi zenu, mioyo yenu isije ikadanganywa, mkageuka na kutumikia miungu mingine na kuiabudu; hasira za Bwana zikawaka juu yenu, Naye akafunga mbingu kusiwe na mvua, wala nchi isitoe matunda yake; mkaangamia kwa upesi mtoke katika nchi nzuri awapayo Bwana." Aya ya 18-21. {8T 81.3}

Kama Waadventista wa Sabato wangetembea katika njia ya Bwana, wakikataa

kuruhusu maslahi ya ubinafsi kuwatawala, Bwana angewabariki sana. Wale ambao wamebaki katika Battle Creek kinyume na mapenzi ya Bwana wamepoteza uzoefu wa thamani na maarifa ya kiroho ambayo wangeweza kupata kupitia kwa, kutii. Wengi wao wamepoteza fadhila za Mungu. Moyo wa kazi umesongwa. Kwa muda mrefu onyo limetolewa, lakini halijazingatiwa. Sababu ya kutokutii huku ni kwamba mioyo na akili za wengi huko Battle Creek haziko chini ya mvuto wa Roho Mtakatifu. Hawatambui ni kazi kubwa kiasi gani iko ya kufanywa. Wamelala. {8T 82.1}

Pale Waadventista wa Sabato wanapohamia miji ambako tayari kuna kanisa kubwa la waumini, wako katika mahali pasipowafaa, na hali yao ya kiroho inaendelea kuwa dhaifu na dhaifu zaidi. Watoto wao wanakabiliwa na majaribu mengi. Ndugu yangu, dada yangu, isipokuwa unahitajika kabisa katika kuendeleza kazi mahali kama hapo, itakuwa busara kwako kwenda mahali ambapo Ukweli bado haujatangazwa, na hapo jitahidi kuonesha ushahidi wa uwezo wako wa kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Fanya bidii za dhati kuamsha hamu ya ukweli wa sasa. Kazi ya nyumba kwa nyumba inafaa pale inapofanywa kwa njia inayofana na ya Kristo. Fanya mikutano, na uhakikishe kuwa ni ya kupendeza. Kumbuka kwamba hii inahitaji jambo fulani zaidi ya kuhubiri. {8T 82.2}

Wengi ambao wameishi kwa muda mrefu sana katika sehemu moja wanatumia muda wao kuwakosoa wale wanaofanya kazi katika njia za Kristo kuwasadikisha na kuwaongoa wenye dhambi. Wanakosoa nia na dhamira za wengine, kana kwamba isingewezekana kwa mtu mwingine yeyote kufanya kazi bila ubinafsi kazi ile ambayo wao wenyewe wanakataa kuifanya. Wao ni vikwazo. Kama wangeenda katika sehemu zile ambako hakuna waumini, na kufanya kazi ili kuongoa roho kwa Kristo, hivi punde wangejishughulisha na kutangaza Ukweli na kuwasaidia wanaoteseka kiasi kwamba wasingekuwa na muda wa kuchambua tabia, wasingekuwa na muda wa kufikiria uovu, kushuku wengine na kisha kuripoti matokeo ya makali ya kufikirika ya akili yao katika kuona yaliyofichika. {8T 82.3}

Hebu wale ambao wameishi kwa muda mrefu sana katika maeneo ambayo kuna makanisa makubwa ya waumini watoke kwenye shamba la mavuno kupanda na kuvuna kwa ajili ya Mwalimu. Watasahau ubinafsi kwa kupata hamu ya kuokoa roho. Wataona kazi nyingi sana za kufanya, kwani kuna wanadamu wenzao wengi sana wa kusaidiwa, kiasi kwamba hawatakuwa na muda wa kutafuta makosa ya wengine. Hawatakuwa na muda wa kufanya kazi katika upande hasi. {8T 83.1}

Kuwakusanya pamoja waumini wengi katika sehemu moja kunahimiza shuku mbaya na mazungumzo mabaya- yenye uovu. Wengi humezwa/hushugulishwa sana na kutafuta na kusikiliza uovu (busy). Wanasahau ni dhambi kubwa kiasi gani wanaifanya. Wanasahau kuwa maneno wanayoyasema hayawezi kamwe

kutanguliwa na kwamba kwa tuhuma zao wanapanda mbegu ambazo zitakua na kuzaa mavuno ya uovu. Mavuno haya ni makubwa kiasi gani hakuna mtu atakayejua mpaka siku ile kuu ya mwisho, wakati kila wazo, neno, na tendo zitakapoletwa hukumuni. {8T 83.2}

Maneno ya uzembe, yasiyo mema ambayo yanasemwa hukua kila yanaporudiwa. Mtu mmoja na mwingine anaongeza neno, hadi ripoti ya uwongo inafikia kipimo kikubwa. Udhalimu mkubwa unafanywa. Kwa tuhuma zao zisizo za haki na hukumu zisizo za haki wambea hawa hudhuru uzoefu wao wenyewe na hupanda mbegu za mfarakano kanisani. Kama wangeweza kuona mambo jinsi Mungu anavyoyaona wangebadilisha mtazamo wao. Wangeweza kutambua jinsi ambavyo wameipuuza kazi ambayo amewapa kuifanya pale ambapo wametafuta kasoro kwa ndugu na dada zao. {8T 83.3}

Muda unaotumiwa katika kukosoa nia na dhamira za watumishi wa Kristo ungeweza kutumika vizuri zaidi katika maombi. Mara nyingi kama wale wakosoaji wangelijua Ukweli juu ya wale ambao wanawakosoa, wangekuwa na mawazo tofauti kabisa juu yao. Ingekuwa bora zaidi kiasi gani ikiwa, badala ya kuwakosoa na kuwalaani wengine, kila mtu angesema: "Lazima nifanyie kazi wokovu wangu mwenyewe. Ikiwa nitashirikiana na Yeye ambaye anatamani kuiokoa roho yangu, lazima nijilinde kwa uangalifu. Lazima niondoe kila uovu maishani mwangu. Lazima niwe kiumbe kipya katika Kristo. Lazima nishinde kila kosa. Ndipo, badala ya kuwadhoofisha wale wanaopambana dhidi ya uovu, nitaweza kuwaimarisha kwa maneno yenye kutia moyo." {8T 83.4}

Hebu wale ambao wametumia kipaji cha kusema kuwakatisha tamaa na kuwavunja moyo watumishi wa Mungu, ambao wanafanya jitihada kuendeleza kusudi la Mungu, wakipanga na kufanya kazi ili kushinda kipingamizi, wamwombe Mungu apate kuwasamehe kwa ajili ya madhara ambayo wameyafanya kwa kazi Yake kwa maoni yao mabaya, ubaguzi na maneno yasiyo mema. Hebu na wafikirie ubaya ambao wameufanya kwa kueneza taarifa za uwongo, kwa kuwahukumu wale ambao hawana haki ya kuwahukumu. {8T 84.1}

Katika Neno la Mungu tumepewa maelekezo ya wazi juu ya njia ambayo tunapaswa kuufuata tunapofikiria kuwa ndugu amekosea. "Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo. La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru. Na tena Mwokozi anasema: "Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele

ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako" Mathayo 18: 15-17; 5:23, 24. {8T 84.2}

"Bwana, ni nani atakayekaa Katika hema yako? Ni nani atakayefanya maskani yake Katika kilima Chako kitakatifu? Ni mtu aendaye kwa ukamilifu, Na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake, Asiyesingizia kwa ulimi wake. Wala hakumtenda mwenziwe mabaya, Wala hakumsengenya jirani yake. Machoni pake mtu asiyefaa hudharauliwa, Bali huwaheshimu wamchao Bwana Ingawa ameapa kwa hasara yake, Hayabadili maneno yake. Hakutoa fedha yake apate kula riba, Hakutwaa rushwa amwangamize asiye na hatia. Mtu atendaye mambo hayo Hataondoshwa milele." Zaburi 15. {8T 84.3}

"Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi. Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa. Basi, mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii? Au utamwambiaje nduguyo, Niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! Mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe? Mnafiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako.” Mathayo 7: 1-5. {8T 85.1}

Mengi yanahusika katika suala la kuhukumu. Kumbuka kwamba hivi karibuni rekodi yako ya maisha itachunguzwa mbele za Mungu. Kumbuka pia kuwa Yeye amesema: “Kwa hiyo, wewe mtu uwaye yote uhukumuye, huna udhuru; kwa maana katika hayo umhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale. Nasi twajua ya kuwa hukumu ya Mungu ni ya Kweli juu yao wafanyao hayo. Wewe binadamu, uwahukumuye wale wafanyao hayo na kutenda yayo hayo mwenyewe, je! Wadhani ya kwamba utajiepusha na hukumu ya Mungu?” Warumi 2:1-3. {8T 85.2} -

Wale ambao walikuja Battle Creek wakati walikuwa na kazi ya kufanya katika kanisa ambalo walitoka, walipoteza roho yao ya umishenari roho na utambuzi wao wa kiroho kwa kuja kwao katika Battle Creek. Hapo walikutana na ufarisayo, kujihesabia haki, ambazo daima ni mtego. Ni mfano wa utauwa bila kuwa na uwezo wake. {8T 85.3}

Nguvu ya Ukweli itakapofurahiwa na kuhisiwa moyoni, kanuni za Ukweli zitakapoletwa katika maisha ya kila siku, kutakuwapo na msukumo mkubwa wa matengenezo katika kanisa la Battle Creek. Punde yatatimizwa Maneno: "Nitageuza na kuangusha." Sasa hatujui ni lini hasa hili litatimizwa, lakini wakati utafika ambapo kutakuwa na kutawanyika kutoka Battle Creek. Wale ambao walihamia Battle Creek bila wito wowote kutoka kwa Bwana wataondoka. - {8T 86.1}

Wafanyakazi waaminifu hawana muda wa kufikiri sana juu ya kasoro za wengine. Wanamwangalia Mwokozi, na kwa kutazama wanabadilishwa kufanana Naye. Yeye Ndiye ambaye mfano Wake tunapaswa kuufuata katika kujenga tabia zetu. Katika maisha Yake duniani alionesha wazi wazi asili ya Kiungu. Tunapaswa kujitahidi kuwa wakamilifu katika mazingira yetu, kama alivyokuwa mkamilifu katika mazingira Yake. Washiriki wa kanisa hawapaswi tena kubaki kuwa wasiojali kuhusu ujenzi wa tabia sahihi. Kwa kujiweka chini ya uumbaji wa Roho Mtakatifu, wanapaswa kutengeneza tabia ambazo ni zinaakisi tabia ya Kiungu. {8T 86.2}

## SURA YA 16
## MATOKEO YA MATENGENEZO

St. Helena, California, Septemba 26, 1901.

Ndugu Ndugu Daniells: Jana asubuhi nilisoma barua yako, ambamo ndani yake unaelezea hamu yako kubwa ya kuona majeshi yenye nguvu ya watendakazi wakitumwa kwenda India na China na nchi zingine za Mashariki (Oriental countries ni nchi 48 hivi kama vile China, Japan, Indonesia, Thailand, Vietnam ). Usiku wa jana maagizo yalitolewa kwangu kwamba kwa sasa juhudi zetu kuu hazipaswi kufanywa hasa kwa ajili ya China au maeneo mengine yaliyo huko Mashariki ya Mbali. Kwanza tuna kazi ya kufanya nyumbani. Taasisi zetu zote –vituo vyetu vya afya na maisha bora, nyumba za uchapaji, na shule - zinapaswa kufikia kiwango cha juu. Kisha watendakazi wanaotumwa kwenye uwanja wa kigeni watafikia kiwango cha juu zaidi. Watakuwa watendakazi dhati, wenye bidii zaidi, na wa kiroho zaidi, na kazi zao zitakuwa na nguvu zaidi. {8T
87.1}

Miaka kadhaa iliyopita Bwana alinipa maagizo maalumu kwamba majengo yanapaswa kujengwa katika maeneo mbalimbali ya huko Marekani, Ulaya, na nchi

zingine kwa uchapishaji wa vitabu mbalimbali vyenye nuru ya Ukweli wa sasa. Yeye Alitoa maelekezo kwamba kila juhudi inapaswa kufanywa katika kutuma ulimwenguni kutoka katika mitambo ya uchapaji ujumbe wa mwaliko na wa onyo. Baadhi watafikiwa na machapisho yetu ambao wasingefikiwa kwa njia nyingine yoyote. Kutoka katika vitabu vyetu na makaratasi miali angavu inapaswa kuangaza ili kuutia nuru ulimwengu kwa Ukweli wa sasa. {8T 87.2}

Watendakazi ambao hawafaidiki na faida zinazopatikana kuhusiana na kusudi la Mungu hawapaswi kuletwa katika ofisi zetu za uchapishaji. Wala suala lenye sifa bainifu ya kuchukiza kuletwa katika taasisi hizi, kwa kuwa kwa kufanya hivyo Ukweli wa Mungu ulio mtakatifu unawekwa katika daraja sawa na mambo ya kawaida. Na pale kazi za nje zinapoletwa, idadi kubwa ya wafanyakazi lazima waajiriwe kulingana na kazi. Hii inaleta usumbufu na mfadhaiko. {8T 87.3}

Nimeoneshwa kuwa makosa yanafanyika katika nyumba zetu za uchapaji. Daima kuna ongezeko la mitambo ya bei kubwa kwa ajili ya kufanya kazi za kibiashara. Kiasi kikubwa cha kazi kimeletwa ambacho hakina uhusiano wowote na kazi ambayo kwa imani na upendo inapaswa kutekelezwa kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Muda na vipaji vimetumika katika kufanya tabaka la kazi ambalo halijaleta utukufu kwa Mungu. Jitihada nyingi zimefanywa katika mielekeo ambayo haifanyi chochote katika kueneza ujuzi wa Ukweli. {8T 88.1}

Ni wakati muafaka wa kulizingatia jambo hili. Kosa hili lazima lisahihishwe. Si hekima kutumia fedha kuanzisha shughuli ambazo zinatumia bila kuzalisha. Inasemekana kwamba nafasi zaidi inahitajika katika nyumba za uchapaji. Lakini kuna nafasi ya kutosha ndani yao, na pale marekebisho sahihi yatakapofanyika, itaonekana kuwa kuna nafasi ya kutosha. {8T 88.2}

Kazi chache sana za kibiashara zinapaswa kupokelewa katika ofisi zetu za uchapishaji, na msitari hata mmoja wa mambo yenye mawazo ya Shetani haipaswi kupokelewa. Uingizaji wa jambo kama hilo huharibu dhana yote ya utakatifu wa taasisi hiyo. Taasisi nzima inahafifishwa. Kuna hatari siku zote, pale mambo ya kawaida yanapochanganywa na yale yaliyo matakatifu, kwamba yale ya kawaida yataruhusiwa kuchukua nafasi ya matakatifu. {8T 88.3}

Je! Bwana anaangaliaje utumiaji wa mitambo ya uchapishaji katika taasisi Zake kuchapisha makosa ya adui? Wakati jambo la kuchukiza linapochanganywa na jambo takatifu kutoka katika mitambo ya uchapaji, baraka Yake haiwezi kukaa juu ya kazi iliyofanywa. Mwalimu wa Kiungu akasema: "Mmepata nini kwa kuleta kazi hii ya nje? Imewaletea machukizo mengi za roho; na wafanyakazi wamelazimika kuharakisha na kuchapisha bila kujali usahihi ili kumaliza jambo kwa muda

uliowekwa. Hii imesababisha mchafuko na migongano. Maneno makali yamezungumzwa, na roho mbaya imeletwa ofisini. Faida ya fedha iliyopatikana, hakika hailinganishwi na hasara ambayo imetokana na kuharakisha watu, kusukuma watu kama mnyapara,  kufanya kazi sana na kukaripia na kuudhika." {8T 88.4}

Bwana awasaidie watu Wake kuona kwamba hii si hekima na kwamba mengi yanapotezwa kuliko kupatikana. Kama miundombinu na mitambo kidogo na wafanyakazi wachache wangekusanywa pamoja mahali pamoja wakati sehemu zingine za shamba la mizabibu zinakosa vifaa na miundombinu; kama fedha nyingi zingetumika kutengeneza miundombinu katika maeneo mbalimbali, Mungu angefurahi zaidi. Si lengo lililotakaswa la kujitakia makuu kwa namna, kwa kujiongoza katika uwekezaji wa fedha nyingi katika sehemu moja. Ni kosa kwa ndugu zetu kusimamia vituo vingi vya uchapaji kwa ajili ya kuchapisha mambo ya kidunia tu. Tunaukaribia mwisho kwa haraka. Uchapishaji na usambazaji wa vitabu na karatasi zilizo na Ukweli wa sasa unapaswa kuwa ndio kazi yetu. {8T 89.1}

Kuna kupuuzwa dhahiri kwa tahadhari na maonyo ambayo yametolewa mara kwa mara. Pale ambapo kuna kumtafuta Bwana na kuungama dhambi, wakati matengenezo yanayohitajika yanafanyika, moyo wa pamoja na bidii itaoneshwa katika kurudisha kile kilichozuiwa. Bwana atadhihirisha upendo Wake wa kusamehe, na fedha itakuja kufuta madeni katika taasisi zetu. {8T 89.2}

## SURA YA 17
## ONYO MAKINI (MAZITO)

*(Soma Kwa Mapitio Na Bodi Ya Herald Novemba, 1901.]*

Kwa Wasimamizi wa Review and Herald

Ndugu Wapendwa: Kusudi la Mungu katika kuanzishwa kwa nyumba ya uchapaji huko Battle Creek ilikuwa kwamba kutoka kwake nuru inapate kuangaza kama taa inayowaka. Hili limewekwa mbele ya wasimamizi. Tena na tena wameambiwa juu ya utakatifu wa ofisi ya Mungu ya uchapishaji na umuhimu wa kudumisha usafi wake. Lakini wamepoteza ufahamu wa Kweli nao wameungana na jitihada za adui kwa kukubali kuchapisha makala na vitabu vyenye makosa hatari zaidi ambayo yanaweza kuweko. Wameshindwa kuona mvuto mbaya wa mawazo kama hayo yenye makosa juu ya wapangaji wa chapa, wasahihishaji wa makosa, na wengine wote wanaohusika na uchapishaji wa jambo kama hilo. Wamekuwa wamesinzia kiroho. {8T 90.1}

Kwa baadhi ya kazi za nje zilizoletwa katika taasisi hii sayansi ya Shetani imewasilishwa katika akili za watendakazi. Kuchapishwa kwa jambo kama hilo ni aibu kwa Mungu. Imefanya sehemu yake katika kuharibu/ kufifisha akili za wafanyakazi. Wasimamizi wamekubali kuyachapisha kwa kiwango cha chini. Faida ingekuwa ni hasara ikiwa kiwango cha juu kabisa ingetakiwa kwa ajili ya kazi hiyo. {8T 90.2}

Nimepokea barua kutoka kwa Mchungaji Daniells kuhusu kuongezwa kwa jengo lingine katika ofisi ya Review and Herald. Jibu ninalolitoa kwa ajili ya jambo hili ni: Hapana, hapana, hapana. Badala ya kufanya ongezeko lolote kwenye majengo yaliyokwisha kusimamishwa, safisha ofisi kutokana na takataka zenye asili ya kishetani, nanyi mtapata nafasi kwa kila mahali. {8T 90.3}

Mungu hafurahishwi na hali ya msongamano wa vitu huko Battle Creek. Ikiwa wafanyakazi wangegawanywa na kiwanda cha uchapishaji kingejengwa katika maeneo mengine, Mungu angependezwa zaidi, na bendera ya Ukweli ingepandishwa katika maeneo ambayo hayajawahi kusikia ujumbe. Kabla hamjaongeza jengo lingine katika ofisi huko Battle Creek, fanya marejesho kamili kwa ajili ya eneo la Kusini (Southern Field+. Hili bado halijafanyika hivyo, kama inapaswa kufanyika. Kila hatua imefanywa kwa kujilazimisha. {8T 90.4}

Dola elfu tano ambazo zingetumika katika nyongeza kwenye majengo ya Review and Herald sasa zinapaswa kuwekezwa katika kazi katika maeneo mengine ambayo injili ya Ukweli bado haijahubiriwa. {8T 91.1}

Ninahisi ogofyo la roho wakati ninapoona ni mashaka ya jinsi gani nyumba yetu ya uchapishaji imepitia. Mitambo ya uchapaji katika taasisi ya Bwana wamekuwa wakichapisha nadharia zinazoangamiza roho za Kanisa la Rumi/Romanism na siri zingine za uovu. Ofisi inapaswa kusafishwa kwa jambo hili la kuchukiza. Ninao ushuhuda kutoka kwa Bwana kwa wale ambao wameweka maandishi kama hayo mikononi mwa wafanyakazi. Mungu anawawajibisha kwa kuwasilisha kwa vijana wa kiume na wa kike matunda ya mti uliokatazwa wa ujuzi wa mema na mabaya. Je! Inawezekana kuwa ninyi hamna habari za maonyo yaliyotolewa kwa Pacific Press juu ya mada hii? Je! Inawezekanakweli kuwa pamoja na ufahamu wa maonyo haya mnapita kwenye uwanja ule ule, huku mkifanya tu vibaya zaidi? Imerudiwa kwenu mara nyingi kwamba malaika wa Mungu wanapitia katika kila chumba hapo ofisini. Je! Hii imefanya picha gani akilini mwenu? {8T 91.2}

Mmetoa maandishi yenye mawazo ya Shetani mikononi mwa wafanyakazi, mkileta kanuni zake za udanganyifu, na zenye kuchafua mbele ya akili zao. Bwana anaangalia tendo hili kwa upande wenu kama kumsaidia Shetani kuandaa mtego wake ili kuzinasa roho. Mungu hatawahesabia kuwa hawana hatia wale ambao wamelifanya jambo hili. Ana majadiliano na wasimamizi wa nyumba ya uchapishaji.

Nimekuwa ninaogopa hata kufungua gazeti la Review, nisije nikaona kwamba Mungu ameitakasa nyumba ya uchapaji kwa moto. 92 {8T 91.3}

Bwana ameniagiza kwamba wale ambao hawawezi kuona uovu wa kushirikiana na Shetani kwa kuchapisha uongo wake ingekuwa bora watafute kazi ambayo haitawaharibu vijana wetu, mwili na roho. Kuna hatari kwamba kiwango cha ukweli na haki vitashushwa kiasi kwamba Mungu ataleta hukumu Zake juu ya wakosaji. {8T 92.1}

Hakika muda umefika sasa ambapo tunapaswa kuelewa ni roho gani imekuwa ikitawala mambo kwa miaka mingi katika ofisi ya Review na Herald. Ninatishika kufikiria kwamba sura iliyo ngumu kabisa kutambua ya umizimu inawekwa mbele ya wafanyakazi, na kwamba inafanywa kwa jinsi ambayo imekusudiwa kuchanganya na kutatanisha akili. Muwe na hakika kwamba Shetani atafuatilia faida aliyopewa jinsi hiyo. {8T 92.2}

Ofisi ya Review na Herald imenajisiwa kama hekalu lilivyonajisiwa, ila tu matokeo yake ndio yamekuwa mabaya na ya kuogofya zaidi mara kumi. Akipindua meza za wabadilisha pesa, Kristo aliwafukuza kondoo na ng'ombe kutoka katika viunga vya hekalu, akisema: "Imeandikwa, Nyumba Yangu itaitwa nyumba ya sala; lakini nyinyi mmeifanya kuwa pango la wezi." Mathayo 21:13. Mbaya hata kuliko kulinajisi hekalu imekuwa ni kuinajisi nyumba ya uchapaji kwa uchapishaji wa maandishi ambayo kamwe hayakupaswa kuwekwa mikononi mwa wafanyakazi katika taasisi ya Mungu. {8T 92.3}

Sheria ya Mungu imevunjwa, kusudi Lake limesalitiwa, na taasisi yake kufanywa kuwa pango la wanyang’anyi. Kazi ya kuchapa na kusambaza wito wa kusisimua wa Ukweli, ambayo ilipaswa kufanywa kuwa ya kwanza, ambayo kwayo muda na vipaji vya wafanyakazi vingetengwa, imezingatiwa kidogo au kutokuzingatiwa kabisa. Kazi za biashara, ambazo baadhi yake ni ya kuchukiza kabisa, kidogo kidogo zimechukua mamlaka ya juu kabisa. Kazi hii imeshughulisha nguvu ambazo zilipaswa kutengwa kwa ajili ya uchapishaji wa machapisho yenye sifa safi kabisa na yenye tabia yenye kuinua kabisa. Muda umepotezwa, vipaji vimetumika vibaya, na fedha zimetumika vibaya. Kazi ambayo ilipaswa kuwa imefanyika imeachwa bila kufanywa. Mawazo ya Shetani yameinuliwa. Nadharia zake zimechapishwa na mitambo ambayo ilipaswa kutumika katika kuandaa Ukweli wa Mungu kwa ajili ya usambazaji. Watu wametamani kupandishwa vyeo wakati ambapo kanuni zao zilikuwa chini ya marufuku ya chuki ya Mungu. Hasara ni bora kabisa kuliko faida ya kufedhehesha. {8T 92.4}

Mungu atafanya nini na wanafiki? Watumishi wa mshahara wanaoutumikia muda na

si Bwana tena. Je mnadhani kuwa Yesu atasimama katika idara ya uchapishaji, kufanya kazi katika akili za wanadamu na malaika Zake wanaohudumu, ili kuufanya Ukweli unaotoka katika mitambo ya uchapaji kuwa nguvu ya kuuonya ulimwengu kuwa mwisho wa vitu vyote umekaribia, wakati Shetani anaruhusiwa kupotosha akili za wafanyakazi katika taasisi hiyo? Nuru niliyo nayo ni: Kataa kuchapisha msitari mwingine wa maandishi haya yenye madhara ya kufisha. Wale ambao wamehusika na kuletwa kwake katika nyumba ya uchapishaji wanahitajika kutubu mbele za Mungu kwa roho yenye kujuta, kwa kuwa ghadhabu Yake imewaka juu yao. Hebu kazi za namna zizuiliwe milele kuingia kwenye nyumba zetu za uchapishaji. Toa muda zaidi kwa ajili ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu vyenye Ukweli wa sasa. Hakikisha kwamba kazi yako katika mwelekeo huu inafikia ukamilifu. Fanya yote yaliyo katika uwezo wako ili kueneza nuru ya mbinguni kote ulimwenguni. {8T 93.1}

Wanafunzi wanaoijifunza kazi ya uchapaji (apprentice) na watendakazi wengine hawapaswi kukurupushwa na kuharakishwa sana kiasi kwamba wanakosa muda wa kuomba. Vijana katika nyumba zetu za uchapishaji wanapaswa kuelimishwa kama vijana waliokuwa katika shule za manabii walivyoelimishwa. Inabidi waandaliwe kwa ajili ya kuanzisha kazi katika maeneo mapya. {8T 93.2}

Ikiwa watu waliosikia ujumbe uliotolewa wakati wa Mkutano - ujumbe mzito kabisa ambao ungeweza kutolewa - wasingekuwa wasiovutiwa au kuguswa moyo kiasi kile, ikiwa kwa dhati na uaminifu wangeomba, "Bwana, unataka nifanye nini?" uzoefu wa mwaka uliopita ungekuwa tofauti sana na jinsi ulivyo. Lakini hawajaacha alama safi nyuma yao. Hawajaungama makosa yao, na sasa wanapita kwenye uwanja ule ule katika mambo mengi, wakifuata njia ile ile mbaya ya utendaji, kwa sababu wameharibu macho yao ya kiroho. {8T 93.3}

Ujumbe wa malaika wa tatu unapaswa kuwaandaa watu kusimama katika siku hizi za hatari. Inabidi utangazwe kwa sauti kubwa na unapaswa kukamilisha kazi ambayo ni wachache tu wanaitambua. {8T 94.1}

Yohana anaandika: "Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji. Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Ufunuo 14: 6-8. Je, hili linafanyikaje? Kwa kuwalazimisha watu kukubali sabato ya uongo. Katika sura ya thelathini na moja ya Kutoka tunaambiwa wazi siku gani ni Sabato ya Bwana. Utunzaji wa Sabato unatangazwa kuwa ishara ya uaminifu wa watu wa Mungu. {8T

94.2}

Mungu anamaanisha hasa kile anachosema. Mtu ameingilia kati ya Mungu na watu, na Bwana amemtuma malaika wa tatu na ujumbe: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira Yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo." Aya ya 9, 10. {8T 94.3}

Watu wa Mungu wanapaswa kuzitunza amri Zake, wakiacha sera zote za ulimwengu. Wakiisha kuzikubali kanuni sahihi za utendaji, wanapaswa kuziheshimu sana kanuni hizi; kwa kuwa ni za kutoka mbinguni. Utii kwa Mungu ni wa thamani kwako kuliko dhahabu au fedha. Kufungiwa nira pamoja na Kristo, kujifunza upole na unyenyekevu Wake, hupunguza migogoro mingi; Maana adui anapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana huinua bendera dhidi yake. {8T
95.1}

Ninawahutubia wale ambao kwa kukubali nafasi za dhamana katika nyumba ya uchapishaji wamechukua juu yao wenyewe jukumu la kuona kuwa wafanyakazi wanapata elimu sahihi. Jitahidini kutambua umuhimu wa kazi yenu. Wale ambao wanaonesha kwa matendo yao kuwa hawafanyi juhudi yoyote ya kutofautisha kati ya vitakatifu na vya kawaida wanaweza kujua kwamba, isipokuwa wametubu, hukumu za Mungu zitawaangukia. Hukumu hizi zinaweza kucheleweshwa, lakini zitakuja. Ikiwa, kwa sababu akili zenu wenyewe si timamu na yenye kuinuliwa, mnatoa athari mbaya na ubaguzi kwa akili zingine, Mungu atakutaka utoe hesabu. Atauliza: "Kwa nini ulifanya kazi ya mwovu wakati ulipaswa kufanya kazi nzuri kwa Bwana?" {8T 95.2}

Katika siku ile kuu ya kutoa hesabu za mwisho mtumishi asiye mwaminifu atakutana na matokeo ya kutokuwa mwaminifu kwake. {8T 95.3}

Ninawatumia hii kwa sababu nina hofu juu yenu. Nguvu yenu ya wafanyakazi inayoongezeka daima ingeweza kutumwa kazini katika maeneo mengine. Katika nyakati za usiku nimekuwa nikiongea nanyi kwa dhati katika mikutano yenu, nikionesha Ukweli kama ulivyo katika Yesu. Lakini baadhi waliukataa. Walikuwa wamevuka uwezo wa kusadikishwa. Walikuwa wamefanya dhambi dhidi ya nuru kuu na ufahamu, wakiikaba pumzi dhamiri yao hadi isingeweza tena kuupenya moyo mgumu. {8T 95.4}

Wengine kwa muda mrefu sana wametoa kafara kanuni kiasi kwamba hawawezi kuona tofauti kati ya vitakatifu na vile vya kawaida. Wale ambao wanakataa kutii maagizo ya Bwana watashuka chini kwa kasi katika njia ya uharibifu. Siku ya kupimwa na ya jaribio iko mbele yetu. Hebu kila mtu oneshe tabia yake ya kweli. Je!

Wewe unachagua uaminifu au uasi? Onesha tabia zenu kama zilivyo kikweli kwa watu na kwa malaika. Tuko salama pale tu tunapojitoa kwa ajili ya haki. Ndipo ulimwengu unapojua ni wapi tutakapopatikana katika siku ile ya majaribio na shida. {8T 96.1}

Kama kazi ile iliyoanzishwa katika Konferensi Kuu (GC) ingeliendelezwa kufikia ukamilifu, nisingeliitwa kuandika maneno haya. Kulikuwako na fursa ya kuungama au kukataa makosa, na katika hali nyingi kukataa kulikuja ili kuepusha matokeo ya ungamo. {8T 96.2}

Isipokuwa kuna matengenezo, msiba mkubwa utaikumba nyumba ya uchapishaji, na ulimwengu utajua sababu. Nimeoneshwa kuwa hakujatokea kumgeukia Mungu kwa kusudi kamili la moyo. Bwana anafedheheshwa katika taasisi zilizowekwa kwa ajili ya heshima Yake. Dharau ya wazi kwa amri za Mungu katika nyumba ya uchapishaji imeweka alama yake juu ya wafanyakazi. Mungu anauliza: "Je! Sitahukumu kwa sababu ya mambo haya?" Niliwaona malaika wa mbinguni wakigeuka kwa nyuso zenye huzuni. Mungu amedhihakiwa kwa ugumu wenu wa moyo, ambao unaendelea kuongezeka daima. Kulingana na wajibu wao itakuwa adhabu ya wale ambao wanaujua Ukweli lakini bado wanadharau amri za Mungu. {8T 96.3}

## SURA YA 18
## MOTO WA REVIEW AND HERALD

St. Helena, California, Januari 5, 1903.

Kwa Ndugu mlioko Battle Creek

Leo nilipokea barua kutoka kwa Mchungaji Daniells kuhusu kuharibiwa kwa ofisi ya Review kwa moto. Ninahisi huzuni sana ninapofikiria hasara kubwa kwa lile kusudi kubwa la Mungu. Ninajua kwamba huu lazima utakuwa ni wakati wa jaribio kubwa sana kwa ndugu wanaosimamia kazi na kwa watendakazi wa ofisi. Ninateseka

pamoja na wale wote wanaoteseka. Lakini sikushangazwa na habari hiyo ya kusikitisha, kwani katika maono ya usiku nimemwona malaika amesimama na upanga kama wa moto ulionyoshwa juu ya Battle Creek. Mara moja, wakati wa mchana, nikiwa na kalamu yangu mkononi, nilipoteza fahamu, na ilionekana kana kwamba upanga huu wa moto ulikuwa ukigeuka kwanza upande mmoja na kisha upande mwingine. Maafa yalionekana kufuata maafa kwa sababu Mungu alifedheheshwa na mpango wa wanadamu kujiinua na kujitukuza wao wenyewe. {8T 97.1}

Asubuhi ya leo nilivutwa kwa maombi ya dhati kwamba Bwana awaongoze wote wanaohusika na ofisi ya Review and Herald watafute kwa uadilifu na bidii, ili wapate kuona ni katika nini wamepuuza ujumbe mwingi ambao Mungu ameutoa. {8T 97.2}

Muda fulani uliopita ndugu katika ofisi ya Review waliomba ushauri wangu kuhusu ujenzi wa jengo lingine. Ndipo nilisema kwamba ikiwa wale waliokuwa wanaunga mkono kuongezwa kwa jengo lingine katika ofisi ya Review na Herald wangeona ramani ya siku za usoni mbele yao, ikiwa wangeweza kuona kile ambacho kingetokea katika Battle Creek, wasingekuwa na hoja juu ya kuweka jengo lingine pale. Mungu alisema: "Neno Langu limedharauliwa; Nami nitageuza na kuangusha." {8T 97.3}

Katika Mkutano Mkuu, uliofanyika Battle Creek mnamo 1901, Bwana aliwapa watu Wake ushahidi kwamba alikuwa akitaka matengenezo na kutoa wito kwa hili. Akili zilisadikishwa, na mioyo iliguswa; lakini kazi kamili haikufanywa. Iwapo mioyo migumu na yenye ukaidi ingevunjika wakati ule kwa toba mbele za Mungu, kungeonekana mojawapo ya maonesho makubwa kabisa ya uweza wa Mungu ambao umewahi kuonekana. Lakini Mungu hakuheshimiwa. Ushuhuda wa Roho Wake haukuzingatiwa. Watu hawakujitenga kutoka katika mazoea ambayo yalikuwa katika upinzani thabiti na kanuni za Ukweli na haki, ambazo zinapaswa kudumishwa katika kazi ya Bwana. {8T 97.4}

Ujumbe kwa kanisa la Efeso na kwa kanisa la Sardi mara nyingi umerudiwa kwangu na Yule anayenipa maagizo kwa watu Wake. " Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso andika; Haya ndiyo anenayo Yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono Wake wa kuume, yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu. Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo; tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya Jina Langu, wala hukuchoka. Lakini Nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, Naja kwako, Nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu." Ufunuo 2: 1-5. {8T 98.1}

"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi andika: "Haya ndiyo anenayo Yeye aliye na

hizo Roho saba za Mungu, na zile nyota saba. Nayajua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa. Uwe mwenye kukesha, ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa. Maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu Wangu. Basi kumbuka jinsi ulivyopokea na jinsi ulivyosikia; yashike hayo na kutubu. Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako." Ufunuo 3: 1-3. {8T 98.2}

Tunaona kutimizwa kwa maonyo haya. Kamwe Maandiko hayajawahi kutimizwa kinagaubaga kabisa kama ambavyo haya yametimizwa. {8T 99.1}

Watu wanaweza kusimamisha majengo yaliyojengwa kwa uangalifu, yasiyoshika moto, lakini mguso mmoja wa mkono wa Mungu, cheche moja kutoka mbinguni, itafutilia mbali kila kimbilio. {8T 99.2}

Imeulizwa ikiwa nina ushauri wowote wa kutoa. Tayari nimekwisha kutoa ushauri ambao Mungu amenipa, nikitumaini kuzuia kuanguka kwa upanga wa moto uliokuwa ukining'inia juu ya Battle Creek. Sasa kwa kuwa kile nilichokiogopa kimekuja - habari ya kuungua kwa jengo la Review and Herald. Wakati habari hii ilipokuja, sikushangaa hata kidogo, na sikuwa na maneno ya kusema. Kile ambacho nililazimika kusema mara kwa mara katika maonyo hakikuwa na matokeo yoyote isipokuwa kuwafanya kuwa sugu wale waliosikia, na sasa naweza tu kusema: Ninasikitika, ninasikitika sana, kwamba ilikuwa ni lazima kwa pigo hili kuja. Nuru ya kutosha imetolewa. Kama ingefanyiwa kazi, nuru zaidi isingelihitajika. {8T 99.3}

Kwa watu wetu, wachungaji na washiriki wa kawaida yaani walei, nimeagizwa kusema: "Mtafuteni Bwana, maadamu anapatikana, Mwiteni, maadamu Yu karibu; Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana," –kwa kuwa wachungaji wengi na washiriki wanatembea katika njia ngeni – "Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa." Isaya 55: 6, 7. {8T 99.4}

Hebu kila nafsi iwe na tahadhari. Adui anafuatilia nyayo zenu safarini. Kuwa macho, ukikesha kwa bidii usije mtego uliofichwa kwa uangalifu na werevu ukawanasa bila kutarajia. Hebu wale walio wazembe na wasiojali wajihadhari siku ya Bwana isije ikawajia kama mwizi ajavyo usiku. Wengi watatanga kutoka katika njia ya unyenyekevu, na, wakiweka kando nira ya Kristo, watatembea katika njia ngeni. Wakiwa wamepofushwa na kufadhaishwa, wataacha njia nyembamba inayoelekea kwenye mji wa Mungu. {8T 99.5}

Mtu hawezi kuwa Mkristo mwenye furaha isipokuwa yeye ni Mkristo anayekesha. Yeye ashindaye ni lazima akeshe; kwa kuwa, pamoja na matatizo ya ulimwengu, makosa, na ushirikina, Shetani anajitahidi kuwavuta wafuasi wa Kristo kutoka Kwake. Haitoshi kwamba tunaepuka hatari za wazi na matendo ya hatari, yanayokinzana. Tunapaswa kukaa karibu na upande wa Kristo, tukitembea katika

njia ya kujikana na kujitoa. Tuko katika nchi ya adui. Yeye aliyefukuzwa kutoka mbinguni ameshuka chini akiwa na nguvu kubwa. Kwa kila mbinu inayowezekana na hila, adui anajitahidi kuzitia roho utumwani. Isipokuwa tumekuwa macho kila wakati tutakuwa windo rahisi kwa udanganyifu wake usiohesabika-usio na idadi. {8T 100.1}

Uzoefu wa wanafunzi katika Bustani ya Gethsemane una somo kwa watu wa Bwana leo. Akiwachukua Petro na Yakobo na Yohana, Kristo alikwenda Gethsemane kuomba. Aliwaambia: "Roho Yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa: kaeni hapa mkeshe. Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akiomba ya kuwa, ikiwezekana, saa hiyo imwepuke. Akasema, Aba, Baba, yote yawezekana Kwako; uniondolee kikombe hiki; walakini, si kama nitakavyo Mimi, bali utakavyo Wewe. Akaja akawakuta wamelala usingizi, akamwambia Petro, Je! Simoni, umelala? Hukuweza kukesha saa moja? Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni, roho i radhi ila mwili ni dhaifu." Marko 14: 34-38. {8T 100.2}

Soma Maneno haya kwa uangalifu. Wengi leo wamelala usingizi, kama walivyokuwa wanafunzi. Hawakeshi na kuomba wasije wakaingia katika majaribu. Hebu tusome na kujifunza sehemu hizo za Neno la Mungu ambazo zina marejeleo ya pekee kwa ajili ya siku hizi za mwisho, zikionesha hatari ambazo zitaelekea kuleta vitisho kwa watu wa Mungu. {8T 100.3}

Tunahitaji utambuzi wenye kupenya ndani, uliotakaswa. Utambuzi huu haupaswi kutumika katika kukosoana na kulaumiana, bali katika kuona alama za nyakati. Tunapaswa kutunza mioyo yetu kwa uangalifu wote, ili tusije tukaiangamiza imani. Wengi ambao hapo awali walikuwa waumini thabiti wa Kweli wamekuwa wazembe kuhusiana na ustawi wao wa kiroho na wanakubali kushindwa, bila upinzani hata kidogo, na njama za Shetani zilizopangwa vizuri. Ni wakati ambapo watu wetu wanapaswa kuchukua familia zao kutoka mijini kwenda katika maeneo mahalia yaliyojitenga zaidi, vinginevyo vijana wengi, na wengi pia wa wale walio wazee kwa miaka, watanaswa na kuchukuliwa na adui. {8T 101.1}

Januari 7, 1903.

Sote tumesikitishwa sana na habari ya hasara mbaya ambao imeijia kusudi la kazi, ile ya kuteketezwa kwa ofisi ya Review and Herald. Katika mwaka mmoja taasisi zetu mbili kubwa zimeharibiwa na moto. Habari za janga hili la hivi karibuni zimetusababisha kuomboleza sana, lakini liliruhusiwa na Bwana kuja juu yetu, na hatupaswi kulalamika, bali tujifunze kutoka kwa hilo somo ambalo Bwana angependa kutufundisha. {8T 101.2}

Maangamizo ya jengo la Review and Herald hayapaswi kupitwa kama kitu ambacho ndani yake hakuna maana. Kila mtu aliye na uhusiano na ofisi hii anapaswa kujiuliza: "Je! ni katika nini ninastahili kupata somo hili? Je! ni katika nini nimetembea kinyume na 'Bwana asema,' kiasi kwamba inabidi alitume somo hili kwangu? Je! Nimejali maonyo na makaripio ambayo Ameyatuma, au nimefuata njia yangu

mwenyewe?" {8T 101.3}

Hebu mruhusu Mungu anayechunguza moyo awakemee wakosaji, na kila mmoja ainame mbele Yake kwa unyenyekevu na toba, akiweka kando kujihesabia haki kote na majivuno yote, akiungama na kuacha kila dhambi, na kumwomba Mungu msamaha, kwa Jina la Mkombozi. Mungu anatangaza, "Yeyote ajaye Kwangu sitamtupa nje kamwe" (Yohana 6:37); na wale ambao kwa dhati wanaojihudhurisha mbele Yake watasamehewa na kuhesabiwa haki, nao watapokea uwezo wa kuwa wana wa Mungu. {8T 101.4}

Ninaomba kwamba wale ambao wameipinga nuru na ushahidi, wakikataa kusikiliza maonyo ya Mungu, wataona katika uharibifu wa ofisi ya Review and Herald wito kwao wa kumrudia Mungu kwa kusudi kamili la moyo. Je! Hawatatambua kwamba Mungu Yuko wazi na dhati ajili yao? Yeye anaposhugulika na mwanadamu, Hatafuti kuharibu maisha, bali kuyaokoa maisha. Katika uharibifu wa hivi karibuni maisha ya watendakazi yalihifadhiwa kwa neema, ili wote wapate fursa ya kuona kwamba Mungu alikuwa akiwasahihisha kwa ujumbe ambao haukutoka katika chanzo cha kibinadamu, bali kutoka juu. Watu wa Mungu wamemwacha; hawakufuata agizo Lake, Naye amewakaribia kwa kuwarekebisha. Lakini Yeye hajaleta ukomeshaji wa uhai-hajakomesha maisha ya watu. Hakuna nafsi hata moja iliyochukuliwa na mauti. Wote wameachwa hai ili wapate kuitambua Nguvu ile ambayo hakuna mtu anayeweza kuipinga. {8T 102.1}

Hebu na tumsifu Bwana kwamba maisha ya watoto Wake yamekuwa ya thamani sana machoni Pake. Angeweza kujatuua nabkua nausga ta watendakazi katika kutokutii kwao na kujitosheleza. Lakini, hapana! Yeye Anasema: "Watapata nafasi nyingine. Nitaruhusu moto uzungumze nao na nitaona kama watatenda kinyume na hatua ya majaliwa Yangu. Nitawajaribu kwa moto nipate kuona kama watajifunza somo ambalo ninatamani kuwafundisha." {8T 102.2}

Wakati kituo cha Sanitarium cha afya, tiba rahisi  na maisha bora cha Battle Creek kilipoharibiwa, Kristo alijitoa mwenyewe kuyalinda maisha ya wanaume na wanawake. Katika uharibifu huu Mungu alikuwa akiwasihi watu Wake wapate kumrudia. Na katika uharibifu wa ofisi ya Review and Herald, na uokoaji wa maisha, Yeye Amekuwa akiwasihi kwa mara ya pili tena. Yeye Anawataka wapate kuona kwamba nguvu itendayo miujiza Yake Yeye asiye na kikomo imetumika kuyaokoa maisha, ili kila mfanyakazi apate fursa ya kutubu na kuongoka. Mungu anasema: "Ikiwa watageukia Kwangu, nitawarudishia furaha ya wokovu Wangu. Lakini ikiwa wataendelea kutembea katika njia yao wenyewe, nitakuja karibu zaidi; na mateso yatakuja juu ya familia zinazodai kuuamini Ukweli, lakini ambazo hazitendi kulingana na uUweli huo, ambazo hazimfanyi Bwana Mungu wa Israeli kuwa hofu yao na utisho wao." {8T 102.3}

Hebu kila mtu na ajichunguze ili kuona kama yuko katika imani. Hebu watu wa Mungu watubu na kuongoka, ili dhambi zao zifutwe wakati nyakati za kuburudishwa

zitakapokuja kutoka kwa uwapo wa Bwana. Hebu waangalie ni kwa nini wameshindwa kutembea katika njia ambayo Mungu ameiweka alama, ambamo ndani yake wameshindwa kusafisha roho zao kwa kuzingatia mashauri Yake. {8T 103.1}

## SURA YA 19
## KILE AMBACHO KINGEWEZA KUWAPO

St. Helena, California, January 5, 1903.
Kwa Kanisa la Battle Creek –

Siku moja saa sita mchana nilikuwa naandika kazi ambayo ingeweza kufanywa katika Mkutano Mkuu uliopita ikiwa wanaume walio katika nafasi za uaminifu walikuwa wamefuata mapenzi na njia ya Mungu. Wale ambao wamekuwa na nuru kubwa hawajatembea katika nuru. Mkutano ulifungwa, na mapumziko hayakufanywa. Wanaume hawakujinyenyekeza mbele za Bwana kama walivyopaswa kufanya, na Roho Mtakatifu hakumwagwa kwao. {8T 104.1}

Nilikuwa nimeandika hadi hapo nilipopoteza fahamu, na kuonekana kuwa nilikuwa ninashuhudia eneo la huko Battle Creek. {8T 104.2}

Tulikusanyika katika ukumbi wa Maskani. Maombi yalitolewa, wimbo wa tenzi wa sifa ukaimbwa, na ombi lilitolewa tena. Maombi ya dhati kabisa yalitolewa kwa Mungu. Mkutano huo ulidhihirishwa na uwepo wa Roho Mtakatifu. Kazi ilizama zaidi, na baadhi ya waliokuwapo walikuwa wakilia kwa sauti. {8T 104.3}

Mmoja aliinuka kutoka katika mkao wake wa kuinama na kusema kwamba katika siku zilizopita hakuwa na umoja na baadhi ya watu na wala hakuhisi upendo kwao, lakini kwa kuwa sasa alijiona jinsi alivyo. Kwa umakini mkuu alirudia ujumbe ule kwa kanisa la Laodikia: " ‘Kwa kuwa wasema, mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu.' Katika kujitosheleza kwangu hivi ndivyo nilivyojisikia" alisema. "'Nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi.' Sasa ninaona kuwa hii ndio hali yangu. Macho yangu yamefunguka. Roho yangu ilikuwa ngumu na isiyo ya haki. Nilijiona kuwa mwenye haki, lakini moyo wangu umevunjika, nami ninaona hitaji langu la ushauri wa thamani wa Yule aliyenichunguza kabisa kwa kinagaubaga. Ajabu, maneno haya ni ya neema na huruma na upendo kiasi gani, 'Nakupa shauri, ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.’” Ufunuo 3:17, 18. {8T 104.4}

Msemaji aliwageukia wale ambao walikuwa wakisali, na kusema: "Tuna jambo la kufanya. Ni lazima tuungame dhambi zetu, na kunyenyekesha mioyo yetu mbele za Mungu. "Alifanya ungamo kwa moyo uliovunjika na kisha akapiga hatua kuwafikia ndugu kadhaa, mmoja baada ya mwingine, na kunyosha mkono wake, akiomba msamaha. Wale aliozungumza nao walisimama kwa miguu yao, wakiungama na kuomba msamaha, na wakakumbatiana, wakilia. Roho ya kuungama ilienea katika mkutano wote. Ulikuwa ni msimu wa Pentekoste. Sifa za Mungu ziliimbwa, na usiku ulivyoendelea sana, hadi karibu na asubuhi, kazi hiyo iliendelea. {8T 105.1}

Maneno yafuatayo yalirudiwa mara kwa mara, kwa dhahiri: " Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu. Tazama, nasimama mlangoni,

nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.” Aya ya 19, 20. {8T 105.2}

Hakuna mtu aliyeonekana kuwa na kiburi kiasi cha kushindwa kufanya ungamo la dhati, na wale ambao waliongoza katika kazi hii ndio walikuwa na uwezo, lakini hapo kabla hawakuwa na ujasiri wa kuungama dhambi zao. {8T 105.3}

Kulikuwapo na shangwe ambazo hazikuwahi kusikika katika Maskani. {8T 105.4}

Kisha nikaamka kutoka katika kupoteza fahamu kwangu, na kwa kitambo sikuweza kuwaza ni wapi nilipolikuwa. Kalamu yangu bado ilikuwa mkononi mwangu. Maneno haya yalinenwa kwangu, "Haya ndiyo ambayo yangeweza kutokea. Yote haya Bwana alikuwa akisubiri kuwatendea watu Wake. Mbingu yote ilikuwa ikisubiri kuonesha neema na ukarimu." Niliwaza kuhusu ni wapi tungelikuwapo kama kazi kamili imekuwa imefanyika katika Mkutano Mkuu wa mwisho (General Konferensi), na uchungu wa kuvunjika matumaini ulinijia wakati nilipogundua kuwa kile nilichokishuhudia hakikuwa uhalisi. - {8T 105.5}

Njia ya Mungu daima ndio njia iliyo sahihi na ya busara. Daima Yeye analeta heshima kwa Jina Lake. Usalama pekee wa mwanadamu dhidi ya mabadiliko ya pupa, yenye tamaa ya makuu ni kuuweka moyo katika upatanifu na Kristo Yesu. Hekima ya mwanadamu si ya kuaminika. Mtu ni kigeugeu, amejaa kujitukuza, kujiinua, ubinafsi, kiburi, na uchoyo. Hebu wafanyakazi wanaotenda kazi ya Mungu wamtumaini Bwana kabisa. Ndipo viongozi watakapodhihirisha kwamba wako tayari kuongozwa, si kwa hekima ya kibinadamu, ambayo haifai kuegemewa kama ulivyo mwanzi uliovunjika, bali kwa hekima ya Bwana, ambaye alisema: "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa.” Yakobo 1: 5 {8T 106.1}

## SURA YA 20
## USAHAULIFU

Wote wanaokiri kuwa wana wa Mungu ningewaalika kutafakari historia ya Waisraeli, kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya mia moja na tano, ya mia moja na sita, na mia moja na saba. Kwa kujifunza Maandiko hayo kwa uangalifu, tunaweza kuthamini, kufurahia na kutambua vyema zaidi wema, rehema, na upendo wa Mungu wetu.

## Wimbo wa Nchi ya Ahadi

"Haleluya. Mshukuruni Bwana, liitieni Jina Lake, Wajulisheni watu matendo Yake. Mwimbieni, mwimbieni kwa zaburi, Zitafakarini ajabu Zake zote. Jisifuni kwa Jina Lake takatifu, Na ufurahi moyo wao wamtafutao Bwana. Mtakeni Bwana na nguvu Zake, Utafuteni uso Wake sikuzote. “Zikumbukeni ajabu Zake alizozifanya, Miujiza Yake na hukumu za kinywa Chake.
Enyi wazao wa Ibrahimu, mtumishi Wake.
Yeye, Bwana, Ndiye Mungu wetu;
Duniani mwote mna hukumu Zake. Yeye Analikumbuka agano Lake milele; Neno lile aliloviamuru vizazi elfu.
Agano alilofanya na Ibrahimu, Na uapo
Wake kwa Isaka. Alilomthibitishia Yakobo liwe amri, Na Israeli liwe agano la milele. Akisema, Nitakupa wewe nchi ya Kanaani, Iwe urithi wenu mliopimiwa.
Walipokuwa watu wawezao kuhesabiwa,
Naam, watu wachache na wageni ndani yake,
Wakatanga-tanga toka taifa hata taifa,
Toka ufalme mmoja hata kwa watu wengine.
Hakumwacha mtu awaonee,
Hata wafalme aliwakemea kwa ajili yao.
Akisema, Msiwaguse masihi wangu,
Wala msiwadhuru nabii zangu.
“Akaiita njaa iijilie nchi,
Akakiharibu chakula chote walichokitegemea.
Alimpeleka mtu mbele yao, Yusufu aliuzwa utumwani. Walimwumiza miguu yake kwa pingu, Akatiwa katika minyororo ya chuma. Hata wakati wa kuwadia neno lake, Ahadi ya Bwana ilimjaribu. Mfalme alituma watu akamfungua, Mkuu wa watu akamwachia.
Akamweka kuwa bwana wa nyumba yake, Na mwenye amri juu ya mali zake zote. Awafunge masheki wake kama apendavyo,
Na kuwafundisha wazee wake hekima.
Israeli naye akaingia Misri,
Yakobo akawa mgeni katika nchi ya Hamu.
Akawajalia watu Wake wazae sana,
Akawafanya kuwa hodari kuliko watesi wao.
Akawajalia watu Wake wazae sana,

Akawafanya kuwa hodari kuliko watesi wao. “Akawageuza moyo wawachukie watu Wake,
Wakawatendea hila watumishi Wake.
Akamtuma Musa, mtumishi Wake, Na Haruni ambaye amemchagua. Akaweka mambo ya ishara zake kati yao,
Na miujiza katika nchi ya Hamu.
Alituma giza, kukafunga giza, Wala hawakuyaasi maneno Yake. Aliyageuza maji yao yakawa damu,
Akawafisha samaki wao.
Nchi yao ilijaa vyura,
Vyumbani mwa wafalme wao. Alisema, kukaja makundi ya mainzi, Na chawa mipakani mwao mwote. Badala ya mvua aliwapa mvua ya mawe, Na moto
wa miali katika nchi yao. Akaipiga mizabibu yao na mitini yao,
Akaivunja miti ya mipaka yao.
Alisema, kukaja nzige,
Na tunutu wasiohesabika;
Wakaila miche yote ya nchi yao, Wakayala matunda ya ardhi yao. Akawapiga wazaliwa wa kwanza katika nchi, Malimbuko ya nguvu zao.
Akawatoa hali wana fedha na dhahabu,
Katika kabila zao asiwepo mwenye kukwaa.
Misri ilifurahi walipoondoka,
Maana kwa ajili yao hofu imewaangukia.

“Alitandaza wingu liwe funiko, Na moto utoe nuru usiku.
Walipotaka akaleta kware,
Akawashibisha chakula cha mbinguni. Akaufunua mwamba, kukabubujika maji, Yakapita pakavuni kama mto.
“Maana alilikumbuka Neno Lake.
Akawatoa watu Wake kwa shangwe,
Na wateule Wake kwa nyimbo za furaha. Akawapa nchi za mataifa, wakairithi kazi ya watu;
Ili wazishike amri Zake, na kuzitii sheria Zake.
“Haleluya.” Zaburi 105

## Wimbo wa Utumwani

"Haleluya.
"Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema,
Kwa maana fadhili Zake ni za milele.
Nani awezaye kuyanena matendo makuu ya Bwana,
Kuzihubiri sifa Zake zote?

Heri washikao hukumu,
Na kutenda haki sikuzote.
Ee Bwana, unikumbuke mimi, Kwa kibali uliyo nayo kwa watu Wako.
Unijilie kwa wokovu Wako,
Ili niuone wema wa wateule Wako. Nipate kuifurahia furaha ya taifa Lako, Na kujisifu pamoja na watu Wako.

**I**

“Tumetenda dhambi pamoja na baba zetu,
Tumetenda maovu, tumefanya ubaya.
Baba zetu katika Misri Hawakufikiri matendo Yako ya ajabu;
Hawakukumbuka wingi wa fadhili Zako;
Wakaasi penye bahari, bahari ya Shamu.

"Lakini akawaokoa kwa ajili ya Jina Lake, Ayadhihirishe matendo Yake makuu.
Akaikemea bahari ya Shamu ikakauka,
Akawaongoza vilindini kana kwamba ni uwanda.
Akawaokoa na mkono wa mtu aliyewachukia,
Na kuwakomboa na mkono wa adui zao.
Maji yakawafunika watesi wao, Hakusalia hata mmoja wao. Ndipo walipoyaamini maneno Yake,
Waliziimba sifa Zake.

**II**

“Wakayasahau matendo Yake kwa haraka,
Hawakulingojea shauri Lake.
Bali walitamani sana jangwani,
Wakamjaribu Mungu nyikani. 15
Akawapa walichomtaka,
Akawakondesha roho zao.
Wakamhusudu Musa matuoni, Na Haruni, mtakatifu wa Bwana. Nchi ikapasuka ikammeza Dathani,
Ikaufunika mkutano wa Abiramu. Moto ukawaka katika mkutano wao, Miali yake ikawateketeza wabaya.
Walifanya ndama huko Horebu,
Wakaisujudia sanamu ya kuyeyuka.
Wakaubadili utukufu wao
Kuwa mfano wa ng'ombe mla majani. “Wakamsahau Mungu, mwokozi wao, Aliyetenda makuu katika Misri.
Matendo ya ajabu katika nchi ya Hamu,

Mambo ya kutisha penye bahari ya Shamu.
Akasema ya kuwa atawaangamiza
Kama Musa, mteule Wake, asingalisimama, Mbele Zake kama mahali palipobomoka,
Ili aigeuze hasira Yake asije akawaharibu.

**III**

"Wakaidharau nchi ile ya kupendeza, Wala hawakuliamini Neno Lake.
Bali wakanung'unika hemani mwao,
Wala hawakuisikiliza sauti ya Bwana.
Ndipo alipowainulia mkono Wake,
Ya kuwa atawaangamiza jangwani,
Na kuwatawanya wazao wao kati ya mataifa,
Na kuwatapanya katika nchi mbali.
Wakajiambatiza na Baal-Peori, Wakazila dhabihu za wafu. Wakamkasirisha kwa matendo yao;
Tauni ikawashambulia.
"Ndipo Finehasi akasimama akafanya hukumu;
Tauni ikazuiliwa.
Akahesabiwa kuwa ana haki
Kizazi baada ya kizazi hata milele.

**IV**

"Wakamghadhibisha penye maji ya Meriba,
Hasara ikampata Musa kwa ajili yao,
Kwa sababu waliiasi roho yake,
Akasema yasiyofaa kwa midomo yake. 3
Hawakuwaharibu watu wa nchi Kama Bwana alivyowaambia;
Bali walijichanganya na mataifa, Wakajifunza matendo yao.
Wakazitumikia sanamu zao, Nazo zikawa mtego kwao. Naam, walitoa wana wao na binti zao Kuwa dhabihu kwa mashetani.
Wakamwaga damu isiyo na hatia,
Damu ya wana wao na binti zao,
Waliowatoa dhabihu kwa sanamu za Kanaani;
Nchi ikatiwa unajisi kwa damu.
Ndivyo walivyotiwa uchafu kwa kazi zao,
Wakafanya uasherati kwa matendo yao. "Hasira ya Bwana ikawaka juu ya watu Wake,
Akauchukia urithi wake.
Akawatia mikononi mwa mataifa,
Nao waliowachukia wakawatawala.
Adui zao wakawaonea, Wakatiishwa chini ya mkono wao.

Mara nyingi aliwaponya,
Bali walikuwa wakimwasi kwa mashauri yao,
Wakadhilika katika uovu wao.
"Lakini aliyaangalia mateso yao, Aliposikia
kilio chao.
Akawakumbukia agano Lake;
Akawahurumia kwa wingi wa fadhili Zake;
Akawajalia kuhurumiwa
Na watu wote waliowateka.

"Ee Bwana, Mungu wetu, utuokoe,
Utukusanye kwa kututoa katika mataifa,
Tulishukuru Jina Lako takatifu,
Tuzifanyie shangwe sifa Zako.

“Na Ahimidiwe Bwana, Mungu wa Israeli,
Tangu milele hata milele.
Watu wote na waseme, Amina.
“Haleluya. Zaburi 106,

**Wimbo wa Waliokombolewa**

"Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, Kwa maana fadhili Zake ni za milele. Na waseme hivi waliokombolewa na Bwana, Wale aliowakomboa na mkono wa mtesi. Akawakusanya kutoka nchi zote,
Mashariki na magharibi, kaskazini na kusini.

I

“Walitanga-tanga jangwani katika njia ya nyika;
Hawakuona mji wa kukaa.
Waliona njaa, waliona na kiu,
Nafsi yao ilikuwa ikizimia ndani yao. Wakamlilia Bwana katika dhiki zao, Akawaponya na shida zao.
Akawaongoza kwa njia ya kunyoka, Wapate kwenda mpaka mji wa kukaa. Na wamshukuru Bwana, kwa Fadhili Zake, Na maajabu Yake kwa wanadamu. Maana hushibisha nafsi yenye shauku, Na nafsi yenye njaa huijaza mema.
"Waliokaa katika giza na uvuli wa mauti,
Wamefungwa katika taabu na chuma,
Kwa sababu waliyaasi Maneno ya Mungu,
Wakalidharau shauri Lake Yeye Aliye juu.

Hata akawadhili moyo kwa taabu,
Wakajikwaa wala hakuna msaidizi.
Wakamlilia Bwana katika dhiki zao, Akawaponya na shida zao. Aliwatoa katika giza na uvuli wa mauti, Akayavunja mafungo yao. Na wamshukuru Bwana kwa fadhili Zake, Na maajabu Yake kwa wanadamu. Maana ameivunja milango ya shaba,
Ameyakata mapingo ya chuma. . . .

II

"Amegeuza mito ikawa jangwa, Na chemchemi za maji zikawa nchi ya kiu. Nchi ya matunda mengi ikawa uwanda wa chumvi, Kwa sababu ya ubaya wao walioikaa.
Amegeuza jangwa ikawa ziwa la maji,
Na nchi kavu ikawa chemchemi za maji. Maana amewakalisha huko wenye njaa, Nao wametengeneza mji wa kukaa.
Wakapanda mbegu katika mashamba,
Na kutia mizabibu iliyotoa matunda yake.
Naye huwabariki wakaongezeka sana, Wala hayapunguzi makundi yao.
"Kisha wakapungua na kudhilika,
Kwa kuonewa na mabaya na huzuni.
Akawamwagia wakuu dharau,
Na kuwazungusha katika nyika isiyo na njia.
Akamweka mhitaji juu mbali na mateso, Akamfanyia jamaa kama kundi la kondoo.
Wanyofu wa moyo wataona na kufurahi,
Na uovu wa kila namna utajifumba kinywa.
"Aliye na hekima na ayaangalie hayo;
Na wazitafakari fadhili za Bwana." Zaburi 107 {8T 107.1}

"Zikumbukeni Siku za Kwanza"

Kwa nini Israeli ya kale walisahau kwa urahisi kiasi kile matendo ya Mungu? Watu hawakuhifadhi katika kumbukumbu zao kazi Zake za ukuu na uweza au Maneno Yake ya onyo. Lau wangekumbuka matendo Yake ya ajabu kwao,
wasingepokea karipio hili:
"Wewe u nani hata ukamwogopa mtu atakayekufa,
Na mwanadamu atakayefanywa kuwa kama majani?
Ukamsahau Bwana, Muumba wako,
Yeye aliyezitanda mbingu,
Na kuiweka misingi ya dunia;
Nawe unaogopa daima mchana kutwa
Kwa sababu ya ghadhabu Yake Yeye aoneaye,

Hapo afanyapo tayari kuharibu;
Nayo i wapi ghadhabu yake aoneaye?" Isaya 51:12, 13 {8T 113.1}

Lakini wana wa Israeli walimsahau Mungu, ambaye wao walikuwa Wake kwa uumbaji na kwa ukombozi. Baada ya kuona matendo Yake yote ya ajabu, walimjaribu. {8T 114.1}

Waisraeli walikabidhiwa Maneno matakatifu. Lakini Neno la Mungu lililofunuliwa lilitafsiriwa vibaya na kutumiwa vibaya. Watu hawa walidharau Neno la Mtakatifu wa Israeli.
"Kwa maana shamba la mizabibu la Bwana wa majeshi ndilo nyumba ya Israeli,
Na watu wa Yuda ni mche Wake wa kupendeza;
Akatumaini kuona hukumu ya haki, na kumbe! Aliona dhuluma;
Alitumaini kuona haki, na kumbe! Alisikia kilio."

"Ole wao ……. lakini hawaiangalii kazi ya Bwana
Wala kuyafikiri matendo ya mikono Yake.
Kwa sababu hiyo watu Wangu wamechukuliwa mateka, kwa kukosa kuwa na maarifa."
"Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema,
Na kwamba wema ni uovu;
Watiao giza badala ya nuru,
Na nuru badala ya giza;
Watiao uchungu badala ya utamu,
Na utamu badala ya uchungu!
"Ole wao
Walio wenye hekima katika macho yao wenyewe,
Na wenye busara katika fikira zao wenyewe!"
115
"Kwa hiyo kama vile mwali wa moto uteketezavyo mabua makavu,
Na kama manyasi makavu yaangukavyo katika mwali wa moto;
Kadhalika shina lao litakuwa kama ubovu,
Na ua lao litapeperushwa juu kama mavumbi;
Kwa sababu wameikataa sheria ya Bwana wa majeshi,
Na kulidharau Neno Lake aliye Mtakatifu wa Israeli." Isaya 5:7, 11-13, 20, 21, 24, ARV {8T 114.2}

### "Yameandikwa ili Kutuonya Sisi"

"Basi mambo hayo … yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya

zamani." 1 Wakorintho 10:11. Onyo hilo linakuja likivuma katika zama zote, hadi kufikia wakati wetu: {8T 115.2}

“Angalieni, ndugu zangu, kusiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho; hapo inenwapo,

“Leo, kama mtaisikia sauti Yake, Msifanye migumu mioyo yenu, Kama wakati wa kukasirisha. Maana ni akina nani waliokasirisha, waliposikia? Si wale wote waliotoka Misri wakiongozwa na Musa?” Waebrania 3:12-16. {8T 115.3}

Je, sisi tunaoishi katika wakati wa mwisho hatuwezi kutambua umuhimu wa maneno haya ya mtume: “Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu Aliye Hai.”? Aya ya 12. {8T 115.4}

Juu yetu inaangaza nuru iliyojikusanywa kutoka zama zilizopita. Kumbukumbu ya usahaulifu wa Israeli imehifadhiwa kwa ajili ya kutuelimisha sisi. Katika zama hii Mungu ameweka mkono Wake kwa ajili ya kukusanya watu kutoka kila taifa, kabila na lugha Kwake. Katika vuguvugu la ujio wa Kristo, Yeye Ametenda kwa ajili ya urithi Wake, kama vile alivyotenda kwa ajili ya Waisraeli katika kuwaongoza kutoka Misri. Katika wakati ule wa kukatishwa tamaa kukubwa, na sikitiko kuu la 1844, imani ya watu Wake ilijaribiwa kama vile ya Waebrania ilivyojaribiwa kwenye Bahari ya Shamu. Kama Waadventista katika siku za awali bado wangeliuamini Mkono uongozao ambao ulikuwa pamoja nao katika uzoefu wao uliopita, basi, wangeuona wokovu wa Mungu. Ikiwa wote waliofanya kazi kwa umoja katika kazi ya 1844 wangepokea ujumbe wa malaika watatu na kuutangaza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, Bwana angetenda kwa nguvu kupitia juhudi zao. Nuru nyingi ingeangazwa juu ya ulimwengu. Miaka mingi iliyopita wakazi wa dunia wangekuwa wamekwisha kuonywa, kazi ya mwisho ingekuwa imekwishakamilika, na Kristo angekuwa amekwishakuja kwa ajili ya ukombozi wa watu Wake. {8T 115.5}

### Ujumbe wa Wakati Huu

Nimeagizwa kunakili maneno ya onyo kwa ndugu na dada zetu walio katika hatari ya kupoteza mwelekeo wa kazi ya pekee kwa ajili ya wakati huu. Bwana ametufanya kuwa maghala ya Ukweli Wake mtakatifu. Tunapaswa kuinuka na kuangaza. Katika kila nchi tunapaswa kutangaza ujio wa pili wa Kristo, katika lugha ya mwandishi wa Ufunuo tukitangaza: “Tazama, Yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili Yake.” Ufunuo 1:7. {8T 116.1}

Je, tunafanya nini? Je, tunatoa ujumbe wa malaika wa tatu? Na Malaika mwingine,

wa tatu, akawafuata [malaika wa kwanza na wa pili] akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira Yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake. Hapa ndipo penye subira ya watakatifu: hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu. Ufunuo 14:12. {8T 116.2}

Amri za Mungu na ushuhuda wa Yesu vimeunganishwa. Zinapaswa kuwasilishwa waziwazi kwa ulimwengu. {8T 117.1}

### Upinzani wa Adui

Katika Neno la Mungu tunaoneshwa matokeo ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu. “Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; Naye akasimama juu ya mchanga wa bahari.” Ufunuo 12:17. Kukataa kutii amri za Mungu, na ushupavu wa kutunza chuki dhidi ya wale wanaozitangaza amri hizi, huongoza kwenye vita vilivyodhamiriwa kabisa kwa upande wa joka, ambaye nguvu zake zote zinaletwa kulemea dhidi ya watu wanaozishika amri za Mungu. “Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:16, 17. {8T 117.2}

Ishara, au muhuri, wa Mungu unafunuliwa katika utunzaji wa Sabato ya siku ya saba, kumbukizi ya Bwana ya uumbaji. "Bwana akasema na Musa, na kumwambia, Kisha, nena wewe na wana wa Israeli, na kuwaambia, Hakika mtazishika Sabato Zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya Mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye ninyi." Kutoka 31:12, 13. Hapa Sabato imetajwa waziwazi kama ishara kati ya Mungu na watu Wake. {8T 117.3}

Alama ya mnyama ni kinyume cha hii - utunzaji wa siku ya kwanza ya juma. Alama hii inawatofautisha wale wanaukubali ukuu wa mamlaka ya upapa na wale wanaoukubali mamlaka ya Mungu. {8T 117.4}

### Kilio Kikuu

Kama ilivyotabiriwa katika sura ya kumi na nane ya Ufunuo, ujumbe wa malaika wa

tatu utatangazwa kwa nguvu nyingi na wale wanaotoa onyo la mwisho dhidi ya yule mnyama na sanamu yake: “Nikaona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, mwenye uwezo mwingi; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Basi, akapaaza sauti kwa nguvu akisema, "Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza; kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake, na wafalme wa nchi wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake. Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake. Mlipeni kama yeye alivyolipa, mkamlipe mara mbili kwa kadiri ya matendo yake. Katika kikombe kile alichokichanganyisha, mchanganyishieni maradufu.” Ufunuo 18:1-6. {8T 118.1}

Huu ndio ujumbe uliotolewa na Mungu upate kutangazwa kwa kilio kikuu cha malaika wa tatu. {8T 118.2}

Wale ambao imani na ari yao inalingana na ujuzi wao wa ile Kweli watadhihirisha uaminifu wao kwa Mungu kwa kuwasilisha Ukweli, katika uwezo Wake wote wa kuokoa, wa kutakasa, kwa wale wanaoshirikiana nao. Maisha yao ya utakatifu na huduma isiyo na ubinafsi yatakuwa katika upatanifu na kanuni kuu za Ufalme wa mbinguni. {8T 118.3}

"**Nawe Umesahau**"

Ni ukweli mzito na wa kutisha kwamba wengi ambao wamekuwa na ari katika kuutangaza ujumbe wa malaika wa tatu sasa wanakuwa wavivu, wazembe na wasiojali! Mpaka kati ya walimwengu na wengi wanaojulikana kuwa Wakristo karibu hauwezi kutofautishwa. Wengi ambao hapo awali walikuwa Waadventista wenye bidii wanapatana na ulimwengu—na matendo yake, desturi zake, ubinafsi wake. Badala ya kuuongoza ulimwengu kutoa utii kwa sheria ya Mungu, kanisa linaungana zaidi na zaidi na ulimwengu katika uasi. Kila siku kanisa linaongolewa na ulimwengu. Ni wangapi wanaodai kuwa Wakristo ni watumwa wa utajiri/mali/fedha! Kuendekeza kwao hamu ya chakula (ulafi), matumizi yao ya pesa ya ubadhirifu kwa ajili ya kukidhi haja za ubinafsi, humfedhehesha na kumvunjia heshima Mungu sana. {8T 118.4}

Na kwa kukosa ari kwa ajili ya uenezwaji wa ujumbe wa malaika wa tatu, wengine wengi, ingawa hawaishi katika uvunjaji dhahiri wa sheria, hata hivyo kwa kweli wanatoa mvuto wao kwa upande wa Shetani kama vile wale wanaotenda dhambi dhidi ya Mungu waziwazi. Watu wengi wanaangamia; lakini ni wachache kiasi gani walio na mzigo kwa ajili ya roho hizi! Kuna uzito wa akili, kukosa hekima, kupooza,

juu ya watu wengi wa Mungu, ambako kunawazuia kuelewa wajibu wa wakati huu. {8T 119.1}

Waisraeli walipoingia Kanaani, hawakulitimiza kusudi la Mungu kwa kumiliki nchi yote. Baada ya kufanya ushindi kwa sehemu, walitulia ili kufurahia matunda ya ushindi wao. Katika kutokuamini kwao na kupenda raha walikusanyika katika sehemu zilizokwisha kutekwa, badala ya kusonga mbele ili kuchukua maeneo mapya. Hivyo wakaanza kumwacha Mungu. Kwa kushindwa kwao kutimiza kusudi Lake walifanya isiwezekane Kwake Bwana, kutimiza ahadi Yake ya baraka kwao. {8T 119.2}

Je, kanisa la leo halifanyi jambo lilo hilo? Ulimwengu mzima ukiwa mbele yao na hitaji la injili, wale wanaojulikana kuwa Wakristo hukusanyika mahali ambapo wao wenyewe wanaweza kufurahia manufaa ya injili. Hawahisi umuhimu wa kumiliki maeneo mapya, wakipeleka ujumbe wa wokovu katika maeneo ya mbali. Wanakataa kutimiza agizo la Kristo: "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Je, watu hawa wana hatia kidogo kuliko lilivyokuwa kanisa la Kiyahudi? {8T 119.3}

## “Chagueni Hivi Leo Mtakayemtumikia”

Kutakuwapo na pambano kali kati ya wale walio waaminifu kwa Mungu na wale wanaoidharau sheria Yake. Kicho kwa sheria ya Mungu kimeangamizwa. Viongozi wa dini wanafundisha amri za wanadamu kuwa ndio kanuni. Kama ilivyokuwa katika siku za Israeli ya kale, ndivyo ilivyo katika zama hizi za ulimwengu. Lakini kwa sababu ya kuenea kwa uasi na dhambi, je, wale ambao wamekuwa na kicho kwa sheria ya Mungu sasa wawe na heshima ndogo kwake? Je, wataungana na nguvu za dunia kuifanya kuwa batili? Waaminifu hawatachukuliwa na mkondo wa uovu. Hawatakidharau kile ambacho Mungu amekitenga wakfu na kuwa kitakatifu. Hawataufuata mfano wa Israeli wa kusahau; watakumbuka jinsi ambavyo Mungu ameshughulika na watu Wake katika nyakati zote, na watatembea katika njia ya amri Zake. {8T 120.1}

Jaribio huja kwa kila mtu. Kuna pande mbili tu. Uko upande gani? {8T 120.2}

## Ngao ya Uweza wa Mungu

Wale wanaozitunza amri za Mungu wanasimama chini ya ngao pana ya Mwenyezi.
"Aketiye mahali pa siri Pake Aliye juu
Atakaa katika uvuli Wake Mwenyezi.
Nitasema, Bwana Ndiye kimbilio langu na ngome yangu,
Mungu wangu nitakayemtumaini.
Maana Yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji,

Na katika tauni iharibuyo.
Kwa manyoya Yake atakufunika,
Chini ya mbawa Zake utapata kimbilio;
Uaminifu Wake ni ngao na kigao.
Hutaogopa hofu ya usiku,
Wala mshale urukao mchana,
Wala tauni ipitayo gizani, Wala uele uharibuo adhuhuri,
Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako.
Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume!
Hata hivyo hautakukaribia wewe. Ila kwa macho yako utatazama,
Na kuyaona malipo ya wasio haki.
“Kwa kuwa Wewe Bwana Ndiwe kimbilio langu;
Umemfanya Aliye juu kuwa makao yako.
Mabaya hayatakupata wewe,
Wala tauni haitaikaribia hema yako. Kwa kuwa atakuagizia malaika Zake Wakulinde katika njia zako zote.
Mikononi mwao watakuchukua,
Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.
Utawakanyaga simba na nyoka,
Mwana-simba na joka utawaseta kwa miguu.
Kwa kuwa amekaza kunipenda
Nitamwokoa; na kumweka palipo juu,
Kwa kuwa amenijua Jina Langu.
Ataniita Nami nitamwitikia;
Nitakuwa pamoja naye taabuni,
Nitamwokoa na kumtukuza;
Kwa siku nyingi nitamshibisha,
Nami nitamwonyesha wokovu Wangu.“ Zaburi ya 91

Bwana Anatawala
"Njoni, tumwimbie Bwana,
Tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu.
Tuje mbele Zake kwa shukrani,
Tumfanyie shangwe kwa zaburi.

“Kwa kuwa Bwana ni Mungu mkuu,
Na Mfalme mkuu juu ya miungu yote. Mkononi Mwake zimo bonde za dunia, Hata vilele vya milima ni Vyake.
Bahari ni Yake, Ndiye aliyeifanya,
Na mikono Yake iliumba nchi kavu.

"Njoni, tuabudu, tusujudu,
Tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba.

"Kwa maana Ndiye Mungu wetu, Na sisi tu watu wa malisho Yake, Na kondoo za mkono Wake.
Ingekuwa heri leo msikie sauti Yake!
Msifanye migumu mioyo yenu;
Kama vile huko Meriba
Kama siku ya Masa jangwani.
Hapo waliponijaribu baba zenu,
Wakanipima, wakayaona matendo Yangu.
"Miaka arobaini nalihuzunika na kizazi kile,
Nikasema, Hao ni watu waliopotoka mioyo,
Hawakuzijua njia Zangu.
Nikaapa kwa hasira Yangu Wasiingie rahani Mwangu.

"Mwimbieni Bwana wimbo mpya, Mwimbieni Bwana, nchi yote.
Mwimbieni Bwana, libarikini Jina Lake, Tangazeni wokovu Wake siku kwa siku. Wahubirini mataifa habari za utukufu Wake,
Na watu wote habari za maajabu Yake.

"Kwa kuwa Bwana ni mkuu mwenye kusifiwa sana.
Na wa kuhofiwa kuliko miungu yote.
Maana miungu yote ya watu si kitu,
Lakini Bwana ndiye aliyezifanya mbingu.
Heshima na adhama ziko mbele Zake,
Nguvu na uzuri zimo katika Patakatifu Pake.

"Mpeni Bwana, enyi jamaa za watu, Mpeni Bwana utukufu na nguvu.
Mpeni Bwana utukufu wa Jina Lake,
Leteni sadaka mkaziingie nyua Zake. Mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu, Tetemekeni mbele Zake, nchi yote.
"Semeni katika mataifa, Bwana ametamalaki;
Naam, ulimwengu umethibitika usitikisike,
Atawahukumu watu kwa adili.

"Mbingu na zifurahi, nchi na ishangilie,
Bahari na ivume na vyote viijazavyo,
Mashamba na yashangilie, na vyote vilivyomo,
Ndipo miti yote ya mwituni iimbe kwa furaha; "Mbele za Bwana, kwa maana Anakuja, Kwa maana Anakuja Aihukumu nchi.

Atauhukumu ulimwengu kwa haki,
Na mataifa kwa uaminifu Wake." Zaburi 95; 96. {8T 120.3}

# SEHEMU YA 3—BARUA KWA MATABIBU

"Kuwaandikieni mambo yale yale hakuniudhi mimi, bali kutawafaa ninyi." Wafilipi 3:1

## SURA YA 21
## THAMANI YA JARIBIO

Njiani Kwenda Copenhagen, Julai 16, 1886.  Kwa Mkurugenzi wa Tiba/Matibabu wa Kituo cha Afya na Maisha Bora [Sanitariamu] cha Battle Creek—

Ndugu Yangu Mpendwa: Nina upendo wa dhati na mwororo kwako, na ningependa kwamba wale wanaokufuatia kwa lawama wangekuacha. Lakini, ndugu yangu, yakupasa kukumbuka kwamba matatizo yote haya pamoja na udhia yamejumuishwa katika “mambo yote” yanayofanya kazi pamoja kwa ajili ya kuwapatia mema wale wanaompenda Mungu. Jicho la Bwana liko juu yako, Naye huwatazama wale wanaokutafsiri vibaya na kukurarua vipande vipande. Lakini kama utakuwa jasiri na moyo mkuu, ikiwa utaisimamisha nafsi yako kwa Mungu, ikiwa utamtumaini Baba yako wa mbinguni kama vile mtoto anavyomtumaini mzazi wake, ikiwa utatenda kwa haki na kupenda rehema, Mungu anaweza na atafanya kazi pamoja nawe. Ahadi Yake ni ya hakika: "Wao wanaoniheshimu Nitawaheshimu." 1 Samweli 2:30. {8T 123.1}

Kumbuka kwamba uzoefu wako si wa kwanza wa aina hiyo. Unakijua kisa cha Yusufu na cha Danieli. Bwana hakuzuia njama za watu waovu; lakini alizifanya hila zao zifanye kazi kwaajili ya kuwapatia mema wale ambao, katikati ya jaribio na pambano, walihifadhi imani na uaminifu wao. {8T 123.2}

Mioto ya tanuru si kwa ajili ya kuangamiza, bali kusafisha, kuadilisha, kutakasa. Bila majaribio na mitihani tusingehisi uhitaji wetu wa Mungu na msaada Wake; na tungekuwa wenye kiburi na wenye kujitosheleza. Katika majaribio yanayokujia wewe ninaona ushahidi kwamba jicho la Bwana liko juu yako na kwamba anamaanisha kukuvuta Kwake. Si walio wazima, bali waliojeruhiwa, ndio wanaomhitaji tabibu; ni wale ambao wamegandamizwa karibu kupita kiwango cha uvumilivu ndio wanaomhitaji msaidizi. Geukia ngome imara. Jifunze somo la thamani kuu: “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi.” Mathayo 11:28. {8T 123.3}

Yesu anakupenda, nami ninafurahishwa ninaposoma juu ya uzoefu unaoupitia, si kwa sababu wewe ni mteswaji, bali kwa sababu huo ni uthibitisho kwangu kwamba Bwana Yesu anakujaribu na kukuthibitisha ili aone kama utakuja Kwake, ili apate kuona kama utaweka tumaini lako Kwake na kupata amani na pumziko katika upendo Wake. Ninakuombea wewe, ili upate kuja Kwake, aliye Chemchemi ya maji yaliyo hai. Huu ndio uzoefu ambao kila mmoja wetu anapaswa kuwa nao ikiwa tutawahi kuishi pamoja na Kristo katika makao ambayo amekwenda kutuandalia. Una masomo ya thamani ya juu kabisa ya kujifunza katika shule ya Kristo, masomo ambayo yatakuongoza kuufanyia kazi wokovu wako mwenyewe kwa hofu na kutetemeka. {8T 124.1}

Ni pale unapofanikiwa, watu wote wanapoongea mema juu yako, ndipo unapokuwa hatarini. Jilinde, uwe katika kituo chako cha ulinzi, kwa maana utajaribiwa. Hofu yangu kubwa kabisa kwako imekuwa kwamba utaweza kupata utajiri mkubwa sana,

na kwamba ungeshindwa kujifunza kwamba tegemeo lako pekee liko kwa Mungu. Umewekwa katika nafasi yenye dhamana na heshima kuu, na kumekuwa na hatari ya wewe kuchanganyikiwa na kupata kizunguzungu na hata kusahau tegemeo lako kwa Mungu. Umewekwa mahali ambapo unaweza kuwa na mvuto mkubwa sana kwa ajili ya wema ikiwa tu utakodoa macho yako kwenye utukufu wa Mungu peke yake. Baba yako wa mbinguni anakupenda, na atakuvuta Kwake kwa majaribio ambayo yanaonekana kwako kuwa makali. {8T 124.2}

Nina shauku ya je dhati kabisa kwamba utaingia katika jiji la Mungu, sio tu kama mkosaji ambaye amesamehewa, bali kama mshindi. Ndugu yangu, Je, wewe utalifikiria hili? Ikiwa wewe ni mkweli na mnyenyekevu na mwaminifu katika maisha haya, utapewa njia nyingi za kuingia. Ndipo mti wa uzima utakuwa wako, kwa kuwa wewe utakuwa mshindi wa dhambi; mji ambao Mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu utakuwa mji wako. Hebu mawazo yako yashike mambo yasiyoonekana. Hebu mawazo yako yachukuliwe hadi kwenye ushahidi wa upendo mkuu wa Mungu kwako.
Katika kutafakari lengo lile ambalo unalifukuzia, utapoteza hisia za uchungu unaoletwa na taabu nyepesi ambazo ni za kitambo tu. {8T 125.1}

## Uzoefu wa Paulo

Copenhagen, Julai 17, 1886.

Paulo alikuwa mtu ambaye alijua maana ya kuwa mshiriki wa mateso ya Kristo. Huna haja ya kwamba nirudie historia ya majaribio yake. Maisha yake yalikuwa ni maisha ya pilikapilika zilizoendelea daima, licha ya kwamba alikabiliwa na udhaifu mwingi. Alifuatwa daima na chuki na uovu wa Wayahudi. Walikuwa na uchungu mwingi mno dhidi yake na walifanya yote wawezayo kumzuia kufanya kazi yake. Lakini bado tunasikia sauti yake ikisikika hadi kufikia wakati wetu: "Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele." "Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu." 2 Wakorintho 4:17, 18; Warumi 8:18. Paulo hakadirii sana juu ya fadhila na faida za maisha ya Kikristo. Ninazungumza bila kusita juu ya jambo hili, kwa maana ninajua mwenyewe kwamba anachosema ni kweli. 126 {8T 125.2}

## Kupumzika Katika Upendo wa Mungu

Paulo anaendelea kusema: “Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba." Aya ya 14, 15. Mojawapo ya somo ambalo tunapaswa kujifunza katika shule

ya Kristo ni kwamba upendo wa Bwana kwetu ni mkuu zaidi sana kuliko ule wa wazazi wetu wa duniani. Tunapaswa kuwa na imani isiyo na shaka na ujasiri kamili Kwake. “Roho Mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja Naye ili tupate na kutukuzwa pamoja Naye." Aya ya 16, 17. {8T 126.1}

Bwana na akusaidie, kama mwanafunzi mwenye bidii katika shule ya Kristo, ujifunze kutua mizigo yako kwa Yesu. Na ikiwa utakuwa huru katika upendo Wake, utatazama juu na mbali kutoka katika majaribio haya yanayokera. Fikiria kile ambacho Yesu amekivumilia kwa ajili yako, na usisahau kamwe kwamba hii ni sehemu ya urithi ambao tumeupokea kama Wakristo, kuwa washirika pamoja Naye wa mateso Yake, ili tuwe washirika pamoja Naye katika utukufu Wake. {8T 126.2}

## Hatari ya Kujitosheleza

Soma ndoto ya Nebukadreza kama ilivyoandikwa katika sura ya nne ya Danieli. Mfalme aliona mti mrefu uliopandwa ardhini. Makundi na mifugo kutoka milimani na vilimani yalifurahia makao yake, na ndege wa angani walijenga viota vyao katika matawi yake. Hivyo ndivyo ulivyowakilishwa ukuu na ustawi wa Nebukadneza. Mataifa yalikusanywa chini ya enzi kuu yake. Ufalme wake uliimarishwa kwa uthabiti katika mioyo ya raia wake watiifu. {8T 126.3}

Mfalme aliona ustawi wake, na kwa sababu hiyo alijivuna. Licha ya maonyo ambayo Mungu alikuwa amempa, alifanya mambo yale yale ambayo Bwana alikuwa amemwambia asifanye. Akautazama ufalme wake kwa kiburi na kusema: “Mji huu sio Babeli mkubwa nilioujenga mimi, uwe kao langu la kifalme, kwa uwezo wa nguvu zangu, ili uwe utukufu wa enzi yangu?” Danieli 4:30. Mara tu maneno yale yalipotamkwa, sentesi ya hukumu ilitamkwa. Akili ya mfalme iliondolewa. Maamuzi ambayo alifikiri kuwa ni makamilifu sana, hekima ambayo alijivunia kuwa nayo, viliondolewa. Johari/kito cha akili, kile kinachomwinua mwanadamu juu ya wanyama, hakuwa nayo tena. {8T 126.4}

Fimbo ya enzi haikushikiliwa tena mkononi mwa mfalme mwenye kiburi na mwenye nguvu. Mtawala hodari ni mwendawazimu. Sasa anatembea pamoja na kundi la ng'ombe ili ale wanavyokula. Yeye ni rafiki wa wanyama wa porini. Paji la uso lililokuwa linavaa taji limeharibika kwa kukosekana kwa mantiki na akili. Amri ilitolewa: "Ukateni mti huu, yafyekeni matawi yake, yapukuteni mbali majani yake, na kuyatawanya matunda yake." Aya ya 14. {8T 127.1}

Kwa hiyo Bwana anajitukuza Mwenyewe kama Mungu wa Kweli na aliye hai. Daudi angeweza kusema vyema kwa mshangao: “Nimemwona mtu asiye haki mkali sana, Akijieneza kama mwerezi wa Lebanoni. Nikapita na kumbe! Hayuko, Nikamtafuta wala hakuonekana." Zaburi 37:35, 36. Acha wanadamu na wainuke kwa kiburi, na Bwana hatawategemeza na kuwazuia wasianguke. Hebu kanisa liwe na kiburi na

majivuno, bila kumtegemea Mungu, lisiinue uweza Wake, na kanisa hilo hakika litaachwa na Bwana, ili kushushwa chini. Hebu watu na wajisifu kwa ajili ya mali, akili, maarifa, au kwa ajili ya chochote isipokuwa Kristo, nao punde watachanganyikiwa. {8T 127.2}

### Mbeba Mzigo Wetu

Ndugu yangu, kumbuka kwamba dunia hii si mbinguni. Kristo alitamka: "Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; Mimi nimeushinda ulimwengu." Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; Maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili Yangu. Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu. 5.13 " Yohana 16:33; Mathayo 5:10-12. {8T 127.3}

Yesu hajakuacha ili ushangazwe na majaribio na matatizo unayokutana nayo. Amekuambia yote juu ya haya kabla, na amekuambia pia kuwa usijiangushe chini kwa huzuni na kukandamizwa wakati majaribu yanapokuja. Mtazame Yesu, Mkombozi wako, na uwe mchangamfu na kufurahi. Majaribio yaliyo magumu kabisa kuweza kustahimili ni yale yanayotoka kwa ndugu zetu, rafiki zetu wa kawaida; lakini hata majaribio haya yanaweza kubebwa kwa subira. Yesu halali katika kaburi jipya la Yusufu. Yeye Amefufuka na amepaa kwenda mbinguni, ili huko apate kutuombea. Sisi tunaye Mwokozi ambaye alitupenda sana hata akafa kwa ajili yetu, ili kupitia Kwake tuwe na tumaini na nguvu na ujasiri, na mahali pamoja Naye katika kiti Chake cha enzi. Yeye Ana uweza na yuko tayari kutusaidia wakati wowote tunapomwomba. {8T 128.1}

Ukijaribu kubeba mizigo yako peke yako utapondwa chini yake. Wewe una majukumu mazito. Yesu anajua juu yake, Naye hatakuacha peke yako ikiwa hutamwacha. Yeye Anaheshimiwa pale unapokabidhi utunzaji wa nafsi yako Kwake kama Muumbaji mwaminifu. Yeye Anakuagizia uitumainie rehema Yake, akiamini kwamba hataki wewe uyabebe majukumu haya mazito kwa nguvu zako mwenyewe. Wewe amini tu, nawe utauona wokovu wa Mungu. {8T 128.2}

Je! unahisi kutotosheleza kwako katika nafasi ya dhamana ambayo unaishikilia? Mshukuru Mungu kwa hili. Kadiri unavyohisi udhaifu wako, ndivyo utakavyoelekea zaidi kumtafuta msaidizi. Mkaribieni Mungu, Naye atawakaribia ninyi. Yakobo 4:8. Yesu anataka uwe na furaha, uwe mchangamfu. Yeye Anataka ufanye kwa vyema kadiri uwezavyo kwa kutumia uwezo ambao Mungu amekupa kisha umtegemee Bwana akusaidie na kuwainua wale ambao watakuwa wasaidizi wako katika kubeba mizigo. {8T 128.3}

Usiruhusu maneno yasiyo mema ya wanadamu yakuumize. Je, wanadamu hawakusema mambo yasiyo mema kumhusu Yesu? Wewe unakosea, na wakati mwingine unaweza kutoa fursa kwa matamshi yasiyo mema; lakini Yesu hakuwahi

kufanya hivyo. Alikuwa safi, asiye na doa, asiye na unajisi. Usitarajie fungu bora zaidi katika maisha haya kuliko alilokuwa nalo Yule Mkuu wa utukufu. Adui zako wanapoona kwamba wanaweza kukuumiza wewe, basi, watafurahi, na Shetani atashangilia. Mwangalie Yesu, na ufanye kazi kwa kuzingatia tu utukufu Wake. Linda moyo wako katika upendo wa Mungu. {8T 129.1}

### Kuangalia Mbali Kutoka kwa Wanadamu

Inawezekana kwamba hata washiriki wa kanisa unaloshiriki watasema na kufanya yale ambayo yatakuhuzunisha. Lakini songa mbele moja kwa moja, ukiwa mtulivu na mwenye amani, ukimtumaini Yesu daima, ukikumbuka kwamba wewe si mali yako mwenyewe, kwamba wewe ni mali ya Kristo, uliyenunuliwa kwa damu ya Mwana mpendwa wa Mungu, na kwamba wewe unashiriki katika kazi Yake, ukijitahidi kuwabariki wanadamu. Hii ni kazi kubwa. Usiruhusu upotovu wa wanadamu ukusukume kutoka katika tumaini thabiti na imani ya kudumu katika ahadi za Mungu. {8T 129.2}

Unaumia pale mtu uliyemfanyia mengi anakuwa adui yako, baada ya kufanywa kuwa chini ya uwezo unaopingana nawe. Lakini je, hufanyi karibu jambo lilo hilo kwa Yesu unapogeuka upande kumwacha? Yeye Amekuwa Rafiki yako bora. Amefanya kila alichoweza ili ajipatie upendo wako. Yeye Ametaka imani yako. Amekualika uje Kwake na mizigo yako yote na huzuni zako zote, na ameahidi Neno Lake kukupa pumziko na amani ikiwa utajitwika nira Yake na kubeba mizigo Yake. Yeye Anatamka kwamba nira Yake ni laini na mzigo Wake ni mwepesi. Onesha kwamba unaliamini hili. Mwamini Mungu kwa alilonena-Mchukue kwa Neno Lake. Hungeweza kamwe kusimama mahali ulipo sasa, ukibeba majukumu ambayo umekwisha kuyabeba, isipokuwa Yesu alikupa msaada wa pekee. Kubali hili. Msifu Mungu kwa msaada ambao amekuwa kwako, na uendelee kumtumainia. {8T 129.3}

Mlete Kristo maishani mwako. Usijisikie kwamba unawajibika kwa mwenendo mbaya wa wengine, hata kama wamo kanisani. Kuna watu kanisani wasio waaminifu wanaomtendea Yesu vibaya zaidi ya wanavyokutendea wewe. Laiti angekuwa duniani, wangemtukana, wangemshutumu, na kumkashifu. "Maana hayana budi kuja mambo ya kukosesha; lakini ole wake mtu yule aliletaye jambo la kukosesha." "Yamfaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari." Mathayo 18:7, 6 . {8T 129.4}

Unabeba mzigo mzito. Ninatamani kwamba kila mtu angeweza kulihisi hili kama ninavyolihisi. Ninatamani ndugu zako wote wangekuwa wakweli na waaminifu kwako, wasikuzuie au kukurudisha nyuma, wasikusifu sana wala kukutukuza, bali wakuangalie kama mtu ambaye Mungu anamtumia kama chombo Chake kufanya kazi iliyotolewa, na kukumbuka kwamba hawapaswi kuyazuia magurudumu kutembea, bali ni lazima kuweka mabega yao kwenye gurudumu, wakisaidia badala ya kuzuia. {8T 130.1}

## Uzito wa Milele wa Utukufu

Tena ninasema: Furahini katika Bwana. Pumzikeni ndani Yake. Mnahitaji nguvu Zake, na uwezo huu mnaweza kuwa nao. Songa mbele kwa uthabiti, kwa ushujaa, kwa ujasiri. Unaweza kukosea katika kuamua, lakini usilegeze kumshikilia Yesu. Yeye ni hekima, Yeye ni nuru, Yeye ni uwezo. Yeye kwenu ni kama Mwamba mkuu katika nchi ya uchovu. Pumzika chini ya uvuli Wake. Unahitaji hekima, na Yesu atakupa. Usiwe mtu asiyeamini. Kadiri unavyosongwa, unavyoeleweka vibaya, unavyosemwa vibaya, unavyotafsiriwa vibaya, ndivyo unavyokuwa na ushahidi zaidi kwamba unafanya kazi kwa ajili ya Bwana, na ndivyo unavyopaswa kushikamana na Mwokozi wako kwa karibu zaidi. Katika magumu yako yote uwe kimya na mtulivu, mvumilivu na mstahamilivu, usilipe ubaya kwa ubaya, bali wema kwa ubaya. Angalia juu ya ngazi. Mungu Yuko juu yake. Utukufu Wake unamulika kila nafsi inayopanda kuelekea mbinguni. Yesu Ndiye ngazi hii. Panda kwa kumtumia, ng'ang'ania Kwake, na hivi karibuni utashuka kutoka kwenye ngazi kuingia katika ufalme Wake wa milele. {8T 130.2}

Ninataka wewe uipate mbingu. Simjui mtu mwingine yeyote ambaye angeweza kufurahia mbingu kuliko wewe, ambaye umefanya kazi bila kuchoka ili kuwafariji wanadamu wanaoteseka, ukijinyima usingizi, ukiacha kula chakula, ukileta raha kidogo tu katika maisha yako. Nyakati fulani haionekani kuwako na mwanga mwingi katika njia yako, ni kivuli kimoja kirefu tu kinachoendelea, cha moja kwa moja. Mateso unayoyaona, wanadamu tegemezi wanaotafuta na kutamani sana kupata msaada, kukutana kwako na wanadamu waovu, waliopotoka – tukio na uzoefu huu ni la jinsi ya kudhoofisha imani yako kwa wanadamu. {8T 130.3}

Ni lazima, kwa kweli, umtazame Yesu, ukikaza macho yako kwenye utukufu ulio juu ya ngazi. Ni kupitia kwa Kristo peke Yake ndiyo unaweza kuwa na hakika ya mbingu, ambapo yote ni usafi, utakatifu, amani, uheri, na mbaraka, ambapo kuna utukufu ambao midomo ya wanadamu haiwezi kuelezea. Karibu zaidi tunavyoweza kufikia maelezo ya thawabu ambayo inamngojea mshindi ni kusema kwamba ni uzito wa utukufu uzidio sana na wa milele. Utakuwa umilele wa furaha, umilele uliobarikiwa, unaoonesha utukufu mpya katika zama zisizo na kikomo. {8T 131.1}

Ni lazima uwepo pale. Chochote unachopoteza hapa, dhamiria kuhakikisha unapata uzima wa milele. Usikate tamaa kamwe. Mara nyingi nimeona kwamba mikono ya milele ilikuwa imekuzunguka wewe, wakati ambapo hukuonekana kutambua au kuthamini unyenyekevu mkuu wa mbingu. Ishi kwa ajili ya Yesu. Unaweza kufanya kazi vizuri zaidi kama daktari katika sanitariamu ikiwa utamfanya Kristo kuwa daktari wako mkuu. Tafuteni kwa bidii taji ya uzima. Fanya biashara/shuguli ya kumtumikia Mungu. Italipa, si katika maisha haya tu, bali pia katika maisha yajayo. Ninahisi kupendezwa sana nawe na mke wako, ninayempenda katika Bwana, kama vile ninavyopendezwa na wanangu na wake zao. Nataka wewe na mkeo muwepo

miongoni mwa waliokombolewa, ili mshiriki katika kutawazwa kwa Kristo. Ninatamani sana kwamba utatokezea kuwa zaidi ya mshindi kupitia Kwake Yeye aliyeyatoa maisha Yake kwa ajili yako. Kwa sababu hiyo, ndugu yangu, nimesema nawe waziwazi. Ninatamani sana kwamba utapaswa kuwa na furaha ya milele. Nafasi yako imekuwa ni yenye majaribio mno. Nimekuwa na hofu kwamba ungeweza kupoteza imani na ujasiri. Ni lazima ukue katika neema na katika ujuzi wa Ukweli. Unapaswa kuwa karibu na ndugu zako. Chochote kitakachokuja, usipoteze imani kwao au kwa Kristo; na ushikilie Ukweli kwa nguvu. {8T 131.2}

Dondoo kutoka kwa barua iliyoandikwa mnamo 1892 kutoka Adelaide, Australia Kusini.—Ndugu yangu, utakutana na majaribio, lakini shikilia sana uadilifu wako. Kamwe usioneshe chochote isipokuwa roho ya uadilifu. Ulimwengu wa mbinguni unalitazama pambano hili. Shetani anakutazama, anatamani sana kuwakuta bila tahadhari, anatamani sana kuwaona mkitenda kwa harara, ili apate kuwashinda. Pigana kiume vita vya Bwana. Fanya hasa kama vile ambavyo Kristo angefanya kama Angekuwa katika nafasi yako. Hebu kusiwe na ugeuzi katika imani au matendo yako. Usiruhusu wewe mwenyewe kuhemkwa juu ya masumbufu yenye kuudhi ambayo yanajitokeza kila wakati. Tulia, mfikirie Yesu, na ufanye yote uwezayo ili kumpendeza. Neema ya Kristo na Roho Mtakatifu ni zawadi za Mungu kwenu, mpate kufanywa imara kwa nguvu zote katika utu wa ndani. {8T 132.1}

## SURA YA 22
## KUWEKEZA KILA KITU BATTLE CREEK)

South Lancaster, Massachusetts, Oktoba 16, 1890.
Kwa Wasimamizi wa Sanitariamu ya Battle Creek—

Ndugu Wapendwa: Nilipokuwa Petoskey nilikuwa na mazungumzo fulani na daktari wenu mkuu kuhusiana na kuanzisha makao ya watoto yatima huko Battle Creek. Nilisema kwamba hili ndilo hasa lililokuwa linahitajika miongoni mwetu kama kanisa, na kwamba katika shughuli za jinsi hii tulikuwa nyuma sana ya madhehebu mengine. {8T 133.1}

Katika mazungumzo yangu nilizungumza juu ya hofu yangu kwamba tulikuwa tukiweka majukumu mengi sana katika kituo kimoja cha Battle Creek, na bado nina maoni hayo hayo. Ni hatari kuweka vitu vingi sana katika kituo kwenye eneo moja. Kiasi kikubwa cha fedha kinatumika katika sehemu hii moja, huku miji inapuuzwa ambayo itakuwa vigumu zaidi na zaidi kufanyiwa kazi. {8T 133.2}

Nimekuwa nikichunguza baadhi ya maandishi yangu, na ninaona kwamba maonyo juu ya jambo hili yalitolewa miaka mingi iliyopita. Imeelezwa wazi kwamba majengo

katika Battle Creek hayapaswi kupanuliwa, kwamba jengo lisiongezwe kwenye jengo ili kuongeza miundombinu/vifaa hapo. Tuliagizwa tusikusanye maslahi katika sehemu hiyo moja, bali kupanua uwanja wetu wa kazi. Kulikuwa na hatari kwamba Battle Creek ingekuwa kama Yerusalemu ya kale - kituo chenye nguvu. Tusipozingatia maonyo haya, maovu yaliyoiharibu Yerusalemu yatakuja juu yetu. Kiburi, kujikweza, kuwapuuza maskini, na upendeleo kwa matajiri - hizi ndizo zilikuwa dhambi za Yerusalemu. Leo, pale majengo makubwa yanapojengwa mahali pamoja, wafanyakazi wanashawishika kujiinua kwa ubinafsi na kiburi. Wanaposhindwa na jaribu hili wao si watenda kazi pamoja na Mungu. Badala ya kutafuta kuongeza majukumu yetu katika Battle Creek, tunapaswa kwa ujasiri na kwa hiari kugawanya majukumu ambayo tayari yapo, tukiyasambaza kwenda katika maeneo mengine mengi. {8T 133.3}

Sisi "tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu." 1 Wakorintho 4:9. Utume wetu ni sawa na ule uliotangazwa na Kristo, mwanzoni mwa huduma Yake, kuwa utume Wake. "Roho wa Bwana Yu juu Yangu," alisema, "Roho wa Bwana Yu juu Yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa” Luka 4:18, 19 . {8T 134.1}

Tunapaswa kuendeleza kazi iliyowekwa mikononi mwetu na Bwana. “Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” "Kwa maana maskini hawatakoma katika nchi milele; ndipo ninakuamuru na kukuambia, Mfumbulie kwa kweli mkono wako nduguyo, mhitaji wako, maskini wako, katika nchi yako." "Basi yoyote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii." Isaya 58:10, 11; Kumbukumbu la Torati 15:11; Mathayo 7:12. {8T 134.2}

Tutajaribiwa kuwa na tamaa, kuwa wenye ulafi wa mali, kukuza tamaa isiyotosheka ya kutaka kupata zaidi. Tukishindwa na jaribu hili na kujisalimisha, litaleta juu yetu hatari zile zile zilizoanguka juu ya Yerusalemu ya kale. Tutashindwa kumjua Mungu na kumwakilisha katika tabia. Tunapaswa kujihadhari sana ili tusije tukaanguka kwa sababu ya kutokuamini, kama ilivyokuwa kwa Wayahudi. Tunapaswa kufanya kazi bila ubinafsi. Tunapaswa kuhisi shauku kubwa katika uanzishwaji na ukuaji wa taasisi nyingine mbali na zile tunazozisimamia. Ninataka kwa dhati kwamba kituo cha afya yaani Sanitarium na maisha bora kingekuwa maili nyingi mbali na Battle Creek. Kutoka katika nuru niliyopewa na Mungu, ninajua hii ingekuwa bora kwa ajili ya hali yake ya kiroho na manufaa. Chuo kilicho karibu na Lincoln, Nebraska,

kitachukua idadi kubwa kutoka Battle Creek, na hivi ndivyo inavyopaswa kuwa. Nuru inapaswa kuangaza
kutoka sehemu zingine, na vile vile kutoka katika Battle Creek. Mungu anapanga kwamba nuru itang'aa kutoka miji tofauti na maeneo mbalimbali. {8T 134.3}

Kuweka vitu vingi sana kwenye kituo katika mahali pamoja ni kosa; inaleta harufu ya ubinafsi. Battle Creek inapokea zaidi ya mgawo wake wa manufaa. Kama majengo muhimu yaliyowekwa huko yangegawanywa na kugawanywa tena, nguvu zingetolewa kwa makanisa mengine. Tunapaswa kufanya kazi bila ubinafsi au uchoyo katika shamba kubwa la mizabibu la Bwana, tukigawanya wakati, fedha, maslahi ya elimu, na taasisi za huduma za kichungaji kwa njia ambayo idadi kubwa iwezekanavyo watapata faida. Tamaa ya ukuu inayowaongoza watu kuweka vituo vingi sana pamoja katika Battle Creek inapaswa kuzuiwa, ili maeneo mengine yapate kubarikiwa na manufaa ambayo baadhi wamepanga kuyaweka kituoni hapo. Katika kuweka vitu vingi sana katika mahali pamoja, elimu isiyo sahihi inatolewa kwa watu. {8T 135.1}

Kupanga kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya Battle Creek si busara. Ulimwengu ni uwanja wetu wa kazi, na fedha zinazotumika katika sehemu hii moja zingekwenda mbali sana katika kuendeleza kazi ya ngumu na ya dharura iliyo mafanikio katika maeneo mengine. Kuna miji mingi ambako ndani yake watu wanahitaji ujumbe wa injili. Badala ya wafanyakazi wetu wengi wenye vipaji kuwekwa katika kituo cha Battle Creek, watu wenye uwezo uliotukuka wanapaswa kupewa madaraja ya utendaji katika maeneo  mahalia mbalimbali. Watu hawa wanapaswa kuwa na shauku iliyo hai katika maeneo mengi, wakishughulikia njia na fedha za kuendeleza kazi. Hawapaswi kwenda kwa uamuzi wao wenyewe, bali wanapaswa kuchanganyika pamoja katika kazi kuu. Mwaka hadi mwaka, kazi inapoimarika katika mahali pale wanapofanyia kazi, wanatakiwa kuwaelimisha na kuwaelekeza watendakazi, na kutuma msaada kwenda katika maeneo mengine. {8T 135.2}

### Kutokuwa na Ubinafsi katika Kazi

Ni lazima kiwekwe kikomo cha upanuzi wa taasisi zetu katika Battle Creek. Shamba ni ulimwengu, na Mungu ana maslahi katika sehemu nyingine za shamba lake kuu la mizabibu. Kuna makanisa na taasisi ambazo yanajitahidi kwa kila senti/chembe ili kupata nafasi hata ya kusimama, ili waweze kuishi. Hebu taasisi zetu zilizofanikiwa zishughulikie kuimarisha mambo yale yaliyosalia yanayotaka kufa. Ni kwa urahisi kiasi gani kanisa kubwa katika Battle Creek lingeweza kutenga kiasi fulani cha fedha zake kwa ajili ya msaada kwa makanisa maskini zaidi, ambayo yanakaribia kupondwa chini ya mzigo wa deni! Kwa nini haya makanisa pacha/wenzi yanaachwa mwaka hadi mwaka kuhangaika na umaskini na madeni? Ubinafsi huleta kifo cha kiroho. Ni wema mkubwa kiasi gani makanisa yetu yenye uwezo zaidi yangeweza kutimiza kama yangeyasaidia makanisa pacha, na kuyafikisha katika hali ya

mafanikio! {8T 135.3}

## Kuwasaidia Wale Wanaohitaji Msaada

Kama mawakala wa Mungu tunapaswa kuwa na mioyo ya nyama, iliyojaa hisani ambayo hutusukuma kuwa msaada kwa wale walio na uhitaji zaidi kuliko sisi wenyewe. Tunapoona ndugu na dada zetu wakihangaika chini ya umaskini na madeni, tunapoona makanisa ambayo yanahitaji msaada wa kifedha, tunapaswa kuonesha shauku isiyo na ubinafsi kwao na kuwasaidia kulingana na kadiri ambayo Mungu ametufanikisha. Iwapo wewe uliye na madaraka juu ya taasisi utaona taasisi zingine zikijitahidi kwa ujasiri kwa ajili ya kupata nafasi, hata ya kusimama ili waweze kufanya kazi inayofanana na kazi za taasisi unazofungamana nazo, usione wivu. {8T 136.1}

Usijitahidi kuisukuma nje nguvu kazi isiwepo kabisa na kujiinua mwenyewe kwa kiburi cha makusudi. Badala yake, punguza baadhi ya mipango yako mikubwa, na kuwasaidia wale wanaofanya jitihada. Wasaidie katika kutekeleza baadhi ya mipango yao ya kuongeza vifaa vyao. Usitumie kila dola katika kupanua miundo-mbinu yako na kuongeza majukumu yako. Hifadhi sehemu ya fedha zako kwa ajili ya kuanzisha katika maeneo mengine taasisi za afya na shule. Utahitaji kuwa na hekima kubwa ya kuweza kujua mahali pa kuziweka taasisi hizi ili watu wanufaike zaidi. Masuala haya yote lazima yafikiriwe kwa uwazi. {8T 136.2}

Wale walio katika nafasi za madaraka watahitaji hekima kutoka juu ili waweze kutenda kwa haki, kupenda rehema, na kuonesha rehema, si kwa wachache tu, bali kwa kila mtu ambaye wanakutana naye. Kristo anafananisha maslahi Yake na yale ya watu Wake, haijalishi wao ni maskini na wahitaji kiasi gani. Misheni lazima zifunguliwe kwa ajili ya watu Weusi (wasio wazungu), na kila mtu ajitahidi kufanya jambo fulani na kulifanya sasa. {8T 137.1}

Kuna haja ya taasisi kuanzishwa katika sehemu mbalimbali, ili wanaume na wanawake wapate kuwekwa kazini ili wafanye kila liwezekanalo katika hofu ya Mungu. Hakuna mtu hata mmoja anayepaswa kuacha kuona utume na kazi yake. Kila mtu anapaswa kulenga kuendeleza kazi iliyowekwa mikononi mwake kufikia matokeo yenye mafanikio. Taasisi zetu zote zinapaswa kulikumbuka hili na kujitahidi kupata mafanikio; lakini wakati uo huo wakumbuke kwamba mafanikio yao yataongezeka kwa kulingana na wanavyofanya ukarimu usiopendelea, wakishiriki neema yao pamoja na taasisi zinazojitahidi kwa ajili ya kupata mahali pa salama. Taasisi zetu zenye usitawi zinapaswa kuzisaidia taasisi zile ambazo Mungu amesema zinapaswa kuishi na kusitawi, lakini ambazo bado zinapambana ili zipate kuwepo. Miongoni mwetu kuna kiasi kidogo sana cha upendo wa kweli usio na ubinafsi. Bwana anasema: “Kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. Yeye asiyependa, hakumjua Mungu; kwa maana Mungu ni upendo." "Tukipendana, Mungu hukaa ndani yetu, na pendo Lake limekamilishwa ndani yetu."

1 Yohana 4:7, 8, 12. Haimpendezi Mungu kuona mwanadamu akiangalia au kushugulikia mambo yake tu, na akifumba macho yake asiangalie masilahi ya wengine. {8T 137.2}

### Kile ambacho Taasisi Moja inaweza Kufanya kwa Nyingine

Katika majaliwa ya Mungu, Kituo cha afya na maisha bora kimefanikiwa sana (Sanitarium), na katika mwaka huu unaokuja wale walio katika madaraka wanapaswa kuzuia matakwa yao. Badala ya kufanya yote wanayotamani kufanya katika kupanua majengo yao, wanapaswa kufanya kazi isiyo na ubinafsi kwa ajili ya Mungu, wakinyosha mkono wa upendo kwa masilahi yaliyowekwa katika maeneo mengine. Ni faida gani wangeweza kutoa kwa ajili kituo cha urejeshaji wa Afya Vijijini, huko St. Helena, kwa kutoa dola elfu chache kwa ajili ya shughuli hii! Mchango kama huo ungewapa ujasiri wale wanaosimamia, kuwatia moyo kusonga kwenda mbele na kwenda juu. {8T 137.3}

Michango ilitolewa kwa ajili ya kituo hiki cha afya na maisha bora cha Battle Creek katika historia yake ya awali, na sasa je, kituo hiki cha afya na maisha bora cha Sanitarium hakipaswi kufikiria kwa makini kile kinachoweza kufanya kwa ajili ya taasisi mwenza wake iliyopo katika Pwani ya Pasifiki? Ndugu zangu mlioko Battle Creek, je, haionekani kuwa ni sawa na agizo la Mungu la kuweka mpaka ya matakwa yenu, kupunguza shughuli zenu za ujenzi, na kuacha kupanua taasisi zetu katika kituo hicho? Kwa nini hamjisikii kwamba ni upendeleo na wajibu wenu kuwasaidia wale wanaohitaji msaada? {8T 138.1}

### Matengenezo Yanayohitajika

Nimeagizwa kwamba matengenezo yanahitajika kulingana na mambo haya, kwamba ukarimu zaidi unapaswa kuenea miongoni mwetu. Kuna hatari ya daima kwamba hata Waadventista wa Sabato watashindwa na tamaa ya ubinafsi ya kutaka makuu nao watatamani kuweka fedha zote na mamlaka katika mashirika yale ambayo wanayasimamia hasa. Kuna hatari kwamba watu wataruhusu hisia za wivu kuinuka mioyoni mwao na kwamba watakuwa na husuda kwa mashirika ambayo ni muhimu kama yale wanayoyasimamia. Wale wanaotunza kwa upendo mkuu neema ile ya Ukristo safi hawawezi kutazama bila kujali sehemu yoyote ya kazi katika shamba kuu la mizabibu la Bwana. Wale ambao wameongoka kweli kweli watakuwa na shauku iliyo sawa kwa kazi inayofanyika katika sehemu zote za shamba la mizabibu na watakuwa tayari kusaidia kwa lolote na popote msaada unapohitajika. {8T 138.2}

Ni ubinafsi ndio unaowazuia watu kupeleka msaada kwenda katika sehemu zile ambapo kazi ya Mungu haina mafanikio kama ilivyo katika taasisi wanayoisimamia. Wale wanaobeba majukumu wanapaswa kutafuta kwa uangalifu mafanikio ya kila tawi la kusudi na kazi ya Mungu. Wanapaswa kuyatia moyo na kuyategemeza mashirika katika maeneo mengine na vile vile mashirika yaliyopo katika maeneo yao.

Hivyo vifungo vya udugu vingeimarishwa kati ya washiriki wa familia ya Mungu duniani, na mlango ungefungwa kwa wivu mdogo-mdogo na kijicho ambavyo cheo na ustawi kwa hakika vitaamsha isipokuwa neema ya Mungu imetawala moyo. {8T 138.3}

“Lakini nasema neno hili,” Paulo aliandika: “Yule apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu. Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema;” mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu. 9.12 Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu; 9.13 kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote. 9.14 Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. 9.15 Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo.” 2 Wakorintho 9:6-8, 11-15 . {8T 139.1}

### Kanuni Hai ya Udugu

Sheria ya Mungu inatimizwa pale tu wanadamu wanapompenda Yeye kwa moyo, akili, roho, na nguvu, na jirani zao kama nafsi zao. Ni udhihirisho wa upendo huu ndio unaoleta utukufu kwa Mungu aliye juu, na duniani amani kwa watu aliowaridhia. Bwana anatukuzwa pale kusudi kuu la sheria Yake linapofikiwa. Ni kazi ya Roho Mtakatifu kutoka zama hadi zama kutoa upendo mioyoni mwa wanadamu, kwa maana upendo ndio kanuni iliyo hai ya udugu. {8T 139.2}

Isiwepo upenu au kona/pembe hata moja ya roho itakayokuwa maficho ya ubinafsi. Mungu anatamani kwamba mpango wa mbingu upate kutekelezwa, na utaratibu na upatanifu wa Kiungu kutoka mbinguni upate kuenea, katika kila familia, katika kila kanisa, katika kila taasisi. Kama upendo huu ungeiathiri jamii, tungeona utimilifu wa kanuni bora za usafi na uungwana wa Kikristo, na katika upendo wa Kikristo kwa wale walionunuliwa na damu ya Kristo. Mabadiliko ya kiroho yangeonekana katika familia zetu zote, katika taasisi zetu, katika makanisa yetu. Mabadiliko haya yanapotokea, mawakala hawa watakuwa ni njia ambazo kwazo Mungu atatoa nuru ya mbinguni kwa ulimwengu na hivyo, kupitia nidhamu na mafunzo ya Kiungu, kuwaandaa wanaume na wanawake kwa ajili ya jamii ya mbinguni. {8T 139.3}

Yesu amekwenda kuandaa makao kwa ajili ya wale wanaojiandaa wenyewe, kupitia kwa upendo na neema Yake, kwa ajili ya makao ya furaha kamili. Katika familia ya Mungu huko mbinguni hatapatikana mtu hata mmoja mwenye ubinafsi. Amani na upatanifu wa nyua za mbinguni hautaharibiwa na uwapo wa mtu mkali/jeuri au asiye

na huruma. Yeye ambaye katika ulimwengu huu anaikuza nafsi yake katika kazi aliyopewa kuifanya kamwe hatauona ufalme wa Mungu isipokuwa amebadilishwa rohoni, isipokuwa amekuwa mpole na mnyenyekevu, akidhihirisha usahili wa mtoto mdogo. {8T 140.1}

### Mweleke Pekee Ulio Salama

Wale walio na majukumu katika taasisi zetu wanapaswa kuitafuta njia ya Bwana kila siku. Hawapaswi kujisikia kuwa wana uwezo wa kuchagua njia yao wenyewe, kwa kuwa kwa kufanya hivyo watatembea katika nuru ya cheche za moto waliouwasha wao wenyewe. Mungu Pekee Ndiye anapaswa kuwa kiongozi wao. Wale wanaotafuta uwanja mpana zaidi, wale ambao wangependa kuwa na uhuru mkubwa kuliko Mungu anavyopanga, wale ambao wanashindwa kumfanya Yeye kuwa mshauri wao, hekima yao, utakaso wao, na haki yao, kamwe hawatashinda taji la uzima. Siku baada ya siku nafsi inahitaji dini ya Kristo. Wale wanaokunywa Roho Wake kwa undani hawatakuwa na tamaa ya makuu yao wenyewe. Watatambua kwamba hawawezi kuwa nje ya milki ya Mungu, kwa kuwa Mungu anatawala kila mahali. {8T 140.2}

Yeye anayetosheka kabisa kupokea agizo Lake kutoka juu atachangamshwa na ahadi za Mungu, kadiri anavyojitahidi kutenda haki na hukumu. Kuwa na imani isiyoyumba kwa Mungu, kuwa mtendaji wa Neno Lake, ni kufuata njia salama. Ushauri wa Mungu hurahisisha mikanganyiko ya shughuli za biashara na ya kazi za nyumbani. Wafuasi wa Kristo wanaofanya kazi kwa kuzingatia utukufu wa Mungu tu watakuwa na hekima ya mbinguni. Lakini ni Ukweli unaotia uchungu kwamba katika makanisa na taasisi zetu kuna upungufu mkubwa wa Ukristo wa Kweli. Bwana na awasaidie wale wanaobeba majukumu kuungana wao kwa wao katika kazi zao na kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. {8T 141.1}

Kristo aliwaambia wanafunzi Wake: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mathayo 5:14, 13. Basi ni muhimu kiasi gani kwamba kila roho utaweka taa yake ikiwa imetengenezwa utambi na kuwaka, ili ipate kuwapa nuru wale wote anaokutana nao. Mungu amewafanya watu Wake kuwa ghala la Ukweli mtakatifu. Vipaji vimekabidhiwa kwao ili wapate kuviendeleza kwa busara, kwa kuwa Mungu anapanga kwamba kwa matumizi ya mara kwa mara vipaji vyao vitazidishwa. {8T 141.2}

### Hatari Itokanayo na Upanuzi

Ndugu zangu, upanuzi wa vituo vyenu, na kuongezeka kwa idadi yenu, si kulingana na alivyoagiza Bwana. Majengo makubwa yanahitaji ufadhili mkubwa, na ufadhili mkubwa unawataka watu wenye elimu na vipaji, na watu wenye uzoefu wa kina wa kidini, kuongoza taasisi katika njia za Mungu; na kuisimamia kwa busara na ustadi kunataka kwamba kuwepo na ongezeko la jumla wa mambo ya kiroho ili kile ambacho Mungu alikipanga kiwe kiwezekane—kimbilio kwa maskini na

wanyenyekevu. Wale walio imara katika Ukweli wasiwekwe kando kwa kuwapendelea wale wanaopenda mambo na anasa za ulimwengu. Bei hazipaswi kuwekwa juu sana ili kukidhi gharama za sasa hivi kiasi kwamba maskini, kwa kiasi kikubwa, watatengwa na manufaa ya sanitariamu. {8T 141.3}

Kwa vipaji, miundombinu na vifaa vilivyopo kwa sasa, haiwezekani kwa daktari mkuu kufanya yale yote ambayo ni muhimu kufanywa katika matawi na idara mbalimbali, kama ambavyo angeweza kutamani kulifanya hili. Haiwezekani kwake kutoa usimamizi wa yeye mwenyewe kuwapo katika sehemu zote za kazi. {8T 142.1}

Jambo hili limefunguliwa mbele yangu tena na tena. Wakati ambapo kuna ukuaji endelevu katika taasisi, wakati ambapo majengo yanatanuka na majukumu yanaongezeka, hakuna ukuaji unaolingana navyo wa vipaji na uwezo unaohitajika kwa ajili ya usimamizi wa shughuli kubwa kiasi hicho. Je, daktari wetu mkuu pamoja na wajumbe wa bodi watalizingatia hili? Ndugu yangu, wewe si mtu wa kuishi milele. Ninamshukuru Bwana kwa kuwa una hekima kama hiyo uliyo nayo ya kutunza afya yako. Lakini huwezi kufanya kama unavyofanya sasa siku zote. Afya yako inaweza kudhoofika. Maisha yako hayana uhakika, na imewekwa mbele yangu kwamba kunapaswa kuwa na nguvu kazi mara tatu zaidi katika sanitariamu kuliko ilivyo kwa sasa. Hata wakati huo, wafanyakazi wote wangekuwa na mengi ya kufanya ikiwa wangefanya kazi yao vizuri. {8T 142.2}

### Suala la Mishahara

Taasisi hii kwa sasa iko katika hali ya neema, na wasimamizi wake hawapaswi kusisitiza juu ya kiwango cha chini cha mishahara ambacho kilikuwa ni muhimu katika miaka yake ya awali. Wafanyakazi wanaostahili, wenye ufanisi wanapaswa kupokea mishahara ifaayo kwa kazi yao, na wanapaswa kuachwa watumie uamuzi wao wenyewe kuhusu matumizi watakayofanya kwa kutumia mishahara yao. Hakuna hali itakayofanya watumikishwe kupita kiasi. Daktari mkuu mwenyewe anapaswa kuwa na mshahara mkubwa. {8T 142.3}

Kwa mganga mkuu ningependa kusema: Ijapokuwa huna suala la mishahara chini ya usimamizi wako binafsi, ni bora kwako kuliangalia kwa makini suala hili; kwa kuwa unawajibika, kama kiongozi wa taasisi. Usiwasihi watenda kazi kufanya kazi kwa kujitoa kafara sana. Zuia shauku/lengo lako la kutaka kupanua taasisi hii na kulimbikiza majukumu. Hebu baadhi ya fedha zinazoingia kwenye sanitariamu zitolewe kwa taasisi zinazohitaji msaada. Hakika hii ni sawa. Inakubaliana na mapenzi na njia ya Mungu, nayo italeta baraka za Mungu juu ya sanitariamu.
{8T 142.4}

Ningependa kusema hasa kwa baraza la wakurugenzi: "Kumbuka kwamba wafanyakazi wanapaswa kulipwa kulingana na uaminifu wao. Mungu anataka tushughulikiane sisi kwa sisi kwa uaminifu makini kabisa. Baadhi yenu mmelemewa

na masumbufu na majukumu, nami nimeelekezwa kwamba kuna hatari ya ninyi kuwa wabinafsi, kutendewa wengine ubaya na kuwadhulumu wale mnaowaajiri." {8T 143.1}

Kila shughuli ya biashara, iwe inahusiana na mfanyakazi mwenye nafasi ya madaraka au mfanyakazi wa hali ya chini kabisa anayehusiana na sanitariamu, inapaswa kuwa kama vile Mungu anavyoweza kukubali. Tembeeni nuruni wakati nuru ingalipo, giza lisije likawajia. Ingekuwa bora zaidi kutumia fedha kidogo katika majengo na kuwapa wafanyakazi wenu ujira unaolingana na thamani ya kazi yao, ukiwatendea rehema na haki. {8T 143.2}

Kutokana na nuru ambayo Bwana amependezwa kunipa, ninajua kwamba Yeye hapendezwi na mambo mengi ambayo yamefanyika kuhusiana na watenda kazi. Mungu hajaweka kila jambo wazi kwangu, lakini maonyo yamekuja kwamba katika mambo mengi kwamba matengenezo thabiti yanahitajika. Nimeoneshwa kwamba kuna haja ya akina baba na akina mama katika Israeli kuunganishwa na taasisi. Wanaume na wanawake wenye kujitoa wanapaswa kuajiriwa, ambao, kwa sababu hawagandamizwi daima na masumbufu na majukumu, wanaweza kuangalia masilahi ya kiroho ya wafanyakazi. Ni muhimu kwamba wanaume na wanawake kama hao wanapaswa kuwa kazini kila wakati katika mielekeo ya kimishenari katika taasisi hii kubwa. Haifanyiki hata nusu ya kile ambacho ingepaswa kufanywa kuhusiana na suala hili. Ilibidi iwe ni sehemu ya wanaume na wanawake hawa kufanya kazi kwa ajili ya waajiriwa katika mielekeo ya kiroho, wakiwapa maagizo ambayo yatawafundisha jinsi ya kuongoa roho, kuwaonesha kwamba hilo linapaswa kufanyika, si kwa kusema sana, bali kwa maisha yenye msimamo thabiti, yaliyo na mfano kama ya Kristo. Wafanyakazi wamewekwa wazi kwa mivuto ya kidunia; lakini badala ya kukalibiwa na mivuto hii, wanapaswa kuwa wamishenari waliowekwa wakfu, wanaotawaliwa na uwezo unaoinua na kutakasa. Hivyo watajifunza jinsi ya kukutana na wasioamini na jinsi ya kuweka mvuto ambao utawaongoa kwa Kristo. -{8T 143.3}

Dondoo kutoka kwa barua iliyoandikwa mnamo 1895 kutoka Cooranbong, New South Wales.--Mungu anayo kazi kwa ajili ya kila muumini anayefanya kazi katika sanitariamu. Kila muuguzi anapaswa kuwa mfereji wa baraka, akipokea nuru kutoka juu na kuiruhusu iangaze kwa wengine. Wafanyakazi hawa hawapaswi kufuata mitindo ya kimaonesho ya wale wanaokuja kwenye sanitariamu kwa ajili ya matibabu, lakini wanapaswa kujiweka wakfu kwa Mungu. Angahewa ambayo inazunguka roho zao inapaswa kuwa na harufu ya uzima kwenda uzima. Majaribu yatawasumbua kutoka kila upande, lakini hebu wamwombe Mungu kwa ajili ya uwapo na uongozi wake. Bwana alimwambia Musa: “Hakika Mimi nitakuwa pamoja nawe;” na kwa kila mfanyakazi mwaminifu, aliyejiweka wakfu ahadi iyo hiyo inatolewa. {8T 144.1}

## SURA YA 23
## ENENDENI KATIKA MAENEO MENGI

Cooranbong, NSW, Julai 15, 1895.

Kwa Tabibu aliyeko Battle Creek-- Ndugu Yangu Mpendwa: Nilipokea barua zako jana na kuzisoma kwa shauku kubwa. Daima ninafurahi kusikia kutoka kwako kuhusu familia yako na taasisi ambayo kwayo unabeba majukumu ambayo yana tabia isiyo na jinsi ya kawaida. Usalama wako pekee ni katika kulitii Neno la Bwana, katika kutembea katika nuru ya uso Wake. Adui anajitahidi daima kubuni mbinu ambazo kwazo anaweza kupata ushindi juu yetu, nasi tunapaswa kuzingatia kwa makini tahadhari zilizotolewa na Mungu. {8T 145.1}

Kama wale ambao hapo awali walikuwa wabeba bendera katika kazi ya Mungu wangetembea katika mielekeo ambayo Ameweka alama, wangeweza kumheshimu vyema zaidi na wangeweza kuongeza kufaa kwao. Huenda baadhi ambao kwa sasa sauti zao zimenyamaza katika mauti wangeweza kuishi ili kuonya, kusihi, na kushauri. Kama wale ambao katika miaka iliyopita waliokuwa wamekabidhiwa majukumu makubwa wangelitii maonyo na kusihi kwa Roho wa Mungu, sasa wangekuwa wanatembea mbele Zake kwa nguvu na ufanisi. Pale watu

wanapowaelimisha wengine kuwategemea na kuwatumainia wao, wakati, kwa kalamu au sauti, wanawaamuru wengine juu ya kile wanachopaswa kufanya, wanafundisha wengine kufanya mwili/mwanadamu kuwa silaha yao, kutoa utukufu kwa wanadamu badala ya Mungu. {8T 145.2}

Tunakuwa salama pale tu tunapomwinua Kristo, tukisifu wema Wake. Isaya asema hivi: “Kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa Mtoto Mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani Mwake; Naye ataitwa Jina Lake, Mshauri wa Ajabu, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi Yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme Wake, kuuthibitisha na kuutengeneza kwa hukumu na kwa haki. Tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo”. Isaya 9: 6, 7. {8T 145.3}

Kuna hatari kwamba watu watapokea ushauri wa wanadamu, wakati kwa kufanya hivyo watalitupilia mbali shauri la Mungu. Loo, ni masomo gani ambayo wote wanapaswa kujifunza kabla ya wao kuelewa kwamba Mungu haoni kama mwanadamu aonavyo. Bwana asema hivi: “Maana mawazo Yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia Zangu;. …. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia Zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo Yangu kuliko mawazo yenu." Isaya 55:8, 9. Isipokuwa kuna matengenezo thabiti miongoni mwa watu wa Mungu, Yeye atageuza uso Wake kutoka kwao. {8T 146.1}

Ndugu yangu, kuna haja ya kuwa macho kwa kukesha, isije, katika Battle Creek, jengo likarundikwa juu ya jengo na kunufaika na heri kurundikwa juu ya heri na kunutaika. Fedha zilizotumika kwa namna hiyo zitatoa ushuhuda dhidi yetu. Unapaswa kuweka mipango ya busara katika utendaji na kutawanya uwezo ambao umejikita katika Battle Creek, ukisambaza nuru ambayo Mungu amekupa. Heri watu wapandao kando ya maji yote. Kadiri inavyowekezwa zaidi katika Battle Creek, ndivyo mahitaji ya uwekezaji wa ziada yatakavyokuwa; lakini hii haiko katika utaratibu wa Mungu, na kabla ya muda mrefu sana kupita, kosa la kuweka maslahi katika kituo cha Battle Creek litafanywa kuwa dhahiri. {8T 146.2}

Katika kuongeza jengo juu ya jengo katika mji wa Battle Creek, tunaunga mkono kupuuzwa kwa maeneo mengine. Heri na kunufaika tele mahali pale humaanisha ufukara mahali pengine. Sehemu zingine za shamba la mizabibu zinanyimwa fedha ambazo wangepaswa kuwa nazo. Fedha zinapaswa kuwekezwa mahali pengine katika kuongoa roho kwa Ukweli na kuandaa nyumba za ibada kwa ajili yao. {8T 146.3}

Mungu amebainisha ukweli kwamba ni wajibu wa wale walio katika Battle Creek kusaidia taasisi Zake katika maeneo mengine. Kama wakili mwenye hekima wa mali unapaswa kutawanya majeshi yako, ukitumia nguvu ya mvuto wako kuwasaidia wale walio gizani wapate kumjua Mungu jinsi alivyo. {8T 146.4}

### Haja ya Mipango Mipana Zaidi

Ni miji mingapi na majiji mangapi ambayo yamepuuzwa kabisa. Watu wetu wanajidhuru wenyewe kwa kusongamana katika sehemu moja. Miti kwenye kitalu inaposongamana sana pamoja na kukonda, haiwezi kukua kiafya na uimara. Pandikiza miti kutoka kwenye kitalu chako kilichojazwa na miche kwa wingi. Mungu hatukuzwi katika kuweka faida nyingi katika kituo kwenye sehemu moja. Toa nafasi ili ikue vizuri; weka mimea yako katika sehemu nyingi, ambapo mtu hatamwegemea mwenzake kwa ajili ya msaada. Ipe nafasi ya kukua. Hili Bwana analitaka kwako. {8T 147.1}

Fedha zinazotumika katika kupanua maslahi yako katika Battle Creek, ambazo tayari zimekua sana na kupita mipaka inayofaa, zinapaswa kutumika katika kuanzisha vituo vya umishenari mahali pengine. Unapaswa kupanua mipango yako na kutanua uwanja wa shughuli zako. Unapaswa kuwatuma watu wenye hekima katika majiji na miji ambayo bado haijasikia ujumbe wa injili. Chagua watu bora unaoweza kuwaweka kama akiba, na uwape fursa ya kuwa walezi na wabeba mizigo. Hebu wapate fursa ya kukuza vipaji ambavyo hapo awali vililala bila kazi. Waweke mahali ambapo wanaweza kutumia uwezo wao waliopewa na Mungu katika kuwaita wenye dhambi watubu. Hebu watu wanaodhihirisha kwamba wanampenda Mungu wapate nafasi ya kufanya jambo kwa ajili Yake. {8T 147.2}

Hebu watu na wajifunze kuomba kwa bidii, na hebu wafanye maombi yao kuwa mafupi na ya moja kwa moja kwa kile kipengele wanachokiomba. Hebu wajifunze kuzungumza juu ya Mkombozi wa ulimwengu na kumwinua Mtu wa Kalvari juu zaidi na zaidi. {8T 147.3}

Mahubiri yote ulimwenguni hayatawafanya wanadamu wahisi kwa kina hitaji la roho zinazoangamia zinazowazunguka. Hakuna kitu kitakachoamsha ndani ya wanaume na wanawaake ari ya kujitoa mhanga kama kuwatuma kwenye mashamba mapya ili kufanya kazi kwa ajili ya wale walio gizani. Waandae wafanyakazi wapate kwenda barabarani na mipakani. Usiwaite wanaume na wanawake kwenye kituo kikuu-makao makuu, ukiwahimiza kuacha makanisa ambayo yanahitaji msaada wao. Watu lazima wajifunze kubeba majukumu. Hakuna hata mmoja kati ya mia miongoni mwetu anayefanya lolote zaidi ya kujihusisha na biashara za kawaida za kidunia. Hatuko macho hata nusu katika kuona thamani ya roho ambazo Kristo alizifia. {8T 147.4}

Tunahitaji watunzaji wa bustani ya miche wenye busara, ambao watapandikiza miti katika maeneo mbalimbali na kuipa mazingira mema ambayo yataiwezesha kukua. Ni wajibu chanya wa watu wa Mungu kwenda katika maeneo yaliyo mbali zaidi. Hebu majeshi yawekwe kazini ili kusafisha eneo jipya, kuanzisha vituo vipya vya mvuto popote ambapo nafasi inaweza kupatikana. Kusanya wafanyakazi wa ambao wana bidii ya kweli ya kimishenari, na waruhusu wasonge mbele kueneza nuru na

maarifa mbali na karibu. Hebu wachukue kanuni hai za matengenezo ya afya kwenda katika jamii ambazo kwa kiasi kikubwa hazijui kanuni hizi. Hebu madarasa yaanzishwe, na maagizo yatolewe kuhusu tiba/matibabu ya magonjwa. {8T 148.1}

Ni ukweli kwamba kupitia kwa mvuto wa sanitariamu Ukweli wa mbinguni umetambuliwa na maelfu. Lakini bado kuna kazi ya kufanywa ambayo imepuuzwa. Pesa zimetumika katika kupanua vituo vya Battle Creek, wakati ambapo Bwana anataka chachu iletwe kwenye donge kubwa la unga, ili unga wote upate kuumuka. Badala ya jengo baada ya jengo kuongezwa kwenye sanitariamu, kunapaswa kwa wakati huu kuwa na taasisi nyingi katika maeneo mengine zilizo na vifaa na miundombinu kamili na zilizo katika hali ya utayari, katika kufanya kazi. {8T 148.2}

Kuna watu ambao wameunganishwa na sanitariamu kwa muda mrefu ambao daima watakuwa vivuli vya mtu mwingine, kama watabakizwa hapo, wakati ambapo, kama wangeruhusiwa kutegemea uamuzi wao wenyewe, wangekuwa watu wa kujitegemea, wenye akili ya kina, wenye uwezo wa kutoa ushauri wa busara. Hebu watu hawa wapate nafasi ya kujifunza kubeba majukumu kwa nguvu za Mungu. Hivyo watapata uzoefu utakaowawezesha kuwapasha wengine Ukweli. {8T 148.3}
149

Lakini badala ya watu kutumwa kutoka Battle Creek, kama Mungu alivyoagiza katika shuhuda za wazi ambazo zimetolewa, maelfu ya dola zimetengwa kwa ajili ya kupanua taasisi na kuongeza miundombinu na vifaa katika Battle Creek. Na wito unakuja kutoka Battle Creek kwa ajili ya kutaka hali zinazofaa zaidi na wafanyakazi zaidi. Lakini lazima kuwepo na mabadiliko. {8T 149.1}

Tunatiwa moyo tunapoona kazi inayofanyika kule Chicago na maeneo mengine machache. Miaka mingi iliyopita majukumu makubwa yaliyoweka kituo katika Battle Creek yalipaswa kuwa yamesambazwa. Unaweza kutazama kwa kuridhika ukuaji unaoenea sana wa sanitariamu huko Battle Creek, lakini Mungu hauangalii kwa ukubali kama wewe. Kama taasisi zingejengwa sehemu zingine, kama watu wangepewa majukumu ya kubeba, kungekuwapo na nguvu nyingi zaidi, ufanisi zaidi katika kazi yetu, nasi tungekuwa tumesogea karibu zaidi kulingana na akili na mapenzi ya Mungu kuliko tulivyofanya. Kama ilivyo, ni watu wachache tu wanabeba majukumu mazito. Ni wachache tu ndiyo wanashika mvuto ambao una uwezo wa kutawala katika usimamizi wa kazi mbali na karibu, wakati ambapo kuna wengi ambao hawabebi mizigo yoyote. {8T 149.2}

Wengi wa wale wanaobeba majukumu mazito wanahitajika kuongolewa. Kristo anawaambia kama alivyomwambia Nikodemo: “Hamna budi kuzaliwa mara ya pili." "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Yohana 3:7, 3 . Wengi wanatawaliwa na roho isiyo ya Kikristo. Bado hawajajifunza katika shule ya Kristo upole na unyenyekevu Wake, na isipokuwa wamebadilika, watashindwa na majaribu ya Shetani. Mwaka hadi mwaka wanabeba majukumu matakatifu, lakini

bado wanathibitisha wenyewe kuwa hawawezi kutofautisha kati ya vitu vitakatifu na vya kawaida. Watu kama hao wataendelea kushika uwezo wa kutawala hadi lini? Neno lao litaruhusiwa hata lini kutukuza au kuangusha, kuhukumu au kuinua? Hadi lini watashikilia uwezo kama ile ambao hakuna mtu anayethubutu kufanya mabadiliko katika mbinu zao? {8T 149.3}

**Jenga Vituo Vipya**

Watu wanatiwa moyo kukaa katika Battle Creek, ili wapate kutoa ushawishi wao katika ujenzi wa Yerusalemu ya kisasa. Hii si kufuatana na mpango wa Mungu. Kwa kufanya hivyo, maeneo mengine yananyimwa miundo mbinu na vifaa ambavyo wangepaswa kuwa navyo. Tanukeni ninyi; Msambae; ndio, lakini si katika sehemu moja tu. Nendeni nje na muanzishe vituo vya mvuto mahali ambapo hakuna chochote, au kidogo sana, kimefanyika. Vunja umma/bonge lako kubwa lilioungana; tawanya miale ya nuru yenye kuokoa katika pembe za dunia zenye giza. Kazi inayofanana na ile ya tai kuvuruga kiota chake inahitajika kufanyika. {8T 150.1}

"Moabu amestarehe tangu ujana wake, naye ametulia juu ya sira zake, wala hakumiminwa kutoka chombo kimoja kutiwa chombo kingine, wala hakwenda kufungwa; kwa hiyo ladha yake anakaa nayo, wala harufu yake haikubadilika." Yeremia 48:11. Hii ni kweli kuhusiana na waumini wengi wanaokuja katika Battle Creek. Wengi wana ari ya vita inayotokea kwa vipindi visivyotabirika, lakini nuru yao ni kama ile ya kimondo kinachomulika mbinguni na kuzimika. {8T 150.2}

Hebu watendakazi wa Mungu walio na nia ya kusudi Lake moyoni wafanye jambo kwa ajili ya watu Weusi (wasio wazungu- colored people) katika eneo la Kusini. Hebu mawakili wa Mungu wasitosheke kwa kuligusa tu eneo hili kwa ncha za vidole vyao. Hebu wale walio katika kiini cha kazi wapange kwa dhati kwa ajili ya eneo hili. Wengi wamezungumza juu yake, lakini wanafanya nini wakiwa kama mawakili wa mali za Mungu? Kwa nini wanajisikia huru kufungia mtaji wa Mungu wa mali katika Battle Creek? Kwa nini wanafanya mambo yale yale hasa ambayo wameonywa wasifanye? Jambo hilo linazidi kuwa zito, kwa kuwa maonyo na kusihi kumetolewa bure. Mikono ya nguvu katika Battle Creek inapanuliwa zaidi na zaidi, ikijitahidi kutawala kazi mbali na karibu, na kukiangamiza kile ambacho hawawezi kukitawala. Ninainua sauti yangu kwa kupinga. Roho anayetawala kwa sasa si Roho wa Bwana. {8T 150.3}

Bwana ameibariki Battle Creek tena na tena kwa kumimina Roho Wake juu ya kanisa na watenda kazi, lakini ni wachache kiasi gani wamehifadhi mvuto wa Roho huyu. Ni wachache kiasi gani wametumia pesa zao kama Mungu alivyoelekeza. Fedha zimetumika katika kuwaelimisha wale walioujua Ukweli, wakati maeneo ambayo hayajaelimika kabisa yamepuuzwa. Kama wachungaji wangetoka kwenda nje kama Kristo alivyowaagiza, kama wangetumia karama walizokabidhiwa kupeleka nuru

kwa wale waliomo gizani, wangepata ujuzi mwingi zaidi wa Mungu na wa Kristo kuliko ambao wamepata kwa kutafuta elimu ya ziada katika shule zetu. {8T 151.1}

### Kushindwa Kuyafahamu Majukumu Yaliyotolewa na Mungu

Je, Mungu hajatupa kazi ya kufanya? Je, hajatuamuru kwenda miongoni mwa mivuto pinzani na kuwaongoa watu kutoka katika makosa kwenda kwenye Ukweli? Kwa nini wale ambao wamekusanyika mara nyingi sana katika makusanyiko makubwa katika Battle Creek hawajaweka katika matendo Ukweli ambao wameusikia? Kama wangeitoa nuru ambayo wameipokea, ni mabadiliko yaliyoje ya tabia yangeonekana. Kwa kila neema iliyotolewa, Mungu angetoa neema. Hawajaithamini kama ambavyo wangepaswa kuithamini kazi ile ambayo imefanywa kwa ajili yao, kama sivyo wangeenda katika sehemu zenye giza duniani ili wapate kuitawanya nuru. Wangeupa ulimwengu ujumbe wa haki kwa imani, na nuru yao wao wenyewe ingekua dhahiri zaidi na zaidi; kwa maana Mungu angefanya kazi pamoja nao. Wengi wameshuka kaburini wakiwa na makosa kwa sababu wale wanaoijua Kweli wameshindwa kuwasilisha maarifa haya yenye thamani kuu ambayo wameyapokea. Kama nuru ambayo imeangaza kwa uhuru kiasi hicho katika Battle Creek ingetawanywa wengi wangeinuliwa na kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. {8T 151.2}

Laiti ndugu na dada zetu wangeuthamini ukweli ipasavyo! Laiti, wangelitakaswa nao! Laiti, wangelitambua kwamba juu yao kuna jukumu la kuwasilisha Ukweli huu kwa wengine! Lakini hawajisikii umuhimu wa kuuishi Ukweli huo, wa kuwa watendaji wa Maneno ya Kristo. Wengi wamejitosheleza. Hawajajazwa na roho ya umishenari ambayo inapaswa kuwahuisha wanafunzi wa Kristo. Kama wangejua maana ya kuwa na utungu kwa ajili ya nafsi za wengine, malaika wa Mungu wangefanya kazi kupitia kwao ili kuwasilisha maarifa ya ile Kweli. Wangeijua Kweli, nayo Kweli ingewaweka huru. Pesa zisingetumika tena katika kuongeza jengo juu ya jengo katika mahali pamoja, bali zingetumika katika kufungua maeneo mapya, katika kusimamisha bendera ya Ukweli katika miji ambayo bado haijafanyiwa kazi. Kanuni za mbinguni zenye kuinua, kutakasa, na za kuadilisha zingeletwa katika jamii na zingefanya kazi kama chachu. - {8T 151.3}

Dondoo kutoka katika barua iliyoandikwa mwaka wa 1899, kutoka Cooranbong, N.S.W., Australia-- Ni mpango wa Mungu kwamba maeneo yale ambayo yana miundo mbinu mingi yashiriki masilahi yao na maeneo yenye uhitaji zaidi. Kanuni hii daima inapaswa kufuatwa katika taasisi zetu zote. Mungu anataka kwamba kuwe na upangaji kidogo kwa ajili ya majengo katika mahali ambapo kazi tayari imeanzishwa, na kwamba fedha zitumwe kwenye maeneo ambako, kwa sababu ya ukosefu wa vifaa, wafanyakazi hufanya kazi kwa hali ngumu mno. {8T 152.1}

## SURA YA 24
## KUSUDI LA MUNGU KWA AJILI YA TAASISI ZAKE

Newtown, Tasmania,
Desemba 1, 1895.

Kwa Msimamizi wa Matibabu wa Sanitariamu Kubwa -- Ndugu Yangu Mpendwa: Kila taasisi inayobeba jina la Waadventista wa Sabato inapaswa kuwa kwa ulimwengu kama Yusufu alivyokuwa huko Misri, na kama Danieli na wenzake huko Babeli. Kwa majaliwa ya Mungu watu hawa walichukuliwa mateka, ili waweze kupeleka kwa mataifa ya kipagani maarifa ya Mungu wa Kweli. Walipaswa kuwa wawakilishi wa Mungu katika ulimwengu wetu. Hawakupaswa kufanya mapatano yo yote na mataifa yenye kuabudu sanamu ambayo walikutana nayo, bali walipaswa kusimama wakiwa waaminifu kwa imani yao, wakibeba kama heshima ya pekee jina lile la wacha/waabudu wa Mungu aliyeziumba mbingu na dunia. Vijana hawa walisimama imara katika kanuni. Waliishi wakiwa na uhusiano wa karibu na Mungu wakimheshimu katika njia zao zote, naye aliwaheshimu. Alikuwa hekima yao. Aliwapa maarifa na ufahamu. {8T 153.1}

Leo watu wa Mungu waliosalia wanapaswa kulitukuza Jina Lake kwa kutangaza ujumbe wa mwisho wa onyo, mwaliko wa mwisho kwa karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo. Njia pekee ambayo kwayo wanaweza kuyatimiza matarajio ya Mungu ni

kwa wao kuwa wawakilishi wa Ukweli kwa ajili ya wakati huu. {8T 153.2}

Bwana ametenda kupitia kwa mawakala wa kibinadamu katika kutimiza unabii. Ameifanya kweli takatifu, ya milele isimame wazi wazi katikati ya uzushi na udanganyifu ambao Kristo alitangaza kuwa ungekuwepo katika siku za mwisho. {8T 153.3}

Ndugu yangu, umewekwa mahali ambapo unaweza kuwa mwakilishi wa Ukweli kwa ajili ya wakati huu. Endelea kuwa karibu na Mwalimu Mkuu. Nilikuona ukiinua juu bendera iliyoandikwa Maneno haya: “Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu." Ufunuo 14:12. Watu kadhaa, baadhi yao ambao ni wale ambao umeunganishwa nao katika sanitariamu, walikuwa wakiwasilisha kwako bendera ambayo ilikuwa na maandishi tofauti. Ulikuwa ukiachia bendera ya Waadventista wa Sabato, na ulikuwa ukinyosha mkono ili upate kushika bendera iliyowasilishwa kwako. Mmoja Mwenye heshima kuu alikujia na kwa bidii kubwa akasema: {8T 153.4}

"Basi, heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini. Bali kwao wasioamini, Jiwe walilolikataa waashi, Limekuwa Jiwe kuu la pembeni. Tena, Jiwe la kujikwaza mguu, na mwamba wa kuangusha, Kwa maana hujikwaza kwa neno lile, wasiliamini,nao waliwekwa kusudi wapate hayo. Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu.” 1 Petro 2:7-9. Ndipo mkono wako ukashika kwa uthabiti ile bendera ya kweli, na maneno haya ya kutia moyo yakasemwa: “Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu Wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari. Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu." Ufunuo 19:7, 8 . {8T 154.1}

Niliarifiwa kuwa wewe pamoja na wafanyakazi wenzako mlikuwa katika hatari ya kuficha kanuni za imani yetu ili mweze kupata ufadhili mkubwa. Kila nukta inayofanywa katika mwelekeo huu, badala ya kupanua mvuto wa Ukweli, itazuia maendeleo yake. {8T 154.2}

Wewe pamoja na washirika wako katika kazi ya sanitariamu mnamhitaji rubani kuwa pamoja nanyi daima, vinginevyo mtaangamia. Hakika ni lazima uelewe hatari yenu. Shetani anafanya kila juhudi apate kuwageuzia katika njia ngeni. Mungu amewatia nguvu. Nafsi yako lazima itakaswe kwa njia ya ile Kweli, ili kwamba uaminifu wako thabiti kwa kanuni upate kuwa dhahiri kwa wote. Kadiri nafsi yako isiyojiweza inavyomtegemea Mungu kikamilifu, ndivyo unavyomfanya kikamilifu kuwa tumaini lako, ndivyo utakavyozidi kuwa na njaa ya mkate wa uzima. {8T 154.3}

Mungu anapaswa kutambuliwa na kuheshimiwa na watu wanaojiita Waadventista wa Sabato. Hapo zamani, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, Ukweli ulitangazwa na madaktari na watumishi katika vituo vyetu vya afya na maisha bora-sanitariamu. Mungu hatakubali kidogo kutoka kwako, bali atatarajia mengi zaidi. Wewe pamoja na washirika wako mnapaswa kufanya kazi kwa imani na uthabiti kuzuia kufifia na kuhakikisha maendeleo. Ni lazima pasiwepo na kupungua kwa kazi yako, hakuna kufichwa kwa kanuni za Ukweli; lazima kuwe na upanuzi wa kituo cha shughuli. Taasisi/ Majengo mengi lazima yawekwe katika maeneo mbalimbali. Kuna hitaji la kuwa na bidii zaidi, imani zaidi, mvuto zaidi, kwa watenda kazi walio watendaji, wenye ari zaidi. {8T 155.1}

Kumbuka kwamba unafanya kazi kwa ajili ya kitambo na umilele. Malaika wa mbinguni wameagizwa kushirikiana na juhudi zako za kuongoa roho. Jitihada za dhati zaidi zinapaswa kufanywa ili kuweka ukweli katika maeneo mbalimbali. Na lazima kusiwepo na kufunikwa kwa awamu yoyote ya ujumbe wetu. Ukweli wa wakati huu lazima utolewe kwa roho zinazotaka kufa. Wale wanaoficha Ukweli kwa namna yoyote ile wanamfedhehesha Mungu. Juu ya mavazi yao kutakuwapo na damu ya roho nyingi. {8T 155.2}

### Kusudi La Mungu Kwa Ajili Ya Kituo Cha Afya Na Maisha Bora-Sanitariumu

Sanitariamu ya Battle Creek ni uwanja mpana wa umishenari. Mungu amekuwa akizisukuma roho kutafuta katika taasisi hii kutoa msaada wa wagonjwa kupata afueni kwa mateso ya kimwili. Yeye Anataka kwamba kila kitu kinachohusiana nayo kiwe ni kile anachoweza Yeye anaweza kukiridhia. {8T 155.3}

Anapendezwa kwamba kanisa dogo lipate kujengwa kuhusiana na sanitariamu, ili wale wanaoitembelea taasisi hiyo wapate fursa ya kusikia wenyewe Ukweli kama ulivyo katika Yesu. Injili ya thamani kuu inapaswa kuwasilishwa kwao, si kwa mtindo dhaifu uliofifia au kuchujwa bali kwa msisitizo wa nguvu,  na mionjo yenye joto. Pale inapowekwa wazi kwamba utauwa ni muhimu kwa ajili ya wokovu, sifa bainishi za imani yetu zitadhihirika, zikitutofautisha na ulimwengu. Lakini yasiwepo masuto na ukosoaji dhidi ya mafundisho yanayoshikiliwa na wengine. Katika ushirikiano wetu na walimwengu tunapaswa kupendekeza imani yetu kwa kuziishi kanuni za Ukristo, kwa staha yote ya Kweli. {8T 155.4}

### Thamani ya Kujifunza Neno la Mungu

Ikiwa wanafunzi wa tiba/udaktari watajifunza Neno la Mungu kwa bidii, watakuwa wameandaliwa vyema zaidi kuelewa masomo yao mengine; kwa maana elimu

daima huja kwa kujifunza kwa bidii Neno la Mungu. Hebu wafanyakazi wetu wa umishenari wa tiba* wafahamu kwamba kadiri wanavyozidi kufahamiana na Mungu na Kristo, na kadiri wanavyoifahamu historia ya Biblia, ndivyo watakavyokuwa tayari zaidi kufanya kazi yao. {8T 156.1}

Wanafunzi katika shule zetu wanapaswa kutamani maarifa ya juu zaidi. Hakuna kitu chochote kitakachowasaidia kuwa na kumbukumbu nzuri kama kujifunza Maandiko. Hakuna kitu chochote kitakachowasaidia hivyo kupata maarifa katika masomo yao mengine. {8T 156.2}

Ikiwa wale wasioamini wanatamani kujiunga na madarasa yenu kwa ajili ya kujifunza umishenari wa tiba, na unafikiri kwamba hawangetoa mvuto ambao ungewavuta wanafunzi wengine kutoka kwenye Ukweli, wape nafasi. Baadhi ya wamishenari wako bora kabisa wanaweza kutoka miongoni mwao. Hawajawahi kuusikia Ukweli, na wanapowekwa mahali ambapo wamezungukwa na mvuto unaodhihirisha Roho ya Bwana, baadhi wataongolewa na Ukweli. Katika mafunzo yanayotolewa, kusiwe na kufichwa kwa kanuni hata moja ya Ukweli wa Biblia. Iwapo kuwaruhusu kuingia katika madarasa yenu wale wasio wa imani yetu kutapelekea kunyamaza kufundisha mada kuu zinazohusu faida yetu ya sasa na ya milele, --mada ambazo daima zinapaswa kuwekwa akilini,--hebu wasiruhusiwe kusajiliwa. Kwa vyovyote vile kusiwepo kanuni ya kutolewa kafara au sifa bainishi za imani yetu ya kufichwa ili kuongeza wanafunzi wa nje katika madarasa yetu. {8T 156.3}

Walimu waaminifu wanapaswa kuwekwa kuwa wasimamizi wa madarasa ya Biblia, walimu ambao watajitahidi kuwafanya wanafunzi waelewe masomo yao, si kwa kuwafafanulia kila kitu, bali kwa kuwataka waeleze kwa uwazi kila fungu la maneno wanalosoma. Hebu walimu hawa wakumbuke kwamba manufaa kidogo yatatimizwa kwa kupitia Neno juujuu kwa haraka. Kuchunguza kwa uangalifu na kujifunza kwa dhati, kwa juhudi kunahitajika ili Neno hili lipate kueleweka moyoni vizuri. Kuna Kweli katika Neno ambazo, kama nyufa katika mawe ya thamani, zimefichwa chini ya umbo la nje. Hazina iliyositirika hugunduliwa pale inapotafutwa, kama vile mchimba madini anavyotafuta dhahabu na fedha. Ushahidi wa Ukweli wa Neno la Mungu uko katika Neno lenyewe. Maandiko ndiyo ufunguo unaofungua Maandiko. Maana ya kina ya Kweli za Neno la Mungu inafunuliwa kwa akili zetu na Roho Wake. {8T 157.1}

Biblia ni kitabu kikuu cha masomo, kitabu cha kiada kwa wanafunzi katika shule zetu. Inafundisha mapenzi yote ya Mungu kuhusu wana na binti za Adamu. Ni kanuni ya maisha, inayotufundisha tabia ambayo ni lazima tuitengeneze kwa ajili ya maisha yajayo. Hatuhitaji nuru hafifu ya mapokeo ili kufanya Maandiko yaeleweke. Vile vile tunaweza kudhani kwamba jua la adhuhuri linahitaji mwangaza hafifu

unaometa wa dunia ili kuyaongezea utukufu. Maneno ya makuhani na wachungaji hayahitajiki ili kuwaokoa wanadamu kutokana na makosa. Wale wanaotafuta ushauri kutoka katika Neno la Mungu watakuwa na nuru. Katika Biblia kila wajibu umewekwa wazi. Kila somo linalotolewa linaeleweka. Kila somo linawadhihirisha kwetu Baba na Mwana. Neno linaweza kuwapa watu wote hekima hata kuupata wokovu. Katika Neno, sayansi ya wokovu imedhihirishwa wazi. Yachunguze Maandiko, kwa maana ni sauti ya Mungu ikinena na roho. {8T 157.2}

## SURA YA 25
## KUSUDI LA MUNGU KATIKA KAZI YA UMISHENARI WA TIBA

Melbourne, N.S.W.,
Februari 3, 1898.

Ndugu Yangu Mpendwa: Nuru maalumu imetolewa kwangu kwamba uko katika hatari ya kuacha kuiona kazi kwa ajili ya wakati huu. Unaweka vizuizi vya kutenganisha kazi yako, pamoja na wale unaowaelimisha, kutoka katika kanisa. Haipaswi kuwa hivi. Wale wanaopokea mafundisho katika mielekeo ya umishenari wa tiba wanapaswa kuongozwa kutambua kwamba elimu yao inabidi iwaandae kufanya kazi bora zaidi kwa kuungana na wachungaji wa Mungu. Unapaswa kukumbuka, ndugu yangu, kwamba Bwana ana watu duniani ambao anawaheshimu. Lakini maneno yako, na jinsi yanavyosemwa mara kwa mara, yanajenga kutokuamini katika nafasi tuliyo nayo kama kanisa. Uko katika hatari ya kushindwa kushikilia imara imani ile ambayo hapo nyuma walikabidhiwa watakatifu, na kuharibu imani yako. Maneno yalisemwa: "Ufa mdogo sana utaizamisha meli. Kiungo kimoja chenye kasoro hufanya mnyororo kutokuwa na thamani." {8T 158.1}

### Waelimishe Wamisionari wa Tiba

Kumbuka, ndugu yangu, kwamba kazi ya umishenari wa tiba haipaswi kuchukua watu kutoka katika huduma, bali ni kuwaweka watu shambani, wenye sifa bora zaidi ya kuhudumu kwa sababu ya maarifa yao ya kazi ya umishenari wa tiba. Vijana wanapaswa kupokea elimu katika mielekeo ya kazi ya umisionari wa tiba na kisha waende kuungana na wachungaji. Hawapaswi kushawishika kujitoa pekee kwa kazi ya kuwaokoa wanadamu walioanguka na waliodhilika. Kazi hiyo inapatikana kila mahali na inapaswa kuunganishwa na kazi ya kuwaandaa watu wapate kuufanya Ukweli wa Biblia kuwa ulinzi wao dhidi ya maneno ya hila ya walimwengu na ya kanisa lililoanguka. Malaika wa tatu anapaswa kusonga mbele kwa uwezo mkuu. Mtu yeyote asiipuuze kazi hii au kuichukulia kuwa ni yenye umuhimu mdogo. 159 Ukweli unapaswa kutangazwa kwa ulimwengu, ili wanaume na wanawake wapate kuiona nuru. {8T 158.2}

## Kazi Yetu kwa Ajili ya Leo

Bwana anasema nini katika sura ya hamsini na nane ya Isaya? Sura nzima ni ya umuhimu wa juu kabisa. “Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii?” Mungu anauliza, “Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakuwa nyuma ukulinde. Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa. {8T 159.1}

"Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; Nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo." Mstari wa 6-9, 13, 14. {8T 159.2}

Hii ni kazi yetu. Nuru tuliyo nayo katika ujumbe wa malaika wa tatu ndiyo nuru ya Kweli. Alama ya mnyama ni kile hasa ambacho imetangazwa kuwa. Si yote kuhusiana na jambo hili hadi sasa yameeleweka, na hayataeleweka hadi kitabu kitakapofunguliwa; lakini kazi makini kabisa inabidi kutimizwa katika ulimwengu wetu. Agizo la Bwana kwa watumishi Wake ni: Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; uwahubiri watu Wangu kosa lao, na nyumba ya Yakobo dhambi zao." Aya ya 1. Ujumbe utakaoyaamsha makanisa unapaswa kutangazwa. Kila

juhudi inapaswa kufanywa kutoa nuru, si kwa watu wetu tu, bali kwa ulimwengu. Nimeagizwa kwamba unabii wa Danieli na Ufunuo unapaswa kuchapishwa katika vitabu vidogo, pamoja na maelezo muhimu, na kutumwa ulimwenguni kote. Watu wetu wenyewe wanahitaji nuru kuwekwa mbele yao kwa njia zilizo wazi zaidi. {8T 159.3}

### Hakuna Badiliko Katika Kusudi la Mungu

Hakupaswi kuwa na mabadiliko katika vipengele vya jumla vya kusudi la Mungu. Inabidii lijitokeze wazi na dhahiri kama ambavyo unabii umeifanya kuwa. Hatupaswi kuingia katika muungano wowote na ulimwengu, tukidhani kwamba kwa kufanya hivyo tunaweza kufanikisha zaidi. Ndugu yangu, kama utasimama katika njia ili kuzuia maendeleo ya kazi katika mielekeo ambayo Mungu ameiweka, utamchukiza sana. Ujumbe wa onyo unapaswa kutolewa, na baada ya kutimiza sehemu yako ya kazi kwa uaminifu, wewe hupaswi kuwazuia watumishi wengine wa Bwana kusonga mbele katika kuifanya kazi ambayo wanapaswa kufanya. Kufanya kazi kwa ajili ya waliodhiliwa na walioanguka hakupaswi kufanywa kuwa ndio mwelekeo mkuu na muhimu kabisa. Kazi hii inapaswa kuunganishwa na kazi ya kuyafundisha makanisa. Watu wetu wanapaswa kufundishwa jinsi ya kusaidia wahitaji na wanadamu waliotengwa na jamii. {8T 160.1}

Hakuna mwelekeo hata mmoja wa imani yetu ambao umetufanya kuwa kama tulivyo unapaswa kudhoofishwa. Tunazo alama za zamani za Ukweli, uzoefu, na wajibu, na tunapaswa kusimama imara katika kuzilinda kanuni zetu, ulimwengu ukiona waziwazi. Kwa mioyo iliyojaa shauku na kusihi, tunapaswa kutoa mwaliko kwa wale walio katika barabara kuu na barabara ndogo. Kazi ya umishenari ya tiba inapaswa kufanywa. Lakini hii ni sehemu moja tu ya kazi ambayo inapaswa kutimizwa, na haipasi kufanywa kuwa ndio yote katika yote. Inapaswa kuwa kwa kazi ya Mungu kama mkono ulivyo kwa mwili. Kunaweza kuwapo Watu wasiostahili ambao wamehusishwa na huduma, lakini bado hakuna mtu hata mmoja anayeweza kuipuuza huduma hii bila kumpuuza Mungu. {8T 160.2}

### Maonyo -Maneno ya Tahadhari

Ndugu yangu, unawakilishwa kwangu kama vile uko katika hatari ya kujitenga na watu wetu, ukijisikia kuwa wewe ni kitu kizima kabisa. Lakini ukijifungamanisha mwenyewe na hao wenye nia kama yako, mbali na kanisa, ambalo ni mwili wa Kristo, utafanya mapatano ambayo yatavunjwa vipande vipande; kwa maana hakuna muungano unaoweza kusimama isipokuwa ule ambao Mungu ameutengeneza. Wale wanaopokea elimu katika mielekeo ya tiba husikia masingizio mara kwa mara ambayo yanalishushia hadhi kanisa na kazi ya utume. Masingizio haya ni mbegu

zitakazochipua na kuzaa matunda. Wanafunzi wanaweza kuelimishwa vyema kutambua kwamba kanisa la Kristo duniani linapaswa kuheshimiwa. Wanahitaji maarifa dhahiri kuhusu sababu za imani yetu. Maarifa haya ni lazima wawe nayo, ili wapate kumtumikia Mungu kwa njia inayokubalika. Fungu juu ya fungu, amri juu ya amri, lazima wapokee ushahidi wa Biblia wa Ukweli kama ulivyo katika Yesu. {8T 161.1}

Ninakusihi, usiingize katika akili za wanafunzi mawazo ambayo yatawafanya wapoteze imani katika wachungaji walioteuliwa na Mungu. Lakini hili unalifanya kwa hakika, kwamba unalifahamu au la. Katika majaliwa Yake Bwana amekuweka katika nafasi ambapo unaweza kumfanyia kazi nzuri kuhusiana na huduma ya injili, kuleta Ukweli mbele ya wengi ambao vinginevyo hawangeifahamu. Majaribu yatakuja kwako kufikiri kwamba ili kuendeleza kazi ya umishenari wa tiba ni lazima ujitenge na mfumo wa kanisa au nidhamu ya kanisa, na usionyeshe moyo a kirafiki. Kusimama hivyo kungekuweka kwenye msingi usio imara. Kazi inayofanywa kwa ajili ya wale wanaokuja kwako kwa ajili ya mafundisho haijakamilika isipokuwa wameelimishwa kufanya kazi kwa kuhusiana na kanisa. {8T 161.2}

Kazi ya umishenari wa tiba haipaswi kufanywa kuwa ndio yote katika yote. Katika jambo hili unavuka mpaka, unapitiliza. Kuna kazi kubwa ya kufanywa. Machapisho yanayofundisha Kweli yanapaswa kusambazwa kila mahali. Wanafunzi wa tiba hawapaswi kuhimizwa kusambaza vitabu vile tu vinavyoshughulikia matengenezo ya afya. Uwe mwangalifu usije ukajikuta kuwa unatekeleza mipango yako mwenyewe, huku ukipuuza mipango ya Mungu. - {8T 161.3}

Dondoo kutoka kwa barua iliyoandikwa mnamo 1895 kutoka Cooranbong, New South Wales.--Ndugu yangu, Bwana Mungu wa Israeli lazima awe mshauri wako. Shetani ameshuka chini kwa nguvu nyingi kufanya kazi na madanganyo yote ya udhalimu. Mtegemee sana Kristo-jidondoshe Kwake kabisa. Umefanya kazi bila kuchoka kuleta matokeo mema. Usifanye makosa sasa. Kamwe, kamwe usijitahidi kuondoa alama hata moja ambayo Bwana amewapa watu Wake. Ukweli unasimama imara juu ya Mwamba wa milele-msingi ambao dhoruba na tufani haziwezi kusogeza kamwe. {8T 162.1}

Kumbuka kwamba mara tu unaporuhusu mvuto wako kuongoza mbali na njia iliyonyoka na nyembamba ambayo Bwana ameiweka kwa ajili ya watu Wake, usitawi wako utakoma; kwa maana Mungu hatakuwa kiongozi wenu. Tena na tena kumbukumbu ya maisha ya Nebukadreza imewasilishwa kwangu ili nikuwasilishie, ili upate kuonywa usiitumainie hekima yako mwenyewe, wala usimfanye mwanadamu kuwa silaha yako. Usiishushe bendera ya Ukweli au kuiruhusu ianguke kutoka mikononi mwako ili upate kuunganisha pamoja na ujumbe makini wa siku hizi za mwisho chochote ambacho kitaelekea kuficha sifa bainishi za imani yetu. {8T 162.2} 163

## SURA YA 26
## ONYO -Maneno Ya Tahadhari

Brisbane, Queensland, Australia,
Oktoba 26, 1898.

Kwa Washauri wa Wanafunzi wa Tiba-- Kuna mzigo rohoni mwangu. Kuna vijana ambao wanahamasishwa kufanya kozi ya masomo ya afya kama vile udaktari ambao wangepaswa kuwa wanajiandaa kwa dhati kabisa kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu. Sio lazima kwa wanafunzi wetu wa tiba kutumia muda wote ambao wanautumia katika masomo ya tiba (Medical Studies). Kazi yao inapaswa kuwa yenye makusudi/kukusudia zaidi ili ipate kuunganishwa na kujifunza Neno la Mungu. Mawazo yanakaziwa ambayo si ya lazima kabisa, na mambo muhimu hayapati usikivu wa kutosha. {8T 163.1}

### Hatari Tunayopaswa Kulindwa Dhidi Yake

Wanafunzi wanapoelimishwa kwa njia hii, wanafanywa wasiweze kutenda kazi inayokubalika kwa Bwana. Usumbufu ambao wanaupitia ili kupata maarifa ya ziada katika mielekeo ya tiba inawafanya wasifae kufanya kazi inavyopasa katika mielekeo ya huduma ya injili. Uchovu wa kimwili na wa kiakili huja kwa sababu ya kuelemewa na masomo, na kwa sababu wanafunzi wanahimizwa kufanya kazi isivyostahili kwa ajili ya waliotengwa na waliodhilika (degraded, wameshushwa hadhi kwa matendo, maneno na mwenendo). Kwa hiyo wengine wanakuwa hawana stahiki kwa ajili ya kazi ambayo wangefanya kama wangeanza kazi ya umishenari mahali pale ilipohitajika na kuruhusu mwelekeo wa tiba uingie kama sehemu muhimu inayohusiana na kazi ya huduma ya injili kwa ujumla, kama vile mkono unavyohusiana na mwili. Maisha hayapaswi kuhatarishwa katika jitihada za kupata

elimu ya tiba (Medical Education). Kuna hatari, katika hali fulani, kwamba wanafunzi wataharibu afya zao na kujifanya kukosa sifa za kufanya kazi ambayo wangeifanya kama wasingekuwa wametiwa moyo bila hekima kuchukua kozi ya tiba (Medical course). {8T 163.2}

Mara nyingi mawazo yenye makosa hunakiliwa akilini, na haya huongoza kwenye njia isiyo ya hekima ya utendaji. Wanafunzi wanapaswa kuwa na muda wa kuongea na Mungu, muda wa kuishi kila saa katika ushirika wa makusudi na kanuni za Ukweli na za haki na za rehema. Kwa wakati huu upelelezi wa moja kwa moja wa moyo ni muhimu. Mwanafunzi lazima ajiweke mahali ambapo anaweza kuchota kutoka katika Chanzo cha nguvu za kiroho na kiakili. Ni lazima atake kwamba kila kusudi linalohitaji huruma na ushirikiano wake liwe na kibali cha akili ambayo Mungu amempa, na dhamiri, ambayo Roho Mtakatifu anaitawala. Hatakiwi kufanya tendo lolote ambalo halipatani na kanuni za kina, zilizo takatifu zinazotoa nuru kwa roho yake na nguvu kwa mapenzi yake. Ni kwa hivyo tu, anaweza kumtolea Mungu utumishi wa juu kabisa. Hapaswi kufundishwa kwamba kazi ya umishenari wa tiba itamfungamanisha kwa mtu yeyote, ambaye ataamuru kazi yake iwe ipi. {8T 164.1}

Kazi ya umishenari wa tiba haipaswi kuvutwa kando na kutengwa na mfumo wa kanisa. Wanafunzi wa tiba (Medical Students) hawapaswi kupokea wazo kwamba wanaweza kujiona kuwa wanawajibika kwa viongozi katika kazi ya tiba peke yao. Wanapaswa kuachwa huru kupokea ushauri kutoka kwa Mungu. Hawapaswi kujidhamini wao wenyewe na mustakabali wao kwa kitu chochote ambacho wanadamu wanaokosea wanaweza kudokeza kwa ajili yao. Hakuna uzi wa ubinafsi unaopaswa kuvutwa kwenye mfumo; hakuna mpango utakaobuniwa ambao ndani yake kuna chembe moja ya udhalimu. Ubinafsi haupaswi kutawala mwelekeo wowote wa kazi. Hebu tukumbuke kwamba kama mtu mmoja mmoja, sisi tunafanya kazi huku tunatazamwa kwa wazi kabisa na ulimwengu wa mbinguni. {8T 164.2}

## Kiwango cha Juu

“Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako." Luka 10:27. Mara tu kabla ya kuwaacha wanafunzi Wake akirudi mbinguni, Kristo alitangaza: "Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo." Hapa tunaona kiwango kikiwa kimeinuliwa juu na juu zaidi. "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Yohana 13:34, 35. Wanafunzi hawakuweza kuelewa maneno ya Kristo kwa wakati ule; lakini baada ya kusulubiwa, kufufuka, na kupaa Kwake waliuelewa upendo Wake kuliko walivyowahi kuuelewa hapo awali. Waliuona ukioneshwa katika mateso Yake katika bustani, katika jumba la hukumu, na katika kifo Chake juu ya msalaba wa Kalvari. {8T 164.3}

## Kufundisha na Kuponya

Watu wa Bwana wanapaswa kuwa kitu kimoja. Hakupaswi kuwa na utengano katika kazi Yake. Kristo aliwatuma mitume kumi na wawili, na baadaye wale wanafunzi sabini, kuhubiri injili na kuponya wagonjwa. "Katika kuenenda kwenu," akasema, "hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure. Mathayo 10: 8. Na walipokwenda wakihubiri ufalme wa Mungu, walipewa uwezo wa kuponya wagonjwa na kutoa pepo wachafu. Katika kazi ya Mungu, kufundisha na uponyaji kamwe havipaswi kutenganishwa. Watu Wake wanaotunza amri wanapaswa kuwa kitu kimoja. Shetani atabuni kila hila ili kuwatenganisha wale ambao Mungu anatafuta kuwafanya kuwa wamoja. Lakini Bwana atajidhihirisha Mwenyewe kama Mungu wa hukumu. Tunafanya kazi chini ya macho ya jeshi la mbinguni. Yupo Mlinzi wa Kiungu kati yetu, anayekagua yote yanayopangwa na kutekelezwa. {8T 165.1}

## SURA YA 27
## SHIKILIA NA IINUE KAZI YA TIBA

Cooranbong, N.S.W., Februari 1, 1899.

Ninahutubia wale walio katika nyadhifa za kuwajibika katika Konferensi Kuu (General Conference) na wale wanaofanya kazi katika mwelekeo wa umishenari wa tiba. Nimeagizwa kuzungumza pia na kanisa la Battle Creek na makanisa yetu mengine yote. {8T 166.1}

Nimeagizwa kusema, kwa kurejelea kazi ya umishenari wa tiba, kwamba kuna hatari ya kugeuza mambo kwa kuelemea sana mwelekeo mmoja. Lakini ninachosema juu ya jambo hili hakipaswi kueleweka kwa maana yoyote ile kwamba ni kuwahalalisha wale ambao wamejiweka kandom na kutokuwa na moyo wa kirafiki na kazi ya umishenari wa tiba. Wapo wengi ambao hawajaiunga mkono kazi hii. Sasa wanapaswa kuwa waangalifu sana jinsi wanavyozungumza kuhusiana na kazi hiyo, kwa maana hawana akili juu ya jambo hilo kwa sababu hawajatembea katika nuru. Bila kujali nafasi yao katika kazi ya Mungu, wanapaswa kuwa waangalifu sana kutotoa matamshi kwa hisia zile ambazo zitakatisha tamaa na kuzizuia konferensi zetu kushikilia kazi hii. Msimamo ambao wengine wameuchukua kuhusu kazi ya umishenari wa tiba unafanya isiwezekane kwa maneno yao juu ya jambo hili kuwa na uzito wowote. Hawaoni kwa uwazi; mashauri yao yamepotoka. {8T 166.2}

Kila tawi la kazi linahitajika, lakini kila tawi la kazi linapaswa kuwa chini ya usimamizi wa Mungu. Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuwa kwa kusudi la Mungu kama mkono wa kuume ulivyo kwa mwili. Isingekuwa sawa kwa nguvu zote za mwili kwenda katika mkono wa kuume, na wala isingekuwa sawa kwa nguvu zote za kazi ya Mungu kutumika katika kazi ya umishenari wa tiba. Huduma ya Neno lazima iendelezwe, na lazima kuwe na umoja, umoja kamili, katika kazi ya Mungu. Wale ambao hawajahisi shauku/kuvutiwa na kazi ya umisionari wa tiba wanaukosea heshima mkono wa kuume wa kazi ya Mungu. Hebu wote kama hao wabadili mtazamo wao kwa kazi hii. Hebu na waseme maneno machache iwezekanavyo hadi pale watakapokuwa wamesimama katika nafasi sahihi. Ukimya ni ufasaha pale ambapo akili haijatakaswa na hivyo haiwezi kutambua mambo ya kiroho. {8T 166.3}

## Haja ya Tahadhari

Kwa sasa kuna haja kubwa ya kuwa na tahadhari. "Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika." Yakobo 1:19. Hebu tuzingatie onyo hili: “Ndugu zangu, nawasihi, waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliyojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, … na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu. Maana utii wenu umewafikilia watu wote; basi nafurahi kwa ajili yenu, lakini nataka ninyi kuwa wenye hekima katika mambo mema, na wajinga katika mambo mabaya." Warumi 16:17-19. {8T 167.1}

“Basi ndugu, nawasihi, kwa Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.” 1 Wakorintho 1: 10 Haya ndiyo mapenzi ya Mungu juu yetu. Je, tutayatii? “Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa kuwa imeandikwa, Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, Na akili zao wenye akili nitazikataa. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu? Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima Yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa. Kwa sababu Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima; bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi; bali kwao waitwao, Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu.” Aya ya 18-24. 168 {8T 167.2}

Ni mabadiliko ya namna gani yangeonekana ikiwa wote walio katika nafasi za kuwajibika wangetambua kwamba wanafanya kazi wakiangaliwa na Mungu aonaye yote. Kinachohitajika sasa ni utendaji huru wa Roho Mtakatifu kwenye akili na moyo.

Bila hili juhudi zetu hazitazaa matunda. Roho anapotufinyanga na kutuunda, maneno na matendo yetu yatadhihirisha shukrani za dhati. {8T 168.1}

### Umuhimu wa Kazi ya Umisionari wa Tiba

Kuna haja kubwa ya ongezeko la maarifa katika kila mwelekeo wa matengenezo ya afya. Wale ambao wamepata upendeleo wa kuusikia Ukweli wanapaswa kuipa tarumbeta sauti ya hakika pale wanapotangaza ujumbe wa malaika wa tatu. Mielekeo maalumu ya kazi inapaswa kuchukuliwa, kama vile kazi ya umishenari wa tiba. Kazi hii inapaswa kuendelezwa ikiungana na ujumbe wa injili kwa wakati wa sasa. Kazi ya dhati ya umishenari wa tiba ni injili kwa matendo. Wale ambao hawawezi kuona mwenendo wa kazi hii hawapaswi kujisikia kuwa wameidhinishwa kutawala awamu yake yoyote hadi pale watakapoelewa pande zake zote. {8T 168.2}

Nataka kusema kwa wazi kwamba Bwana ametimiza mema makuu kupitia katika kazi ya umishenari wa tiba, na kwamba Amemtumia tabibu wetu kiongozi kama wakala Wake aliyeteuliwa. Si kila kitu katika kazi ya tiba kimekuwa bila dosari. Pamoja nayo yamechanganywa mambo mengi ambayo yameharibu utakatifu wake. Lakini Bwana atachukua usimamizi wa kusudi Lake, naye ataona kwamba halikosi na kulingana katika tawi hili moja. Kazi hii haitaharibiwa ikiwa kanisa litainuka na kuangaza, likidhihirisha kwamba nuru yake imekuja, na kwamba utukufu wa Bwana umezuka juu yake. {8T 168.3}

Watendakaziwa umisionari wa tiba inabidi wasafishwe, watakaswe, kuboreshwa na kuadilishwa. Wanapaswa kupanda hadi kiwango cha juu kabisa cha ubora. Wanapaswa kukalibiwa/kufinyangwa na kuundwa kwa mfano wa Kiungu. Ndipo wataona kwamba matengeneza ya afya na kazi ya umisionari wa tiba zinapaswa kufungwa na mahubiri ya.8T 168.4}

Sababu inayowafanya washiriki wa kanisa wasilielewe tawi hili la kazi ni kwamba hawaifuati nuru, wakitembea hatua kwa hatua kumfuata Kiongozi wao mkuu. Kazi ya umisionari wa tiba ni ya Mungu nayo inabeba saini Yake. Kwa sababu hii, hebu mwanadamu aweke mikono yake mbali nayo na asitamani kuisimamia kulingana na mawazo yake mwenyewe. {8T 169.1}

Ujumbe wetu ni ujumbe wa ulimwengu wote. Na wakati ambapo fedha hazipaswi kutumika zote katika mwelekeo mmoja wa kazi, ili kwamba ujumbe wa mwisho wa injili usiweze kupelekwa katika maeneo mapya, kazi ya umisionari wa tiba haipaswi kushushiwa hadhi kwa namna yoyote ile; haipaswi kuwakilishwa kama kazi duni. Ulimwengu ni hospitali kubwa ya mkoma maskini wa dhambi; umeharibiwa na wakazi wake, na mateso yameenea kote ulimwenguni. Bwana amempa tabibu wetu kiongozi kazi ya kusaidia kuwaandaa watu ili wapate kusimama katika siku ile kuu ya Mungu. Lakini anapaswa kutenda kazi chini ya usimamizi wa Mungu. Kuna

baadhi ya mambo katika kazi Yake ambayo yatalazimika kufanyizwa katika mfano wa karibu na kanuni za Mtendakazi Mkuu. {8T 169.2}

## Chanzo cha Upungufu Kanisani

Yeye ambaye ameteuliwa kuchukua sehemu katika kazi kwa ajili ya wakati huu anapaswa kuhisi jukumu zito lililo juu yake. Tunafanya kazi kwa ajili ya umilele. Tukiula mkate uliotoka mbinguni tutakuwa kama Kristo katika roho na tabia. Tunaishi katika zama ambazo hazipaswi kuwa na uvivu wa kiroho. Kila nafsi inapaswa kuchajiwa na mkondo wa umeme wa mbinguni wa maisha. Swali mara nyingi huulizwa: "Ni nini sababu ya upungufu wa nguvu za kiroho katika kanisa?" Jibu linakuja: "Washiriki huruhusu akili zao kuvutwa mbali na Neno la Mungu." Tunajengwa kimwili kutokana na kile tunachokula, na kwa jinsi hiyo hiyo sifa bainifu ya hali yetu ya kiroho inaamuliwa na chakula kinachotolewa kwa akili. Tunapaswa kuipa akili na moyo lishe sahihi kwa kula mwili na kunywa damu ya Mwana wa Mungu. {8T 169.3}

Kristo anatangaza: "Amin, amin, nawaambia, Yeye aniaminiye yuna uzima wa milele……. Mimi Ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakachotoa Mimi ni mwili Wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu. Aulaye mwili Yangu anao uzima wa milele; Nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili Wangu ni chakula cha Kweli, na damu Yangu ni kinywaji cha kweli. Aulaye mwili Wangu na kuinywa damu Yangu hukaa ndani Yangu, Nami hukaa ndani yake……. Kama vile Baba aliye hai alivyonituma Mimi, Nami ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa Mimi. Yohana 6:47-57. {8T 169.4}

Ni lazima tukae ndani ya Kristo, na Kristo lazima Yeye akae ndani yetu; "kwa kuwa sisi tu watendakazi pamoja na Mungu." Kazi ya Mkristo ni kazi ya mtu binafsi. Hebu watenda kazi wa Mungu waache kutafuta makosa, maana hii ni dhambi. Hebu wafanye vizuri kama vile wanavyofikiri kwamba wafanyakazi wenzao wanapaswa kufanya. Ni fursa kwao kuishi ndani ya Kristo kwa kuula mkate wa uzima. Wale wanaofanya hivi watakuwa na uzoefu wenye afya, unaokua, na haki ya Mungu itawatangulia wanapofanya kazi iliyotajwa katika sura ya hamsini na nane ya Isaya. {8T 170.1}

## Kwa Kila Mtu Kazi Yake

Kila tawi la kazi ya Mungu linapaswa kutambuliwa. "Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa

wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe" Waefeso 4:11, 12. Maandiko haya yanaonesha kwamba kutakuwa na watenda kazi mbalimbali, vyombo mbalimbali. Kila mmoja ana kazi tofauti. Hakuna mtu anayehitajika kushikilia kazi ya mwingine, na, ingawa hajafunzwa, ajaribu kuifanya. Mungu amempa kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake. Mtu mmoja anaweza kufikiri kwamba cheo chake kinampa mamlaka ya kuwaamuru wafanyakazi wengine, lakini sivyo hivyo. Bila kujua kazi yao, angepanua mahali anapopaswa kupunguza, na kupunguza mahali anapopaswa kupanua kwa sababu anaweza kuona sehemu ile tu ya shamba la mizabibu anakofanyia kazi. {8T 170.2}

Ishi kwa ajili ya Mungu. Fanya mafundisho ya Mwokozi kuwa sehemu ya maisha yako. Njia yako itaangazwa na nuru safi, inayong'aa. Utapata kutiwa mafuta kutoka mbinguni na utazuiliwa kufanya makosa makubwa ya kijinga-hutaboronga mambo. Usiwe makini sana juu ya kazi unayoifanya katika sehemu moja ya shamba la Bwana la mizabibu kiasi kwamba huwezi kutambua kazi ambayo wengine wanafanya katika sehemu zingine za shamba la mizabibu. Wanaweza kuwa wanakuza vipaji vyao kwa uaminifu ili waweze kuvirudisha, kwa Mungu wao, vikiwa vimeongezeka maradufu. Hebu kila mtu na aitazame vyema kazi yake mwenyewe, akihakikisha kwamba imekamilika, pasipo doa wala kunyanzi kuharibu ukamilifu wake. Kisha mwache Mungu aseme: "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya Bwana wako." Mathayo 25:23. {8T 171.1}

## SURA YA 28
## UMOJA WA JUHUDI

Cooranbong, N.S.W.,
Aprili 17, 1899.

Kwa Tabibu Aliyekanganyikiwa—

Ndugu Yangu Mpendwa: Nina shauku kubwa kwako na kwa kazi yako, na ninaomba kwamba Bwana apate kuongoza kalamu yangu ninapokuandikia. Bwana amekufanya wewe kuwa mtu wa uteuzi Wake, na malaika wa Mungu wamekuwa wasaidizi wako. Bwana amekuweka katika nafasi uliyo nayo, si kwa sababu wewe huwezi kukosea, bali ni kwa sababu anatamani kuiongoza akili yako kwa Roho Wake Mtakatifu. Yeye Anatamani uwape wale ambao unakutana nao maarifa ya Ukweli wa

sasa. Majukumu mazito na ya kutisha yamekabidhiwa kwako, na kwa vyovyote vile usiruhusu kujiingiza katika mtego wa kazi ambayo itadhoofisha mvuto wako kwa Waadventista wa Sabato. Bwana amekuchagua wewe kujaza nafasi ya uteuzi Kwake, kusimama mbele ya taaluma ya tiba, sio ili upate kutengenezwa na mivuto ya kidunia, bali ili upate kuzitengeneza akili. Kila siku unapaswa kuwa chini ya usimamizi wa Mungu. Yeye Ndiye Bwana na Muumba wako, Mkombozi wako. Yeye Ana kazi kwako ya kufanya, si iliyotengwa na Waadventista wa Sabato, bali iliyounganishwa nao. Wewe unapaswa kuwa baraka kubwa kwa ndugu zako huku ukiwapa elimu ambayo [Mungu] amekupa. {8T 172.1}

Kupitia kwako Mungu amefanya kazi na bado anatamani kufanya kazi, akikuheshimu kwa kukukabidhi majukumu muhimu. "Sisi tu watenda kazi pamoja na Mungu." 1 Wakorintho 3: 9. Yeye Atakutumia wewe na pamoja na mimi na kila mwanadamu anayeingia katika utumishi Wake, ikiwa tutajisalimisha chini ya uongozi Wake. Kila mmoja anapaswa kusimama katika mnara wake wa ulinzi, akisikiliza kwa makini yale ambayo Roho atamwambia, akikumbuka kwamba kila neno na tendo lake huweka alama, si kwa tabia yake mwenyewe, bali kwa tabia za wale ambao anahusiana nao. {8T 172.2}

## Jengo la Mungu

"Ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu." Aya ya 9. Kielelezo hiki kinawakilisha tabia ya mwanadamu, ambayo inapaswa kufanyiwa kazi, hatua kwa hatua. Kila siku Mungu hufanyia kazi jengo Lake, pigo juu ya pigo la nyundo, ili kulikamilisha jengo, lipate kuwa hekalu takatifu Kwake. Mwanadamu anapaswa kushirikiana na Mungu. Kila mtenda kazi anapaswa kuwa vile Mungu amepanga apate kuwa, akijenga maisha yake kwa matendo safi, maadilifu, ili hatimaye tabia Yake ipate kuwa jengo lenye ulinganifu, hekalu zuri, linaloheshimiwa na Mungu na wanadamu. Hakupaswi kuwa na dosari katika jengo hilo, kwa kuwa ni la Bwana. Kila jiwe lazima liwekwe barabara kwa ukamilifu, ili liweze kustahimili shinikizo linalowekwa juu yake. Jiwe moja lililowekwa vibaya litaathiri jengo zima. Kwako wewe na kwa kila mfanyakazi mwingine, Mungu anatoa onyo hili: “Jihadharini jinsi mnavyojenga, ili jengo lenu listahimili majaribio ya dhoruba na tufani, kwa sababu limejengwa juu ya msingi wa Mwamba wa milele. Weka jiwe juu ya msingi ulio imara, ili upate kujiweka tayari kwa ajili ya siku ya kupimwa na kujaribiwa, wakati ambapo wote wataonekana kama walivyo hasa." {8T 173.1}

## Hekalu la Mawe Yaliyo Hai

Onyo hili Mungu analitoa kwangu kuwa ni muhimu hasa kwa ajili ya ustawi wenu. Yeye Anakupenda kwa upendo usiopimika. Anawapenda ndugu zako katika imani,

na anafanya kazi pamoja nao kwa kusudi sawa na lile ambalo kwalo anafanya kazi pamoja na wewe. Kanisa Lake duniani linapaswa kuchukua ulinganifu wa Kiungu mbele ya ulimwengu kama hekalu lililojengwa kwa mawe yaliyo hai, kila moja likiakisi nuru. Linapaswa kuwa nuru ya ulimwengu kama mji uliojengwa juu ya mlima ambao hauwezi kusitirika. Limejengwa kwa mawe yaliyowekwa pamoja, jiwe linalojipachika kwa jiwe lingine kwa kutosha barabara, na kufanya jengo imara, na madhubuti. Si mawe yote yana umbo au sura moja. Baadhi ni makubwa, baadhi ni madogo; lakini kila moja lina nafasi yake ya kujaza. Na thamani ya kila jiwe inaamuliwa na mwanga unaoakisi. Huu ni mpango wa Mungu. Yeye Anatamani wafanyakazi Wake wote wajaze nafasi zao walizopangiwa katika kazi kwa ajili ya wakati huu. {8T 173.2}

Tunaishi kati ya hatari za siku za mwisho. Tunapaswa kwa hekima kukuza kila nguvu ya kiakili na ya kimwili; kwa sababu wote wanahitajika ili kulifanya kanisa kuwa jengo litakalowakilisha hekima ya Mbunifu mkuu. Vipaji tulivyopewa na Mungu ni karama Zake, na vinapaswa kutumiwa katika uhusiano unaofaa baina na ya mtu na mwenzake ili kufanya kitu kimoja kikamilifu kabisa. Mungu hutoa vipaji, nguvu za akili; mwanadamu anaumba tabia. {8T 174.1}

## Mawakala Mbalimbali

Bwana ametenda kazi pamoja nawe, akikuwezesha kutenda sehemu yako kama mtenda kazi Wake; lakini kuna watenda kazi wengine pia ambao wanapaswa kutenda sehemu yao kama mawakala Wake. Hawa husaidia kutengeneza mwili mzima. Wote wanapaswa kuunganishwa kama sehemu za kiumbe kimoja kikuu. Kanisa la Bwana linaundwa na mawakala hai, wanaofanya kazi, ambao hupata uwezo wao wa kutenda kutoka kwa Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yao. Wanapaswa kuendeleza kwa upatanifu kazi ile kubwa iliyo juu yao. Mungu amekupa kazi yako. Lakini anao mawakala wengine, nao amewapa kazi yao, ili wote, kupitia kwa utakaso wa ile Kweli, wapate kuwa viungo vya mwili wa Kristo, vya nyama Yake na mifupa Yake. Tunapomwakilisha Kristo, tunatenda kwa ajili ya muda kitambo na kwa ajili ya umilele; na watu, hata watu wale waipendao dunia na anasa zake, wanatufahamu kwamba tumekuwa pamoja na Yesu na tumejifunza Kwake. {8T 174.2}

## Ukweli ni Mmoja

Watu wa Mungu hawapaswi kuwa katika mchafuko, wakikosa utaratibu na amani, msimamo na uzuri. Bwana anafedheheshwa sana wakati mafarakano yanapokuwepo kati ya watu Wake. Ukweli ni mmoja Umoja ule ambao Mungu anautaka ni lazima ukuzwe siku baada kwa siku kama tungeliitikia ombi la Kristo.

Mfarakano ambao unajitahidi kuwepo miongoni mwa wale wanaoungama kuwa kuuamini ujumbe wa mwisho wa rehema kutolewa kwa ulimwengu, lazima usipate nafasi; kwa maana utakuwa kikwazo cha kutisha kwa maendeleo ya kazi ya Mungu. Watumishi Wake wanapaswa kuwa kitu kimoja, kama Kristo alivyo umoja na Baba; nguvu zao, zilizoangaziwa, kuvuviwa, na kutakaswa, lazima ziunganishwe ili kufanya kitu kizima kikamilifu. Wale wanaompenda Mungu na kuzitunza amri Zake hawapaswi kujitenga; wanapaswa kuja karibu pamoja. {8T 174.3}

## Maneno ya Kufariji

Bwana hawaachi watenda kazi Wake waaminifu. Kumbuka kwamba maisha yetu katika ulimwengu huu ni safari tu, kwamba mbingu ndio maskani tunayoyaendea. Uwe na imani kwa Mungu. Ikiwa maneno yangu yamejeruhi na kuchubua roho yako, ninasikitika; Ninajeruhiwa na kuchubuliwa pia. Kazi yetu, kazi ya ajabu, kazi kubwa, tuliyopewa na Mungu, inatuunganisha moyo na roho pamoja. Usithubutu kuvua silaha zako. Inabidi uzivae hadi mwisho. Bwana atakapokuweka huru, itakuwa ni wakati wako wa kuweka silaha zako miguuni Pake. Wewe umejiandikisha katika jeshi Lake kuhudumu hadi mwisho wa vita, nawe hutajiaibisha na kumfedhehesha Mungu kwa kutoroka. {8T 175.1}

Bwana na akufungulie mambo mengi ambayo ameyafungua kwangu. Shetani anavizia fursa yake ya kulifedhehesha kusudi la Mungu. Nimeoneshwa hatari yako, na pia nimeoneshwa malaika wako mlinzi akikuhifadhi tena na tena kutoka kwako wewe mwenyewe, akikuzuia usije ukaiangamiza imani. Ndugu yangu, iinue bendera, iinue juu, wala usizimie moyo wala kukata tamaa. {8T 175.2}

Nimewapa viongozi katika Konferensi Kuu na Halmashauri ya Misheni, nuru niliyopewa na Mungu: kwamba wewe na wao mnapaswa kushauriana pamoja; kwamba, badala ya kujiweka pembeni bila moyo wa kirafiki, wanapaswa kuwa watumishi pamoja nawe; kwamba ulikuwa umeteuliwa na Mungu kusimama katika nafasi ya dhamana, na unahitaji msaada badala ya lawama. {8T 175.3}

Katika uzito wa shauku yangu kwamba unapaswa kutengeneza njia zilizonyoka kwa ajili ya miguu yako, nimekuandikia maneno ya dhati, lakini kamwe, kamwe, si kwa ajili ya kukushutumu au kukuhukumu. Laiti Mungu angekufanya uelewe kwamba shauku yangu ya kina kwako haijabadilika hata kidogo. Nina shauku ya dhati kabisa kwamba utasimama imara katika Mungu, ukiwa thabiti, ukiwa umejaribiwa, na kuwa Kweli. Ninajua kwamba Bwana anataka upate na taji ya ushindi. - {8T 176.1}

"Alipopaa juu aliteka mateka, Akawapa wanadamu vipawa……Naye aliyeshuka Ndiye Yeye aliyepaa juu sana kupita mbingu zote, ili avijaze vitu vyote. Naye alitoa wengine

kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike Kweli katika upendo na kukua hata tumfikie Yeye katika yote, Yeye aliye kichwa, Kristo. Katika Yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo." Waefeso 4:16. {8T 176.2}

## SURA YA 29
## KRISTO NDIYE NJIA YA MAOMBI NA BARAKA

Balaclava, Victoria, Australia,
Machi 25, 1898.

Kwa Tabibu wa Sanitariamu—

Ndugu Yangu Mpendwa: Nimepokea barua zako. Ninaona kuwa una vita ngumu ya kifedha kwa karibu. Ninafurahi sana kwamba unaweza kusikiza matumaini katika maneno haya: "Au azishike nguvu Zangu, Afanye amani Nami; Naam, afanye amani Nami." Isaya 27: 5. Hebu tumwamini Mungu. Hebu tuweke matumaini yetu Kwake. Yeye Anafahamu yote kuhusu hali ambayo tumewekwa ndani Yake, na atafanya kazi

kwa niaba yetu. Yeye Anaheshimiwa pale tunapomtumainia, tukimletea fadhaa zetu zote. “Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu,” Kristo anasema, “hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana.” Yohana 14:13. Manufaa na ruzuku za Mungu kwa niaba yetu hazina kikomo. Kiti cha neema chenyewe kinakaliwa na Yule anayeturuhusu kumwita Yeye Baba. {8T 177.1}

Lakini "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16 Yehova hakuona mpango wa wokovu kuwa umekamilika ukiwa umevikwa na upendo Wake tu. Amemweka katika madhabahu Yake Wakili aliyevikwa asili yetu. Kama Mwombezi wetu, kazi ya ofisi ya Kristo ni kututambulisha kwa Mungu kama wana na binti Zake. Yeye Anawaombea wale wanaompokea. Kwa damu Yake Mwenyewe amelipa fidia yao. Kwa wema Wake anawapa uwezo wa kuwa washiriki wa familia ya kifalme, watoto wa Mfalme wa mbinguni. Na Baba anaonesha upendo Wake usio na kikomo kwa Kristo kwa kupokea na kuwakaribisha marafiki wa Kristo kama marafiki Zake. Yeye Ameridhika na upatanisho uliofanywa. Anatukuzwa kwa kufanyika mwili, uzima, mauti, na upatanisho wa Mwanawe. {8T 177.2}

Katika Jina la Kristo maombi yetu yanapaa kwenda kwa Baba. Yeye anatuombea, na Baba anaweka wazi hazina zote za neema Yake kuwa fungu letu, ili sisi tuzifurahie na kuwagawia wengine. “Ombeni kwa Jina Langu,” Kristo asema. Sisemi kwamba nitawaombea kwa Baba; kwa maana Baba Mwenyewe anawapenda ninyi. Tumieni Jina Langu. Hii itayapa maombi yenu ufanisi, na Baba atawapa utajiri wa neema Yake. Kwa hiyo ombeni, nanyi mtapata, ili furaha yenu itimizwe.” {8T 178.1}

Kristo Ndiye kiungo kati ya Mungu na mwanadamu. Yeye Ameahidi maombezi Yake binafsi. Anaweka manufaa yote ya haki Yake upande wa mwombaji. Kristo anasihi kwa ajili ya mwanadamu, na mwanadamu, anayehitaji msaada wa Kiungu, anajiombea mbele za Mungu, akitumia nguvu ya mvuto wa Yule aliyetoa maisha Yake kwa ajili ya maisha ya ulimwengu. Tunapokiri mbele za Mungu utambuzi wetu wa stahiki za Kristo, harufu nzuri hutolewa kwa maombezi yetu. Tunapomkaribia Mungu kupitia manufaa ya stahili ya Mkombozi, Kristo anatuweka karibu na upande Wake, akituzungushia mkono Wake wa kibinadamu, wakati kwa mkono Wake wa Kiungu anashika kiti cha enzi cha Mungu cha milele. Yeye Anaweka stahili Zake, kama uvumba wenye harufu tamu, ndani ya chetezo iliyo mikononi mwetu, ili kuthibitisha maombi yetu. Yeye Anaahidi kusikia na kujibu dua zetu. {8T 178.2}

Ndio, Kristo amekuwa njia ya maombi kati ya mwanadamu na Mungu. Pia amekuwa njia ya baraka kati ya Mungu na mwanadamu. Yeye Ameunganisha Uungu na ubinadamu. Wanadamu wanapaswa kushirikiana Naye kwa ajili ya wokovu wa roho zao wenyewe, na kisha kufanya juhudi za dhati, za kudumu ili kuwaokoa wale

wanaokaribia kufa. {8T 178.3}

Ni lazima sote tufanye kazi sasa, kungalipo mchana; kwa maana usiku waja ambapo mtu hataweza kufanya kazi. Nina moyo mkuu katika Bwana. Kuna nyakati ambapo ninaoneshwa dhahiri kwamba katika makanisa yetu kuna hali fulani ya mambo ambayo haitazisaidia bali itazizuia roho. Halafu nina saa, na wakati mwingine siku kadhaa, za uchungu mkali. Wengi wa wale walio na ujuzi wa Ukweli hawayatii Maneno ya Mungu. Mvuto wao si bora kuliko mvuto wa walimwengu. Wanazungumza kama ulimwengu na kutenda kama ulimwengu. Moyo wangu unaumia kiasi gani ninapofikiri jinsi Mwokozi anavyoaibishwa na tabia zao zisizo kama za Kristo! Lakini baada ya uchungu kupita, ninahisi kufanya kazi kwa bidii zaidi kuliko hapo awali kurejesha roho maskini, ili waweze kudhihirisha sura ya Mungu. {8T 178.4}

Omba, ndiyo, omba kwa imani na tumaini isiyotikisika. Malaika wa agano, hata Bwana wetu Yesu Kristo, Ndiye Mpatanishi anayehakikisha kukubaliwa kwa maombi ya waumini Wake. {8T 179.1}

## SURA YA 30
## MANENO YA KUTIA MOYO

Cooranbong, N.S.W.,
Desemba 12, 1899.

Kwa Msimamizi wa Tiba wa Sanitariamu ya Battle Creek—

Ndugu Yangu Mpendwa: Unazungumza kana kwamba huna marafiki. Lakini Mungu ni rafiki yako, na Dada White ni rafiki yako. Umedhani kwamba nilikuwa nimepoteza imani kwako; lakini, ndugu yangu mpendwa, kama nilivyokuandikia hapo awali, ninajua ya kuwa Bwana amekuweka katika nafasi yenye dhamana kubwa sana, ukisimama kama ulivyo, tabibu ambaye Kwake Bwana ametoa maarifa na ufahamu,

ili upate kutenda haki na hukumu, na kudhihirisha roho ya kweli ya umishenari katika taasisi iliyoanzishwa kuwasilisha Ukweli kinyume na makosa. {8T 180.1}

Ndugu yangu, Bwana hajakuacha uende vitani kwa gharama zako mwenyewe. Yeye Amekupa hekima, na upendeleo kutoka kwa Mungu na wanadamu. Yeye Amekuwa msaidizi wako. Amekuchagua wewe kama wakala Wake wa kuuinua ukweli katika Sanitariamu ya Battle Creek kama ambavyo haiinuliwi katika taasisi za tiba za ulimwengu. Lilikuwa ni kusudi Lake kwamba Sanitariamu ya Battle Creek ipate kujulikana kama taasisi ambapo Bwana anathibitishwa na kuzingatiwa kila siku kama Mfalme wa ulimwengu. "Naye hufanya kama atakavyo, katika jeshi la mbinguni, na katika hao wanaokaa duniani; wala hapana awezaye kuuzuia mkono Wake, wala kumwuliza, Unafanya nini Wewe?" Danieli 4:35. {8T 180.2}

Bwana anapanga kwamba kutangazwa kwa ujumbe wa malaika wa tatu kutakuwa ndio kazi ya juu kabisa, kubwa kabisa inayofanywa katika ulimwengu wetu kwa wakati huu. Amekuheshimu wewe kwa kukuweka katika nafasi yenye dhamana kubwa sana katika kazi Yake. Hukupaswa kutenganisha mvuto wako kutoka kwa huduma ya injili. Katika kila mwelekeo wa kazi yako ulipaswa kuleta ufahamu na utiifu kwa Ukweli. Nafasi uliyopewa na Bwana ilikuwa chini Yake katika mfumo wa utawala wa Kiungu. Ulipaswa kujifunza kutoka kwa Yesu, Mwalimu Mkuu, ukipanga na kufanya kazi kupatana na mfano Wake. Ulipaswa kumfanya Mungu kuwa wa kwanza, ukilitii Neno Lake daima. Katika hili nguvu yako ingepatikana. {8T 180.3}

Ulipaswa kuwa tabibu mwaminifu wa roho pia na miili ya wale walio chini ya usimamizi wako. Ikiwa ungetimiza dhamana hii, ukitumia ipasavyo vipaji ulivyopewa na Mungu, usingekuwa umefanya kazi peke yako. Yeye ambaye kamwe hafanyi makosa alikuwa anaongoza. Ni uweza wa Roho Mtakatifu peke yake ndio unaoweza kuweka roho kuwa tamu na yenye harufu nzuri, laini na yenye upole, ukimwezesha mtenda kazi kunena maneno sahihi kwa wakati ufaao. {8T 181.1}

Hujawa mtu asiye na makosa. Mara nyingi umeshindwa kuzuia hasira. Ndipo maneno yako hayakuwa vile yalivyopaswa kuwa. Wakati fulani ulikuwa dikteta na mshurutishaji. Lakini pale ulipojitahidi kujitawala nafsi, malaika wa Mungu walishirikiana nawe, kwa sababu, kupitia kwako, Mungu alikuwa akifanya kazi ya kuutukuza Ukweli Wake na kuufanya upate utambuzi wa heshima duniani. Mungu alikupa hekima, si kwamba jina lako lipate kukuzwa, bali kwamba wale wanaokuja kwenye sanitariamu katika Battle Creek wapate kuondoka na mawazo mazuri kuhusu kazi ya Waadventista wa Sabato na heshima kwa kanuni ambazo ni msingi wa kazi yao. Heshima unayopewa haikuja kwako kwa sababu ulikuwa mwenye haki kuliko watu wote, bali ni kwa sababu Mungu alitaka kukutumia wewe kama Chombo Chake. {8T 181.2}

### Kusudi la Mungu katika Kuanzisha Sanitariamu

Lilikuwa ni kusudi la Mungu kwamba katika sanitariamu, wamishenari, walimu na matabibu wangepata maarifa ya ujumbe wa malaika wa tatu, ambao unajumuisha mambo mengi sana. Malaika wa Mungu walipaswa kuwa nguvu yako katika kazi ambayo ilipaswa kufanywa ili Sanitariamu ya Battle Creek ipate kujulikana kama taasisi iliyo chini ya usimamizi maalumu wa Mungu. Hisia ya umishenari na huruma iliyotawala katika taasisi hii ilikuwa ni matokeo ya kazi iliyofanywa huko na mawakala wa mbinguni wasioonekana. Mungu alisema: “Nimeona vema kuonesha ishara na maajabu. Kwa uwezo Wangu nalitukuza Jina Langu." Wengi wametoka katika sanitariamu wakiwa na mioyo mipya. Badiliko limekuwa dhahiri. Hawa, wanaporudi nyumbani kwao, wamekuwa kama nuru ulimwenguni. Sauti zao zimesikika zikisema: “Njoni, sikieni, ninyi nyote mnaomcha Mungu, Nami nitayatangaza aliyonitendea roho yangu. Nimeuona ukuu Wake; Nimeonja wema Wake." {8T 181.3}

### Kazi ya Ulimwengu Wote

Bwana amenionesha kwamba kama adui angeweza kwa njia yoyote ile kuigeuza upande kazi katika njia zisizo sahihi, na hivyo kuzuia maendeleo yake, atafanya hivyo. Watu wetu wengi wamefanya uwekezaji bila kukaa chini na kuhesabu gharama, bila kujua kama kulikuwa na pesa za kutosha kuendeleza kazi iliyoanzishwa. Ujinga-kutofikiria mambo ya wakati ujao umeoneshwa. Watu wameshindwa kuona kwamba shamba la mizabibu la Bwana linajumuisha ulimwengu. {8T 182.1}

Mapato ya sanitariamu ambazo zimeanzishwa hayapaswi kuchukuliwa ili kuendeleza mielekeo mingi ya kazi kwa ajili ya watu wa tabaka la chini katika miji yetu miovu. Fedha nyingi ambazo zimetumika kuendeleza kazi hii kubwa na inayoongezeka kila mara zingepaswa, kwa agizo la Bwana, kuwa zimetumika katika kujenga taasisi katika nchi zingine, ambapo nuru ya matengenezo ya afya haijaangaza. Sanitariamu, za gharama ndogo kuliko zile zilizo kubwa zilizojengwa Marekani, zilipaswa kujengwa katika nchi nyingi. Hivyo miundo mbinu hii ingetengenezwa ambavyo, inapokuwa na nguvu, ingesaidia kutengeneza miundombinu mingine katika maeneo mengine. {8T 182.2}

Bwana hana upendeleo. Lakini amewasilishwa vibaya na watenda kazi Wake. Yale ambayo yangepaswa kufanywa katika sehemu nyingi tofauti za shamba Lake la mizabibu yamezuiliwa sana, kwa sababu watu katika kiini cha kazi wameshindwa kuona jinsi ambavyo kazi ingeweza kuendelezwa katika sehemu za mbali zaidi za shamba la mizabibu. Katika baadhi ya sehemu za shamba kazi imefanywa kupita kiasi. Kwa njia hii pesa zimemezwa/zimetumika zote zile ambazo zingetumiwa kuwawezesha wafanyakazi katika sehemu zingine za shamba la mizabibu kusonga mbele bila kizuizi katika kusimamisha bendera ya Ukweli katika maeneo mapya. Baadhi ya sehemu za shamba la mizabibu hazipaswi kunyimwa ili kwamba fedha

zipate kutumika kwa uhuru katika sehemu nyingine za shamba. {8T 182.3}

Mwanadamu anahukumu kulingana na hukumu yake yenye kikomo. Mungu anaangalia sifa bainifu ya matunda yaliyozaliwa na kisha anauhukumu mti. Katika Jina la Bwana ninatoa wito kwa wote kufikiria kazi ambayo tunatakiwa kuifanya na jinsi kazi hii itakavyoendelezwa. Ulimwengu ni shamba la mizabibu la Bwana, nalo linapaswa kufanyiwa kazi. {8T 183.1}

Si idadi kubwa ya taasisi, majengo makubwa, na maonesho ya nje ambayo Mungu anataka, bali ni utendaji kwa upatanifu wa watu wa pekee, watu walioteuliwa na Mungu na wenye thamani kubwa, waliounganа kila mmoja na mwenzake, maisha yao yakiwa yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kila mtu anapaswa kusimama katika fungu lake na mahali pake, akitoa mvuto sahihi katika mawazo, maneno, na matendo. Wakati wafanyakazi wote wa Mungu watakapofanya hivi, wala si kabla ya wakati huo, kazi Yake itakuwa kitu kizima kikamilifu, chenye ulinganifu. {8T 183.2}

## Onyo

Mungu anataka taasisi Zake na watoto Wake wateule, walioasiliwa kumheshimu Yeye kwa kudhihirisha sifa za tabia ya Kikristo. Kazi ambayo injili inajumuisha kama kazi ya umisionari ni kazi ya halisi, iliyo kubwa, ambayo itang'aa zaidi na zaidi hadi kufikia siku ile kamilifu. Mungu hataki imani ya watu Wake ichukue sura au mwonekano wa kazi ya hisani ambayo sasa inaitwa kazi ya umishenari wa tiba. Fedha na vipaji vya watu Wake havipaswi kuzikwa katika mitaa michafu ya watu maskini waliobanana kule New York au Chicago (Geto au Slums). Kazi ya Mungu inapaswa kuendelezwa katika mielekeo sahihi. {8T 183.3}

Kujinyima na kujitolea kunapaswa kuoneshwa. Tunapaswa kufanya kazi kama Kristo alivyofanya kazi, kwa usahili na upole, katika unyenyekevu na kujiweka wakfu. Hivyo tutawezeshwa kufanya kazi Iliyo tofauti na kazi nyingine zote za kimishenari katika ulimwengu wetu. {8T 183.4}

Kuna wengi wa wale wanaopaswa kuokolewa kutoka kwenye shimo ambamo wameanguka ambao hawawezi kutegemewa kama washauri, au kuaminiwa kushiriki katika kazi katika siku hizi za mwisho. Adui amedhamiria kuchanganya makosa na Ukweli. Ili apate kufanya hivyo anatumia fursa anayopewa na tabaka la wanyonge ambalo kwa ajili yao kazi nyingi na fedha zinatumika, tabaka ambalo hamu yao ya chakula imepotoshwa kupitia kwa anasa, roho zao zimedhulumiwa, tabia zao zimeumbuka kwa kuundwa vibaya na kuharibika, ambao tabia na matamanio yao ni dhalili, wanaowaza maovu kwa desturi. Watu kama hao wanaweza kubadilishwa tabia; lakini ni wachache kiasi gani ambao kwao kazi hii ni kamili na ya kudumu! {8T 184.1}

Wengine watatakaswa kupitia ile Kweli; lakini wengi hufanya badiliko la juujuu tu

katika mienendo na mazoea yao, na kisha hudhania kwamba wao ni Wakristo. Wanapokelewa katika ushirika wa kanisa, lakini ni usumbufu mkubwa na taabu katika utunzaji. Kupitia kwao Shetani anajaribu kupanda katika kanisa mbegu za wivu, udanganyifu, ukosoaji, na lawama. Hivyo anajaribu kuwapotosha washiriki wengine wa kanisa. Tabia ambayo imewatawala tangu utotoni, ambayo iliwafanya waachane na vizuizi vyote na kuwashusha kwenye udhalilifu, bado inawatawala. Wanaripotiwa kuwa wameokolewa, lakini mara nyingi sana muda unaonesha kwamba kazi iliyofanywa kwa ajili yao haikuwafanya wawe watoto watiifu wa Mungu. Katika kila kuinuka kwa jambo dogo, linalodhaniwa kuleta hisia za kero. Wanathamini uchungu, ghadhabu, na uovu wa kudhamiria. Kwa maneno yao roho wanaonesha kwamba hawajazaliwa mara ya pili. Mielekeo yao ni ya kushuka chini, inayoelekea kwenye ufisadi na tamaa ya mwili. Hawaaminiki, hawana shukrani, si watakatifu. Hivyo ndivyo ilivyo kwa wote ambao hawajaongoka kwa dhati. Kila mmoja wa wahusika hawa walioharibika, wasiobadilishwa, anakuwa mtendakazi mwenye mafanikio wa Shetani, akizua mfarakano na ugomvi. {8T 184.2}

Bwana ameiwekea alama njia yetu ya kufanya kazi. Kama kanisa hatupaswi kuiga na kutumbukia katika mbinu za Jeshi la Wokovu. Hii si kazi ambayo Bwana ametupa tuifanye. Wala si kazi yetu kuwashutumu na kusema maneno makali dhidi yao. Kuna roho za thamani sana, na zenye kujitoa katika Jeshi la Wokovu. Tunapaswa kuwatendea kwa wema. Ndani ya Jeshi hili kuna roho waaminifu, wanaomtumikia Bwana kwa unyofu na ambao wataona nuru kuu zaidi, wakisonga mbele katika kuukubali Ukweli wote. Wafanyakazi wa Jeshi la Wokovu wanajaribu kuwaokoa wale waliopuuzwa, na kuonewa. Usiwakatishe tamaa. Waache wafanye kazi ya jinsi hiyo kwa mbinu zao na kwa njia zao wenyewe. Lakini Bwana ameonesha wazi kazi ambayo Waadventista wa Sabato wanapaswa kuifanya. Mikutano ya kambi na mikutano ya mahema inapaswa kufanyika. Ukweli kwa ajili ya wakati huu unapaswa kutangazwa. Ushuhuda thabiti uliodhamiriwa unapaswa kutolewa. Na hotuba zinapaswa kuwa sahili kiasi kwamba watoto wanaweza kuzielewa. {8T 184.3}

### Kumsaidia au Kumzuia Bwana

Wapo wale wanaoingia katika kazi ya umishenari wa tiba ambao wako katika hatari ya kuleta ndani yake hisia za kuchukiza walizozipokea katika elimu yao ya awali. Wanatakiwa kutekeleza kanuni zilizowekwa katika Neno la Mungu, vinginevyo kazi itaharibiwa na mawazo waliyokuwa nayo zamani kabla ya kupata ujuzi. Tunapofanya kazi kwa uwezo wote uliotakaswa ambao Mungu ametupa, tunapoweka kando mapenzi yetu kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, wakati nafsi inaposulubishwa siku kwa siku, ndipo matokeo mazuri yanapoonekana. Tunasonga mbele kwa imani, tukijua kwamba Bwana wetu ameahidi kufanya kazi aliyokabidhiwa Yeye, na kwamba ataitimiza; kwa kuwa Yeye hafanyi kosa wala kushindwa. {8T 185.1}

Watumishi wa Bwana ni mawakili tu. Bwana atafanya kazi kupitia wao watakapojisalimisha Kwake ili wafanyiwe kazi na Roho Mtakatifu. Wakati kwa imani wanadamu wanajiweka wenyewe katika mikono ya Bwana, wakisema, “Mimi hapa Bwana, nitume mimi,” Yeye anawakubali kwa ajili ya huduma. Lakini wanadamu hawapaswi kuzuia mipango Yake kwa hila za tamaa ya kutaka makuu. Kwa miaka mingi Bwana amekuwa na mapambano na watu Wake kwa sababu wamefuata maamuzi yao wenyewe na hawakutegemea hekima ya Mwenyezi Mungu. Hebu watenda kazi na waangalie wasije wakaingia katika njia ya Bwana, wakizuia maendeleo ya kazi Yake, wakifikiri kwamba hekima yao yatosha kwa ajili ya kupanga kwa mafanikio na kusonga mbele kwa kazi. Wakifanya hivi, Bwana atarekebisha makosa yao. Kwa Roho Yake ya Kiungu, Yeye anawaelimisha na kuwafunza watenda kazi Wake. Anatengeneza majaliwa Yake Mwenyewe ili kuendeleza kazi Yake kulingana na akili na mapenzi Yake. {8T 185.2}

### Kusudi la Mungu kwa Ajili ya Watendakazi Wake

Iwapo wanadamu watajinyenyekesha tu mbele za Mungu, kama hawatakuza maamuzi yao kuwa ndio uwezo wote wa kuongoza, kama watampatia Bwana nafasi ya kupanga na kufanya kazi, Mungu atatumia sifa alizowapa kwa namna ambayo italitukuza Jina Lake. Yeye Atawatakasa wafanyakazi Wake kutokana na ubinafsi wote, akikata matawi ambayo yangejisokota kuzunguka vitu visivyotakiwa, akipogoa mzabibu ili upate kuzaa matunda. Mungu Ndiye Mkulima mkuu. Atafanya kila kitu katika maisha ya wale ambao ni watenda kazi pamoja na Kristo kutii sana kusudi Lake kuu la ukuaji na uzaaji matunda. Ni mpango Wake, kwa kuwapatanisha watumishi Wake siku kwa siku ili wapate kufanana na sura ya Kristo, kwa kuwafanya kuwa washiriki wa asili ya Kiungu, awasababishe kuzaa matunda kwa wingi. Yeye Anataka watu Wake, kupitia uzoefu halisi katika ukweli wa injili, wawe wamishenari wa kweli, imara, waaminifu, wa hakika kwa vitendo na uzoefu. Angewataka waoneshe matokeo ya juu zaidi, matakatifu zaidi, na ya wazi zaidi kama ambavyo bado kudhihirishwa katika siku zetu hizi. {8T 186.1}

Mfinyanzi huchukua udongo mikononi mwake na kufinyanga na kuunda kulingana na mapenzi yake mwenyewe. Anaukanda na kuufinyanga. Anauchanachana kisha anaubonyeza pamoja. Anaulowesha kisha anaukausha. Anauacha ulale kwa muda bila kuugusa. Udongo mfinyanzi huu unapoweza kufinyangika/kupindika au kunyumbulika kwa urahisi kabisa, anaendelea na kazi ya kuutengenezea chombo. Anautengeneza katika umbo na kwenye gurudumu anaupunguza na kuing'arisha. Anaukausha kwenye jua na kuuoka katika tanuru/kabuli. Hivyo unakuwa chombo kinachofaa kwa matumizi. Hivyo ndivyo Mfanyakazi Mkuu anavyotamani kutufinyanga na kutuunda. Na kama vile udongo ulivyo mikononi mwa mfinyanzi, ndivyo tunavyopaswa kuwa mikononi Mwake. Hatupaswi kujaribu kufanya kazi ya mfinyanzi. Sehemu yetu ni kujisalimisha kwa kufinyangwa na Mfanyakazi Mkuu. {8T 186.2}

## Hitaji la Washauri Wenye Hekima

Bwana amewateua Matabibu katika sanitariamu kusimama kama walinzi waaminifu. Kupitia kwao Mungu anataka kufanya kazi ambayo ni lazima ifanyike katika taasisi hii. Walipaswa kuwa wasaidizi wako. Kupitia kwao mawazo yalipaswa kufanywa kuhusiana na kazi ya kuwafariji wanadamu wanaoteseka. {8T 187.1}

Lakini umetaka ushauri wa wengine kando ya watenda kazi-wenzako. Mawazo safi, mapya yalihitajika katika ushauri wako, kwa kuwa si mipango yako yote ilibeba sifa za kiungu. Umekuwa ukiziyumbisha akili za wale waliounganishwa nawe katika kazi ya umishenari wa tiba, hadi wewe pamoja na wao mmekuwa kama watu waliopotea katika ukungu wa kutokuwa na uhakika. {8T 187.2}

Nilielekezwa na Bwana kwamba jaribu lako lingekuwa ni kufanya kazi yako ya umishenari wa tiba isimame huru kutoka kwa konferensi. Lakini mpango huu haukuwa sawa. Niliona kwamba usingeweza kupanga kama ulivyokuwa ukifanya, au kutekeleza mawazo yako, bila madhara kwako wewe mwenyewe na kwa kusudi la Mungu. {8T 187.3}

## Msaidizi wa Kiungu

Ndugu yangu, kama daktari-mpasuaji umekuwa na wagonjwa mahututi wa kushughulikia, na nyakati fulani woga umekuja juu yako. Ili kutekeleza majukumu haya magumu, ulijua kwamba kazi ya haraka lazima ifanywe na kwamba hakuna hatua za udanganyifu zilipaswa kufanywa. Tena na tena ilibidi upite haraka kutoka kazi moja hadi nyingine. Ni nani amekuwa pembeni mwako ulipokuwa unafanya upasuaji huu muhimu na dharura kwa wakati mwingine? Ni nani amekufanya udumu kuwa mtulivu na mwenye kujiamini katika hali ya hatari, akikupa utambuzi wa haraka, hodari, kuona kwa wazi, mishipa ya fahamu iliyo thabiti, na usahihi mahiri? Bwana Yesu amemtuma malaika Wake pembeni mwako ili akuambie la kufanya. Mkono umewekwa juu ya mkono wako. Yesu, na si wewe, ameongoza mwendo wa kifaa chako. Wakati fulani umegundua hili, na utulivu wa ajabu ukaja juu yako. Hukuthubutu kufanya haraka, na bado ulifanya kazi kwa wepesi, ukijua kwamba hakukuwa na wakati wa kupoteza. {8T 187.4}

Bwana amekubariki sana. Umekuwa chini ya uongozi wa Mungu. Wengine ambao hawakujua Uwepo unakuongoza kufanya kazi pamoja nawe walikupa utukufu wote. Madaktari mashuhuri wameshuhudia upasuaji wako na kuusifu umahiri wako. Hili limekuwa la kupendeza kwako. Umeheshimiwa sana na Mungu kwamba Jina Lake, si lako, linapaswa kutukuzwa; lakini siku zote hujaweza kustahimili kuona kwa Asiyeonekana. Umekuwa na hamu ya kujipatia sifa, na hujaweka tegemeo lako lote kwa Mungu nyakati zote. Hujakuwa tayari kutii ushauri wa watumishi wa Bwana.

Kwa hekima yako mwenyewe umepanga mambo mengi. Bwana angependa uheshimu huduma ya injili. Wakati ule hasa ulipohitaji utambuzi, ili upate kuona, si upande mmoja tu wa kazi, bali pande zote, ulichagua washauri waliokuwa chini ya karipio la Mungu. Ulikuwa tayari kuungana nao ikiwa wangeunga mkono mapendekezo yako. {8T 188.1}

Kwa maombi na kujiweka wakfu, kwa kumtafuta Bwana kwa ajili ya hekima na kujisalimisha kwa uongozi Wake, ungezuiwa kuanzisha shughuli nyingi ambazo zimezaliwa, si kwa mapenzi ya Mungu, bali kwa mapenzi ya mwanadamu. Ulipewa kazi uliyopangiwa. Bali umepuuza mambo ya maana sana ili kuchukua, kwa roho ya harara, pasipo kushauriwa na Bwana wala ndugu zako, mambo yaliyo ya umuhimu mdogo. Ndugu zako wangeweza kukupa ushauri, lakini ulidharau neno lolote ambalo lingeliingilia mipango yako. Hii imekuweka katika nafasi ngumu. Lau ungedumu katika kazi yako uliyopangiwa, Mungu angekufanya zaidi na zaidi kuwa mtendakazi mwenye mafanikio pamoja Naye. {8T 188.2}

Bwana anataka akili yako ichanganyike na kupatana na akili zingine. Wakati mwingine, pale watumishi Wake walipotofautiana na wewe, hili ndilo jambo hasa ambalo Mungu alitaka walifanye. Lakini ulishughulikia ushauri wao kwa namna ambayo baadaye walinyamaza walipopaswa kusema. Mungu anawataka wale aliowaweka katika nafasi za dhamana kutenda haki na maamuzi na hukumu kwa hekima yote. {8T 189.1}

## Mizigo Ambayo Bwana Hajaitoa

Bwana alikupa kazi yako, sio ili ifanywe kwa kukurupuka, bali kwa namna ya utulivu, na busara. Bwana kamwe hashurutishi maendeleo ya haraka, yenye utata au hatua ngumu. Lakini wewe umejikusanyia majukumu ambayo Bwana, Baba Mwenye rehema, hakuweka juu yako. Wajibu ambao kamwe Yeye hakuagiza ufanye yanafukuzana bila mpango, wajibu mmoja baada ya mwingine. Kamwe watumishi Wake hawapaswi kuacha wajibu mmoja ukiwa umeharibika au kutokukamilika ili kushika mwingine. Yeye afanyaye kazi katika utulivu wa hofu ya Mungu hatafanya kazi bila mpangilio, kwa hofu kwamba kitu fulani kitazuia mpango unaotarajiwa. {8T 189.2}

Si mizigo yote ambayo umekuwa ukiibeba imewekwa juu yako na Bwana. Matokeo ya wewe kubeba mizigo hii ya ziada yanaonekana kote shambani. Kama ungedumu katika kazi yako uliyopangiwa, ukifanya kazi kwa ajili ya tabaka la watu ambao Bwana alitaka, kwa njia ya sanitariamu, kuwafikia kwa Ukweli wa sasa, na ujumbe ule ambao Mungu amewapa watu Wake ili wapate kuutoa kwa ulimwengu, mengi

zaidi yangelitimizwa katika kuwaleta wateule wa Mungu mbele ya watu wenye vyeo vya juu. Mengi zaidi yangetimizwa ili kuonesha njia na kazi na uweza wa Mungu. Sanitariamu ilipaswa kuwa shahidi Wake kwa niaba ya Ukweli - Ukweli ulioinuliwa, unaotakasa. Bwana alikufanya wewe, ndugu yangu, kuwa chombo Chake cha heshima. Yeye Hakuhitaji kamwe kutoka kwako kazi moja ambayo ingezuia kazi yako kuhusiana na taasisi ambayo ingesimama kwa ajili kuutetea Ukweli, kufanya kazi fulani kwa ajili ya Mungu, ikiangaza nuru katika njia ya maelfu. {8T 189.3}

Unayo kazi kubwa na takatifu ya kufanya. Kama utashikilia kwa uaminifu sehemu uliyopewa, kwa kutumia ujuzi uliopewa utawezeshwa kufanya kazi kwa wepesi, ingawa hutaonekana kuwa na haraka. Macho yako yakifumbuliwa, utaona umaskini mkubwa wa maeneo ya misheni. Utaona kuwa watenda kazi huko wanakwamishwa kwa kila hatua, huku pesa za Bwana zinatumika kuendeleza shughuli na taasisi za nyumbani, kiasi kwamba ujumbe unaopaswa kutolewa kwa ulimwengu mzima, unasahauliwa. {8T 190.1}

Mungu huwavutia watu mbalimbali kuwa watenda kazi pamoja Naye. Mtu mmoja hana mamlaka ya kukusanya majukumu mengi juu yake yeye mwenyewe. Bwana angetaka tabibu ambaye mengi sana yanamtegemea apate kufungamana Naye kwa karibu kiasi kwamba roho yake haitakasirishwa na mambo madogo madogo. Bwana anakutaka wewe uwe mmoja wa watenda kazi wenye ufanisi kabisa katika taaluma ya tiba, bila kudharau chochote, bila kukosa heshima, bila kuharibu chochote, ukijua kuwa una Mshauri aliye karibu pembeni mwako, kwa ajili ya kukuhimili na kukutia nguvu, kuipa roho yako amani na utulivu. Msisimko wa akili na mashaka ya roho yatafanya mkono kutokuwa na umahiri. Mguso wa Kristo juu ya mkono wa daktari huleta nguvu ya utendaji, utulivu, ujasiri, na uwezo. {8T 190.2}

Ninakuandikia kama vile mama anavyomwandikia mwanawe. Ningekusaidia kama ningeweza. Ningekuja kukuona kama ningejisikia kuwa ni wajibu wangu kuacha kazi hapa Australia, lakini sithubutu kulifanya hili. Umejijengea matumaini na umekuza mipango bila kuzingatia ipasavyo jinsi mnara huu unavyopaswa kukamilika. Kama mtu anayejua, kama mtu ambaye ameruhusiwa kuona matokeo ya kazi ambayo umejitolea kuifanya, ninakuomba na kutoa wito kwako, usimame na kutafakari. Mungu anajua umbo lako-fremu ya mwili wako. Anajua kuwa wewe ni mavumbi tu. Bila shaka utahitaji ushauri, si wa wale tu ambao wamekutia moyo kuendelea katika kazi ambayo unaiona kuwa ni ya muhimu sana, bali ni ushauri wa watu ambao, kwa wakati wa sasa, wanaweza kuona vizuri zaidi kuliko unavyoona matokeo yale ambayo yataifuata kazi fulani. {8T 190.3}

Usitupe nyuma yako kama kitu kisicho na maana maonyo yale ambayo bado hujayaelewa. Ikiwa utapokea ujumbe wa maonyo unayotumiwa, utaokolewa kutokana na jaribio kubwa. {8T 191.1}

Dondoo kutoka kwa barua iliyoandikwa mnamo mwaka wa 1899 kutoka Wellington, New Zealand--Hatupaswi kuruhusu mashaka na masikitiko yetu kutafuna roho zetu na kutufanya kuwa na kiherehere na pupa. Kusiwe na ugomvi, mawazo mabaya au kunena kwa ubaya, tusije tukamkasirisha Mungu. Ndugu yangu, kama utafungua moyo wako kwa ajili ya wivu na shuku mbaya, Roho Mtakatifu hawezi kukaa nawe. Jitahidi kupata utimilifu ulio ndani ya Kristo. Fanya kazi katika mielekeo Yake. Hebu kila wazo na neno na tendo vimdhihirishe Yeye. Unahitaji ubatizo wa kila siku wa upendo ambao katika siku za mitume uliwafanya wote kuwa na nia moja. Upendo huu utaleta afya kwa mwili, akili, na roho. Izungushie nafsi yako angahewa ambayo itaimarisha maisha ya kiroho. Kuza na kupalilia imani, tumaini, ujasiri, na upendo. Ruhusu amani ya Mungu itawale moyoni mwako. Kisha utawezeshwa kutekeleza majukumu yako. Roho Mtakatifu atatoa ufanisi wa Kiungu, hadhi tulivu, iliyotiishwa, kwa juhudi zako zote za kupunguza mateso. Utashuhudia kwamba umekuwa pamoja na Yesu. {8T 191.2} 192

## SURA YA 31
## THAMANI YA NENO LA MUNGU

Oakland, California, Juni 13, 1901.

Kwa Tabibu na Mkewe-- Ndugu na Dada Wapendwa: Safari yetu ya kuelekea nyumbani ilikuwa ni yenye mafanikio. Nilihudhuria mikutano katika sehemu nyingi. Huko Indianapolis nilishangazwa kukutana na idadi kubwa ya waumini. Nilizungumza mara mbili pale. Bwana alinipa ujumbe kwa watu hawa sawa na ule uliotolewa kule Battle Creek kuhusiana na makosa ambayo yamejipenyeza kati yetu. Watu hawa walikuwa tayari kusikia na kulipokea neno hili. {8T 192.1}

Makosa yanapokuja kwenye safu zetu, hatupaswi kuingia kwenye mabishano juu yake. Tunapaswa kwa uaminifu kutoa ujumbe wa karipio, na kisha tunapaswa kuzielekeza akili za watu mbali na mawazo dhanifu, yasiyo sahihi, tukiwasilisha uUweli kinyume na makosa. Uwasilishaji wa mada za mbinguni utaifungulia akili kanuni zile ambazo zinasimama juu ya msingi unaodumu kama vile umilele. {8T 192.2}

Wale waumini ambao imani zao za Kikristo ni shupavu na thabiti, ambao tabia zao ni za thamani thabiti, ni wa msaada mkubwa kwa Bwana. Hakuna kitakachoweza kuwaondoa katika imani. Ukweli kwao ni hazina ya thamani. {8T 192.3}

Ukweli wa Mungu unapatikana katika Neno Lake. Wale wanaojisikia kwamba ni lazima wautafute Ukweli wa sasa mahali pengine wanatakiwa wapate kuongoka upya. Wana tabia mbaya za kurekebisha, njia mbaya za kuachwa. Wanatakiwa kutafuta upya Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu, ili ujenzi wao wa tabia upate kulingana na masomo ya Kristo. Pale wanapoacha mawazo yao ya kibinadamu na kuchukua majukumu waliyopewa na Mungu, wakimtazama Kristo na kubadilishwa kufanana na mfano Wake, wanasema: "Karibu na Wewe, Mungu wangu, karibu zaidi." {8T 192.4}

Tukiwa na Neno la Mungu mkononi tunaweza kusogea karibu, hatua kwa hatua, kwa upendo uliowekwa wakfu kwa Yesu. Roho wa Mungu anapojulikana vyema zaidi, Biblia itakubaliwa kuwa msingi pekee wa imani. Watu wa Mungu watapokea Neno kama majani ya mti wa uzima, yaliyo na thamani kuliko dhahabu safi iliyosafishwa kwa moto, na yenye uwezo wenye nguvu katika kutakasa kuliko wakala mwingine yeyote. {8T 192.5}

### Thawabu ya Kujifunza Neno kwa Uaminifu

Kristo na Neno Lake wanapatana kabisa. Vikipokewa na kutiiwa, vinafungua njia ya hakika kwa miguu ya wote walio tayari kutembea katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru. Ikiwa watu wa Mungu wangefurahia Neno Lake, tungekuwa na mbingu katika kanisa hapa chini. Wakristo wangekuwa na shauku, njaa, katika kulichunguza Neno. Wangekuwa na hamu ya muda ule wa kulinganisha maandiko na Maandiko na kulitafakari Neno. Wangekuwa na shauku zaidi kwa ajili ya nuru ya neno kuliko kwa gazeti la asubuhi, magazeti la wiki/mwezi/mwaka, au riwaya. Tamaa yao kubwa kabisa ingekuwa ni kuula mwili na kunywa damu ya Mwana wa Mungu. Na matokeo yake maisha yao yangekubaliana na kanuni na ahadi za Neno. Mafundisho yake yangekuwa kwao kama majani ya mti wa uzima. Yangekuwa ndani yao

chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele. Manyunyu ya neema yenye kuburudisha yangeburudisha na kuhuisha roho, na kuwafanya wasahau taabu na uchovu wote. Wangeimarishwa na kutiwa moyo na Maneno ya uvuvio. {8T 193.1}

Wachungaji wangetiwa moyo na imani ya Kiungu. Maombi yao yangeonesha unyofu na bidii, yakijaa uhakika wa Kiungu wa Ukweli. Uchovu ungesahaulika katika nuru ya mbinguni. Ukweli ungefumwa pamoja na maisha yao, na kanuni Zake za mbinguni zingekuwa kama kijito baridi, kinachotiririka, kikituliza na kuburudisha roho daima. {8T 193.2}

Falsafa ya Bwana ndio kanuni ya maisha ya Mkristo. Kiumbe chote kinajazwa na kanuni za mbinguni zitoazo uhai. Pilikapilika za sifuri/bure zinazochukua muda wa watu wengi sana husinyaa kwenye nafasi yake sahihi mbele ya utii maridhawa wa Biblia wenye kutakasa. {8T 193.3}

Biblia, na Biblia peke yake, inaweza kuleta matokeo haya mazuri. Ni hekima ya Mungu na uweza wa Mungu, nayo inafanya kazi kwa uwezo wote katika moyo unaoipokea. Ni vilele vya juu kiasi gani tungeweza kuvifikia ikiwa tungepatanisha mapenzi yetu na mapenzi ya Mungu! Ni uweza wa Mungu ndio tunaouhitaji, popote tulipo. Upuuzi unaolisumbua kanisa hulifanya kuwa dhaifu, zembe na lisilojali. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wanatafuta na kutamani sana kupata njia ambazo kwazo watawasilisha kwa ulimwengu kanuni takatifu za Ukweli. {8T 194.1}

Taa za bandia zinaweza kuonekana, zikidai kuja kutoka mbinguni, lakini haziwezi kuangaza kama nyota ya utakatifu, nyota yenye uangavu wa mbinguni, kuongoza miguu ya msafiri na mgeni kuingia katika mji wa Mungu. Nuru bandia zitachukua nafasi ya ile ya Kweli, na roho nyingi zitadanganywa kwa kitambo. Mungu apishe mbali isije ikawa hivyo kwetu. Nuru ya Kweli sasa inaangaza, nayo itaziangazia roho ambamo madirisha yamefunguliwa kuelekea mbinguni. {8T 194.2}

## SURA YA 32
## KAZI KWA AJILI YA WAKATI HUU

St. Helena, California, Juni 25, 1903.
Kwa Matabibu Wetu wa Sanitariamu—

Ndugu Zangu Wapendwa: Wale wanaosimama katika nafasi za dhamana katika kazi ya Bwana wanawakilishwa kama walinzi kwenye kuta za Sayuni. Mungu anawaita ili wapige tarumbeta ya hatari miongoni mwa watu. Na isikike katika uwanda wote. Siku ya ole, ya kuacha ukiwa na uharibifu, iko juu ya wote watendao maovu. Kwa ukali wa pekee mkono wa Bwana utawaangukia walinzi ambao wameshindwa kuweka mbele ya watu katika mistari iliyo wazi wajibu wao Kwake Yeye ambaye kwa uumbaji na kwa ukombozi Ndiye mmiliki wao. {8T 195.1}

Ndugu zangu, Bwana anawaita ninyi kuuchunguza moyo kwa makini. Yeye Anakuiteni kuupamba Ukweli katika utendaji wenu wa kila siku na katika kutendeana kwenu ninyi kwa ninyi. Yeye Anahitaji kwenu imani ile itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa roho. Ni hatari kwenu kuchezea madai matakatifu ya dhamiri, ni hatari kwenu kuweka kielelezo ambacho huwaongoza wengine katika mwelekeo usio sahihi. {8T 195.2}

Wakristo wanapaswa kuchukua pamoja nao, popote waendapo, harufu nzuri ya haki ya Kristo, wakionesha kwamba wanakubaliana na mwaliko: "mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Mathayo 11:29. Je! mnajifunza kila siku katika shule ya Kristo-- mnajifunza jinsi ya kuondoa shaka na shuku mbaya, kujifunza jinsi ya kuwa wa haki na waadilifu katika kushughulika kwenu na ndugu zenu, kwa ajili yenu wenyewe, na kwa ajili ya Kristo? {8T 195.3}

Ukweli wa sasa unaongoza kwenda mbele na kwenda juu, ukiwakusanya wahitaji, walioonewa, wanaoteseka, na watu fukara. Wote watakaotaka kuja inabidi waletwe zizini. Katika maisha yao kutapaswa kufanyika matengenezo ambayo yatawafanya Kuwa washiriki wa familia ya kifalme, watoto wa Mfalme wa mbinguni. Kwa kusikia ujumbe wa Ukweli, wanaume na wanawake wanaongozwa kuikubali Sabato na kuungana na kanisa kwa ubatizo. Wanapaswa kuichukua alama ya Mungu kwa kuitunza/kuishika Sabato ya uumbaji. Wanapaswa kujua wenyewe kwamba kutii amri za Mungu kunamaanisha uzima wa milele. {8T 195.4}

Fedha na kazi ya bidii vinaweza kuwekezwa kwa usalama katika kazi kama hii, kwa kuwa ni kazi ambayo itadumu. Hivyo wale ambao wamekufa katika makosa na dhambi wanaletwa katika ushirika na watakatifu na kuketishwa katika ulimwengu wa roho mbinguni, pamoja na Kristo. Miguu yao inawekwa juu ya msingi imara. Wanawezeshwa kufikia kiwango cha juu, hata vilele vya juu kabisa vya imani, kwa sababu Wakristo hutengeneza njia zilizonyoka kwa ajili ya miguu yao, ili vilema wasije wakageuzwa kutoka katika njia. {8T 196.1}

Kila kanisa linapaswa kufanya kazi kwa ajili ya wale wanaoangamia walio ndani ya mipaka yake na kwa ajili ya wale walio nje ya mipaka yake. Washiriki wanapaswa kung'aa kama mawe yaliyo hai katika hekalu la Mungu, wakiakisi nuru ya mbinguni. Hakuna kazi ya kubahatisha, isiyo na malengo,nusunusu, ya hovyo ovyo, ya kigeugeu inapasa kufanyika. Kushikilia kwa nguvu roho za watu zilizo karibu na kuangamia kunamaanisha zaidi ya kumwombea mlevi na kisha, kwa sababu huyu mlevi analia machozi na kukiri uchafu wa roho yake, wewe unamtangaza kuwa ameokoka. Tena na tena vita lazima ipiganwe. {8T 196.2}

Hebu washiriki wa kila kanisa wajisikie kuwa ni wajibu wao maalumu kufanya kazi kwa ajili ya wale walio katika ujirani wao. Hebu kila mmoja anayedai kusimama chini ya bendera ya Kristo ajisikie kwamba ameingia katika uhusiano wa agano na Mungu, kwa ajili ya kufanya kazi ya Mwokozi. Hebu wale wanaofanya kazi hii wasichoke katika kutenda mema. Wakati waliokombolewa watakaposimama mbele za Mungu, roho za thamani kubwa zitakuwa na mwitikio kwa majina ya wale ambao watakuwapo pale kwa sababu ya juhudi za uaminifu, na uvumilivu zilizofanywa kwa niaba yao, kusihi kwingi na ushawishi wa dhati ili wapate kukimbilia Ngome. Hivyo ndivyo wale ambao katika dunia hii wamekuwa watenda kazi pamoja na Mungu watakavyopata thawabu yao. {8T 196.3}

Wachungaji wa makanisa yanayopendwa na wengi, yale ambayo ni maarufu, hawataruhusu Ukweli uwasilishwe kwa watu kutoka katika mimbari zao. Adui anawaongoza kuupinga Ukweli kwa ukali, hiana, uchungu na nia ya kuwadhuru wengine. Uwongo hutengenezwa. Uzoefu wa Kristo na watawala wa Kiyahudi unarudiwa. Shetani anajitahidi kuficha kila mwale wa nuru inayoangaza kutoka kwa Mungu kwenda kwa watu Wake. Anafanya kazi kupitia kwa wachungaji kama alivyofanya kupitia kwa makuhani na watawala katika siku za Kristo. Je, wale wanaojua Ukweli watajiunga na ushirika Wake, kuwazuia, kusumbua, kuwaaibisha na kuwageuza kando wale wanaojaribu kufanya kazi kwa njia iliyowekwa na Mungu ili kuendeleza kazi Yake, kusimamisha bendera ya Ukweli katika maeneo ya giza? {8T 197.1}

## Ujumbe Wetu

Ujumbe wa malaika wa tatu, unaojumuisha ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili, ndio ujumbe wa wakati huu. Tunapaswa kuiinua juu sana bendera ambayo imeandikwa: "Amri za Mungu na imani ya Yesu." Hivi karibuni ulimwengu utakutana na Mtoa Sheria Mkuu kuhusiana na sheria Yake iliyovunjwa. Huu sio wakati wa kusahau masuala makubwa yaliyo mbele yetu. Mungu anawaita watu Wake wapate kuitukuza sheria na kuifanya iheshimike. {8T 197.2}

Nyota za asubuhi zilipoimba/walipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu zilipopaza sauti kwa furaha, Sabato ilitolewa kwa ulimwengu, ili mwanadamu apate kukumbuka daima kwamba katika siku sita Mungu aliumba ulimwengu. Alipumzika katika siku ya saba, akiibariki kama siku ya pumziko Lake, na kuitoa kwa viumbe Aliowaumba, ili waweze kumkumbuka kama Mungu wa Kweli na aliye hai. Kwa uweza Wake mkuu, licha ya upinzani wa Farao, Mungu aliwakomboa watu Wake kutoka Misri, ili wapate kuitunza sheria ile iliyotolewa katika bustani Edeni. Aliwaleta hadi Sinai ili wapate kusikia kutangazwa kwa sheria hii. {8T 197.3}

Kwa kuwatangazia wana wa Israeli Amri Kumi kwa sauti Yake Mwenyewe, Mungu alionesha umuhimu Wake. Kwa fahari ya kutisha, Yeyealidhihirisha ukuu na mamlaka Yake kama Mtawala wa ulimwengu. Hili alilifanya ili apate kuwavutia watu kwa utakatifu wa sheria Yake na umuhimu wa kuitii. Uweza na utukufu ambavyo kwavyo sheria ilitolewa hudhihirisha umuhimu wake. Ni imani iliyotolewa hapo nyuma, kwa watakatifu na Kristo Mkombozi wetu inayozungumza kutoka Sinai. {8T 198.1}

## Ishara ya Uhusiano Wetu na Mungu

Kwa utunzaji wa Sabato wana wa Israeli walipaswa kutofautishwa na mataifa mengine yote. "Hakika mtazishika Sabato Zangu" Kristo alisema "kwa kuwa ni ishara kati ya Mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye ninyi." “Ni ishara kati ya Mimi na wana wa Israeli milele; kwani kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika." “Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni Agano la milele. Kutoka 31: 1317. {8T 198.2}

Sabato ni ishara ya uhusiano uliopo kati ya Mungu na watu Wake, ishara ya kwamba wao ni raia Wake watiifu, kwamba wanaitunza sheria Yake kuwa takatifu. Utunzaji wa Sabato ni njia iliyoteuliwa na Mungu ya kuhifadhi maarifa juu Yake Yeye Mwenyewe na kutofautisha kati ya raia Wake waaminifu na wavunjaji wa sheria Yake. Hii ndiyo imani iliyotolewa hapo nyuma kwa watakatifu, wanaosimama mbele ya ulimwengu kwa nguvu ya maadili, wakidumisha imani hii kwa uthabiti. {8T 198.3}

Tutakuwa na upinzani tutakapoutangaza ujumbe wa malaika wa tatu. Shetani ataleta kila hila iwezekanayo ili kuifanya kuwa bure imani ile iliyokabidhiwa kwa watakatifu hapo nyuma. “Na wengi watafuata ufisadi wao; na kwa hao njia ya Kweli itatukanwa. 2.3 Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambao hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii.” 2 Petro 2:2, 3. Lakini licha ya upinzani, wote wanapaswa kusikia Maneno ya Ukweli. {8T 199.1}

Sheria ya Mungu ni msingi wa matengenezo yote yanayodumu. Tunapaswa kuwasilisha kwa ulimwengu kwa mipaka iliyo wazi na dhahiri hitaji la kutii sheria hii. Utii kwa sheria ya Mungu ndio motisha kubwa kabisa kwa ajili ya bidii ya kazi, tasnia, uwekezaji/uwekevu, Ukweli, na matendo ya haki kati ya mwanadamu na mwanadamu. {8T 199.2}

Sheria ya Mungu inapaswa kuwa ndio njia ya elimu katika familia. Wazazi wako chini ya wajibu mzito kabisa wa kuitii sheria hii, wakiwawekea watoto wao kielelezo cha uadilifu mkamilifu kabisa. Watu walio katika nafasi za dhamana, ambao mvuto wao unaenea sana, wanapaswa kuzilinda vyema njia na kazi zao, wakiweka hofu ya Bwana mbele yao daima. "Kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima." Zaburi 111:10. Wale wanaoisikiliza sauti ya Bwana kwa bidii na kuzishika amri Zake kwa furaha watakuwa miongoni mwa ile hesabu ya watakaomwona Mungu. "BWANA akatuamuru kuzifanya amri hizi zote, tumche Bwana, Mungu wetu, tuone mema siku zote, ili atuhifadhi hai kama hivi leo. Tena itakuwa haki kwetu, tukitunza kufanya maagizo haya yote mbele ya Bwana, Mungu wetu, kama alivyotuagiza." Kumbukumbu la Torati 6:24, 25 . {8T 199.3}

Kazi yetu kama waumini katika Ukweli ni kuwasilisha mbele ya ulimwengu kutokubadilika kwa sheria ya Mungu. Wachungaji na walimu, wadaktari na wauguzi, wanafungwa na agano na Mungu kuwasilisha umuhimu wa kutii sheria Yake. Tunapaswa kutofautishwa kama watu wanaoshika amri. Bwana amesema kwa uwazi kwamba ana kazi ya kufanywa kwa ajili ya ulimwengu. Je, itafanywaje? Hebu tujitahidi kutafuta njia iliyo bora kabisa na kisha tuyatende mapenzi ya Bwana. {8T 199.4}

Ulimwengu huu ni shule ya mafunzo kwa ajili ya shule ya juu zaidi, maisha haya ni maandalizi ya maisha yajayo. Hapa tunapaswa kujiandaa kwa ajili ya kuingia nyua za mbinguni. Hapa tunapaswa kupokea na kuamini na kutenda Ukweli hadi tuwe tayari kwa ajili ya makao pamoja na watakatifu walio katika nuru. {8T 200.1}

Sanitariamu zetu zinapaswa kuanzishwa kwa lengo moja – utangazaji wa Ukweli kwa ajili ya wakati huu. Na zipaswa kuongozwa/kuendeshwa kiasi kwamba mvuto wa dhati kwa ajili ya ukweli utawekwa katika akili za wale wanaozijia kwa ajili ya kupata matibabu. Mwenendo wa kila mfanyakazi unapaswa kuhubiri upande wa haki. Sisi tunao ujumbe wa onyo wa kuuhubiri ulimwengu, na bidii yetu, kujitoa kwetu kwa ajili ya utumishi kwa Mungu, yapasa kutoa ushahidi juu ya Ukweli. {8T 200.2}

## SURA YA 33
## MTAZAMO MPANA ZAIDI

St. Helena, California, Oktoba 30, 1903.

Kwa Wamishenari wa Tiba-- Kristo, Mmishenari mkuu wa Tiba, alikuja katika ulimwengu wetu kama mfano mkamilifu wa Ukweli wote. Ukweli haukunyong'onyea midomoni Mwake, haukuwahi kushindwa mikononi Mwake. Maneno ya Ukweli yalianguka kutoka katika midomo Yake yakiwa na usafi na uwezo wa ufunuo mpya. Yeye Alifunua siri za ufalme wa mbinguni, akitoa tunu moja baada ya nyingine ya Ukweli-Kito baada ya kito. {8T 201.1}

Kristo alizungumza kwa mamlaka. Kila Ukweli ulio muhimu kwa ajili ya watu kujua aliutangaza kwa moyo wa kujiamini usiosita wenye maarifa yakini. Hakusema chochote chenye urembo wa kudhania-dhania au cha kusukumwa na hisia wala akili. Hakuwasilisha maoni yoyote ya kijinga, hakuna maoni ya wanadamu. Hakuna maneno ya upuuzi, hakuna nadharia za uwongo zilizovikwa lugha nzuri, zilizotoka midomoni Mwake. Kauli alizozitoa zilikuwa ni Ukweli uliothibitishwa na maarifa binafsi. Aliona mbele mafundisho ya uwongo ambayo yangeujaza ulimwengu, lakini hakuyatangaza. Katika mafundisho Yake alijikita katika kanuni zisizobadilika za Neno la Mungu. Alizikuza Kweli sahili, zilizo katika vitendo na ambazo watu wa kawaida wangeweza kuzielewa na kuzileta katika uzoefu wa kila siku. {8T 201.2}

Kristo angeweza kuwafungulia wanadamu Kweli za kina kabisa za sayansi. Angeweza kuzifungua siri ambazo zimehitaji karne nyingi za kazi ya taabu na utafiti ili zipenye ndani ya moyo. Angeweza kutoa mapendekezo katika mielekeo ya kisayansi ambayo yangeweza kutoa mambo ya kuwazia na kichocheo cha uvumbuzi hadi mwisho wa wakati. Lakini hakufanya hivi. Yeye Hakusema lolote ili kuridhisha udadisi au kutosheleza tamaa ya makuu ya mwanadamu kwa kufungua milango kwa ajili ya ukuu wa kidunia. Katika mafundisho Yake yote, Kristo alileta mawazo ya wanadamu kukutana Akili isiyo na kikomo. Yeye Hakuwaelekeza watu kujifunza nadharia za watu kuhusu Mungu, Neno Lake, au kazi Zake. Aliwafundisha kumwona Mungu kama anavyodhihirishwa katika kazi Zake, katika Neno Lake, na kwa majaliwa Yake. {8T 201.3}

### Ushindi wa Kristo Juu ya Kutokuamini

Alipokuwa katika dunia hii, Mwana wa Mungu alikuwa ni Mwana wa Adamu; lakini kulikuwa na nyakati ambapo Uungu Wake ulijitokeza ghafla. Ndivyo ilivyokuwa pale

alipomwambia yule aliyepooza: "Jipe moyo mkuu, mwanangu, umesamehewa dhambi zako." Mathayo 9:2. {8T 202.1}

“Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi, “wakifikiri” si waziwazi bali “mioyoni mwao,” wakisema, “Ni nani huyu asemaye maneno ya kukufuru? Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke yake? " Marko 2:6; Luka 5:21. {8T 202.2}

“Naye Yesu, hali akijua mawazo yao, akasema, Mbona mnawaza maovu mioyoni mwenu? Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, Ondoka, uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (amwambia yule mwenye kupooza) Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako.” Mathayo 9:4-6. {8T 202.3}

Mmishenari mkuu wa tiba aliziondoa dhambi za yule aliyepooza na kisha akamwasilisha kwa Mungu kama mtu aliyesamehewa. Naye akampa pia uponyaji wa kimwili. Mungu alikuwa amempa Mwanawe uwezo wa kukishika kiti cha enzi cha milele. Wakati ambapo Kristo alisimama kwa nafsi Yake Yeye Mwenyewe, aliakisi fahari na mng’ao nafasi wa heshima ambayo Alikuwa ameishikilia ndani ya nuru yenye kusitawisha ya kiti cha enzi cha milele. {8T 202.4}

Katika tukio lingine Kristo alitoa ombi: "Baba, ulitukuze Jina Lako." Na kwa kujibu "ikaja sauti kutoka mbinguni, Nimelitukuza, Nami nitalitukuza tena." Yohana 12:28. {8T 202.5}

Ikiwa sauti hii haikuwagusa wale wenye mioyo migumu, ikiwa uweza ambao Kristo aliudhihirisha katika miujiza Yake mikuu haikuwafanya Wayahudi kuamini, hatupaswi kushangaa sana kutambua kwamba wanaume na wanawake leo wako katika hatari, kupitia ushirika wa daima na wale wasioamini, ya kudhihirisha ukafiri uleule ambao Wayahudi walioudhihirisha, na kukuza ufahamu uleule uliopotoka. {8T 202.6}

Ninapata huzuni isiyoelezeka ninapotafakari yale ambayo yamefunguliwa mbele yangu kuhusu hali ya mambo huko Battle Creek na vituo vingine vya kazi yetu, ambapo nuru kuu imekuwa ikimulika. Hapo awali, mambo yanapooneshwa kuwa mabaya, kulikuwapo na utambuzi wa kosa, na hilo likafuatiwa na ungamo, toba, na matengenezo kamili. Lakini hivi karibuni hakujakuwapo na mawakili waaminifu wa kuzuia maovu ambayo yalihitaji kuzuiwa. Je, tunaweza, basi, kushangazwa kwamba kuna upofu mkubwa wa kiroho? {8T 203.1}

Wale wanaohusika katika huduma ya injili wanatakiwa kujifunza kutoka kwa Kristo

upole na unyenyekevu Wake, na kuongoka kabisa, ili maisha yao yaweze kuushuhudia ulimwengu uliokufa katika makosa na dhambi kwamba wamezaliwa upya tena, wamezaliwa kwa mara ya pili. Wafanyakazi wa umisionari wa tiba, pia, wanahitajika kuongoka. Watakapoongoka, mvuto wao utakuwa nguvu ya wema duniani. Watakuwa tayari kupokea ushauri na msaada kutoka kwa ndugu zao, kwa sababu wametakaswa kupitia Ukweli. Kila siku watapokea neema tele kutoka mbinguni ili kuwagawia wengine. {8T 203.2}

Kwa kila mmoja wa mawakala Wake wateule Bwana hutuma ujumbe: "Shika nafasi yako katika kituo chako cha kazi, kisha simama imara kuitetea haki." Kwa wote nimeagizwa kusema: "Tafuta mahali pako. Usipokee hisia za kuwaziwa/kufikirika za watu ambao hawajafundishwa na Mungu. Kristo anangoja kukupa ufahamu wa mambo ya mbinguni, akingoja kuhuisha mapigo yako ya kiroho kwa shughuli iliyofanywa upya. Usiendelee kuweka chini madai ya siku zijazo, maslahi ya milele kwa ajili ya mambo ya kawaida ya maisha haya. "Hamwezi kumtumikia  Mungu na mali." Mathayo 6:24. Amkeni, ndugu zangu, amkeni." {8T 203.3}   204

Upana wa kazi ya injili kwa umishenari wa tiba haueleweki. Kazi ya umishenari wa tiba inayotakiwa sasa ni ile iliyoainishwa katika agizo ambalo Kristo aliwapa wanafunzi Wake kabla tu ya kupaa Kwake. “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani,” alisema. "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi. siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Mathayo 28:18-20 {8T 204.1}

Maneno haya yanaonesha shamba letu na kazi yetu. Shamba letu ni ulimwengu; kazi yetu ni utangazaji wa Kweli zile ambazo Kristo alikuja katika ulimwengu wetu kuzitangaza. Wanaume na wanawake wanapaswa kupata fursa ya kupata ujuzi wa Ukweli wa sasa, fursa ya kujua kwamba Kristo ni Mwokozi wao, kwamba Mungu aliupenda ulimwengu sana, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee. bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16 {8T 204.2}

### Onyo Dhidi ya Uwekaji wa Mamlaka katika Sehemu Moja  (Centralization)

Kristo aliujumuisha na kuukumbatia ulimwengu katika kazi Yake ya umishenari, na Bwana amenionesha kwa ufunuo kwamba si mpango Wake kwa vituo vikubwa kujengwa, kwamba taasisi kubwa zianzishwe, na kisha fedha za watu wetu katika sehemu zote za dunia kumalizwa katika kutegemeza taasisi kubwa chache, wakati haja za nyakati zinataka jambo fulani lifanyike, kadiri majaliwa yanvyofungua njia, katika sehemu nyingi. Viwanda vya Taasisi au Vituo vya Misheni vinapaswa kufunguliwa/kuanzishwa katika maeneo mbalimbali duniani kote (viwanda vya

chakula, uchapishaji, shule, vituo vya afya, Ofisi ya Konferensi nk). Kwanza sehemu moja, na kisha nyingine, ya shamba la mizabibu itaingiwa, hadi maeneo yote yamelimwa. Jitihada zinapaswa kufanywa popote penye uhitaji mkubwa zaidi. Lakini hatuwezi kuendeleza vita hivi vikali na wakati uo huo kufanya matumizi ya ubadhirifu wa fedha katika maeneo machache. {8T 204.3}

Sanitariamu ya Battle Creek ni kubwa mno. Watendakazi wengi zaidi watahitajika kuwahudumia wagonjwa wanaokuja. Sehemu moja ya kumi ya idadi ya wagonjwa wanaokuja kwenye taasisi hiyo ni wengi zaidi ya idadi ile inayoweza kuhudumiwa kwa matokeo bora katika kituo kimoja cha umishenari wa tiba. Vituo vinapaswa kuwekwa katika miji yote ambayo haijafahamu kazi kubwa ambayo Bwana angefanya ili kuuonya ulimwengu kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia. “Kuna mengi mno,” amesema Mwalimu Mkuu, “katika sehemu moja.” (miundo mbinu, makanisa mahalia, taasisi mbalimbali nk) {8T 205.1}

Hebu wale ambao wamejiandaa wenyewe kushiriki katika kazi ya umishenari wa tiba katika nchi za kigeni waende mahali ambapo wanatazamia kupafanya kuwa uwanja wao wa kazi, na kuanza kazi moja kwa moja miongoni mwa watu, wakijifunza lugha kadiri wanavyofanya kazi. Punde watajikuta kwamba wanaweza kufundisha kweli sahili za Neno la Mungu. {8T 205.2}

### Sehemu Iliyopuuzwa Iliyo Karibu Nasi

Kuna uwanja mzuri sana katika nchi hii, eneo kubwa ambalo halijafanyiwa kazi. Jamii ya watu weusi, wanaofikia idadi ya maelfu kwa maelfu, inasihi na kuvuta wema na huruma ya kila muumini wa Kristo aliye wa kweli na wa vitendo. Watu hawa hawaishi katika nchi ya kigeni, wala hawazisujudii sanamu za miti na mawe. Wanaishi miongoni mwetu, na tena na tena, kupitia shuhuda za Roho Wake, Mungu ametoa wito wa usikivu wetu kwao, akituambia kwamba hapa kuna wanadamu waliopuuzwa. Uwanja huu mpana upo mbele yetu bila kufanyiwa kazi, ukitaka nuru ambayo Mungu ametukabidhi kama dhamana (Mwaka 1865 Kulikuwa wa Waamerika weusi 4.5 Milioni). {8T 205.3}

## SURA YA 34
## KRISTO MFANO WETU

St. Helena, California, Oktoba 30, 1903.
Kwa Wamishenari wa Tiba

Kinachohitajika zaidi na wamisionari wa tiba ni uongozi wa Roho wa Bwana. Wale wanaofanya kazi kama Kristo, Mmishenari Tiba mkuu, alivyofanya kazi ni lazima wawe na akili na nia ya kiroho. Lakini si wote wanaofanya kazi ya umishenari wa tiba wanaomwinua Mungu na Ukweli Wake. Si wote wanaojiweka chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Wengine wanaleta kwenye kujenga msingi mbao, nyasi, na mabua—nyenzo ambazo hazitastahimili jaribio la moto. {8T 206.1}

Ninaomba kwamba nipate hekima na uwezo kutoka kwa Mungu ili nipate kuwasilisha kwenu kile ambacho kinafanyiza kazi ya injili kwa umishenari wa tiba. Hili ni tawi kubwa na muhimu la kazi yetu ya kimadhehebu. Lakini wengi wamezisahau kanuni safi, zenye kuiadilisha ambazo ni msingi wa kazi ya umishenari wa tiba inayokubalika. {8T 206.2}

Katika shajara yangu nimekuta yafuatayo, yaliyoandikwa mwaka mmoja uliopita: Oktoba 29, 1902. Asubuhi ya leo niliamka mapema. Baada ya kuomba kwa dhati na bidii sana kwa ajili ya kupata hekima na uwazi wa akili, ili niweze kuelezea inavyostahili mambo yale yaliyosisitizwa juu ya usikivu wangu, niliandika kama kurasa kumi za maagizo. Ninajua kwamba Bwana alinisaidia kuandika katika karatasi jambo muhimu ambalo lingepaswa kuja mbele ya watu Wake. {8T 206.3}

Ninapoandika hivyo, ninapata hisi kali sana, lakini baada ya maagizo kuandikwa, faraja huja akilini mwangu; kwani wakati huo ninajua kwamba somo lililowasilishwa kwangu halitapotea, ingawa mada hiyo inaweza kupita kutoka katika akili yangu. Ni wale tu wanaotambua kwamba msalaba ndio kiini cha matumaini kwa familia ya wanadamu wanaweza kuelewa injili ambayo Kristo alifundisha. Yeye Alikuja katika ulimwengu huu si kwa ajili ya madhumuni mengine isipokuwa kumweka mwanadamu kwenye nafasi ya juu mbele ya dunia na ulimwengu wa mbinguni. Alikuja kutoa ushuhuda kwamba wanadamu walioanguka, kwa njia ya imani katika uwezo Wake na ufanisi Wake kama Mwana wa Mungu, wanaweza kuwa washiriki

wa asili ya Uungu. Yeye peke yake Ndiye angeweza kufanya upatanisho kwa ajili ya wenye dhambi na kufungua malango ya paradiso kwa ajili ya jamii iliyoanguka. Alijitwalia, si asili ya malaika, bali asili ya mwanadamu, na katika ulimwengu huu aliishi maisha yasiyotiwa doa na dhambi. “Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na Kweli.” “Bali wote waliompokea, Yeye aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu.” Yohana 1:14, 12. {8T 206.4}
Kwa maisha na kifo Chake Kristo alifundisha kwamba ni katika utiifu kwa amri za Mungu tu ndipo mwanadamu anaweza kupata usalama na ukuu wa kweli "Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi." Zaburi 19:7. Sheria ya Mungu ni nakala ya tabia Yake. Ilitolewa kwa mwanadamu hapo mwanzo kama kipimo cha utii. Katika zama zilizofuata sheria hii ilisahauliwa. Mamia ya miaka baada ya Gharika Ibrahimu aliitwa, na kwake ilitolewa ahadi ya kwamba wazao wake wangepaswa kuiinua sheria ya Mungu. Hatimaye baada ya muda kupita, Waisraeli waliingia Misri, ambako kwa miaka mingi walipata mateso makali sana mikononi mwa Wamisri. Baada ya kukaa utumwani kwa takribani miaka mia nne, Mungu aliwakomboa kwa onesho la ajabu la uweza Wake. Alijidhihirisha kwa Wamisri kama Mtawala wa ulimwengu, Yule aliye Mkuu kuliko miungu yote ya kipagani. {8T 207.1}

Pale Sinai sheria ilitolewa kwa mara ya pili. Katika Fahari ya kutisha Bwana alinena maagizo yake na kwa kidole Chake mwenyewe akazinakshi Amri Kumi juu ya mbao za mawe. {8T 207.2}

Kupitia karne nyingi, tunaona kwamba ilifika wakati ambapo sheria ya Mungu ilibidi idhihirishiwe tena kwa wazi kama kipimo cha utii. Kristo alikuja kuthibitisha madai matakatifu ya sheria. Yeye Alikuja kuishi maisha ya utii kwa matakwa yake na hivyo kuthibitisha uongo juu ya shtaka lililotolewa na Shetani kwamba haiwezekani kwa mwanadamu kuitunza sheria ya Mungu. Kama mwanadamu alikutana na majaribu na kushinda kwa nguvu alizopewa na Mungu. Kadiri alivyokwenda huko na huko akitenda mema, akiwaponya wote walioteswa na Shetani, aliweka wazi kwa wanadamu tabia ya sheria ya Mungu na asili ya huduma Yake. Maisha Yake yanashuhudia kwamba inawezekana kwetu pia kutii sheria ya Mungu. {8T 207.3}

Kristo kamwe hakuchepuka kutoka katika utiifu kwa kanuni za sheria ya Mungu. Kamwe hakufanya jambo lolote kinyume na mapenzi ya Baba Yake. Mbele ya malaika, wanadamu, na mapepo aliweza kusema Maneno ambayo kutoka katika midomo mingine yoyote yangekuwa makufuru: "Nafanya sikuzote yale yampendezayo." Yohana 8:29. Siku baada ya siku kwa miaka mitatu adui Zake walimfuata, wakijaribu kupata doa fulani katika tabia Yake. Shetani, pamoja na washirika wake wote wa uovu, walitahidi kumshinda; lakini hawakupata chochote Kwake ambacho kwacho wangeweza kujinufaisha. Hata mashetani walilazimika

kukiri: "Wewe Ndiwe Mtakatifu wa Mungu." {8T 208.1}

## Kujitoa Mhanga

Ni lugha gani ingeweza kuelezea kwa nguvu upendo wa Mungu kwa familia ya kibinadamu kama unavyooneshwa na thawabu ya Mwana Wake wa pekee kwa ajili ya ukombozi wetu? Yule Asiye na hatia alibeba adhabu ya wakosaji. Lakini "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." "Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye." " Amwaminiye Yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini Jina la Mwana pekee wa Mungu." Yohana 3:16-18. {8T 208.2}

Kristo alijitoa Mwenyewe, kuwa kafara ya upatanisho, kwa ajili ya kuokoa ulimwengu uliopotea. Alitendewa jinsi tulivyostahili, ili sisi tutendewe jinsi anavyostahili. Alihukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu, ambazo hakuwa na fungu, ili sisi tuweze kuhesabiwa haki kwa haki Yake, ambayo sisi hatukuwa na fungu ndani yake. Yeye Alikufa kifo ambacho kilikuwa chetu, ili sisi tupate uzima ambao ulikuwa Wake. "Kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Isaya 53: 4–5 {8T 208.3}

Kristo alijaribiwa katika mambo yote kama sisi tunavyojaribiwa, na Yule ambaye hapo awali alisimama kwa uaminifu kando Yake katika nyua za mbinguni. Mwangalie Mwana wa Mungu katika jangwa la majaribu, wakati wa udhaifu mkuu aliposhambuliwa vibaya na majaribu makali kabisa. Mwone wakati wa miaka Yake ya huduma, akishambuliwa kila upande na majeshi ya uovu. Mtazame kwa imani katika uchungu Wake msalabani. Haya yote aliyapitia kwa ajili yetu. {8T 209.1}

Maisha ya kidunia ya Kristo, yaliyojaa kazi za taabu na kujitoa kafara, yalichangamshwa na wazo kwamba Yeye hangetaabika bure. Kwa kutoa maisha Yake kwa ajili ya maisha ya wanadamu, Angeuvuta ulimwengu kurudi kwenye uaminifu Wake. Ingawa ubatizo wa damu lazima kwanza upokelewe, ingawa dhambi za ulimwengu zingeilemea roho Yake isiyo na hatia, lakini, kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake, alichagua kustahimili msalaba na kuidharau aibu. {8T 209.2}

Jifunze fasili ya Kristo ya mmisionari wa kweli: "Mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe." Marko 8:34. Kumfuata Kristo, kama inavyosemwa katika maneno haya, si kujifanya, si utani, Yesu anatazamia wanafunzi Wake kufuata kwa makini nyayo Zake, wakistahamili kile Alichokistahamili, wakipitia kile alichokipitia, wakishinda kama Yeye alivyoshinda. Yeye Anangoja kwa hamu kuwaona wafuasi Wake bayana wakidhihirisha roho ya kujitoa. {8T 209.3}

Wale wanaompokea Kristo kama mwokozi wao binafsi, wakichagua kuwa washirika wa mateso Yake, kuishi maisha Yake ya kujinyima, kustahamili aibu kwa ajili Yake,

wataelewa maana ya kuwa wamishenari wa tiba wa dhati na kweli. {8T 209.4}

Wakati wamisionari wetu wote wa tiba watakapoishi maisha mapya katika Kristo, watakapochukua neno Lake kama mwongozo wao, watakuwa na ufahamu wa wazi zaidi wa kile kinachofanyiza kazi ya Kweli ya umisionari wa tiba. Kazi hii itakuwa na maana ya kina zaidi kwao wanapotoa utii kamili kwa sheria iliyonakshiwa kwenye mbao za mawe kwa kidole cha Mungu, ikijumuisha ile amri ya Sabato, ambayo Kristo Mwenyewe aliwaambia wana wa Israeli kupitia Musa, akisema: {8T 209.5}

"Bwana akasema na Musa, na kumwambia, Kisha, nena wewe na wana wa Israeli, na kuwaambia, Hakika mtazishika Sabato Zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya Mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye ninyi… …" Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele. Ni ishara kati ya Mimi na wana wa Israeli milele.” Kutoka 31: 13-17. {8T 210.1}

Hebu tujifunze Neno la Mungu kwa bidii, ili tuweze kutangaza kwa nguvu ujumbe unaopaswa kutolewa katika siku hizi za mwisho. Wengi wa wale ambao nuru ya maisha ya kujitoa ya Mwokozi inawaangazia wanakataa kuishi maisha yanayopatana na mapenzi Yake. Hawako tayari kuishi maisha ya kujitoa kwa ajili ya manufaa ya wengine. Wanatamani kujiinua wenyewe. Kwa watu kama hao ukweli na haki vimepoteza maana yake, na mvuto wao usio kama wa Kristo unawaongoza wengi kugeuka kando kutoka kwa Mwokozi. Mungu anawaita watenda kazi wa kweli, walio imara, ambao maisha yao yatapinga ushawishi wa wale wanaofanya kazi dhidi Yake. {8T 210.2}

Kwa kila mfanyakazi wa umishenari wa tiba nimeagizwa kusema: Mfuate Kiongozi wako. Yeye Ndiye Njia, na Kweli, na uzima. Yeye Ndiye mfano wako. Juu ya watenda kazi wote wa umishenari wa tiba huegemea wajibu wa kuyazingatia maisha ya Kristo ya utumishi usio na ubinafsi. Wanapaswa kukaza macho yao kwa Yesu, Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yao. Yeye Ndiye Chanzo cha nuru yote, chemchemi ya baraka zote. {8T 210.3}

### Kuitetea Haki kwa Dhati

Mungu huwaita watenda kazi Wake, katika zama hizi zenye upungufu wa uchaji Mungu na kanuni zilizopotoshwa, kudhihirisha hali maridhawa ya kiroho, yenye mvuto. Ndugu na dada zangu, hili Mungu analitaka kutoka kwenu. Kila nukta ya mvuto wenu inapaswa kutumika kwa upande wa Kristo. Mnapaswa sasa kuviita vitu kwa majina yao sahihi na kusimama imara kuutetea Ukweli kama ulivyo katika Yesu. {8T 210.4}

Inampasa kila mtu ambaye maisha yake yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu kuja mbele sasa na kupambana/kupigana kwa ajili ya imani ile iliyowahi kutolewa kwa watakatifu. Ukweli lazima ulindwe na ufalme wa Mungu uendelezwe

mbele vile ambavyo ingelikuwa kama Kristo mwenyewe angelikuwapo hapa duniani. Kama angalikuwa hapa angevutwa kuwakemea wengi ambao, ingawa wanadai kuwa wamishenari wa tiba, bado hawajachagua kujifunza kutoka kwa Mmishenari Mkuu wa Tiba upole na unyenyekevu Wake. Katika maisha ya baadhi ya watu wanaoshikilia nyadhifa za juu katika kazi ya umisionari wa tiba, ubinafsi/umimi umekuzwa. Hadi pale watu kama hao watakapoondoa kila tamaa ya kujiinua wenyewe, hawawezi kutambua waziwazi tabia ya Kristo, wala hawawezi kufanya kazi aliyoifanya. {8T 211.1}

Wakati Roho Mtakatifu anapotawala akili za washiriki wetu wa kanisa, kutaonekana katika makanisa yetu kiwango cha juu zaidi katika usemi, katika huduma, hali ya kiroho, kuliko inavyoonekana sasa. Washiriki wa kanisa wataburudishwa kwa maji ya uzima, na watenda kazi, wakifanya kazi chini ya Kichwa kimoja, yaani Kristo, watamdhihirisha Bwana wao katika roho, kwa neno, kwa matendo, na watahimizana wao kwa wao kusonga mbele katika kazi hii kuu, ya wakati wa mwisho ambayo tunajishughulisha nayo. Kutakuwa na ongezeko maridhawa katika umoja na upendo, ambalo litatoa ushuhuda kwa ulimwengu kwamba Mungu alimtuma Mwanawe kufa kwa ajili ya ukombozi wa wenye dhambi. Ukweli mtakatifu utainuliwa; na kadiri unavyoangaza kama taa iwakayo, tutauelewa kwa uwazi zaidi na zaidi. {8T 211.2}

Ukweli wa kupimia kwa ajili ya wakati huu si uzushi wa akili ya mwanadamu yeyote. Umetoka kwa Mungu. Ni falsafa ya Kweli na dhati kwa wale wanaoitenga kwa ajili ya kazi maalumu. Kristo alifanyika mwili ili kwamba sisi, kupitia kuuamini Ukweli, tupate kutakaswa na kukombolewa. Hebu wale wanaoushikilia Ukweli katika haki waamke na wasonge mbele, wakiwa wamevaa utayari wa injili ya amani, kuutangaza Ukweli kwa wale wasioujua. Hebu wafanye njia zilizonyoka kwa ajili ya miguu yao, ili viwete wasije wakapotoshwa kutoka katika njia. {8T 211.3}

Sasa tunapaswa kuungana na kwa kazi ya Kweli ya umishenari wa tiba kuandaa njia kwa ajili ya Mfalme wetu ajaye. Lakini hebu tukumbuke kwamba umoja wa Kikristo haumaanishi kwamba utambulisho wa mtu mmoja unapaswa kuzamishwa ndani ya ule wa mwingine; wala haumaanishi kwamba akili ya mtu mmoja iongozwe na kutawaliwa na akili ya mtu mwingine. Mungu hajampa mwanadamu yeyote uwezo ule ambao wengine, kwa maneno na matendo, wanajitahidi kutaka kuwa na haki nayo. Mungu anahitaji kila mtu kusimama akiwa huru na kufuata maelekezo ya Neno. {8T 212.1}

Hebu na tuongezeke katika ujuzi wa Kweli, tukitoa sifa na utukufu wote Kwake Yeye aliye Mmoja na Baba. Acha tujitahidi kwa dhati na bidii kupata kupakwa mafuta ya mbinguni, Roho Mtakatifu. Hebu tuwe na Ukristo safi, unaokua, ili katika nyua za mbinguni hatimaye tuweze kutangazwa kuwa wakamilifu kabisa katika Kristo. {8T 212.2}

"Haya, Bwana arusi; tokeni mwende kumlaki." Mathayo 25:6. Msipoteze muda

wowote sasa wa kuinua na kuwasha taa zenu na kurekebisha utambi vizuri. Msipoteze muda wowote wa kutafuta umoja kamili kila mtu na mwenzake. Lazima tutarajie matatizo. Majaribio yatakuja. Kristo, Nahodha wa wokovu wetu, alifanywa mkamilifu kwa njia ya mateso/kuteseka. Wafuasi Wake watakabiliana na adui mara nyingi na watajaribiwa vikali, lakini hawahitaji kukata tamaa. Kristo anawaambia: "Jipeni moyo; Mimi nimeushinda ulimwengu." Yohana 16:33. {8T 212.3}

Mistari ifuatayo inaonesha vita vya Mkristo: Nilidhani kwamba njia ya Mkristo kwenda mbinguni Ingekuwa angavu kama wakati wa majira ya joto na changamfu kama asubuhi. Wewe umenionesha njia; ilikuwa giza na yenye kuparuza, Yenye miamba iliyochongoka, yote iliyosongwa na miiba;

Niliota kuhusu thawabu na umashuhuri wa mbinguni;
Niliomba tawi la mitende, na joho, na taji;
Niliomba, Nawe ulinionesha msalaba na kaburi. {8T 212.4}

## SEHEMU YA 4—JIHADHARINI

"Kesheni, simameni imara katika Imani, fanyeni kiume, mkawe hodari. Mambo yenu yote na yatendeke katika upendo." 1 Wakorintho 16:13, 14.

# SURA YA 35
# MASOMO KUTOKA WAKATI ULIOPITA

## Uwekezaji wa Mamlaka Chini ya Makao Makuu-GC (ujumuishaji)

Ulikuwa ni mpango wa Mungu kwamba baada ya Gharika, katika kutimiliza amri aliyopewa Adamu, wanadamu watawanyike wenyewe kote duniani, ili wapate kuijaza na kuitiisha. {8T 213.1}

Lakini wazao wa Nuhu walipoongezeka kwa idadi, uasi ulijitokeza. Wale waliotaka kuacha kuzuiwa na sheria ya Mungu waliamua kujitenga na waabudu wa Yehova. Walidhamiria kuweka jumuiya yao kuwa na umoja katika jamii moja na kuanzisha ufalme ambao hatimaye ungejumuisha dunia nzima. Katika uwanda wa Shinari waliazimia kujenga mji, na ndani yake mnara ambao ungekuwa ajabu ya dunia. Mnara huu ulipaswa kuwa mrefu kiasi kwamba hakuna mafuriko yangeweza kupanda kufikia kilele, mkubwa sana kiasi kwamba hakuna kitu kingeweza kuufagilia mbali. Hivyo walitumaini kupata usalama wao wenyewe na kuwafanya wasimtegemee Mungu. {8T 213.2}

Muungano huu ulitokana na uasi dhidi ya Mungu. Wakazi wa uwanda wa Shinari walianzisha ufalme wao kwa ajili ya kujiinua, si kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kama wangefaulu, mamlaka kuu ingelitawala, ikiondoa haki na kuanzisha dini mpya. Ulimwengu ungekatishwa tamaa. Nadharia zenye makosa zingepotosha akili kutoka katika utii wa sheria za Mwenyezi Mungu, na sheria ya Yehova ingepuuzwa na kusahauliwa. Lakini Mungu kamwe hauachi ulimwengu bila mashahidi Wake. Wakati huu kulikuwa na watu waliojinyenyekesha mbele za Mungu na kumlilia. "Ee Mungu," walisihi, "ingilia kati ya kusudi Lako, na mipango na mbinu za wanadamu." Na"BWANA akashuka ili auone mji na mnara, waliokuwa wakiujenga wanadamu." Mwanzo 11:5. Malaika walitumwa ili kuharibu makusudi ya wajenzi. {8T 213.3}

Mnara ulikuwa umefikia kimo cha juu sana, na ilikuwa haiwezekani kwa wafanyakazi waliokuwa juu kuwasiliana moja kwa moja na wale waliokuwa chini; kwa hiyo watu waliwekwa katika vituo mbalimbali, kila mmoja kupokea maagizo na kutoa taarifa kwa yule anayefuata chini yake juu ya vifaa vinavyohitajika, au maelekezo mengine kuhusu kazi hiyo. Ujumbe ulipokuwa ukipitishwa kwa jinsi hiyo kutoka kwa mmoja hadi mwingine, lugha ilichanganywa, hivyo vifaa viliagizwa ambayo havikuhitajika, na maelekezo yaliyopokelewa mara nyingi yalikuwa kinyume cha yale yaliyotolewa. Machafuko, mkanganyiko na fadhaa vilifuata. Kazi zote zikasimama. Haikuwezekana tena kuwa na amani au ushirikiano. Wajenzi hawakuweza kabisa kutoa maelezo ya kutokuelewana kwa ajabu kati yao, na kwa ghadhabu na kukatishwa tamaa walilaumiana wao kwa wao. Ghasia zao ziliishia kwenye ugomvi

na umwagaji damu. Radi kutoka mbinguni zilipasua sehemu ya juu ya mnara na kuitupa chini. Wanadamu walifanywa kuhisi kwamba Yupo Mungu anayetawala mbinguni na kwamba Yeye Ana uwezo wa kutatiza, kukanganya na kuzidisha machafuko ili apate kuwafundisha wanadamu kwamba wao ni wanadamu tu. {8T 214.1}

Mungu huvumilia kwa muda mrefu upotovu wa wanadamu, akiwapa nafasi ya kutosha kwa ajili ya toba; lakini anazingatia hila zao zote za kupinga mamlaka ya sheria Yake ya haki na takatifu. {8T 214.2}

Hadi kufikia wakati huu wote walikuwa wakizungumza lugha moja; sasa wale ambao wangeweza kuelewana usemi waliungana katika makundi makundi; wengine walienda njia moja, na wengine njia nyingine. "Kutoka huko Bwana akawatawanya waende usoni pa nchi yote." Aya ya 9. {8T 215.1}

Katika siku zetu Bwana anatamani kwamba watu Wake watawanyike duniani kote. Hawatakiwi kuanzisha koloni. Yesu alisema: “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Marko 16:15. Wanafunzi walipofuata matakwa yao ya kubaki kwa idadi yao kubwa katika Yerusalemu, mateso yaliruhusiwa kuja juu yao, nao wakatawanywa katika sehemu zote za ulimwengu uliokaliwa. {8T 215.2}

Kwa miaka mingi ujumbe wa maonyo na kusihi umekuwa ukija kwa watu wetu, ukiwahimiza waumini wasonge mbele kwenye shamba kubwa la mavuno la Bwana na kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya nafsi za watu. {8T 215.3}

Kutoka katika shuhuda zilizoandikwa katika mwaka wa 1895 na 1899 ninanakili aya zifuatazo: {8T 215.4}

“Wafanyakazi wa Kweli wa umishenari hawatatengeneza makoloni. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wasafiri na wageni duniani. Uwekezaji wa kiasi kikubwa cha fedha katika ujenzi wa kazi mahali pamoja hauko katika utaratibu wa Mungu. Miundo mbinu inabidi iwekwe katika maeneo mengi. Shule na sanitariamu zinapaswa kuanzishwa mahali ambapo sasa hakuna chochote cha kuwakilisha Ukweli. Maslahi haya hayapaswi kuanzishwa kwa madhumuni ya kupata pesa, lakini kwa madhumuni ya kueneza Ukweli. Ardhi inapaswa kupatikana mbali na miji, ambapo shule zinaweza kujengwa ambamo vijana wanaweza kupewa elimu katika fani za kilimo na ufundi. {8T 215.5}

"Kanuni za Ukweli wa sasa zinapaswa kuenea zaidi. Wapo wale wanaofikiri kwa mtazamo usio sahihi. Kwa sababu ni rahisi zaidi kuweka kazi katika sehemu moja, wanaunga mkono msongamano wa kila kitu katika eneo moja. Uovu mkubwa ndio

matokeo. Maeneo ambayo yangepaswa kusaidiwa yameachwa fukara. {8T 215.6}

“Niseme nini kwa watu wetu kitakachowaongoza kufuata njia ambayo itakuwa kwa ajili ya manufaa yao ya sasa na ya baadaye? Je, wale walio katika Battle Creek hawatatilia maanani nuru ile waliyopewa na Mungu? Je, hawatajikana nafsi zao, kuinua msalaba, na kumfuata Yesu? Je, hawatatii wito wa Kiongozi wao wa kuondoka Battle Creek na kujenga taasisi na majengo katika maeneo mengine? Je, hawatakwenda mahali penye giza duniani ili kusimulia kisa cha upendo wa Kristo, wakimtumainia Mungu kuwapa mafanikio? {8T 216.1}

"Si mpango wa Mungu kwa watu wetu kusongamana katika Battle Creek. Yesu anasema: “Nendeni mkafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu. Ondokeni kutoka katika mahali ambapo hamhitajiki. Simamisha bendera ya Ukweli katika miji na majiji ambayo haijasikia ujumbe. Tayarisheni njia kwa ajili ya ujio Wangu. Wale walio katika barabara kuu na viunga wanapaswa kusikia wito.' {8T 216.2}

“Bwana ataifanya jangwa kuwa mahali patakatifu, pale watu Wake, wakiwa wamejazwa na roho ya umisionari, watasonga mbele kutengeneza vituo kwa ajili ya kazi Yake, kuanzisha sanitariamu, ambapo wagonjwa na wanaoteseka wataweza kutunzwa; na shule, ambapo vijana. wataweza kuelimishwa katika mielekeo na nyanja sahihi." {8T 216.3}

“Imesisitizwa kuwa kulikuwa na faida kubwa kuwa na taasisi nyingi kiasi hicho katika uhusiano wa karibu, kwamba zingekuwa nguvu kila moja kwa mwenzake na zingeweza kutoa msaada kwa wale wanaotafuta elimu na ajira. Hii ni kulingana na kufikiri kwa mwanadamu; itakubalika kuwa, kwa mtazamo wa wanadamu, faida nyingi hupatikana kwa kurundika majukumu mengi huko Battle Creek; lakini maono yanapaswa kupanuliwa. {8T 216.4}

Licha ya ushauri wa mara kwa mara kinyume chake, watu waliendelea kupanga kwa ajili ya kuunganishwa kwa mamlaka, kwa ajili ya kufunga taasisi nyingi chini ya utawala mmoja. Kazi hii ilianzishwa kwa mara ya kwanza katika ofisi ya Review and Herald. Mambo yaliyumbishwa kwanza kuelekea njia moja kisha nyingine. Adui wa kazi yetu ndiye aliyechochea wito wa ujumuishaji wa kazi ya uchapishaji chini ya mamlaka moja ya kutawala katika Battle Creek. {8T 216.5}

Ndipo wazo likaungwa mkono kwamba kazi ya umishenari wa tiba ingeendelea sana ikiwa taasisi zetu zote za matibabu na maslahi mengine ya umishenari wa tiba yangefungwa chini ya utawala wa chama cha wamishenari wa tiba katika Battle Creek. {8T 217.1}

Niliambiwa kwamba ni lazima nipaze sauti yangu kuonya dhidi ya hili. Hatukupaswa kuwa chini ya utawala wa watu ambao hawakuweza kujitawala wao wenyewe na

ambao hawakuwa tayari kuwa watiifu kwa Mungu. Hatukupaswa kuongozwa na watu ambao walitaka neno lao liwe ndio nguvu inayotawala. Uendelezaji wa tamaa ya kuwa na mamlaka ya kuongoza, na kuwatawala watu yamekuwa dhahiri sana, na Mungu alituma onyo baada ya onyo, akipiga marufuku mashirikisho na kujiimarisha katika kujumuisha taasisi katika sehemu moja. Alituonya dhidi ya kujifunga wenyewe ili kutimiza makubaliano fulani ambayo yangewasilishwa na watu wanaofanya kazi kwa bidii ili wapate kutawala mijongeo na utendaji ya ndugu zao. {8T 217.2}

### Kituo cha Elimu

Bwana hafurahishwi na baadhi ya mipangilio ambayo imefanywa huko Battle Creek. Ametangaza kwamba maeneo mengine yananyimwa muru na faida ambazo zimewekwa chini ya kituo kikuu na kuzidishwa katika Battle Creek. Haimpendezi Mungu kwamba vijana wetu kutoka sehemu zote za nchi waitwe kuja Battle Creek, kufanya kazi katika sanitariamu, na kupata elimu yao. Tunaporuhusu hili, mara nyingi tunakuwa na hatia ya kuyanyima maeneo yenye uhitaji hazina yao ya thamani kabisa. {8T 217.3}

Kupitia nuru iliyotolewa katika shuhuda, Bwana ameelekeza kwamba hataki wanafunzi kuacha shule zao za nyumbani na sanitariamu ili waelimishwe katika Battle Creek. Yeye Alituagiza tuondoe chuo kutoka mahali hapa. Hili lilifanyika, lakini taasisi zilizobaki zilishindwa kufanya kile walichopaswa kufanya ili kushiriki na maeneo mengine faida ambazo bado zilijikita katika Battle Creek. Bwana alionesha kutokupendezwa Kwake kwa kuruhusu majengo makuu ya taasisi hizi kuharibiwa kwa moto. {8T 218.1}

Licha ya uthibitisho wa wazi wa majaliwa ya Bwana katika mioto hii yenye kuharibu, baadhi miongoni mwetu hawajasita kudharau kauli kwamba majengo haya yaliteketezwa kwa sababu watu walikuwa wakigeuza mambo katika mielekeo ambayo Bwana hangeweza kuikubali. {8T 218.2}

Watu wamekuwa wakitoka kwenye kanuni sahihi, ambazo kwa ajili ya utangazaji wake taasisi hizi zilianzishwa. Wameshindwa kufanya kazi ile hasa ambayo Mungu aliagiza ifanywe ili kuwatayarisha watu wa “kujenga mahali palipokuwa ukiwa” na kusimama mahali palipobomoka, kama inavyowakilishwa katika sura ya hamsini na nane ya Isaya. Katika Andiko hili kazi tunayopaswa kufanyika imefafanuliwa wazi kuwa ni kazi ya umishenari wa tiba. Kazi hii inapaswa kufanywa kila mahali. Mungu ana shamba la mizabibu; Naye Anataka kwamba shamba hili la mizabibu lifanyiwe kazi bila ubinafsi. Hakuna sehemu zinazopaswa kupuuzwa. Sehemu iliyopuuzwa zaidi inahitaji wamishenari waliokodoa macho zaidi kufanya kazi ambayo, kupitia kwa Isaya, Roho Mtakatifu ameionesha: {8T 218.3}

“Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? “Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri; Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, mwenye kutengeneza mahali palipobomoka, mwenye kurejeza njia za kukalia. Isaya 58:6, 10-12. - {8T 218.4}

Kwa ajili ya Jina Lake Mwenyewe, Mungu hataruhusu watu wakaidi na wenye kujitegemea kutekeleza mipango yao isiyotakaswa. Yeye Atawapatiliza kwa sababu ya upotovu wao wa vitendo. "Hapana amani kwa wabaya, asema Mungu wangu." Isaya 57:21. Lakini katika hukumu Zake Bwana atakumbuka rehema. Anatangaza: {8T 219.1}

"Kwa kuwa sitashindana na watu siku zote, wala sitakuwa na hasira siku zote; maana roho ingezimia mbele Zangu, na hizo nafsi nilizozifanya. Kwa sababu ya uovu wa kutamani kwake naliona hasira, nikampiga; nalificha uso Wangu, nikaona ghadhabu; naye akaendelea kwa ukaidi, kuifuata njia ya moyo wake mwenyewe. Nimeziona njia zake; Nami nitamponya; nitamwongoza pia, nitamrudishia faraja zake, yeye na hao wanaomlilia. Mimi nayaumba matunda ya midomo; Amani, amani, kwake yeye aliye mbali, na kwake yeye aliye karibu; asema Bwana; Nami nitamponya.” Isaya 57:16-19. {8T 219.2}

“Maana Roho za watu Wangu itashindwa mbele Zangu,” asema BWANA, “kama ningewatendea sawasawa na upotovu wao. Wasingeweza kustahamili chuki na ghadhabu Yangu. Nimeiona njia potovu za kila mwenye dhambi. Mwenye kutubu na kufanya matendo ya haki, basi Mimi nitamwongoa na kumponya, na nitamrejesha katika fadhili Zangu." {8T 219.3}

Kuhusu wale ambao wamedanganywa na kupotoshwa na watu ambao hawajajitoa wakfu, Bwana asema: “Mwelekeo wao wa matendo haujapatana na mapenzi Yangu; lakini kwa ajili ya haki ya kusudi Langu, kwa ajili ya Ukweli, nitaponya kila mtu ambaye ataliheshimu Jina Langu. Wanaotubu wote wa Israeli watauona wokovu Wangu. Mimi, BWANA, ninatawala, Nami nitaijaza sifa na shukrani mioyo ya wote walio karibu na walio mbali, naam, wote wanaotubu wa Israeli, waliozishika njia Zangu.” {8T 219.4}

“Maana Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye Jina Lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa Mimi mahali palipoinuka, palipo Patakatifu; tena pamoja na yeye

aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu." Aya ya 15. {8T 220.1}

## SURA YA 36
## VIJANA WETU WATAFUNDISHWAJE?

Yohana Mbatizaji, mtangulizi wa Kristo, alipata mafunzo yake ya awali kutoka kwa wazazi wake. Sehemu kubwa ya maisha yake ilitumika nyikani, ili asiweze kushawishika kwa kutazama uchaji Mungu mlegevu wa makuhani na marabi au kwa kujifunza kanuni na mapokeo yao, ambavyo kwa hivyo kanuni sahihi zilipotoshwa na kudharauliwa. Walimu wa kidini wa siku hizo walikuwa wamepofuka sana kiroho kiasi kwamba hawakuweza kutambua sifa za wema wenye asili ya mbinguni. Kwa muda mrefu sana walikuwa wamelea kiburi, husuda, na wivu kiasi kwamba walifasiri Maandiko ya Agano la Kale kwa namna ambayo ingeharibu maana yake ya kweli. Ilikuwa ni uchaguzi wa Yohana kuacha starehe na anasa za maisha ya mjini kwa ajili ya nidhamu kali ya nyikani. Hapa mazingira yake yalikuwa yanafaa kwa ajili ya mazoea ya usahili na kujinyima. Bila kuingiliwa na kelele za ulimwengu, hapa angeweza kujifunza masomo ya asili, ya ufunuo, na ya majaliwa. Maneno ya malaika kwa Zakaria yalikuwa yamerudiwa mara kwa mara kwa Yohana na wazazi wake waliomcha Mungu. Tangu utotoni utume wake uliwekwa mbele yake, na aliikubali dhamana hii takatifu. Kwake upweke wa jangwani ulikuwa ni kimbilio la kufurahisha kutoka kwa jamii ambayo shuku, kutoamini na uchafu vilikuwa vimeenea kila mahali. Hakuamini uwezo wake yeye mwenyewe wa kuweza kustahamili majaribu na akajificha kutoka kwa mgusano wa mara kwa mara na dhambi asije akasahau dhambi yake iliyopitiliza. {8T 221.1}

Lakini maisha ya Yohana hayakutumika kwa uvivu, huzuni ya kujinyima raha na anasa, au kujitenga kwa ubinafsi. Mara kwa mara alitokeza kwenda kujichanganya na watu; na daima alikuwa mtazamaji aliyevutiwa na kile kinachopita ulimwenguni. Kutoka kimbilio lake ya tulivu alitazama matukio yaliyokuwa yanajitokeza. Kwa maono yaliyoangaziwa na Roho wa Mungu alijifunza tabia za wanadamu, ili apate kuelewa jinsi ya kufikia mioyo yao na ujumbe wa mbinguni. - {8T 221.2}

Kristo aliishi maisha ya mmisionari wa kweli wa tiba. Anatutaka tujifunze maisha Yake kwa bidii, ili tujifunze kufanya kazi kama Yeye alivyofanya. {8T 222.1}

Mama Yake alikuwa mwalimu Wake wa kwanza wa kibinadamu. Kutoka katika midomo yake, na kutoka katika vitabu vya manabii, Alijifunza mambo ya mbinguni. Aliishi katika nyumba ya mkulima mdogo, na kwa uaminifu na kwa furaha Alitenda sehemu Yake katika kubeba mizigo ya nyumbani. Alikuwa Amiri Jeshi wa mbinguni,

na malaika walikuwa wanafurahia kutimiza Neno Lake; sasa alikuwa mtumishi aliye aliye tayari, Mwana Mwenye upendo na mtiifu. Alijifunza kazi ya ufundi na kwa mikono Yake Mwenyewe alifanya kazi katika kiwanda cha seremala pamoja na Yusufu. Katika vazi sahili la mfanyakazi wa kawaida Alitembea katika mitaa ya mji, akienda na kurudi kutoka katika kazi Yake duni. {8T 222.2}

Kwa watu wa zama hizo thamani ya vitu iliamuliwa na maonesho ya nje. Kadiri dini ilivyopungua uwezo wake, iliongezeka kwa Fahari/kujionyesha. Walimu wa wakati huo walitafuta kuwa na heshima kwa kujionesha na majivuno. Kwa haya yote maisha ya Yesu yalionesha tofauti dhahiri. Maisha yake yalionesha kutokufaa kwa vitu vile ambavyo wanadamu waliviona kuwa muhimu sana maishani. Hakutafuta shule za wakati Wake, pamoja na kukuza kwao vitu vidogo na kudunisha kwao vitu vikubwa. Elimu yake ilipatikana kutoka kwa vyanzo vilivyoteuliwa na mbingu, kutokana na kazi yenye manufaa, kutokana na kujifunza Maandiko na mambo ya asili, na kutokana na uzoefu wa maisha—vitabu vya masomo vya Mungu, vilivyojaa mafundisho kwa wote wanaokuja kwavyo kwa moyo ulio tayari, jicho linaloona, na moyo wenye ufahamu. {8T 222.3}

“Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu Yake.” Luka 2:40. {8T 223.1}

Akiwa amejiandaa hivyo, alikwenda kwenye utume Wake, katika kila dakika ya mawasiliano Yake na wanadamu akiweka juu yao mvuto wa kubariki, uwezo wa kubadilisha, wa namna ambayo ulimwengu haujawahi kushuhudia. {8T 223.2}

## Maneno ya Onyo

Tunaishi katika wakati wa hatari ya pekee kwa vijana. Shetani anajua kwamba mwisho wa ulimwengu uko karibu kuja, na ameazimia kutumia vizuri kila fursa kwa ajili ya kuwashinikiza vijana wa kiume na wa kike kumtumikia. Atabuni hila nyingi sana za kughilibu ili apate kuwapoteza. Tunapaswa kufikiria kwa makini maneno ya onyo yaliyoandikwa na mtume Paulo: {8T 223.3}

"Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini? Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye Hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu. Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu wa kiume na wa kike,” 2 Wakorintho 6:14-18. {8T 223.4}

Nuru ya pekee imetolewa kwangu kuhusu kwa nini tunaweza kufanya mengi zaidi

kwa ajili ya Bwana kwa kuanzisha sanitariamu nyingi ndogo ndogo kuliko kwa kujenga taasisi chache kubwa za tiba. Katika taasisi kubwa kungekusanyika pamoja wengi ambao si wagonjwa sana, lakini ambao, kama watalii, wanatafuta pumziko na raha. Hawa wangelazimika kuhudumiwa na wauguzi na watumishi. Vijana wa kiume na wa kike, ambao tangu miaka yao ya awali kabisa wamekingwa dhidi ya ushirika wa dunia, kwa jinsi hiyo wangekutanishwa na wapenda anasa za dunia wa kila namna, na kwa vyovyote wangeathiriwa na kile wanachokiona na kusikia. Wangekuwa kama wale ambao wanashirikiana nao, wakipoteza usahili na staha ambavyo baba na mama Wakristo wamevilinda na kuvilea kwa mafundisho makini na maombi ya dhati. {8T 223.5}

Tunaishi katikati ya hatari za siku za mwisho. Jambo fulani la wazi ni lazima lisemwe ili kuwaonya watu wetu dhidi ya hatari ya kuruhusu watoto wanaohitaji malezi na mafundisho ya wazazi, kuondoka nyumbani kwao kwenda mahali ambapo watakutanishwa na walimwengu wapenda anasa, wasio na dini. {8T 224.1}

Katika nyumba nyingi baba na mama wameruhusu watoto kutawala. Watoto kama hao wako katika hatari kubwa zaidi, wanapokutanishwa na mivuto inayopingana na utauwa, kuliko wale ambao wamejifunza kutii. Kwa kuwa hawajapata mafunzo muhimu ya kinidhamu, wanafikiri kwamba wanaweza kufanya watakavyo. Maarifa ya jinsi ya kutii yangewaimarisha waweze kupinga majaribu, lakini maarifa haya wazazi wao hawajawapa. Wakati vijana hawa wasio na nidhamu wanapoingia kwenye taasisi kubwa, ambapo kuna mivuto mingi iliyo kinyume na mambo ya kiroho, wanakuwa katika hatari kubwa, na mara nyingi kukaa kwao katika taasisi hiyo ni madhara kwao wenyewe na kwa taasisi. {8T 224.2}

Nimeagizwa kuwaonya wazazi ambao watoto wao hawana uthabiti wa kanuni au uzoefu ulio wazi wa Kikristo wasiwaondoe nyumbani kwenda sehemu za mbali, na kuwafanya wasiwepo [nyumbani] kwa miezi mingi na labda kwa miaka mingi, na, huenda, ikawa ni kupanda katika akili zao mbegu za kutokuamini na ukafiri. Ni salama zaidi, na bora zaidi, kuwapeleka vijana kama hao kwenye shule na sanitariamu zilizo karibu na nyumbani kwao. Hebu vijana ambao wanajenga tabia wawekwe mbali na mahali ambapo wangelazimika kuchanganyika na kundi kubwa la wasioamini, na ambapo majeshi ya adui yameweka kambi madhubuti. {8T 224.3}

Hebu juhudi za dhati zifanywe na wasimamizi wa sanitariamu zetu kubwa kuwaajiri watu wazima (wazee) kama watumishi katika taasisi hizi. Katika maono ya usiku nilikuwa katika kusanyiko kubwa, ambapo jambo hili lilikuwa linafikiriwa. Kwa wale waliokuwa wakipanga kuwapeleka watoto wao wasio na nidhamu kule Battle Creek, Mmoja mwenye mamlaka alisema: {8T 225.1}

"Je unathubutu kufanya jaribio hili? Wokovu wa watoto wako ni wa thamani kuliko elimu watakayoipokea mahali hapa, ambapo daima wanakabiliwa na mvuto wa wasioamini. Wengi wanaokuja katika taasisi hii hawajaongoka. Wamejawa na kiburi

na hawana uhusiano na Mungu kupitia katika imani. Wengi wa vijana wa kiume na wa kike wanaowahudumia walimwengu hawa wamekuwa na uzoefu mdogo tu wa Kikristo, na wananaswa kwa urahisi katika mitego inayotegwa kwa ajili ya miguu yao.” {8T 225.2}

"Ni nini kifanyike ili kurekebisha uovu huu?" mtu fulani aliyekuwepo aliuliza. Mnenaji yule akajibu: “Kwa kuwa mmejiweka wenyewe katika nafasi hii ya hatari, hebu wanaume na wanawake Wakristo walio na umri mkubwa wenye tabia thabiti waletwe katika taasisi ili kuweka mvuto wa kinyume kwa ajili ya haki. Utekelezaji wa mpango kama huo ungeongeza gharama za uendeshaji wa sanitariamu, lakini unaweza kuwa njia ya kufaa ya kuilinda ngome na kuwakinga vijana waliomo katika taasisi hii kutokana na mivuto inayotia uchafu ambayo kwa sasa wamewekwa wazi. {8T 225.3}

"Wazazi, walezi, wawekeni watoto wenu katika shule za mafunzo ambapo mivuto ni sawa na ile ya shule ya nyumbani inayoendeshwa ipasavyo; shule ambazo walimu watawaendeleza mbele hatua kwa hatua na ambamo angahewa ya kiroho ni harufu ya uzima iletayo uzima." {8T 225.4}

Maneno ya maonyo na maagizo ambayo nimeandika kuhusu kuwapeleka vijana wetu
Battle Creek kwa ajili ya kupata mafunzo ya utumishi katika kusudi la Bwana si maneno ya bure. Baadhi ya vijana wanaomcha Mungu watastahimili jaribio hilo, lakini si salama kwetu kuwaacha hata wale walio waangalifu sana bila uangalizi na ulinzi wetu bora. Kwa vyovyote vile kwamba vijana wetu ambao wamepokea mafundisho na maelekezo ya hekima kutoka kwa wazazi wanaomcha Mungu wataendelea kutakaswa kupitia ile kweli au la, kunategemea sana mvuto ambao, baada ya kuondoka nyumbani kwao, wanakutana nao miongoni mwa wale wanaotazamia kutoka kwao kupata mafundisho ya Kikristo. {8T 226.1}

Nimeagizwa kurudia kwa ndugu na dada zetu onyo na ushauri ambao Paulo alilituma kwa kanisa la Thesalonike: {8T 226.2}

“Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi; lakini yuko azuiaye sasa, hata atakapoondolewa. Hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa Chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo Kwake; yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu." 2 Wathesalonike 2:7-12. {8T 226.3}

"Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana, kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate

wokovu, katika kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli; aliyowaitia ninyi kwa injili yetu, ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo. Basi, ndugu, simameni imara, mkayashike mapokeo mliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu. Na Bwana wetu Yesu Kristo Mwenyewe, na Mungu Baba yetu, aliyetupenda akatupa faraja ya milele na tumaini jema, katika neema, awafariji mioyo yenu, na kuwafanya imara katika kila neno na tendo jema." 2 Wathesalonike 2:13-17. {8T 226.4}

**Septemba, 1903.**

Ninapofikiria hali ya mambo katika Battle Creek, ninatetemeka kwa ajili ya vijana wetu wanaokwenda pale. Nuru niliyopewa na Bwana, kwamba vijana wetu wasikusanyike Battle Creek kupokea elimu yao, haijabadilika hata kidogo. Ukweli kwamba sanitariamu imejengwa tena haibadilishi nuru ile. Jambo ambalo hapo awali lilifanya Battle Creek kuwa mahali pasipofaa kwa ajili ya elimu ya vijana wetu linapafanya kutokufaa leo kwa kadiri mvuto unavyohusika. {8T 227.1}

Wakati wito ulipokuja wa kuhama kutoka Battle Creek, ombi lilikuwa: "Tuko hapa, na imara kabisa. Itakuwa jambo lisilowezekana kuhama bila gharama kubwa sana." {8T 227.2}

Bwana aliruhusu moto kuteketeza majengo makuu ya Review and Herald na sanitariamu, na hivyo kuondoa pingamizi kuu lililosisitizwa dhidi ya kuhama kutoka Battle Creek. Lilikuwa ni kusudi Lake kwamba badala ya kujenga upya sanitariamu hii moja kubwa, watu wetu wangetengeneza majengo katika sehemu mbalimbali. Hizi sanitariamu ndogo ndogo zilipaswa kuwa zimeanzishwa mahali ambapo ardhi ingeweza kupatikana kwa madhumuni ya kilimo. Ni mpango wa Mungu kwamba kilimo kihusianishwe na kazi ya sanitariamu na shule zetu. Vijana wetu wanahitaji elimu itakayopatikana katika mielekeo hii ya kazi. Ni vyema, na zaidi ya kuwa vyema – ni lazima kwamba juhudi zifanywe kutekeleza mpango wa Bwana kuhusiana na hili. {8T 227.3}

Je, tuwatie moyo vijana wetu wa kiume na wa kike wenye matumaini sana kwenda Battle Creek ili kupata mafunzo yao kwa ajili ya huduma ambapo watakuwa wamezungukwa na mivuto mingi ambayo inapotosha? Bwana amenifunulia baadhi ya hatari ambazo vijana waliounganishwa kwenye sanitariamu kubwa sana watalazimika kukutana nazo. Wengi walio matajiri, wanaume na wanawake ambao wanafadhili taasisi (wanaweza kuwa wateja) watakuwa chanzo cha majaribu kwa watumishi. Baadhi ya watumishi hawa watapendwa na wagonjwa matajiri na kupewa vishawishi vikali vya kuajiriwa nao. Kupitia mvuto wa maonesho ya kidunia ya baadhi ya wale ambao wamekuwa wageni kwenye sanitariamu, magugu yamepandwa tayari katika mioyo ya vijana wa kiume na wa kike walioajiriwa kama watumishi na wauguzi. Hii ndiyo njia ambayo kwayo Shetani anafanya kazi. {8T 228.1}

Kwa sababu sanitariumu ipo mahali ambapo haipaswi kuwa, je, Neno la Bwana kuhusu elimu ya vijana wetu lisizingatiwe? Je, tuwaruhusu vijana wetu wenye akili sana waliomo katika makanisa yote ya konferensi zetu wawekwe mahali ambapo baadhi yao watanyang'anywa usahili na unyenyekevu wao kupitia kwa kukutana kwao na wanaume na wanawake ambao hawana hofu ya Mungu mioyoni mwao? Je, wasimamizi wa konferensi zetu wataruhusu vijana wetu, ambao, katika shule zilizo kwa ajili ya watenda kazi Wakikristo, wangeweza kutengenezwa wafae kwa ajili ya utumishi wa Bwana, wavutwe mahali ambapo kwa miaka mingi Bwana amekuwa akiwaita watu Wake wapate kuhama? {8T 228.2}

Tunatamani vijana wetu wafunzwe kiasi kwamba wataweka mvuto wa kuokoa katika makanisa yetu, wakifanya kazi kwa ajili ya umoja mkubwa na uchamungu wa kina zaidi. Watu wanaweza wasione umuhimu wa wito kwa familia kuondoka Battle Creek na kukaa mahali ambapo wanaweza kufanya kazi ya injili ya umisionari wa tiba. Lakini Bwana amesema. Je, tulihoji Neno Lake? {8T 228.3}

### Hakuna Muda wa Kuchelewa

Miongoni mwetu wapo vijana wengi wa kiume na wa kike ambao, kama vishawishi vingeondolewa, wangechukua mwelekeo wa kawaida kusoma kwa miaka kadhaa masomo yatakayowaandaa kwa ajili ya utumishi. Lakini je, italipa? Muda ni mfupi. Watenda kazi kwa ajili ya Kristo wanahitajika kila mahali. Kunapaswa kuwa na watenda kazi mia moja wenye bidii, waaminifu nyumbani na kwenye maeneo ya misioni ugenini ambako sasa yuko mmoja tu. Njia kuu na njia ndogo bado hazijafanyiwa kazi bado. Vishawishi vya haraka vinapaswa kuondolewa kwa wale ambao sasa wanapaswa kushiriki katika kazi ya Bwana. {8T 229.1}

Dalili zinazoonesha kwamba kuja kwa Kristo kumekaribia zinatimia haraka. Bwana anawaita vijana wetu kufanya kazi kama wahubiri na wainjilisti, kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba katika sehemu ambazo bado hazijasikia ukweli. Anazungumza na vijana wetu akisema: "Ninyi si mali yenu wenyewe, maana mlinunuliwa kwa thamani: basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu." Wale ambao watafanya kazi chini ya maelekezo ya Mungu watabarikiwa ajabu. Wale ambao katika maisha haya wanafanya kila liwezekanalo watapata kufaa kwa ajili ya maisha ya baadaye, ya kutokufa. {8T 229.2}

Bwana anawaita wale waliounganishwa na sanitariamu zetu, nyumba za uchapaji, na shule kuwafundisha vijana kufanya kazi ya uinjilisti. Wakati na nguvu zetu havipaswi kutumiwa sana katika kuanzisha sanitariamu nyingi, maduka ya vyakula, na migahawa kiasi kwamba mielekeo mingine ya kazi ipuuzwe. Vijana wa kiume na wa kike wanaopaswa kushiriki katika huduma, katika kazi ya Biblia, na katika kazi ya uinjilisti wa vitabu hawapaswi kufungwa na kazi za mitambo (za kila siku zinazojirudia rudia). {8T 229.3}

Vijana wanapaswa kutiwa moyo kuhudhuria shule zetu za mafunzo kwa ajili ya watendakazi Wakikristo, ambazo zinapaswa kufanana zaidi na zaidi na shule za manabii. Taasisi hizi zimeanzishwa na Bwana, na zikiendeshwa kwa kupatana na kusudi Lake, vijana waliopelekwa hapo watatayarishwa haraka kushiriki katika mielekeo mbalimbali ya kazi ya umisionari. Wengine watafunzwa kuingia shambani kama wauguzi wamisionari, wengine kama wainjililisti wa nyumba kwa nyumba, na wengine kama wachungaji. {8T 230.1}  231

## Mgawanyo wa Majukumu

St. Helena, California, Agosti 4, 1903.
Kwa Viongozi katika Kazi ya Tiba—

Ndugu Wapendwa: Nina ujumbe kwa ajili yenu. Nimeagizwa kusema kwamba si mipango yote inayohusiana na usimamizi wa kazi ya umisionari wa tiba lazima ianzie Battle Creek. Kazi ya umisionari wa tiba ni kazi ya Mungu, na katika kila konferensi na kila kanisa tunapaswa kuchukua msimamo thabiti dhidi ya kuiruhusu kutawaliwa kwa ubinafsi. {8T 231.1}

Baada ya kupokea habari kuhusu mkutano mzuri wa maungamo na umoja uliofanyika kule Battle Creek nilikuwa nikiandika katika shajara yangu na nilikuwa karibu kuandika shukrani niliyohisi kwa sababu mabadiliko yalikuwa yamekuja, ndipo mkono wangu ulipozuiwa, na yakaja kwangu maneno: "Usiandike. Hakuna mabadiliko kwa ajili ya kilicho bora yaliyofanyika. Mafundisho ambayo yanageuza roho kutoka kwenye ukweli yanawasilishwa kama ya thamani kubwa. Mafundisho yanafundishwa ambayo yanaongoza kwenye mapito na njia zilizokatazwa; mafundisho yanafundishwa ambayo huelekeza katika njia ya pembeni na njia zilizokatazwa; mafundisho yanayowaongoza wanadamu kutenda kulingana na mielekeo yao wenyewe na kutimiza makusudi yao yasiyotakaswa; mafundisho ambayo, yakipokelewa, yangeharibu hadhi na uwezo wa watu wa Mungu, na kuficha nuru ambayo vinginevyo ingewajia kupitia vyombo vilivyowekwa na Mungu.” {8T 231.2}

Viongozi katika kazi yetu ya utabibu pale Battle Creek wamejitahidi kuunganisha taasisi zetu za tiba kwa haraka, kulingana na mipango yao. Licha ya maonyo mengi waliyopewa kwamba hili lisifanywe, wamedhamiria kuziunganisha taasisi hizi kwa njia fulani ili kazi zetu zote za tiba ziwe chini ya udhibiti wao. {8T 231.3}

Katika siku za nyuma niliandika mengi juu ya mada hii, na mimi lazima sasa nirudie maonyo yaliyotolewa, kwa maana inaonekana kuwa vigumu kwa ndugu zangu kuelewa nafasi ya hatari waliyopo. {8T 231.4}

"Bwana anakataza kuweka kila sanitariamu na nyumba za kuogea zilizoanzishwa kuwa chini ya utawala mmoja – zote zikiunganishwa na taasisi ya tiba Battle Creek. Wasimamizi wa Sanitariamu ya Battle Creek wanayo kazi kubwa yakufanya sasa. Wanapaswa kutoa nguvu zao kwa ajili ya kazi ya kuifanya sanitariumu kile inachopaswa kuwa. {8T 232.1}

"Mtu mmoja hapaswi kufikiri kuwa anaweza kutawala dhamiri za watendakazi wote

wa tiba. Wanadamu wanapaswa kumwangalia Bwana Mungu wa mbinguni peke Yake kwa ajili ya hekima na uongozi. {8T 232.2}

“Katika kuanzisha na kuendeleza taasisi za matibabu, ndugu zetu hawapaswi kuombwa kufanya kazi kwa mujibu wa mipango ya mamlaka ya kifalme inayotawala. Mabadiliko lazima yafanyike. Mpango wa kuunganisha kila taasisi ya matibabu kwa shirika kuu huko Battle Creek lazima usitishwe. Mpango huu Mungu ameukataza. {8T 232.3}

“Kwa miaka mingi nimeagizwa kwamba kuna hatari, hatari ya kudumu, kwamba ndugu zetu watatafuta ruhusa kwa wanadamu wenzao kufanya hili au lile, badala ya kumwangalia Mungu. Hivyo wanakuwa wanyonge, na kuruhusu wafungwe na vizuizi vilivyowekwa na wanadamu visivyokubaliwa na Mungu. Bwana anaweza kuzivutia akili na dhamiri kufanya kazi Yake chini ya kifungo Kwake, na katika roho ya udugu ambayo inakubaliana na kanuni za sheria Yake……. {8T 232.4}

"Mungu anaujua wakati ujao. Yeye Ndiye ambaye tunapaswa kutafuta mwongozo kwake. Hebu tumwamini atuelekeze katika maendeleo ya nyanja mbalimbali ya kazi Yake. Hebu yeyote asijaribu kufanya kazi kwa kufuata misukumo isiyotakaswa. . . . {8T 232.5}

“Mgawanyo wa Konferensi Kuu hadi Unioni Konferensi za maeneo mbalimbali ulikuwa ni mpango wa Mungu. Katika kazi ya Bwana kwa ajili ya siku hizi za mwisho hapapaswi kuwa na vituo vya Yerusalemu, hakupaswi kuwa na mamlaka ya kifalme. Na kazi katika nchi mbalimbali haipaswi kuunganishwa kwa mikataba ya kazi yenye kitovu chake Battle Creek, kwa maana huu si mpango wa Mungu. Ndugu wanapaswa kushauriana pamoja, kwa maana wote tupo chini ya uongozi wa Mungu katika sehemu moja ya shamba lake la mizabibu kama ilivyo katika sehemu nyingine. Ndugu wanapaswa kuwa na umoja wa moyo na roho, kama vile Kristo na Baba walivyo umoja. Fundisha hili, tenda hili, ili tuwe kitu kimoja na Kristo katika Mungu, sote tukifanya kazi ya kujengana. {8T 232.6}

“Mamlaka ya kifalme yaliyooneshwa hapo awali katika Konferensi Kuu huko Battle Creek hayapaswi kuendelezwa. Taasisi ya uchapaji haipaswi kuwa ufalme kwa yenyewe. Ni muhimu kwamba kanuni zinazotawala katika masuala ya Konferensi Kuu zidumishwe katika usimamizi wa kazi ya uchapishaji na kazi ya Sanitariamu. Mtu asifikirie kuwa sehemu ya kazi ambayo ameunganishwa nayo ina umuhimu mkubwa zaidi kuliko sehemu nyingine. {8T 233.1}

"Kazi ya elimu lazima ifanyike katika kila sanitariumu ambayo itaanzishwa. Mungu ana utawala juu ya kazi, na hakuna mtu anayepaswa kuhisi kwamba kila kitu kinachofanywa katika sanitariamu iliyoanzishwa lazima kwanza kiwasilishwe kwenye kundi moja la watu. Njia hii Mungu ameikataza. Mungu Yule Yule aliyewaelekeza matabibu pale Battle Creek atawaelekeza wanaume na wanawake walioitwa kumtumikia Bwana katika sehemu mbalimbali za shamba lake la

mizabibu. {8T 233.2}

“Sheria za wanadamu na mipango ya wanadamu inaundwa ambayo haikubaliki na Mungu. Haitaonekana kuwa harufu ya uzima iletayo uzima. Ninalazimika kuiinua ishara ya hatari. Wasimamizi wa kila taasisi yetu wanahitaji kuwa na akili zaidi kuhusiana na kazi zao binafsi, si kwa kutegemea taasisi nyingine, bali, huku wakihifadhi utambulisho wa kazi yao, kwa kumtazama Mungu kama Mwalimu wao na kwa kuonesha imani yao Kwake kupitia huduma yao ya moyo wote. Kisha watakuza talanta na uwezo." {8T 233.3}

“Kristo anahitaji huduma ya daraja la juu zaidi ya ile ambayo imetolewa Kwake. Watu walio katika nafasi za madaraka wanapaswa, kwa kupitia kupokea nguvu za Roho Mtakatifu, kumdhihirisha Mkombozi kwa uwazi zaidi kuliko ambavyo wamemdhihirisha. Mungu asiye na kikomo aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee kama kafara kwa ajili yetu, ili kwamba sisi, kwa kumpokea kwa imani na kutenda wema Wake, tusipotee, bali tuwe na uzima wa milele. Ndugu zangu, mnadhani anachukuliaje ukosefu huo mkubwa wa shauku ya kiroho inayodhihirishwa juu ya rekodi ya dhabihu isiyo na kikomo iliyotolewa kwa ajili ya wokovu wetu? {8T 234.1}

"Tamaa zote za makuu za mwanadamu, kujisifu kote, lazima ziwekwe mavumbini. Nafsi, nafsi yenye dhambi, inabidi kushushwa, si kuinuliwa. Kwa utakatifu katika maisha ya kila siku tunapaswa kumdhihirisha Kristo kwa wale wanaotuzunguka. Asili potovu ya mwanadamu inapaswa kutiishwa, sio kuinuliwa. Kwa hivyo tu ndipo tutaweza kuwa wasafi na wasio na unajisi. Tunapaswa kuwa wanyenyekevu, wanaume na wanawake waaminifu. Kamwe tusikae juu ya kiti cha hukumu. Mungu anadai kuwa wawakilishi Wake wawe safi na watakatifu, wakidhihirisha uzuri wa utakaso. Njia daima inapaswa kubaki bila kizuizi, ili Roho Mtakatifu awe na njia iliyo wazi; vinginevyo wengine wataifunika kazi ambayo lazima ifanywe ndani ya moyo wa kawaida ili kukamilisha tabia ya Kikristo; nao watadhihirisha kutokukamilika kwao wenyewe kwa namna ambayo itabatilisha kweli ya Mungu, ambayo ni thabiti kama kiti cha enzi cha milele. Wakati Mungu akiwaita walinzi Wake kuinua ishara ya hatari, wakati huohuo anawasilisha mbele yao maisha ya Mwokozi kama kielelezo cha kile wanachopaswa kuwa na kufanya ili waokolewe. {8T 234.2}

"Kwa ajili ya wanafunzi wake Kristo aliomba: "Uwatakase kwa ile kweli; Neno lako ndiyo kweli." Hisia ya kupendeza, yenye kujitosheleza si ushahidi wa utakaso. Rekodi ya uaminifu hutunzwa kwa matendo yote ya watoto wa wanadamu. Hakuna kinachoweza kufichwa machoni pa Aliye juu na Mtakatifu akaaye milele. Wengine humfanya Kristo kuaibika kwa ajili ya ubunifu wao, mipango na hila. Mungu hapendezwi na mwenendo wao, kwa maana Bwana Yesu anadharauliwa na roho zao na kazi zao. Wanasahau maneno ya mtume: "Tumefanywa kuwa tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu." 1 Wakorintho 4:9. {8T 235.1}

“Maagizo ambayo Bwana ametoa kuhusu kazi Yake yanaonesha njia sahihi. Mipango ya Mungu na mawazo ya Mungu ni ya juu sana kuliko mipango ya mwanadamu na mawazo ya mwanadamu kama vile mbingu zilivyo juu kuliko dunia. Sauti ya Mungu inapaswa kusikika, hekima Yake inapaswa kuongoza. Ameeleza mpango Wake katika neno Lake na katika shuhuda ambazo Ametuma kwa watu Wake. Kazi ile tu ambayo itafanywa kwa mujibu wa kanuni za neno Lake ndiyo itakayosimama imara milele. {8T 235.2}

## SURA YA 37

## UONGOZI

St. Helena, California,
Novemba 17, 1903.

Katika magazeti ya kila siku ya miji mbalimbali kumetokea makala yanayoonesha kwamba kuna ugomvi kati ya Dk. Kellogg na Mama Ellen G. White kuhusu ni nani kati yao atakuwa kiongozi wa Waadventista wa Sabato. Niliposoma makala hizi nimefadhaika na huzuni kupita kiasi kwamba mtu yeyote angeweza kuelewa kazi yangu na kazi ya Dk. Kellogg vibaya kiasi hicho hata kuchapisha upotoshaji huo. Hakujawahi kuwa na mabishano kati ya Dk. Kellogg na mimi kuhusu suala la uongozi. Hakuna aliyewahi kunisikia nikidai nafasi ya uongozi wa dhehebu. {8T 236.1}

Nina kazi ya kufanya yenye wajibu mkubwa—kutoa kwa kalamu na kwa sauti maagizo ninayopewa, si kwa ajili ya Waadventista wa Sabato peke yao, bali kwa ulimwengu. Nimechapisha vitabu vingi, vikubwa na vidogo, na baadhi ya hivi vimetafsiriwa katika lugha kadhaa. Hiyo ndiyo kazi yangu—kuwafungulia wengine Maandiko kama ambavyo Mungu alivyoyafungua kwangu. {8T 236.2}

Mungu hajaweka mamlaka yoyote ya kifalme katika Kanisa la Waadventista wa Sabato ili kuitawala jamii nzima au kutawala tawi lolote la kazi. Yeye Hajaweka kwamba mzigo wa uongozi uwe juu ya watu wachache. Majukumu yanagawanywa kati ya idadi kubwa ya watu wenye uwezo.
{8T 236.3}

Kila mshiriki wa kanisa anayo sauti katika kuchagua maofisa wa kanisa. Kanisa linachagua maofisa wa majimbo yao ya Konferensi. Wajumbe waliochaguliwa katika Konferensi huchagua maofisa wa Unioni, na wajumbe waliochaguliwa katika Unioni huchagua maofisa wa Konferensi Kuu. Kwa utaratibu huu kila konferensi, kila taasisi, kila kanisa, na kila mtu binafsi, iwe mmoja kwa mmoja au kupitia kwa uwakilishi, anayo sauti katika uchaguzi wa watu wanaobeba majukumu makuu katika Konferensi Kuu (General Conference). {8T 236.4}

## Uzoefu wa Awali

Katika siku za mwanzo za kazi yetu ya kanisa Bwana alimteua Mzee James White kama mmoja ambaye, kwa kuunganishwa na mke wake, na chini ya uongozi maalumu wa Bwana, alipaswa kuchukua sehemu ya kwanza katika kuendeleza kazi hii. {8T 237.1}

Historia ya jinsi kazi ilivyopanuka inajulikana. Kiwanda cha uchapaji kilianzishwa kwanza huko Rochester, New York, na baadaye kuhamishiwa Battle Creek, Michigan. Na katika miaka ya baadaye Nyumba ya uchapaji ilianzishwa kwenye Pwani ya Pasifiki. {8T 237.2}

Ninamshukuru Bwana kwamba alitupa upendeleo wa kuwa na sehemu ya kutenda katika kazi hii tangu mwanzo. Lakini si kwa wakati ule ama tangu kazi hii ilipokua kwa kiasi kikubwa, kipindi ambacho majukumu yamesambazwa sana, Je, kuna mtu yoyote aliyenisikia nikidai uongozi wa watu hawa. {8T 237.3}

Tangu mwaka 1844 hadi sasa nimepokea ujumbe kutoka kwa Bwana nami nimewapa watu Wake. Hiyo ndiyo kazi yangu—kuwapa watu nuru ambayo Bwana ananipa. Nimeagizwa kupokea na kuwasilisha ujumbe Wake Bwana. Mimi sitakiwi kujitokeza mbele ya watu kama mwenye cheo kingine chochote isipokuwa cha mjumbe mwenye ujumbe. {8T 237.4}

Kwa miaka mingi Dk. J. H. Kellogg ameshikilia nafasi ya Tabibu mkuu katika kazi ya matibabu inayofanywa na Waadventista wa Sabato. Isingewezekana kwake kutenda kama kiongozi wa kazi ya jumla. Hii haijawahi kuwa sehemu yake, na kamwe haiwezi kuwa. {8T 237.5}

## Mungu Kiongozi Wetu

Ninaliandika hili ili wote wajue kwamba hakuna malumbano au mgogoro kati ya Waadventista wa Sabato kuhusu suala la uongozi. Bwana Mungu wa mbinguni Ndiye Mfalme wetu. Yeye Ndiye kiongozi ambaye tunaweza kumfuata kwa usalama, kwa maana Yeye hakosei kamwe. Hebu tumheshimu Mungu na Mwanawe, ambaye kupitia Kwake anawasiliana na ulimwengu. {8T 238.1}

Mungu angefanya kazi kwa nguvu, na kutenda mambo makuu kwa ajili ya watu Wake leo kama wangejiweka kikamilifu chini ya uongozi Wake. Wanahitaji uwepo wa Roho Mtakatifu kila wakati, na kukaa ndani Yake. Ikiwa kungekuwa na maombi zaidi katika mabaraza ya wale wanaobeba majukumu, Na kunyenyekesha sana moyo mbele za

Mungu, tungeliona ushahidi mwingi wa uongozi wa Mwenyezi Mungu, na kazi yetu ingesonga mbele haraka.. {8T 238.2}

## SURA YA 38
## WAMOJA NA KRISTO KATIKA MUNGU

Bwana anawaita watu wenye imani ya Kweli na wenye akili timamu/balansi;;, watu wanaotambua tofauti kati ya Kweli na uongo. Kila mmoja anapaswa kujihadhari, akijifunza na kutenda masomo yaliyotolewa katika sura ya kumi na saba ya Yohana, na kuhifadhi imani hai katika Ukweli kwa wakati huu. Tunahitaji kujitawala nafsi kule ambako kutatuwezesha kuleta mienendo yetu kupatana na ombi la Kristo. {8T 239.1}

Maagizo niliyopewa na Yule Mwenye mamlaka ni kwamba tunapaswa kujifunza kujibu ombi lililoandikwa katika sura ya kumi na saba ya Yohana. Tunapaswa kufanya ombi hili kuwa somo letu la kwanza. Kila mchungaji, kila mmishenari wa tiba, anapaswa kujifunza sayansi ya ombi hili. Ndugu na dada zangu, ninawaomba mzingatie maneno haya na kuja katika kujifunza kwenu mkiwa na utulivu, unyenyekevu, roho iliyotubu, na nguvu maridhawa za akili zinazotawaliwa na Mungu. Wale wanaoshindwa kujifunza masomo yaliyomo katika ombi hili wako katika hatari ya kufanya maendeleo ya upande mmoja, ambayo hakuna mafunzo yajayo yataweza kusahihisha kikamilifu. {8T 239.2}

“Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami ndani yako; hao nao wawe ndani Yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba Wewe Ndiwe uliyenituma. {8T 239.3}

Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama Sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, Nawe ndani Yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa wewe Ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda Mimi." {8T 239.4}

"Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja Nami popote nilipo, wapate na kuutazama utukufu Wangu ulionipa Mimi; kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi ulimwengu. Baba Mwenye haki, ulimwengu haukukujua; lakini Mimi nalikujua, na hao wamejua ya kuwa Ndiwe uliyenituma. Nami naliwajulisha Jina Lako, tena nitawajulisha hilo; ili pendo lile ulilonipenda Mimi liwe ndani yao, Nami Niwe ndani

yao." Yohana 17:20-26. {8T 239.5}

Ni kusudi la Mungu kwamba watoto Wake wapatane kwa umoja. Je, hawatarajii kuishi pamoja katika mbingu moja? Je, Kristo amegawanyika dhidi Yake Mwenyewe? Je, atawapa watu Wake mafanikio kabla hawajasafisha takataka za shuku mbaya, hiana na mafarakano, kabla ya watenda kazi, kwa umoja wa kusudi, hawajatoa moyo na akili na nguvu kwa ajili ya kazi iliyo takatifu kiasi hicho machoni pa Mungu? Umoja huleta nguvu; utengano, udhaifu. Tukiungana sisi kwa sisi, tukifanya kazi pamoja kwa upatanifu kwa ajili ya wokovu wa wanadamu, kwa hakika tutakuwa “watenda kazi pamoja na Mungu.” Wale wanaokataa kufanya kazi kwa upatanifu humfedhehesha Mungu sana. Adui wa roho anafurahi kuwaona wakifanya kazi kwa makusudi yanayokinzana/yanayokingamana wao kwa wao. Watu hao wanatakiwa kukuza upendo wa ndugu na upole wa moyo. Kama wangeweza kuweka kando pazia linalofunika wakati ujao na kuona matokeo ya mfarakano wao bila shaka wangeongozwa kutubu. {8T 240.1}

Ulimwengu unatazama kwa furaha utengano kati ya Wakristo. Ukafiri unapendwa sana. Mungu anahitaji mabadiliko kati ya watu Wake. Muungano na Kristo na sisi kwa sisi ndio usalama wetu pekee katika siku hizi za mwisho. Hebu tusimruhusu Shetani kusonda kidole kwa washiriki wetu wa kanisa, akisema: "Tazama jinsi ambavyo watu hawa, wanaosimama chini ya bendera ya Kristo, wanavyochukiana wao kwa wao. Hatuna cha kuogopa kutoka kwao wakati ambapo wanatumia nguvu nyingi zaidi kupigana wao kwa wao kuliko kufanya vita dhidi ya majeshi yangu." {8T 240.2}

Baada ya kushuka kwa Roho Mtakatifu wanafunzi walitoka kwenda kumtangaza Mwokozi aliyefufuka, shauku yao pekee ilikuwa ni, wokovu wa roho. Walifurahia utamu wa ushirika na watakatifu. Walikuwa wapole, wenye hadhari, wenye kujikana nafsi, waliokuwa tayari kutoa chochote kwa ajili ya Ukweli. Katika ushirikiano wao wa kila siku walidhihirisha upendo ambao Kristo alikuwa amewaamuru kuudhihirisha. Kwa maneno na matendo yasiyo na ubinafsi walijitahidi kuwasha upendo huu katika mioyo mingine. {8T 241.1}

Waumini daima walipaswa kutunza upendo uliojaza mioyo ya mitume baada ya kushuka kwa Roho Mtakatifu. Walipaswa kwenda mbele kwa utii wa hiari wa amri mpya: “Kama vile Nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Yohana 13:34. Walipaswa kuungana kwa karibu zaidi na Kristo ili wawezeshwe kutimiza matakwa Yake. Uweza wa Mwokozi ambaye angewahesabia haki kwa haki Yake ulipaswa kukuzwa. {8T 241.2}

Lakini Wakristo wa awali walianza kutafuta kasoro kati yao. Wakifikiri sana juu ya makosa, na kutoa nafasi kwa ukosoaji usio na huruma, walimsahau Mwokozi na upendo mkuu alioudhihirisha kwa wenye dhambi. Wakawa watiifu sana kuhusiana na ushikaji wa taratibu za nje, wenye kujali sana kuhusu nadharia ya imani, wasio na

huruma zaidi katika ukosoaji wao. Katika bidii yao ya kuwahukumu wengine walisahau makosa yao wenyewe. Walisahau somo la upendo wa ndugu ambalo Kristo alikuwa amewafundisha. Na, cha kusikitisha zaidi, hawakutambua hasara yao. Hawakutambua kwamba furaha na shangwe zilikuwa zikiondoka katika maisha yao, na kwamba punde tu wangetembea gizani, wakiwa wameufungia upendo wa Mungu nje ya mioyo yao. {8T 241.3}

Mtume Yohana alitambua kwamba upendo wa ndugu ulikuwa unafifia katika kanisa, na alielezea sana juu ya jambo hili. Hadi kufikia siku ya kifo chake, aliwahimiza waumini waweke katika vitendo upendo wa kudumu kati yao. Barua zake kwa makanisa zimejazwa na wazo hili. "Wapenzi, na mpendane," anaandika; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu……. Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye……" Wapenzi, ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana." 1 Yohana 4:7-11. {8T 241.4}

Katika kanisa la Mungu leo upendo wa ndugu umekosekana sana. Wengi wa wale wanaokiri kumpenda Mwokozi hupuuza kuwapenda wale ambao wameunganishwa nao katika ushirika wa Kikristo. Sisi ni wa imani moja, washiriki wa familia moja, wote watoto wa Baba mmoja wa mbinguni, wenye tumaini moja lenye baraka la kutokufa. Je, ni kwa ukaribu na upendo kiasi gani kifungo kinachotuunganisha kinapaswa kuwa. Watu wa ulimwengu wanatutazama kuona kama imani yetu inaweka mvuto wa kutakasa mioyoni mwetu. Wao ni wepesi wa kutambua kila kasoro katika maisha yetu, kila kutofautiana katika matendo yetu. Hebu tusiwape nafasi ya kuilaumu imani yetu. {8T 242.1}

Si upinzani wa ulimwengu unaotuhatarisha zaidi; ni uovu unaotunzwa mioyoni mwa wale waumini bayana ndio unaoleta maafa yetu makubwa kabisa na kurudisha nyuma maendeleo ya kazi ya Mungu. Hakuna njia ya hakika zaidi ya kudhoofisha hali yetu ya kiroho kuliko kuwa na husuda, kutiliana shaka, kutafuta makosa, hiana na shuku mbaya. "Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani. Maana hapo palipo wivu na ugomvi ndipo palipo machafuko, na kila tendo baya. Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki. Na tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani." Yakobo 3:15-18. {8T 242.2}

Upatanifu, maelewano na muungano uliopo kati ya watu wenye tabia mbalimbali ndio ushuhuda wenye nguvu kabisa unaoweza kutolewa kwamba Mungu alimtuma Mwanawe ulimwenguni ili apate kuwaokoa wenye dhambi. Ni upendeleo kwetu kutoa ushahidi huu. Lakini, ili kulifanya hili, ni lazima tujiweke chini ya utawala wa Kristo. Tabia zetu lazima zifinyangwe/ziongozwe ili ziwe katika upatanifu na tabia Yake, nia zetu lazima zisalimishwe kwa mapenzi Yake. Kisha tutafanya kazi pamoja bila wazo la mgongano. {8T 242.3}

Tofauti ndogo ndogo zinazozingatiwa huongoza kwenye matendo yanayoharibu ushirika wa Kikristo. Hebu tusimruhusu adui kupata ushindi juu yetu. Hebu tuendelee kumkaribia Mungu na kukaribiana sisi kwa sisi. Ndipo tutakapokuwa kama miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, na kumwagiliwa na mto wa uzima. Na ni kwa wingi kiasi gani tutakavyozaa matunda! Je! Kristo hakusema: "Hivyo hutukuzwa Baba Yangu, kwa vile mzaavyo sana"? Yohana 15:8. {8T 243.1}

Moyo wa Mwokozi umeelekezwa juu ya wafuasi Wake kutimiza kusudi la Mungu katika kimo na kina chake chote. Wanapaswa kuwa wamoja ndani Yake, ingawa wametawanyika kote ulimwenguni. Lakini Mungu hawezi kuwafanya wamoja katika Kristo isipokuwa wawe tayari kuacha njia yao wenyewe kwa ajili ya njia Yake. {8T 243.2}

Wakati ombi la Kristo linapoaminiwa kikamilifu, wakati maagizo Yake yanapoletwa katika maisha ya kila siku ya watu wa Mungu, umoja katika utendaji utaonekana katika safu zetu. Ndugu atafungwa kwa ndugu kwa vifungo vya dhahabu vya upendo wa Kristo. Roho wa Mungu peke yake Ndiye anayeweza kuleta umoja huu. Yeye aliyejitakasa Mwenyewe Ndiye anayeweza kuwatakasa wanafunzi Wake. Wakiwa wameungana pamoja Naye, wataungana wao kwa wao katika imani takatifu kabisa. Tunapojitahidi kuwa na umoja huu kwa namna ambayo Mungu anataka tujitahidi, umoja huu utatujia. {8T 243.3}

## SURA YA 39
## WASHIRIKI WALEI WASONGE MBELE

Kuna kazi kubwa zaidi iliyo juu ya mshiriki mmoja mmoja wa kanisa kuliko vile wanavyotambua. Hawayafahamu madai ya Mungu. Wakati umefika ambapo kila njia na fedha inapaswa kubuniwa na kutumiwa ili kuweza kusaidia katika kuwatayarisha watu kusimama katika siku ile ya Mungu. Ni lazima tuwe macho kabisa, huku tukikataa kuruhusu fursa zenye thamani kupita bila kutumiwa vizuri. Ni lazima tufanye yote tuwezayo ili tuweze kuzivuta roho zipate kumpenda Mungu na kushika amri Zake. Yesu anahitaji hili kwa wale wanaoujua Ukweli. Je, dai Lake halina maana au mashiko? Je, maisha ya Kristo si mfano kwetu? Je, hatuwiwi na Mwokozi deni la upendo, la kazi ya bidii, isiyo na ubinafsi kwa ajili ya wokovu wa wale ambao kwaajili yao aliotoa maisha Yake? {8T 244.1}

Washiriki wengi wa makanisa yetu makubwa hawafanyi lolote unapolinganisha. Wangeweza kutimiza kazi nzuri ikiwa, badala ya kukusanyika pamoja, wangetawanyika katika sehemu ambazo bado hazijafikiwa na Ukweli. Miti

iliyopandwa kwa karibu sana haistawi wala kunawiri. Hupandikizwa na mtunza bustani, ili ipate nafasi ya kukua na isidumae na kuwa dhaifu. Sheria iyo hiyo ingefanya kazi vizuri kwa makanisa yetu makubwa. Wengi wa washiriki wanakufa kiroho kwa kukosa kazi hii hii. Wanakuwa dhaifu na kukosa ufanisi. Kama wangehamishwa, wangekuwa na nafasi ya kukua wakiwa na nguvu na juhudi. {8T 244.2}

Si kusudi la Mungu kwamba watu Wake waanzishe koloni au kukaa pamoja katika makundi makubwa kwenye jumuiya fulani. Wanafunzi wa Kristo ni wawakilishi Wake duniani, na Mungu anakusudia kwamba watawanyike kote juu ya nchi, katika miji midogo, miji mikubwa, na vijiji, kama nuru katikati ya giza la ulimwengu. Wanapaswa kuwa wamishenari kwa ajili ya Mungu, wakishuhudia kwa imani na matendo yao ukaribu wa kuja kwa Mwokozi. {8T 244.3}

Washiriki, walei wa makanisa yetu wanaweza kukamilisha kazi, ambayo hadi sasa, wameianza kwa udogo sana. Asiwepo mtu atakayehamia sehemu mpya kwa ajili ya manufaa ya kidunia tu; bali palipo na fursa ya kupata riziki, hebu familia zilizo na msingi mzuri katika Ukweli ziingie, familia moja au mbili katika sehemu, wakifanya kazi kama wamishenari. Wanapaswa kuhisi upendo kwa ajili ya roho, mzigo wa kutenda kazi kwa ajili yao, na wanapaswa kuchunguza kujua jinsi ya kuwaleta katika Kweli. Wanaweza kugawanya machapisho yetu, kufanya mikutano katika nyumba zao, kufahamiana na majirani zao, na kuwaalika waje kwenye mikutano hii. Hivyo wanaweza kuiruhusu nuru yao kuangaza katika matendo mema. {8T 245.1}

Hebu watenda kazi wasimame imara katika Mungu, wakilia, wakiomba, wakifanya kazi kwa ajili ya wokovu wa wanadamu wenzao. Kumbukeni kwamba mnapiga mbio, mkitafuta taji ya umilele. Wakati wengi wanapenda sifa za wanadamu kuliko fadhila za Mungu, hebu ninyi mfanye kazi kwa unyenyekevu. Jifunzeni kuiweka imani katika matendo kwa kuwafanya jirani zenu wawepo mbele ya kiti cha neema na kumsihi Mungu aiguse mioyo yao. Kwa njia hii kazi ya umishenari yenye kuleta matokeo yanayotakiwa inaweza kufanyika. Wengine wataweza kufikiwa ambapo hawangeweza kumsikiliza mchungaji au mwinjilisti wa vitabu. Na hivyo wale wanaofanya kazi katika maeneo mapya watajifunza njia bora zaidi za kuwafikia watu na wanaweza kuandaa njia kwa ajili ya watenda kazi wengine. {8T 245.2}

Uzoefu wa thamani unaweza kupatikana kwa mtu anayejihusisha na kazi hii. Huyu awe mtu mwenye mzigo juu ya moyo wake wa roho za jirani zake. Ni lazima awe na msaada wa Yesu. Atakuwa mwangalifu kiasi gani katika kutembea kwa tahadhari, ili maombi yake yasizuiliwe, ili dhambi yoyote inayolelewa kwa kupendwa isimtenge na Mungu. Huku akiwasaidia wengine, mtenda kazi kama huyo anapata nguvu na uelewa wa kiroho yeye mwenyewe, na katika shule hii ya unyenyekevu anaweza akapata sifa za kuingia katika uwanja mpana zaidi. {8T 245.3}

Kristo anasema: " Hivyo hutukuzwa Baba Yangu, kwa vile mzaavyo sana." Yohana 15:8. Mungu ametujalia uwezo na ametukabidhi vipaji ili tuvitumie kwa ajili Yake. Kila mtu amepewa kazi yake—si kazi tu katika shamba lake la nafaka na ngano, bali kazi ya bidii na ya kudumu kwa ajili ya wokovu wa roho za watu. Kila jiwe katika hekalu la Mungu lazima liwe jiwe hai, jiwe linalong'aa, likiakisi nuru kwa ulimwengu. Hebu walei wafanye yote wawezayo; na kadiri wanavyotumia talanta walizonazo, Mungu atazidi kuwapa neema na uwezo zaidi. Shughuli zetu nyingi za umishenari zimelemaa kwa sababu kuna wengi wanaokataa kuingia katika milango ya kunufaisha na ufanisi ambayo inafunguliwa mbele yao. Hebu wote wanaouamini ukweli waanze kufanya kazi. Fanya kazi iliyo karibu nawe; fanya kitu chochote, hata kama ni kidogo, kuliko kuwa, kama watu wa Merozi, wasiofanya kitu chochote. {8T 246.1}

Hatutapungukiwa mali kama tu tutasonga mbele tukimtumaini Mungu. Bwana Yuko tayari kufanya kazi kubwa kwa wote wanaomwamini kweli kweli. Ikiwa washiriki walei wa kanisa wataamka kufanya kazi wanayoweza kuifanya, wakienda vitani kwa nia na gharama yao wenyewe, kila mmoja akiona ni kiasi gani anachoweza kutimiza katika kuvuta roho kuja kwa Yesu, tutaona wengi wakiacha safu za Shetani na kusimama chini ya bendera ya Kristo. Kama watu wetu watatenda kulingana na nuru inayotolewa katika maneno haya machache ya maagizo, bila shaka tutauona wokovu wa Mungu. Uamsho wa ajabu utafuata. Wenye dhambi wataongoka, na roho nyingi zitaongezeka kanisani. Tunapoleta mioyo yetu katika umoja na Kristo, na maisha yetu kuwa katika upatanifu na kazi Yake, Roho iliyoshuka juu ya wanafunzi Siku ile ya Pentekoste itashuka juu yetu. {8T 246.2}

## SURA YA 40
## JE! TUTAKUTWA TUMEPUNGUA?

St. Helena, California, Aprili 21, 1903.

Nafasi yetu ulimwenguni si kama ilivyopaswa kuwa. Tuko mbali na pale tulipopaswa kuwa kama uzoefu wetu wa Kikristo ungekuwa katika upatanifu na nuru na fursa tulizopewa, kama tangu mwanzo tungesonga daima kwenda mbele na kwenda juu. Kama tungetembea katika nuru ambayo tumepewa, kama tungeandama kumjua Bwana, njia yetu ingekua yenye kung'aa zaidi na zaidi. Lakini wengi wa wale ambao wamekuwa na nuru ya pekee wamefanana sana na ulimwengu kiasi kwamba ni kwa shida sana unaweza kuwatofautisha na walimwengu. Hawajitokezi na kusimama kama watu wa pekee wa Mungu, walioteuliwa na wa thamani kubwa. Ni vigumu kupambanua kati ya yule amtumikiaye Mungu na yule asiyemtumikia. {8T 247.1}

Katika mizani ya Patakatifu kanisa la Waadventista wa Sabato litapaswa kupimwa. Litahukumiwa kwa fursa na upendeleo ambao limekuwa navyo. Kama uzoefu wake wa kiroho haulingani na manufaa ambayo Kristo, kwa gharama isiyo na kikomo, alilikabidhi, ikiwa baraka zilizotolewa kwake hazijaleta stahiki kuifanya kazi iliyokabidhiwa kwake, juu yake itatamkwa hukumu: "Umeonekana kuwa umepunguka." Kwa nuru iliyotolewa, fursa zilizotolewa, litahukumiwa. {8T 247.2}

### Kusudi La Mungu Kwa Ajili Ya Watu Wake

Mungu ameweka akiba upendo, furaha, amani, na ushindi wa kupendeza kwa wote wanaomtumikia katika roho na kweli. Watu Wake wanaozishika amri wanapaswa kusimama daima wakiwa tayari kwa ajili ya huduma. Wanapaswa kupokea ongezeko la neema na nguvu, na ongezeko la maarifa ya utendaji wa kazi ya Roho Mtakatifu. Lakini wengi hawako tayari kupokea karama za thamani za Roho ambazo Mungu anasubiri kuwapa. Hawafiki juu na juu zaidi kwa ajili ya uwezo kutoka juu ili kwamba kupitia karama zilizotolewa, waweze kutambulika kama watu wa pekee wa Mungu, wenye bidii katika kazi njema. {8T 247.3}

### "Ukatubu, Ukayafanye Matendo ya Kwanza"

Maonyo mazito, yanayodhihirika katika uharibifu wa vifaa vinavyothaminiwa sana kwa ajili ya utumishi, yanatuambia: "Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza." Ufunuo 2:5. Kwa nini kuna utambuzi hafifu kiasi hicho wa hali halisi ya kiroho ya kanisa? Je upofu haukuwaangukia walinzi waliosimama juu ya kuta za Sayuni? Je, si watumishi wengi wa Mungu wamekuwa wasiojali na wenye kuridhika, kana kwamba nguzo ya wingu wakati wa mchana na nguzo ya moto wakati wa usiku imekaa juu ya Patakatifu? Je, hawapo wale walio katika nafasi za dhamana, wanaokiri kumjua Mungu, ambao katika maisha na tabia zao wanamkana? Je, si wengi wa wale wanaojihesabu kuwa wateule Wake, watu wa pekee wameridhika kuishi bila uthibitisho kwamba kwa kweli Mungu Yuko miongoni mwao ili kuwaokoa kutoka kwenye mitego na mashambulizi ya Shetani? {8T 248.1}

Je, tusingekuwa na nuru kubwa zaidi wakati huu ikiwa, hapo awali, tungepokea maonyo ya Bwana, kukiri uwepo Wake, na kuacha mazoea yote yaliyo kinyume na mapenzi Yake? Kama tungefanya hivi, nuru ya mbinguni ingeangaza ndani ya hekalu la nafsi, na kutuwezesha kuufahamu Ukweli na kumpenda Mungu sana na jirani zetu kama nafsi zetu. Loo, Ni kwa ukubwa kiasi gani Kristo anavunjiwa heshima na wale ambao, wanakiri kuwa Wakristo, wakifedhehesha Jina wanalolibeba kwa kushindwa kufanya maisha yao yapatane na madai yao, kwa kushindwa kutendeana wao kwa wao kwa upendo na heshima ambayo Mungu anatazamia waidhihirishe ndani yao

katika maneno mazuri/mema, ukarimu na matendo ya uungwana na staha! {8T 248.2} 249

Nguvu kutoka chini zinachochewa kwa nguvu sana. Vita na umwagaji damu ndio matokeo. Angahewa ya kimaadili imetiwa sumu na matendo ya kikatili na ya kutisha. Roho ya mashindano inaenea; imejaa kila mahali. Nafsi nyingi zinatawaliwa na roho ya ulaghai, au biashara za udanganyifu. Wengi watajitenga na imani, wakizikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani. Hawatambui ni roho gani inayowashikilia. {8T 249.1}

## Kushindwa Kumheshimu Mungu

Yeye aonaye chini ya uso, ambaye husoma mioyo ya watu wote, asema hivi kwa wale ambao wamekuwa na nuru kubwa: “Hawahuzunishwi na hawashangazwi kwa sababu ya hali yao ya kimaadili na ya kiroho. “Naam, wamezichagua njia zao wenyewe, na nafsi zao zafurahia machukizo yao. Mimi Nami nitachagua mapigo yao, nitaleta hofu zao juu yao; kwa sababu nilipoita, hawakuitika; na niliponena, hawakusikia; bali walifanya yaliyo maovu machoni Pangu, na kuyachagua nisiyoyafurahia." “Ndio maana Mungu ameruhusu watawaliwe na nguvu ya udanganyifu ili waendelee kuuamini uongo; ,” kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa. “bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu.” Isaya 66:3, 4; 2 Wathesalonike 2:11, 10, 12. {8T 249.2}

Mwalimu wa kimbingu aliuliza: “Ni udanganyifu gani wenye nguvu zaidi unaoweza kuidanganya akili kuliko kujifanya kuwa unajenga juu ya msingi ufaao na kwamba Mungu anakubali kazi zako, wakati kwa uhalisia unafanya mambo mengi kulingana na kanuni za kiulimwengu na unamtendea Yehova dhambi? Loo, ni udanganyifu mkuu, upotofu unaovutia sana, unaochukua umiliki wa akili wakati watu ambao wamewahi kuijua Kweli, wanapodhani kuwa namna ya utauwa ni roho na uwezo uliomo ndani yake; pale wanapodhani kuwa wao ni matajiri na wameongezeka katika mema na hawana haja ya chochote, na huku katika hali halisi ni wahitaji wa kila kitu." {8T 249.3}

Mungu hajabadili mtazamo juu ya watumishi Wake waaminifu ambao wanaweka mavazi yao bila doa. Lakini wengi wanalia, “Amani na salama,” wakati uharibifu wa ghafla unakuja juu yao. Isipokuwa tu kuna toba kamili, isipokuwa tu wanadamu wamenyenyekesha mioyo yao kwa kukiri na kuupokea Ukweli kama ulivyo katika Yesu, hawataingia mbinguni kamwe. Utakaso utakapotokea katika safu zetu, hatutaweza kutulia kamwe, tukijisifu kuwa matajiri na wenye mali nyingi, wasiohitaji chochote. {8T 250.1}

Ni nani anayeweza kusema kwa kweli: "Dhahabu yetu imejaribiwa katika moto; nguo zetu hazijatiwa doa na ulimwengu"? Nilimwona Mwalimu wetu akinyosha kidole kwenye mavazi ya kile kinachoitwa haki. Akiwavua, aliweka wazi unajisi ulio ndani.

Kisha akaniambia: “Je, huoni jinsi walivyoficha kwa udanganyifu unajisi wao na uozo wa tabia zao? 'Mji huu uliokuwa mwaminifu umekuwaje kahaba!' Nyumba ya Baba Yangu inafanywa kuwa nyumba ya biashara, mahali ambapo uwapo wa Mungu na utukufu Wake umeondoka! Kwa sababu hiyo kuna udhaifu, na nguvu inakosekana." {8T 250.2}

### Wito wa Kufanya Matengenezo

Isipokuwa kanisa, ambalo kwa sasa limetiwa chachu na ukengeufu wake, limetubu na kuongoka, litakula matunda ya matendo yake yenyewe, hadi litakapojichukia lenyewe sana. Litakapoupinga uovu na kuchagua lililo jema, litakapomtafuta Mungu kwa unyenyekevu wote na kuufikia mwito wake mkuu katika Kristo, likisimama juu ya jukwaa la Ukweli wa milele na kwa imani likishikilia mafanikio yaliyotayarishwa kwa ajili Yake, litaponywa. Litajitokeza katika usahili na usafi uliotolewa na Mungu, likitenganishwa na mitego ya kidunia, likionesha kwamba kweli imelifanya liwe huru kweli kweli. Ndipo washiriki wake watakuwa wateule wa Mungu, wawakilishi Wake. {8T 250.3}

Wakati umefika kwa ajili ya matengenezo kamili kufanyika. Matengenezo haya yanapoanza, roho ya maombi itamchochea kila muumini na itaondoa katika kanisa roho ya mafarakano na ugomvi. Wale ambao wamekuwa hawaishi katika ushirika wa Kikristo watakaribiana kila mmoja na mwenzake. Mshiriki mmoja anayefanya kazi katika njia sahihi atawaongoza washiriki wengine kuungana pamoja Naye katika kufanya maombi kwa ajili ya ufunuo wa Roho Mtakatifu. Hakutakuwa na mkanganyiko wowote, kwa sababu wote watakuwa katika upatanifu na nia ya Roho. Vizuizi vinavyowatenganisha muumini na muumini vitavunjwa, na watumishi wa Mungu watazungumza jambo moja. Bwana atashirikiana na watumishi Wake. Wote wataomba kwa ufahamu ombi ambalo Kristo aliwafundisha watumishi Wake: “Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.” Mathayo 6: 10 {8T 251.1}

## SURA YA 41

## KWENDA NYUMBANI-Safari ya Kuelekea Nyumbani

Ninaposikia juu ya majanga mabaya ambayo hutokea juma baada ya juma, najiuliza: Mambo haya yanamaanisha nini? Maafa ya kutisha yanafuatana kwa haraka. Ni mara ngapi tunasikia matetemeko ya ardhi na vimbunga, uharibifu wa moto na mafuriko, na upotevu mkubwa wa maisha na mali! Dhahiri majanga haya ni milipuko geugeu ya nguvu zinazoonekana kuwa hazina mpangilio, zisizodhibitiwa, lakini ndani Yake kusudi la Mungu laweza kusomwa. Ni miongoni mwa njia ambazo Yeye

hutumia kuwaamsha wanaume na wanawake juu ya hali yao ya hatari. {8T 252.1}

Kuja kwa Kristo ni karibu zaidi kuliko wakati tulipoanza kuamini. Pambano kuu linakaribia mwisho wake. Hukumu za Mungu ziko katika nchi. Zinazungumza kwa maonyo mazito, zikisema: “Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu Yuaja.” Mathayo 24:44. {8T 252.2}

Lakini wapo wengi, wengi katika makanisa yetu ambao wanajua kidogo maana halisi ya Ukweli wa wakati huu. Ninawasihi wasipuuze ishara za nyakati zinazotimia, ambazo husema waziwazi kwamba mwisho umekaribia. Lo, ni wengi kiasi gani ambao hawajatafuta wokovu wa nafsi zao hivi karibuni watafanya maombolezo ya uchungu: “Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha, wala sisi hatukuokoka!”{8T 252.3}

Tunaishi katika matukio ya mwisho ya historia ya dunia hii. Unabii unatimia kwa haraka. Saa za hukumu ya upelelezi zinapita haraka. Hatuna muda- hata kidogo - wa kupoteza. Hebu tusikutwe tumelala katika kituo chetu cha ulinzi. Hebu yeyote asiseme moyoni mwake au kwa vitendo vyake: “Bwana wangu amekawia kuja.” Hebu ujumbe wa kurudi upesi kwa Kristo usikike kwa Maneno ya dhati ya onyo. Hebu tuwashawishi wanaume na wanawake kila mahali kutubu na kuikimbia ghadhabu inayokuja. Hebu tuwaamshe kwa ajili ya maandalizi ya mara moja, kwa maana hatujui hata kidogo yale yaliyo mbele yetu. Hebu wachungaji na washiriki walei waende kwenye mashamba yanayoiva ili kuwaambia wasiojihusisha na wasiojali wamtafute Bwana maadamu anapatikana. Wafanyakazi watapata mavuno yao popote pale wanapotangaza Kweli zilizosahaulika za Biblia. Watawapata wale ambao wataukubali Ukweli na kutoa maisha yao kwa ajili ya kuzileta roho kwa Kristo. {8T 252.4}

Bwana Yu karibu kuja, na lazima tujitayarishe kukutana Naye kwa amani. Na tuazimie kufanya yote tuwezayo kuwapa nuru wale wanaotuzunguka. Hatupaswi kuwa na huzuni, bali wachangamfu, na tunapaswa kumweka Bwana Yesu mbele yetu daima. Yeye anakuja hivi karibuni, na lazima tuwe tayari na kungojea kuonekana Kwake. Lo, itakuwa utukufu wa jinsi gani kumwona na kukaribishwa kama waliokombolewa Wake! Tumengoja kwa muda mrefu, lakini tumaini letu halipaswi kufifia. Ikiwa tu tutamwona Mfalme katika uzuri Wake tutabarikiwa milele. Ninahisi kama ni lazima nipaze sauti kwa nguvu: "Naelekea nyumbani! Homeward bound" Tunakaribia wakati ambapo Kristo atakuja kwa nguvu na utukufu mkuu kuchukua waliokombolewa hadi kwenye makao yao ya milele. - {8T 253.1}

“Katika siku hiyo watasema, Tazama, huyu Ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie; Huyu Ndiye Bwana tuliyemngoja, Na tushangilie na kuufurahia wokovu

Wake.” Isaya 25:9. - {8T 253.2}

“Piteni, piteni, katika malango; Itengenezeni njia ya watu; Tutieni, tutieni barabara; toeni mawe yake; Twekeni bendera kwa ajili ya kabila za watu. Tazama, Bwana ametangaza habari mpaka mwisho wa dunia, Mwambieni binti Sayuni, Tazama, wokovu wako unakuja; Tazama, thawabu Yake i pamoja Naye, Na malipo Yake yako mbele Zake. Nao watawaita, Watu watakatifu, Waliokombolewa na Bwana; Nawe utaitwa, Aliyetafutwa, Mji usioachwa." Isaya 62:10-12. {8T 253.3}

Katika kazi kuu ya mwisho, kabla tu ya kufunga kazi, tutakutana na fadhaa ambayo hatutajua jinsi ya kushughulika nayo; lakini tusisahau kwamba zile Nguvu Kuu Tatu za mbinguni zinafanya kazi, kwamba mkono wa Kiungu uko kwenye gurudumu, na kwamba Mungu atatimiza ahadi Zake. Atakusanya kutoka ulimwenguni watu ambao watamtumikia kwa haki. {8T 254.1}

“Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi Mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe Kwangu; ili nilipo Mimi, nanyi mwepo.” Yohana 14:1-3 {8T 254.2}

Kwa muda mrefu tumengoja kurudi kwa Mwokozi wetu. Lakini hata hivyo ni ahadi ya hakika. Hivi karibuni tutakuwa katika maskani yetu tuliyoahidiwa. Hapo Yesu atatuongoza kando ya kijito kilicho hai kinachotiririka kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu na atatufafanulia giza na shida ambazo kwazo alitupitisha katika dunia hii ili kukamilisha tabia zetu. Hapo tutaona kwa wazi uzuri wa Edeni iliyorejeshwa. Tukizitupa miguuni pa Mkombozi taji alizoweka juu ya vichwa vyetu, na kugusa vinubi vyetu vya dhahabu, tutazijaza mbingu zote sifa kwa Yeye Aketiye juu ya kiti cha enzi. {8T 254.3}

# SEHEMU YA 5—MAARIFA YA MUHIMU

"Nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo." 2 Wakorintho 4:6.

## SURA YA 42
## MUNGU KATIKA ASILI

Kabla ya kuingia kwa dhambi, hakuna wingu lililotua juu ya mawazo ya wazazi wetu wa kwanza ili kuvuruga mtazamo wao juu ya tabia ya Mungu. Walikuwa katika upatanifu kamili kwa mapenzi ya Mungu. Kwa ajili ya kuwasitiri, nuru nzuri, nuru ya Mungu, iliwazunguka. Nuru hii iliyo angavu na kamilifu ilitia nuru kila kitu walichokikaribia. {8T 255.1}

Asili ilikuwa kitabu chao cha kujifunzia-Kitabu cha kiada. Katika bustani ya Edeni uwapo wa Mungu ulioneshwa wazi, sifa Zake zilidhihirishwa, katika vitu vya asili vilivyowazunguka. Kila kitu ambacho macho yao yalitua juu yake kilizungumza nao. Vitu vya Mungu visivyoonekana, "hata uweza Wake wa milele na Uungu," vilionekana waziwazi, vikieleweka kwa vitu vilivyoumbwa. {8T 255.2}

### Matokeo ya Dhambi

Lakini ingawa ni kweli kwamba hapo mwanzo Mungu aliweza kutambulika katika maumbile ya asili, haimaanishi kwamba baada ya Anguko maarifa kamili ya Mungu yalifunuliwa katika ulimwengu wa asili kwa Adamu na uzao wake. Asili iliweza kuwasilisha masomo yake kwa mwanadamu asiye na hatia. Lakini uasi ulileta doa juu ya dunia na kuingilia kati ya asili na Mungu wa hiyo asili. Kama Adamu na Hawa

wasingemuasi Muumba wao, wangebaki katika njia ya unyofu kamili, wangeendelea kujifunza kuhusu Mungu kupitia katika kazi Zake. Lakini walipomsikiliza mjaribu na kumtenda Mungu dhambi, nuru ya mavazi ya mbinguni ya kutokuwa na hatia iliondoka kwao. Wakiwa wamenyang'anywa nuru ya mbinguni, hawakuweza tena kutambua tabia ya Mungu katika kazi za mikono Yake. {8T 255.3}

Na kwa kutokutii kwa mwanadamu mabadiliko yalifanyika katika asili yenyewe (uumbaji). Yakiwa yameharibiwa na laana ya dhambi, maumbile ya asili yanaweza kutoa ushuhuda usio mkamilifu kuhusu Muumba. Hayawezi kudhihirisha tabia Yake katika ukamilifu wake. {8T 256.1}

### Mwalimu wa Kiungu

Tunamhitaji Mwalimu wa Kiungu. Ili ulimwengu usibaki gizani, katika giza la milele la kiroho, Mungu alikutana nasi kupitia kwa Yesu Kristo. Kristo Ndiye "Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu." Yohana 1:9 "Nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu" inafunuliwa "katika uso wa Yesu Kristo" 2 Wakorintho 4:6. Nuru ya Kristo, inayoangazia ufahamu wetu, na kuangaza juu ya uso wa maumbile ya asili, hutuwezesha bado kusoma somo la upendo wa Mungu katika kazi Zake alizoziumba. {8T 256.2}

### Asili Humshuhudia Mungu

Mambo ya asili ambayo tunayatazama leo yanatupa dhana hafifu ya uzuri na utukufu wa Edeni. Hata hivyo bado mengi ambayo ni mazuri yamebakia. Asili inashuhudia kwamba Mmoja asiye na kikomo katika uweza, mkuu wa wema, rehema, na upendo, aliumba dunia na kuijaza kwa maisha na furaha. Hata katika hali yake mbaya, vitu vyote vinafunua kazi ya mikono ya Msanii Mkuu. Ingawa dhambi imeharibu sura na uzuri wa vitu vya asili, ingawa athari ya kazi ya mkuu wa uwezo wa anga inaweza kuonekana juu yake, lakini bado inazungumza juu ya Mungu. Katika waridi mwitu, michongoma, miiba, magugu, tunaweza kusoma sheria ya laana; lakini kutoka kwenye uzuri wa vitu vya asili, na kutoka kwenye urekebishaji wake wa ajabu katika kukidhi mahitaji yetu na furaha yetu, tunaweza kujifunza kwamba Mungu bado anatupenda, kwamba rehema Yake bado inadhihirishwa katika ulimwengu.

"Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu,
Na anga laitangaza kazi ya mikono Yake.
Mchana husemezana na mchana,
Usiku hutolea usiku maarifa.
Hakuna lugha wala maneno,
Sauti yao haisikilikani." Zaburi 19:1-3. {8T 256.3}

### Kushindwa kwa Mwanadamu Kuitafsiri Asili (nature)

Mbali na Kristo sisi bado hatuna uwezo wa kutafsiri kwa usahihi lugha ya asili. Somo gumu zaidi na la kufedhehesha ambalo mwanadamu anapaswa kujifunza ni uzembe wake mwenyewe katika kukosa ufanisi katika kutegemea hekima ya mwanadamu, na kushindwa kwa hakika kwa juhudi zake za kuisoma asili kwa usahihi. Peke yake hawezi kuifasiri asili bila kuiweka juu ya Mungu. Yeye yuko katika hali sawa na ile ya Waathene (Matendo 17 Wagiriki), ambao, katikati ya madhabahu zao zilizowekwa wakfu kwa ibada ya maumbile ya asili, walikuwa na kibao kimoja chenye maandiko yasema: "Kwa Mungu asiyejulikana." Hakika Mungu alikuwa hajulikani kwao. Yeye hajulikani kwa wote ambao, bila uongozi wa Mwalimu wa Kiungu, hujiingiza katika kuitafiti asili. Kwa hakika watafikia mahitimisho yasiyo sahihi. {8T 257.1}

Katika hekima yake ya kibinadamu ulimwengu haumjui Mungu. Watu hawa wa ulimwengu wenye hekima hukusanya maarifa yasiyo kamili juu Yake kutokana na kazi Zake alizoziumba; lakini maarifa haya, yako mbali sana na kuwapa mawazo yaliyotukuka juu ya Mungu, mbali sana na kuziinua akili na nafsi, na kumleta mtu kamili kupatana na mapenzi Yake, huelekea kuwafanya wanadamu kuwa waabudu sanamu. Katika upofu wao wanaiinua asili na sheria za asili juu ya Mungu wa hiyo asili. {8T 257.2}

Mungu ameruhusu gharika ya nuru kumwagika juu ya ulimwengu kupitia uvumbuzi wa sayansi na sanaa; lakini wakati wale watu wanaodai kuwa wanasayansi wanapotoa sababu juu ya mambo haya kwa mtazamo wa kibinadamu tu, bila shaka watafanya makosa. Akili za juu zaidi, ikiwa haziongozwi na Neno la Mungu, huchanganyikiwa katika majaribio yao ya kuchunguza uhusiano wa sayansi na mafunuo. Muumbaji na kazi Zake Yuko juu ya ufahamu wao; na kwa sababu haya hayawezi kuelezewa na sheria za asili, historia ya Biblia inaelezwa kuwa si ya kutegemewa. {8T 257.3}

Wale wanaotilia shaka uaminifu wa rekodi ya Maandiko Matakatifu wameiachia nanga yao na wameachwa wakitapatapa huku na kule wakipiga miamba ya kumkana Mungu. Wakati wanapojikuta hawana uwezo wa kumpima Muumbaji na kazi Zake kwa maarifa yao yasiyokamilika ya kisayansi (wanasayansi wa maarifa madogo), wanahoji na kutilia mashaka uwapo wa Mungu na wanaelekeza Uweza ule usio na kikomo kuwa unatokana na asili. {8T 258.1}

Katika sayansi ya Kweli hakuwezi kuwa na kitu chochote kinyume na Mafundisho ya Neno la Mungu, kwa maana yote mawili yana Mwandishi/Mwanzilishi mmoja. Uelewa sahihi wa vyote viwili utathibitisha kila wakati kuwa vinakubaliana. Ukweli, iwe katika maumbile ya asili au katika mafunuo, upo katika upatanifu kamili wenyewe kwa wenyewe katika udhihirisho wake wote. Lakini akili isiyotiwa nuru na Roho wa Mungu daima itakuwa gizani kwa habari ya uweza wake. Hii ndiyo sababu mawazo ya wanadamu kuhusu sayansi mara nyingi yanapingana na mafundisho ya

Neno la Mungu. {8T 258.2}

## Kazi ya Uumbaji

Kazi ya uumbaji haiwezi kamwe kuelezewa na sayansi. Ni sayansi gani inayoweza kuelezea fumbo la maisha kweli? {8T 258.3}

Nadharia ya kwamba Mungu hakuumba maada alipoiumba dunia haina msingi. Katika uundaji wa ulimwengu wetu, Mungu hakuwiwa kutumia vitu vilivyokuwepo hapo awali. Kinyume chake, vitu vyote, vya kimwili au vya kiroho, vilisimama mbele za Bwana Yehova kwa sauti Yake na viliumbwa kwa kusudi Lake Yeye Mwenyewe. Mbingu na jeshi lake lote, nchi na vitu vyote vilivyomo, si kazi ya mkono Wake tu; vilifanyika kwa pumzi ya kinywa Chake. {8T 258.4}

“Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri. Waebrania 11:3.

“Kwa Neno la Bwana mbingu zilifanyika,
Na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa Chake.
Hukusanya maji ya bahari chungu chungu,
Huviweka vilindi katika ghala.
Nchi yote na imwogope Bwana,
Wote wakaao duniani na wamche.
Maana Yeye alisema, ikawa;
Na Yeye aliamuru, ikasimama." Zaburi 33:6-9. {8T 259.2}

## Sheria za Asili

Katika kusimama juu ya sheria za maada na sheria za asili, wengi wanasahau, kama si kukataa, wakala wa kudumu na wa moja kwa moja wa Mungu. Wanatoa wazo kwamba asili hutenda bila kumtegemea Mungu, ikiwa na mipaka yake yenyewe na uwezo wake wenyewe wa kufanya kazi. Katika akili zao kuna tofauti dhahiri kati ya yale ya asili na yale yasiyo ya ulimwengu. Asili inahusishwa na sababu za kawaida, zisizounganishwa na uweza wa Mungu. Nguvu ya uhai inahusishwa na maada, na asili inafanywa kuwa muungu. Inadhaniwa kuwa maada huwekwa katika mahusiano fulani na kuachwa kutenda kutokana na sheria zilizowekwa ambazo Mungu Mwenyewe hawezi kuziingilia; kwamba asili imejaliwa kuwa na sifa fulani na kuwekwa chini ya sheria, na kisha inaachwa yenyewe kutii sheria hizi na kufanya kazi iliyoamriwa awali. {8T 259.2}

Hii ni sayansi ya uongo; hakuna kitu katika neno la Mungu cha kuitegemeza. Mungu habatilishi sheria Zake, lakini anatenda kazi kupitia hizo daima, akizitumia kama vyombo Vyake. Hazifanyi kazi peke yake. Mungu Yupo daima kazini katika asili. Yenyewe ni mtumishi Wake, inayoongozwa kama apendavyo. Asili katika kazi yake

inashuhudia uwapo wa akili na wakala hai wa nafsi inayotembea katika kazi Zake zote kulingana na mapenzi Yake. Si kwa uwezo wa asili uliomo ndani ya asili mwaka baada ya mwaka dunia hutoa neema zake na kuendelea na mwendo wake kulizunguka jua. Mkono wa uweza usio na kikomo unafanya kazi daima kuiongoza sayari hii. Ni uweza wa Mungu unaotumiwa kila muda mfupi ambao huiweka katika nafasi yake katika mzunguko wake. {8T 259.3}

Mungu wa mbinguni daima Yupo kazini. Ni kwa uweza Wake kwamba mimea inafanywa kusitawi, kwamba kila jani hutokea na kila ua huchanua. Kila tone la mvua au tone la theluji, kila unyasi, kila jani na ua na kichaka, humshuhudia Mungu. Vitu hivi vidogo vya kawaida vinavyotuzunguka hutufundisha somo kwamba hakuna kitu ambacho hakijulikani kwa Mungu asiye na kikomo, hakuna kitu ambacho ni kidogo sana kwa uangalizi Wake. {8T 260.1}

Utaratibu kufanya kazi wa mwili wa mwanadamu hauwezi kueleweka kikamilifu; unawasilisha siri ambazo huwashangaza wenye akili zaidi. Si kama matokeo ya mashine, ambayo, ikiisha kuwashwa, inaendelea kutenda kazi yake, kwamba mapigo ya moyo hudunda na pumzi hufuata pumzi. Katika Mungu tunaishi na tunatembea na kuwa na uhai wetu. Kila pumzi, kila pigo la moyo, ni uthibitisho endelevu wa uweza wa Mungu aliyepo kila wakati. {8T 260.2}

Ni Mungu Ndiye anayefanya jua litokeze katika mbingu. Yeye hufungua madirisha ya mbinguni na kutoa mvua. Huyafanya majani kukua juu ya milima. "Ndiye atoaye theluji kama sufu: Huimwaga barafu yake kama majivu," “Atoapo sauti Yake, pana mshindo wa maji mbinguni,……. Huifanyia mvua umeme, Huutoa upepo katika hazina zake." Zaburi 147:16; Yeremia 10:13. {8T 260.3}

Bwana daima Yupo kazini katika kushikilia na kutumia kama watumishi Wake vitu alivyovifanya. Kristo alisema: "Baba Yangu anatenda kazi hata sasa, Nami ninatenda kazi." Yohana 5:17. {8T 260.4}

### Siri za Uweza wa Mungu

Watu wenye akili za kubwa kabisa hawawezi kuelewa siri za Yehova kama zinavyodhihirishwa katika asili. Uvuvio wa Mwenyezi Mungu huuliza maswali mengi ambayo mwanazuoni wa kina zaidi hawezi kuyajibu. Maswali haya hayakuulizwa ili tupate kuyajibu, bali ili kuelekeza mawazo yetu kwenye siri za kina za Mungu na kutufundisha kwamba hekima yetu ina mipaka; kwamba katika mazingira ya maisha yetu ya kila siku kuna mambo mengi ambayo yapo juu ya ufahamu wa akili zenye kikomo; kwamba hukumu na makusudi ya Mungu hayawezi kupimwa. Hekima Yake haichunguziki. {8T 261.1}

Wakosoaji wenye mashaka wanakataa kumwamini Mungu kwa sababu kwa akili zao zenye kikomo hawawezi kufahamu uweza usio na kikomo ambao kwa huo Yeye

hujidhihirisha kwa wanadamu. Lakini Mungu anapaswa kutambuliwa zaidi kupitia kwa yale ambayo hayafichui kwa wanadamu kuhusu Yeye kuliko yale yaliyo wazi kwa ufahamu wetu wenye kikomo. Yote mawili, katika ufunuo wa kiungu na katika asili, Mungu amewapa wanadamu mafumbo ili kuongoza imani yao. Hili ni lazima liwe hivyo. Tunaweza kutafiti daima, tukiuliza maswali daima, tukijifunza daima, na bado mbele kuna mengi zaidi yaliyosheheni, yasiyo na kikomo.

"Ni nani aliyeyapima maji kwa konzi ya mkono Wake,
Na kuzikadiri mbingu kwa shubiri,
Na kuyashika mavumbi ya dunia katika pishi,
Na kuipima milima kwa uzani,
Na vilima kama kwa mizani?
Ni nani aliyemwongoza roho ya Bwana,
Na kumfundisha kwa kuwa mshauri Wake?  . . . .
Tazama, mataifa ni kama tone la maji katika ndoo,  Huhesabiwa kuwa kama mavumbi membamba katika mizani;
Tazama, Yeye huvinyanyua visiwa kama ni kitu kidogo sana.

Lebanoni nayo hautoshi kwa kuni,
Wala wanyama wake hawatoshi kwa kafara.
Mataifa yote huwa kama si kitu mbele Zake;
Huhesabiwa kwake kuwa duni ya si kitu,
Na ubatili.  Basi, mtamlinganisha Mungu na nani?
Au mtamfananisha na mfano wa namna gani? ……
Je! Hamkujua? Hamkusikia? Hamkuambiwa tokea mwanzo?
Hamkufahamu tangu kuwekwa misingi ya dunia?
Yeye Ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia,
Na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi;
Yeye Ndiye azitandazaye mbingu kama pazia na
Kuzikunjua kama hema ya kukaliwa …….
Mtanifananisha na nani, basi,  Nipate kuwa sawa Naye?
Asema Yeye Aliye Mtakatifu.
Inueni macho yenu juu, mkaone;
Ni nani aliyeziumba hizi;
Aletaye nje jeshi lao kwa hesabu;
Aziita zote kwa majina; kwa ukuu wa uweza Wake,
Na kwa kuwa Yeye ni hodari kwa nguvu Zake;
Hapana moja isiyokuwapo mahali pake.
Mbona unasema, Ee Yakobo,
Mbona unanena, Ee Israeli, Njia yangu imefichwa,
Bwana asiione, na hukumu yangu imempita Mungu wangu asiiangalie?

Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele,
Bwana, Muumba miisho ya dunia,
Hazimii, wala hachoki; akili Zake hazichunguziki.
Huwapa nguvu wazimiao,
Humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo.
Hata vijana watazimia na kuchoka,
Na wanaume vijana wataanguka;
Bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya;
Watapanda juu kwa mbawa kama tai;
Watapiga mbio, wala hawatachoka;
Watakwenda kwa miguu,
Wala hawatazimia." Isaya 40:12-31 {8T 261.2}

## SURA YA 43
## MUNGU MWENYE NAFSI

Uweza mkuu unaofanya kazi katika asili yote na kutegemeza vitu vyote siyo, kama wanadamu wengine wanasayansi wanavyouwasilisha, kuwa ni kanuni tu iliyoenea kote, na nishati inayochochea kazi. Mungu ni roho; Na bado Yeye ni Nafsi yenye mwili, kwa maana mwanadamu aliumbwa kwa mfano Wake. {8T 263.1}

### Asili si Mungu

Kazi ya mikono ya Mungu katika asili si Mungu Mwenyewe ndani ya asili. Vitu katika asili ni onesho la tabia ya Mungu; kupitia kwavyo tunaweza kuelewa upendo Wake, uweza Wake, na utukufu Wake; lakini hatupaswi kuichukulia asili kuwa ni Mungu. Ustadi wa kisanii wa wanadamu huzalisha kazi nzuri sana, vitu vinavyopendeza macho na vitu hivi hutupatia wazo la mbuni; lakini vitu vilivyotengenezwa si

mwanadamu mwenyewe. Si kazi, bali mtenda kazi ndiye anayehesabiwa kuwa anastahili heshima. Kwa hivyo, ingawa asili ni onesho la mawazo ya Mungu, si asili bali ni Mungu wa hiyo asili ambaye anapaswa kuinuliwa.

"Miungu hiyo isiyofanya mbingu na nchi, hiyo itaangamia katika nchi,
Nayo itatoweka chini ya mbingu."
"Fungu la Yakobo, siye kama hawa;
Maana Ndiye aliyeviumba vitu vyote."
"Yeye Ameiumba dunia kwa uweza Wake,
Ameuthibitisha ulimwengu kwa hekima Yake,
Na kwa ufahamu wake amezitandika mbingu." Yeremia 10:11, 16, 12

"Mtafuteni Yeye afanyaye Kilimia na Orioni,
Na kukigeuza kivuli cha mauti kuwa asubuhi,
Na kuufanya mchana kuwa giza kwa usiku;
Yeye ayaitaye maji ya bahari, na kuyamwaga juu ya uso wa nchi;
Bwana, ndilo Jina Lake" Amosi 5:8 {8T 263.2}

## Mungu Mwenye Nafsi Alimuumba Mwanadamu

Katika uumbaji wa mwanadamu ilidhihirishwa nguvu ya Mungu Mwenye nafsi. Mungu alipomfanya mtu kwa mfano Wake, umbo la mwanadamu lilikuwa kamilifu katika mipangilio yake yote, lakini halikuwa na uhai. Kisha Mungu Mwenye nafsi, aliyeko Mwenyewe (hakuumbwa) akapuliza ndani ya umbo hilo pumzi ya uhai, na mtu akawa nafsi hai, yenye kupumua na yenye akili. Sehemu zote za mwanadamu ziliwekwa katika utendaji. Moyo, ateri, vena, ulimi, mikono, miguu, hisi, utambuzi wa akili - vyote vilianza kazi yao, na vyote viliwekwa chini ya sheria. Mtu akawa nafsi hai. Kupitia kwa Yesu Kristo Mungu Mwenye nafsi alimuumba mwanadamu na kumpa akili na uwezo. {8T 264.1}

Mwili wetu haukufichika Kwake tulipoumbwa kwa siri. Macho Yake yaliuona mwili wetu, bado ukiwa si mkamilifu; na katika kitabu Chake viungo vyetu vyote viliandikwa, wakati hata kimojawapo hakijakuwapo bado. {8T 264.2}

Juu ya viumbe vyote vya daraja la chini, Mungu alipanga kwamba mwanadamu, kazi kuu na taji kabisa ya uumbaji Wake, angepaswa kuonesha na kuelezea mawazo Yake na kudhihirisha utukufu Wake. Lakini mwanadamu hatakiwi kujiinua yeye mwenyewe kuwa kama Mungu.

"Mfanyieni Bwana shangwe…
Mtumikieni Bwana kwa furaha;

Njoni mbele Zake kwa kuimba.

“Jueni kwamba Bwana Ndiye Mungu;  Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu Wake;
Tu watu Wake, na kondoo wa malisho Yake.

“Ingieni malangoni Mwake kwa kushukuru;
Nyuani Mwake kwa kusifu;
Mshukuruni, lihimidini Jina Lake.”

“Mtukuzeni Bwana, Mungu wetu;
Sujuduni mkiukabili mlima Wake mtakatifu;
Maana Bwana, Mungu wetu, Ndiye mtakatifu.”
Zaburi 100:1-4; 99:9. {8T 264.3}

## Mungu Amedhihirishwa Katika Kristo

Kama nafsi yenye mwili, Mungu amejifunua katika Mwanawe. Yesu, mng’ao wa utukufu wa Baba, "na chapa ya nafsi Yake." (Waebrania 1: 3), duniani alipatikana katika umbo kama mwanadamu. Kama Mwokozi binafsi, Yeye alikuja ulimwenguni. Kama Mwokozi binafsi, Yeye alipaa juu. Kama Mwokozi binafsi, Yeye anatuombea katika nyua za mbinguni. Mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, Yeye ni mhudumu kwa niaba yetu " Mtu mfano wa Mwanadamu." Ufunuo 1:13. {8T 265.1}

Kristo, Nuru ya ulimwengu, alifunika mng'ao wa Uungu Wake unaotia kiwi na akaja kuishi kama mwanadamu miongoni mwa wanadamu, ili waweze, bila kuangamizwa, kumfahamu Muumba wao. Hakuna mtu ambaye amemwona Mungu wakati wowote isipokuwa kama Yeye anavyodhihirishwa kupitia kwa Kristo. {8T 265.2}

“Mimi na Baba Yangu tu umoja,” Kristo alitangaza. "Hakuna amjuaye Mwana, ila Baba; wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana, na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia." Yohana 10:30; Mathayo 11:27. {8T 265.3}

Kristo alikuja kuwafundisha wanadamu kile ambacho Mungu anataka wajue. Katika mbingu juu, katika nchi, katika maji mapana ya bahari, tunaona kazi ya mikono ya Mungu. Vitu vyote vilivyoumbwa vinashuhudia kuhusu uwezo Wake, hekima Yake, na upendo Wake. Lakini si kutoka katika nyota au bahari au mtoto wa jicho tunaweza kujifunza juu ya nafsi ya Mungu kama inavyodhihirishwa katika Kristo. {8T 265.4}

Mungu aliona kwamba ufunuo ulio wazi zaidi kuliko asili ulihitajika ili kuionesha nafsi Yake na tabia Yake. Yeye Alimtuma Mwanawe ulimwenguni ili kufunua, kwa kadiri inavyoweza kuvumiliwa na macho ya wanadamu, asili na sifa za Mungu asiyeonekana. {8T 265.5}

Kama Mungu angetaka awakilishwe kama yule anayekaa mwenyewe katika vitu vya asili, - katika ua, mti, nyasi, - Je, Kristo hangezungumza juu ya hili kwa wanafunzi Wake alipokuwa duniani? Lakini katika mafundisho ya Kristo Mungu hasemwi hivyo kamwe. Kristo na mitume walifundisha waziwazi Ukweli wa kuwapo kwa Mungu Mwenye Nafsi. {8T 265.6}

Kristo alifunua yote juu ya Mungu ambayo wanadamu wenye dhambi wangeweza kustahimili bila kuangamizwa. Yeye Ndiye Mwalimu wa Kiungu, Mwelimishaji, Mfunuaji. Kama Mungu angefikiri kwamba tunahitaji mafunuo mengine zaidi ya yale yaliyofanywa kupitia kwa Kristo na katika neno Lake lililoandikwa, angeyatoa. {8T 266.1}

### Ufunuo wa Kristo wa Mungu kwa Wanafunzi

Hebu na tujifunze Maneno ambayo Kristo aliyasema katika chumba cha juu katika usiku kabla ya kusulubiwa Kwake. Alikuwa anakaribia saa Yake ya kujaribiwa, na alitaka kuwafariji wanafunzi Wake, ambao wangejaribiwa na kupimwa vikali. {8T 266.2}

Yesu aliwaambia, "Msifadhaike mioyoni mwenu. Mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali…. {8T 266.3}

“Tomaso akamwambia, Bwana, sisi hatujui uendako; nasi twaijuaje njia? Yesu akamwambia, Mimi Ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi. Kama mngalinijua Mimi, mngalimjua na Baba; tangu sasa mnamjua, tena mmemwona.” {8T 266.4}

“Bwana, utuonyeshe Baba,” Filipo alisema, “Na itatutosha. Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona Mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? Husadiki ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, na Baba Yu ndani yangu? Hayo Maneno niwaambiayo Mimi siyasemi kwa shauri Langu; lakini Baba akaaye ndani Yangu huzifanya kazi Zake." Yohana 14:1-10. {8T 266.5}

Wanafunzi walikuwa bado hawajaelewa Maneno ya Kristo kuhusu uhusiano Wake na Mungu. Mengi ya mafundisho Yake bado yalikuwa giza kwao. Waliuliza maswali mengi ambayo yalidhihirisha kutokujua kwao uhusiano wa Mungu na wao na kuhusu masilahi yao ya sasa na ya wakati ujao. Kristo alitaka wawe na ujuzi ulio wazi zaidi, ulio dhahiri zaidi wa Mungu. {8T 266.6}

“Hayo nimesema nanyi kwa mithali,” Alisema; "saa yaja ambapo sitasema nanyi tena kwa mithali, lakini nitawapa waziwazi habari ya Baba." Yohana 16:25. {8T 267.1}

Siku ya Pentekoste Roho Mtakatifu alipomiminwa juu ya wanafunzi, walielewa kweli ambazo Kristo alikuwa amezisema kwa mifano. Mafundisho ambayo yalikuwa mafumbo na siri kwao yaliwekwa wazi. Uelewa uliowajia kwa kumwagwa kwa Roho uliwafanya waaibishwe na nadharia zao za kufikirika. Dhana na tafsiri zao zilikuwa ni upumbavu zikilinganishwa na maarifa ya mambo ya mbinguni ambayo sasa waliyapokea. Waliongozwa na Roho, na nuru ikaangaza katika ufahamu wao ambao hapo awali ulikuwa umetiwa giza. {8T 267.2}

Lakini wanafunzi walikuwa bado hawajapokea utimilizaji kabisa wa ahadi ya Kristo. Walipokea maarifa yote ya Mungu ambayo wangeweza kustahimili, lakini utimilizaji kabisa wa ahadi ambayo Kristo angewaonesha waziwazi juu ya Baba ulikuwa bado unakuja. Hivyo ndivyo ilivyo leo. Maarifa yetu juu ya Mungu ni ya sehemu tu na si makamilifu. Pambano litakapokwisha na Mwanadamu Kristo Yesu akawakiri mbele za Baba watendakazi Wake waaminifu, ambao, katika ulimwengu wa dhambi, wametoa ushuhuda wa Kweli kwa ajili Yake, watayafahamu waziwazi yale ambayo sasa ni siri kwao. {8T 267.3}

Kristo alichukua pamoja Naye hadi kwenye nyua za mbinguni ubinadamu Wake uliotukuzwa. Kwa wale wanaompokea, anawapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ili hatimaye Mungu awapokee kama Wake, wapate kuishi pamoja Naye milele zote. Ikiwa, katika maisha haya, wao ni waaminifu kwa Mungu, hatimaye "watamwona uso Wake; na Jina Lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao." Ufunuo 22:4. Nayo furaha ya mbinguni ni nini isipokuwa kumwona Mungu? Ni furaha gani kubwa zaidi ingeweza kuja kwa mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema ya Kristo kuliko kuutazama uso wa Mungu na kumjua kama Baba? {8T 267.4}

## Ushuhuda wa Maandiko

Maandiko yanaonesha waziwazi uhusiano kati ya Mungu na Kristo, nayo yanadhihirisha waziwazi nafsi na hali ya pekee ya Kila Mmoja Wao. {8T 268.1}

"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa Yeye aliufanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu Wake na chapa ya nafsi Yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza Wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; amefanyika bora kupita malaika, kwa kadiri jina aliloliirithi lilivyo tukufu kuliko lao. Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wo wote, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena, Mimi nitakuwa Kwake Baba, Na Yeye atakuwa Kwangu Mwana? ” Waebrania 1:1-5. {8T 268.2}

Mungu ni Baba wa Kristo; Kristo ni Mwana wa Mungu. Kristo amepewa nafasi iliyotukuka. Amefanywa kuwa sawa na Baba. Mashauri yote ya Mungu yamefunguliwa kwa Mwanawe. {8T 268.3}

Yesu aliwaambia Wayahudi: “Baba Yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi……… Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo Yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile. Kwa kuwa Baba ampenda Mwana, Naye humwonyesha yote ayatendayo Mwenyewe.” Yohana 5:17-20. {8T 268.4}

Hapa tena inaoneshwa nafsi ya Baba na Mwana, ikionesha umoja uliopo kati Yao. {8T 269.1}

Umoja huu unaoneshwa pia katika sura ya kumi na saba ya Yohana, katika sala ya Kristo kwa ajili ya wanafunzi Wake: {8T 269.2}

“Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami ndani Yako; hao nao wawe ndani Yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba Wewe Ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama Sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, Nawe ndani Yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa Ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda Mimi." {8T 269.3}

Kauli ya ajabu! Umoja uliopo kati ya Kristo na wanafunzi Wake hauharibu nafsi ya kila Mmoja. Wao ni Wamoja katika kusudi, akili, katika tabia, lakini si katika nafsi. Hivyo ndivyo Mungu na Kristo walivyo mmoja. {8T 269.4}

Uhusiano kati ya Baba na Mwana, na nafsi za wote wawili, unawekwa wazi katika andiko hili: “Bwana wa majeshi asema hivi, ya kwamba, Tazama, Mtu huyu Ndiye ambaye Jina Lake ni Chipukizi;

Naye atakua katika mahali Pake,
Naye atalijenga hekalu la Bwana…
Naye atauchukua huo utukufu;
Ataketi akimiliki katika kiti Chake cha enzi;
Na kutakuwa na kuhani katika kiti Chake cha enzi;
Na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili." Zekaria 6:12, 13. {8T 269.5}

## "Mungu wa Milele"

Katika Neno, Mungu ananenwa kama "Mungu wa milele." Jina hili linajumuisha zama za kipindi cha nyuma, cha sasa na cha baadaye. Mungu ni wa milele hata milele. Yeye Ndiye wa Milele.

“Mungu wa milele Ndiye makazi yako, Na mikono ya milele i chini yako. Na mbele yako amemsukumia mbali adui;
Akasema, Angamiza.
Na Israeli anakaa salama,
Chemchemi ya Yakobo peke yake,

Katika nchi ya ngano na divai;
Naam, mbingu zake zadondoza umande.
U heri, Israeli. Ni nani aliye kama wewe,
Taifa lililookolewa na Bwana!
Ndiye ngao ya msaada wako,
Na upanga wa utukufu wako;
Na adui zako watajitiisha chini yako,
Nawe utapakanyaga mahali pao pa juu.”
Kumbukumbu la Torati 33:27-29,

"Kabla haijazaliwa milima, wala hujaiumba dunia,
Na tangu milele hata milele Ndiwe Mungu.
Wamrudisha mtu mavumbini,
Usemapo, Rudini, enyi wanadamu.
Maana miaka elfu machoni Pako Ni kama siku ya jana ikiisha kupita,
Na kama kesha la usiku.
Wawagharikisha, huwa kama usingizi,
Asubuhi huwa kama majani yameayo.
Asubuhi yachipuka na kumea,
Jioni yakatika na kukauka." Zaburi 90: 2-6

"Basi, utujulishe kuzihesabu siku zetu, Tujipatie moyo wa hekima."
"Utushibishe asubuhi kwa fadhili Zako,
Nasi tutashangilia na kufurahi siku zetu zote.
Utufurahishe kwa kadiri ya siku ulizotutesa,
Kama miaka ile tuliyoona mabaya.
Matendo Yako na yaonekane kwa watumishi wako,
Na adhama Yako kwa watoto wao.
Na uzuri wa Bwana, Mungu wetu,
Uwe juu yetu, Na kazi ya mikono yetu utufanyie thabiti,
Naam, kazi ya mikono yetu uithibitishe."
Zaburi 90:12, 14-17.
“Bwana ametamalaki,
Amejivika adhama, Bwana amejivika,
Na kujikaza nguvu. Naam,
Ulimwengu umethibitika usitikisike;
Kiti Chako kimekuwa thabiti tokea zamani;
Wewe Ndiwe uliye tangu milele. "
Zaburi 93: 1, 2.

**Fadhili Zake za Upendo**

"Kwa kuwa Neno la Bwana lina adili,
Na kazi Yake yote huitenda kwa uaminifu.
Huzipenda haki na hukumu,
Nchi imejaa fadhili za Bwana."
"Heri taifa ambalo Bwana ni Mungu wao, Watu aliowachagua kuwa urithi Wake."
Tazama, jicho la Bwana li kwao wamchao, Wazingojeao fadhili Zake. Yeye huwaponya nafsi zao na mauti,
Na kuwahuisha wakati wa njaa.
Nafsi zetu zinamngoja Bwana;
Yeye Ndiye msaada wetu na ngao yetu.
Maana mioyo yetu itamfurahia Yeye,
Kwa kuwa tumelitumainia Jina Lake takatifu.
Zaburi 33: 4, 5, 12, 18-21 "Nalimtafuta
Bwana akanijibu,
Akaniponya na hofu zangu zote.
Wakamwelekea macho wakatiwa nuru, Wala nyuso zao hazitaona haya. Maskini huyu aliita, Bwana akasikia, Akamwokoa na taabu zake zote.
Malaika wa Bwana hufanya kituo,
Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa. Onjeni mwone ya kuwa Bwana Yu mwema; Heri mtu yule anayemtumaini.
Mcheni Bwana, enyi watakatifu Wake, Yaani,
Wamchao hawahitaji kitu.
Wana-simba hutindikiwa, huona njaa;
Bali wamtafutao Bwana hawatahitaji kitu chochote kilicho chema.
"Walilia, Naye Bwana akasikia, Akawaponya na taabu zao zote.
Bwana Yu karibu nao waliovunjika moyo, Na waliopondeka roho huwaokoa. " Zaburi 34: 4-10, 17, 18
"Bwana huzikomboa nafsi za watumishi Wake; Aya ya 22.
“Bwana amejaa huruma na neema,
Haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili.
Yeye hatateta sikuzote, Wala hatashika hasira Yake milele.
Hakututenda sawasawa na hatia zetu, Wala hakutulipa kwa kadiri ya maovu yetu.
Maana mbingu zilivyoinuka juu ya nchi,
Kadiri ile ile rehema Zake ni kuu kwa wamchao.
Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi. Kama vile baba awahurumiavyo watoto Wake,
Ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao.
Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, Na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi.
Mwanadamu siku zake zi kama majani; Kama ua la kondeni ndivyo asitawivyo.

Maana upepo hupita juu yake, kumbe haliko! Na mahali pake hapatalijua tena.
Bali fadhili za Bwana zina wamchao Tangu milele hata milele,
Na haki Yake ina wana wa wana;
Maana, wale walishikao agano Lake, Na kuyakumbuka maagizo Yake ili wayafanye. Zaburi 103: 8-18 {8T 270.1}

## Utunzaji Wake Wenye Kujali

Mungu wetu anazo mbingu na dunia chini ya amri Yake, na anajua tu kile tunachokihitaji. Sisi tunaweza kuona kidogo tu kilicho mbele yetu; "Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni Pake Yeye aliye na mambo yetu." Waebrania 4:13.

Juu ya mahangaiko ya dunia Yeye ameketi katika kiti cha enzi; vitu vyote viko wazi katika uangalizi Wake wa Kiungu; na kutokea umilele Wake mkuu na mtulivu, Yeye Anaagiza yale ambayo majaliwa Yake yanaona kuwa ni bora. {8T 272.1}

Hakuna hata shomoro anayeanguka chini bila Baba kujua. Chuki ya Shetani dhidi ya Mungu inampelekea kufurahi kuwaaharibu hata viumbe bubu (wasio na akili nyingi). Ni kwa njia tu ya ulinzi wa Mungu ndipo ndege huhifadhiwa ili kutufurahisha na nyimbo zao za furaha. Lakini Yeye hasahau hata shomoro. "Msiogope basi; bora ninyi kuliko mashomoro wengi." Mathayo 10:31.
"Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana.
Wewe, Bwana, Mungu wangu,
Umejifanya mkuu sana;
Umejivika heshima na adhama.
Umejivika nuru kama vazi;
Umezitandika mbingu kama pazia;
Na kuziweka nguzo za orofa zake majini.
Huyafanya mawingu kuwa gari Lake,
Na kwenda juu ya mabawa ya upepo,
Huwafanya malaika Zake kuwa pepo,
Na watumishi Wake kuwa moto wa miali.
Uliiweka nchi juu ya misingi yake, Isitikisike milele.
Uliifunika kwa vilindi kama kwa vazi,
Maji yalikuwa yakisimama juu ya milima.
Kwa kukemea kwako yakakimbia,
Kwa sauti ya radi Yako yakaenda zake kasi, Yakapanda milima, yakatelemka mabondeni,
Mpaka mahali ulipoyatengenezea.
Umeweka mpaka yasiupite,

Wala yasirudi kuifunikiza nchi.
Hupeleka chemchemi katika mabonde;
Zapita kati ya milima; Zamnywesha kila mnyama wa kondeni; Punda mwitu huzima kiu yao. Kandokando hukaa ndege wa angani; Kati ya matawi hutoa sauti zao. Huinywesha milima toka orofa zake; Nchi imeshiba mazao ya kazi zako.
Huyameesha majani kwa makundi,
Na maboga kwa matumizi ya mwanadamu;
Ili atoe chakula katika nchi,
Na divai imfurahishe mtu moyo wake.
Aung'aze uso wake kwa mafuta,
Na mkate umburudishe mtu moyo wake.
Miti ya Bwana nayo imeshiba,
Mierezi ya Lebanoni aliyoipanda.
Ndimo ndege wafanyamo vitundu vyao, Na korongo, misunobari ni nyumba yake. Milima mirefu ndiko waliko mbuzi wa mwitu, Na magenge ni kimbilio la wibari. Aliufanya mwezi kwa ajili ya nyakati, Jua latambua kuchwa kwake.
Wewe hufanya giza, kukawa usiku,
Ndipo atambaapo kila mnyama wa mwitu. Wana-simba hunguruma wakitaka mawindo,
Ili kutafuta chakula chao kwa Mungu.
Jua lachomoza, wanakwenda zao, Na kujilaza mapangoni mwao. Mwanadamu atoka kwenda zake
kazini, Na kwenye utumishi wake
mpaka jioni.
Ee Bwana, jinsi yalivyo mengi matendo Yako!
Kwa hekima umevifanya vyote pia.
Dunia imejaa mali zako.
Bahari iko kule, kubwa na upana,
Ndimo mlimo viendavyo visivyohesabika,
Viumbe hai vidogo kwa vikubwa.
Ndimo zipitamo merikebu,
Ndimo alimo lewiathani uliyemwumba acheze humo.
Hao wote wanakungoja Wewe,
Uwape chakula chao kwa wakati wake.
Wewe huwapa, Wao wanakiokota;
Wewe waukunjua mkono wako,
Wao wanashiba mema;
Wewe waficha uso wako, Wao wanafadhaika;
Waiondoa pumzi yao, wanakufa, Na kuyarudia mavumbi yao, Waipeleka roho yako, wanaumbwa, Nawe waufanya upya uso wa nchi. Utukufu wa Bwana na udumu milele; Bwana na ayafurahie matendo Yake. Aitazama nchi, inatetemeka; Aigusa

milima, Inatoka moshi.
Nitamwimbia Bwana maadamu ninaishi;
Nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai;
Kutafakari kwangu na kuwe kutamu Kwake;
Mimi nitamfurahia Bwana." Zaburi 104:1-34

"Kwa mambo ya kutisha utatujibu, Katika haki, Ee Mungu wa wokovu wetu.
Wewe uliye tumaini la miisho yote ya dunia, Na la bahari iliyo mbali sana, Milima waiweka imara kwa nguvu zako, Huku ukijifunga uweza kama mshipi.
Wautuliza uvumi wa bahari. . . .
Na ghasia ya mataifa. . . .
Milango ya asubuhi na jioni waifurahisha. . . .
Umeuvika mwaka taji ya wema wako;
Mapito yako yadondoza unono." Zaburi 65:5-11

"Bwana huwategemeza wote waangukao, Huwainua
wote walioinama chini.
Macho ya watu wote yakuelekea Wewe,
Nawe huwapa chakula chao wakati wake.
Waufumbua mkono Wako,
Wakishibisha kila kilicho hai matakwa yake." Zaburi 145:14-16 {8T 273.1}

### Rehema Yake Ya Uvumilivu

Hakuna mzazi wa kidunia aliyewahi kumsihi kwa bidii mtoto anayekosea kama Yeye ambaye alituumba anavyomsihi mkosaji. Hakuna, shauku ya upendo wa mwanadamu iliyowahi kumfuata mwenye moyo usiotubu kwa mialiko ya upole kiasi hicho:

"Lakini hukuniita, Ee Yakobo,
Bali umechoka Nami, Ee Israeli." Isaya 43:22.

“Enyi watu Wangu, nimewatenda nini?
Nami nimewachosha kwa habari gani? Shuhudieni juu Yangu. Mika 6:3.

"Israeli alipokuwa mtoto, nalikuwa nikimpenda,
Nikamwita Mwanangu atoke Misri." Hosea 11:1.

“Maana, sehemu ya Bwana ni watu Wake,
Yakobo ni kura ya urithi Wake.
Yeye Alimkuta katika nchi ya ukame,
Na katika jangwa tupu litishalo;
Alimzunguka, akamtunza;
Akamhifadhi kama mboni ya jicho;
Mfano wa tai ataharikishaye kioto chake;

Na kupapatika juu ya makinda yake,
Alikunjua mbawa zake, akawatwaa,
Akawachukua juu ya mbawa zake." Kumbukumbu la Torati 32:9-11

"Hawakulishika agano la Mungu;
Wakakataa kuenenda katika sheria Yake." Zaburi 78:10.

"Kadiri walivyowaita
Ndivyo walivyoondoka na kuwaacha. . . .
Lakini nalimfundisha Efraimu kwenda kwa miguu;
Naliwachukua mikononi Mwangu;
Hawakujua ya kuwa naliwaponya. Naliwavuta kwa kamba za kibinadamu, Kwa mafungo ya upendo. . . .
Na watu Wangu wamejipinda kuniacha;
Ingawa wawaita kwenda Kwake Aliye juu,
Hapana hata mmoja atakayemtukuza. Hosea 11:2-7

"Lakini Yeye, kwa kuwa anayo rehema, Husamehe uovu wala haangamizi.
Mara nyingi huipishia mbali ghadhabu Yake,
Wala haiwashi hasira Yake yote.
Akakumbuka ya kuwa wao ni kiwiliwili,
Upepo upitao wala haurudi." Zaburi 78:38, 39. {8T 275.1}

Ingawa "Akaziacha nguvu zake kutekwa, Na fahari yake mkononi mwa mtesi.," lakini alisema, "fadhili Zangu sitamwondolea yeye, Wala sitafanya uaminifu Wangu kuwa uongo." Zaburi 78:61; 89:33. {8T 276.1}

"Je! Efraimu siye Mwanangu mpendwa? Je! Siye mtoto apendezaye? Maana kila nisemapo Neno juu Yake, ningali nikimkumbuka sana; kwa sababu hiyo moyo Wangu unataabika kwa ajili yake; bila shaka nitamrehemu, asema Bwana." Yeremia 31:20

"Niwezeje kukuacha, Efraimu?
Niwezeje kukuponya, Israeli?
Niwezeje kukufanya kama Adma? Niwezeje kukuweka kama Seboimu? Moyo wangu umegeuka ndani Yangu,
Huruma Zangu zimewaka pamoja.
Sitatumia ukali wa hasira Yangu,
Sitarudi kumwangamiza Efraimu;
Kwa maana Mimi ni Mungu,
Si mwanadamu Mimi;
Mimi Ndiye aliye Mtakatifu katikati yenu;
Wala sitaingia ndani ya mji na hasira." Hosea 11:8, 9

"Ee Israeli, mrudie Bwana, Mungu wako;
Maana umeanguka kwa sababu ya uovu wako.
Chukueni maneno pamoja nanyi,
Mkamrudie Bwana; mkamwambie,
Ondoa maovu yote, uyatakabali yaliyo mema. . . .
Ashuru hatatuokoa; hatutapanda farasi;
Wala hatutaiambia tena kazi ya mikono yetu,
Ninyi ndinyi miungu yetu;
Maana Kwako Wewe wasio na baba hupata rehema." Hosea 14:1-3

"Watakwenda kumfuata Bwana. . . .
Nao watoto watakuja kutoka magharibi wakitetemeka.
Watakuja wakitetemeka kama shomoro,
Toka Misri, na kama hua,
Toka nchi ya Ashuru;
Nami nitawakalisha katika nyumba zao,
Asema Bwana. Hosea 11:10, 11

"Mimi nitawaponya kurudi nyuma kwao;
Nitawapenda kwa ukunjufu wa moyo;
Kwa maana hasira Yangu imemwacha.
Nitakuwa kama umande kwa Israeli;
Naye atachanua maua kama nyinyoro,
Na kuieneza mizizi yake kama Lebanoni.
Matawi yake yatatandaa,
Na uzuri wake utakuwa kama uzuri wa mzeituni,  Na harufu yake kama Lebanoni.
Na wao wakaao chini ya uvuli Wake watarejea;
Watafufuka kama ngano,
Na kuchanua maua kama mzabibu. . . .
Efraimu atasema, Mimi nina nini tena na sanamu?
Mimi nimeitika, Nami nitamwangalia.
Mimi ni kama mberoshi wenye majani mabichi.
Kwangu mimi yamepatikana matunda yako.
Ni nani aliye na hekima,
Naye atayafahamu mambo haya?
Ni nani aliye na busara, naye atayajua?
Kwa maana njia za Bwana zimenyoka,
Nao wenye haki watakwenda katika njia hizo;
Bali waasio wataanguka ndani Yake.  Hosea 14:4-9

"Ni nani aliye Mungu kama Wewe,
Mwenye kusamehe uovu,
Na kuliachilia kosa la watu wa urithi wake waliosalia?

Yeye Hashiki hasira Yake milele,
Kwa maana Yeye hufurahia rehema.
Yeye Atarejea na kutuhurumia;
Atayakanyaga maovu yetu;
Nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari." Mika 7:18, 19. {8T 276.2}

"Bwana alinitokea zamani, akisema, Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili Zangu." "Kwa maana Bwana amemweka huru Yakobo, amemkomboa mkononi mwake aliyekuwa hodari kuliko yeye."
"Ndipo bikira atafurahi katika kucheza, na vijana na wazee pamoja; maana nitageuza masikitiko yao kuwa furaha, Nami nitawafariji, na kuwafurahisha waache huzuni zao."
"Na watu Wangu watashiba kwa wema Wangu, asema Bwana." Yeremia 31:3, 11, 13, 14.

"Imba, Ee binti Sayuni; piga kelele,
Ee Israeli; Furahi na kushangilia kwa moyo wako wote,
Ee binti Yerusalemu. Bwana ameziondoa hukumu zako,
Yeye Amemtupa nje adui yako; Mfalme wa Israeli, naam,
Yeye Bwana, Yu katikati yako; Hutaogopa uovu tena.
Katika siku ile Yerusalemu utaambiwa,
Usiogope, Ee Sayuni; mikono yako isilegee.
Bwana, Mungu wako, Yu katikati yako Shujaa awezaye kuokoa;
Yeye Atakushangilia kwa furaha kuu,
Yeye Atakutuliza katika upendo Wake,
Yeye Atakufurahia kwa kuimba." Sefania 3:14-17

"Kwa maana Ndivyo alivyo MUNGU, Mungu wetu. Milele na milele Yeye Ndiye atakayetuongoza." Zaburi 48:14. {8T 278.1}

## SURA YA 44
## MAARIFA YA UONGO NA YA KWELI KUHUSU MUNGU

### Nadharia za Kukisia

(Nadharia za Kufikirika au kusadikika ambazo ni za uongo; dhana zisizo na ushahidi thabiti)

"Mambo ya siri ni ya Bwana, Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele, ili tuyafanye Maneno yote ya sheria hii." Kumbukumbu la Torati 29:29. Ufunuo Wake Mwenyewe ambao Mungu ametoa katika Neno Lake ni kwa ajili yetu kuusoma/kujifunza. Huu tunaweza kuutafuta ili tuweze kuelewa. Lakini zaidi ya huu hatupaswi kupenya. Akili ya hali ya juu inaweza kujishughulisha mpaka ikachoka kwa kubahatisha kuhusu asili ya Mungu; lakini juhudi hazitakuwa na matunda. Tatizo hili halijawekwa kwetu kulitafutia ufumbuzi. Hakuna akili ya mwanadamu inayoweza kumfahamu Mungu kwa kina. Hebu na asijaribu mwadamu yeyote mwenye kikomo kumtafsiri Yeye. Yeyote asijiingize katika kukisia/kudhania kuhusu asili Yake. Hapa ukimya ni sawa na kunena kwa ufasaha. Yeye Mwenye maarifa yote hajadiliki-Yeye Yu Juu ya majadiliano. {8T 279.1}

Hata malaika hawakuruhusiwa kushiriki mashauri kati ya Baba na Mwana wakati mpango wa wokovu ulipowekwa. Wale wanadamu ambao wanatafuta kujipenyeza ndani ya siri za Aliye Juu wanaonesha ujinga wao wa mambo ya kiroho na ya umilele. Ingekuwa ni vyema sana kwao, wakati sauti ya rehema bado inasikika, wangenyenyekea hadi kwenye mavumbi na kumsihi Mungu awafundishe njia Zake. {8T 279.2}

Sisi hatujui kuhusu Mungu kama watoto wadogo, lakini kama watoto wadogo tunaweza kumpenda na kumtii. Badala ya kukisia juu ya asili Yake au haki yake ya kipekee ya kifalme, hebu tuzingatie Neno alilosema: " Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu." Zaburi 46:10.

“Je! Wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu?
Je, waweza kuufikilia upeo wa huyo Mwenyezi? Ni juu mno kama mbingu; waweza kufanya nini wewe? Ni wenye kina kuliko kuzimuni; waweza kujua nini wewe?
Cheo Chake ni kirefu kuliko dunia,
Ni kipana zaidi ya bahari. Ayubu 11:7-9.

"Bali hekima itapatikana wapi?
Na mahali pa ufahamu ni wapi?
Mwanadamu hajui thamani yake,
Wala haionekani katika nchi ya walio hai.
Vilindi vyasema, Haimo ndani yangu;
Na bahari yasema, Haiko kwangu.
Haipatikani kwa dhahabu,
Wala fedha haitapimwa iwe thamani yake.
Haiwezi kutiwa thamani kwa dhahabu ya Ofiri,
Wala kwa shohamu ya thamani nyingi,

Wala kwa yakuti ya samawi.
Dhahabu na vioo haviwezi kulinganishwa nayo;
Wala kubadili kwake hakutakuwa kwa vyombo vya dhahabu safi.
Havitatajwa fedhaluka wala bilauri;
Naam, kima cha hekima chapita marijani.
Yakuti ya rangi ya manjano ya Kushi haitasawazishwa nayo,
Wala haitatiwa kima kwa dhahabu safi.
Basi hekima yatoka wapi?
Na mahali pa ufahamu ni wapi? . . . .
Uharibifu na Mauti husema,
Tumesikia habari zake kwa masikio yetu.
Mungu Ndiye aijuaye njia yake,
Naye anajua mahali pake.

“Maana anatazama hata miisho ya nchi,
Na kuona chini ya mbingu nzima…… Hapo alipoiwekea mvua amri, Na njia kwa umeme wa radi.
Ndipo alipoiona na kuitangaza;
Aliithibitisha, naam, na kuichunguza.
Kisha akamwambia mwanadamu,
Tazama, kumcha Bwana ndiyo hekima,
Na kujitenga na uovu ndio ufahamu." Ayubu 28:12-28. {8T 279.3}

Si kwa kuchunguza vitu vilivyofichika katika dunia au kwa juhudi za bure za kutaka kupenya kwenye mafumbo na siri za nafsi ya Mungu hekima hupatikana. Inapatikana, badala yake, kwa kupokea kwa unyenyekevu ufunuo ambao Yeye amekuwa radhi kuutoa, na kwa kuyafanya maisha yakubaliane na mapenzi Yake. {8T 280.1}

### Ukuu wa Mungu Wetu

Kutoka kwenye taswira zilizotolewa na Roho Mtakatifu kwa manabii Wake, hebu tujifunze ukuu wa Mungu wetu. Nabii Isaya anaandika: {8T 281.1}

"Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi Lake zikalijaza hekalu. Juu Yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka. Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu Wake. Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti Yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi. {8T 281.2}

“Ndipo niliposema, Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa Majeshi. {8T 281.3}

"Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu; akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa." Isaya 6:1-7

"Hapana hata mmoja aliye kama Wewe, Ee Bwana; Wewe Ndiwe uliye Mkuu,
na Jina Lako ni Kuu katika uweza. Ni nani asiyekucha Wewe, Ee mfalme wa mataifa?" Yeremia 10:6, 7,

"Ee Bwana, umenichunguza na kunijua.
Wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu; Umelifahamu wazo langu tokea mbali. Umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu,
Umeelewa na njia zangu zote.
Maana hamna neno ulimini mwangu Usilolijua kabisa, Bwana.
Umenizingira nyuma na mbele, Ukaniwekea mkono Wako.
Maarifa hayo ni ya ajabu, yanishinda mimi,
Hayadirikiki, siwezi kuyafikia." Zaburi 139:1-6

"Bwana wetu ni Mkuu na mwingi wa nguvu,
Akili Zake hazina mpaka." Zaburi 147:5 {8T 281.4}

"Yeye hufunua mambo ya fumbo na ya siri; huyajua yaliyo gizani, na nuru hukaa Kwake." Danieli 2:22. {8T 282.1}

“Asema Bwana, ajulishaye hayo tangu milele.” “Maana ni nani aliyeijua nia ya Bwana? Au ni nani aliyekuwa mshauri Wake? Au ni nani aliyempa Yeye kitu kwanza, naye atalipwa tena? Kwa kuwa vitu vyote vyatoka Kwake, viko kwa uweza Wake, tena vinarejea Kwake. Utukufu una Yeye milele.” Matendo 15:18; Warumi 11:34-36. {8T 282.2}

"Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana," "ambaye Yeye peke Yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una Yeye hata milele." 1 Timotheo 1:17; 6:16

"Yeye hutandaza kaskazi juu ya nafasi isiyo na kitu, Na kuutundika ulimwengu pasipo kitu. Huyafunga maji ndani ya mawingu yake mazito; Na hilo
wingu halipasuki chini yake…….
Amepiga duara kuwa ni mpaka juu ya uso wa maji,

Hata hapo mwanga na giza vinapopakana. Ayubu 26:7-10.

“Nguzo za mbingu zatetemeka,
Na kustaajabu kwa kukemea Kwake.
Huichafua bahari kwa uwezo Wake. . . .
Hizo mbingu hupambwa kwa roho Yake;
Mkono Wake umemchoma nyoka aendaye mbio.
Tazama, hivi ni viunga tu vya njia Zake;
Na jinsi yalivyo madogo manong'ono tusikiayo katika habari Zake!
Lakini ngurumo za uweza Wake ni nani awezaye kuelewa nazo? Ayubu 26:11-14

"Bwana ana njia Yake katika kisulisuli na tufani,
na mawingu ni mavumbi ya miguu Yake." Nahumu 1:3
"Ni nani aliye mfano wa Bwana,
Mungu wetu aketiye juu;
Anyenyekeaye kutazama,
Mbinguni na duniani?" Zaburi 113:5, 6

“Bwana Ndiye Mkuu Mwenye kusifiwa sana, Wala ukuu Wake hautambulikani. Kizazi kwa kizazi kitayasifu matendo Yako,
Kitayatangaza matendo Yako makuu. Nitaifikiri fahari ya utukufu wa adhama Yako, Na matendo Yako yote ya ajabu. Watu watayataja matendo Yako ya kutisha,
Nami nitausimulia ukuu Wako.
Watalihubiri kumbukumbu la wema Wako mkuu.
Wataiimba haki Yako……

“Ee Bwana, kazi Zako zote zitakushukuru,
Na wacha Mungu Wako watakuhimidi.
Wataunena utukufu wa ufalme Wako, Na kuusimulia uweza Wako.
Ili kuwajulisha watu matendo Yake makuu, Na utukufu wa fahari ya ufalme Wake. Ufalme Wako ni ufalme wa zamani zote,
Na mamlaka Yako ni ya vizazi vyote…….

“Kinywa changu kitazinena sifa za Bwana;
Wote wenye mwili na walihimidi Jina Lake takatifu milele na milele” Zaburi 145:3-21 {8T 282.3}

## Maonyo Dhidi ya Kiburi

Tunapojifunza zaidi na zaidi juu ya vile Mungu alivyo, na jinsi sisi wenyewe tulivyo mbele ya macho Yake, tutaogopa na kutetemeka mbele Yake. {8T 283.1}

Hebu watu wa leo wachukue onyo kutoka kwa hatima ya wale ambao
katika nyakati za zamani kwa kiburi walitumia bila aibu kile ambacho Mungu alikuwa ametangaza kuwa ni kitakatifu. Wakati Waisraeli walipodiriki kufungua sanduku wakati liliporudi kutoka katika nchi ya Wafilisti, kuthubutu kwao kusiko na heshima kuliadhibiwa vikali. “Basi Bwana aliwapiga baadhi ya watu wa Beth-shemeshi, kwa sababu wamechungulia ndani ya hilo sanduku la Bwana, wapata watu sabini, na watu hamsini elfu; nao watu wakalalamika, kwa kuwa Bwana amewapiga watu kwa uuaji mkuu. Nao watu wa Beth-shemeshi wakasema, Ni nani awezaye kusimama mbele za Bwana, Huyu Mungu mtakatifu? Naye atapanda kwenda kwa nani kutoka kwetu?” 1 Samweli 6:19, 20 {8T 283.2}

Tena, fikiria hukumu ambayo ilimpata Uza. Kama ilivyokuwa katika enzi za Daudi, sanduku lilikuwa likipelekwa Yerusalemu, Uza alinyosha mkono wake kulizuia lisianguke. Kwa **ujuvi/presumption** wa kugusa ishara ya uwapo wa Mungu, alipigwa na mauti ya papo hapo. {8T 284.1}

Kwenye kichaka kinachowaka moto, wakati Musa, bila kutambua uwapo wa Mungu, aligeuka kando kutazama mandhari nzuri, amri ilitolewa: {8T 284.2}

“Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. . . . Musa akaficha uso wake; kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu." Kutoka 3:5, 6. {8T 284.3}

"Ikawa hapo Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, akavua macho yake na kuangalia, na tazama, Mtu Mume akasimama kumkabili mbele yake, Naye alikuwa na upanga wazi mkononi Mwake; Yoshua akamwendea, na kumwambia, Je! Wewe U upande wetu, au upande wa adui zetu? Akasema, La, lakini nimekuja sasa, nili Amiri wa Jeshi la Bwana. Yoshua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, akamwuliza, Bwana Wangu aniambia nini mimi mtumishi Wake? Huyo Amiri wa Jeshi la Bwana akamwambia Yoshua, Vua viatu vyako miguuni mwako; kwa kuwa mahali hapo usimamapo ni Patakatifu. Yoshua akafanya vivyo. Yoshua 5:1315. {8T 284.4}

Katika Patakatifu na hekalu, ambazo zilizokuwa alama za kidunia za makao ya Mungu, chumba kimoja kilikuwa kitakatifu kwa ajili ya uwapo Wake Bwana. Pazia lililopambwa kwa makerubi mlangoni pake halikupasa kuinuliwa na mkono wowote isipokuwa mmoja. Kuinua pazia hilo na kuingia ndani kwenye siri takatifu za Patakatifu pa Patakatifu pasipo kuamriwa ilikuwa ni mauti. Kwa maana juu ya Kiti cha Rehema na malaika walioinama, wakiabudu ulikaa utukufu wa Mtakatifu kuliko wote, utukufu ambao hakuna mtu angeweza kuutazama na kuishi. Katika siku moja

katika mwaka iliyoamriwa kwa ajili ya huduma katika Patakatifu pa Patakatifu, kuhani mkuu aliingia mbele za uso wa Mungu kwa kutetemeka, wakati moshi wa uvumba ulifunika asiweze kuuona utukufu ule. Katika nyua zote za hekalu kila sauti ilinyamazishwa tuli. Hakuna makuhani waliohudumu kwenye madhabahu. Majeshi ya waabuduo, waliinama kwa kicho cha ukimya, wakipeleka maombi yao kusihi rehema za Mungu. {8T 284.5}

"Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani." 1 Wakorintho 10:11 "Lakini Bwana Yumo ndani ya hekalu Lake takatifu; dunia yote na inyamaze kimya mbele Zake." Habakuki 2:20.
"Bwana ametamalaki, mataifa wanatetemeka;
Ameketi juu ya makerubi, nchi inatikisika.
Bwana katika Sayuni ni Mkuu,
Naye ametukuka juu ya mataifa yote.
Na walishukuru Jina Lake kuu la kuhofiwa;
Ndiye mtakatifu." Zaburi 99:1-3

"Bwana Yu katika hekalu Lake takatifu.
Bwana ambaye kiti Chake kiko mbinguni,
Macho Yake yanaangalia;
Kope Zake zinawajaribu wanadamu."
"Maana nimekula majivu kama chakula, Na kukichanganya kinywaji Changu na machozi." Zaburi 11:4; 102:19.
"Toka mahali pake aketipo Huwaangalia wote wakaao duniani.
Yeye aiumbaye mioyo yao wote Huzifikiri kazi zao zote."
"Nchi yote na imwogope Bwana,
Wote wakaao duniani na wamche." Zaburi 33:14, 15, 8. {8T 285.1}

Mwanadamu hawezi kumfahamu Mungu kwa kuchunguza. Hebu yeyote asitafute kwa mkono wa ujuvi/kiburi kuinua pazia linaloficha utukufu Wake. "Hukumu Zake hazichunguziki, wala njia Zake hazitafutikani!" Warumi 11:33. Ni uthibitisho wa rehema Zake kuwa kipo kinachouficha uweza Wake; kwani kuinua pazia linaloficha uwapo wa Kiungu ni mauti. Hakuna akili ya mwanadamu inayoweza kupenya kwenye usiri ambamo Mwenye Nguvu zote anakaa na kufanya kazi. Ni yale tu ambayo anaona yanafaa kudhihirisha, ndiyo tunayoweza kuyafahamu kuhusu Yeye. Uwezo wa kufikiri na kupembua mambo lazima ukubali mamlaka iliyo kubwa kuizidi. Moyo na akili lazima ziiname kwa MIMI NIKO. {8T 285.2}

### Kristo ni Ufunuo wa Mungu

Yote ambayo mwanadamu anahitaji kujua au anayoweza kufahamu kuhusu Mungu yamefunuliwa katika maisha na tabia ya Mwanawe. {8T 286.1}

“Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, Huyu Ndiye aliyemfunua.” Yohana 1:18. {8T 286.2}

Kwa kuuvaa ubinadamu, Kristo alikuja kuwa mmoja pamoja na wanadamu na kwa wakati uo huo kumdhihirisha Baba yetu wa mbinguni kwa wanadamu wenye dhambi. Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu Zake katika mambo yote. Alifanyika mwili, kama sisi tulivyo. Alikuwa na njaa na kiu na kupata uchovu. Alitegemezwa na chakula na kuburudishwa na usingizi. Alishiriki fungu la wanadamu, na bado alikuwa Mwana wa Mungu asiye na hatia. Alikuwa mgeni na msafiri hapa duniani – alikuwa ulimwenguni, lakini si wa ulimwengu huu; alijaribiwa kama wanaume na wanawake wa leo wanavyojaribiwa, lakini bado aliishi maisha bila dhambi. {8T 286.3}

Mpole, Mwenye huruma, Mwenye moyo mwema, anayejali wengine kila wakati, Aliwakilisha tabia ya Mungu, na bila kukoma alijishughulisha kila wakati katika kumtumikia Mungu na wanadamu. {8T 286.4}

"Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, ... amejaa neema na Kweli." Aya ya 14. {8T 286.5}

"Jina lako nimewadhihirishia," Alisema, "watu wale ulionipa katika ulimwengu," "ili pendo lile ulilonipenda Mimi liwe ndani yao." Yohana 17: 6, 26. {8T 286.6}

“Wapendeni adui zenu,” aliwaambia; “waombeeni wanaowaudhi, tendeni mema, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni;” “kwa kuwa Yeye ni mwema kwa wasiomshukuru, na waovu.” “maana Yeye huwaangazia jua Lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.” “Basi, iweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma. Mathayo 5:44, 45; Luka 6:35, 36. {8T 286.7}

### Utukufu wa Msalaba

Ufunuo wa upendo wa Mungu kwa wanadamu kitovu chake ni msalaba. Umuhimu wake kamili ulimi hauwezi kutamka; kalamu haiwezi kuielezea; akili ya mwanadamu haiwezi kuelewa kwa undani. Kwa kutazama msalaba wa Kalvari tunaweza tu kusema: "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16. {8T 287.1}

Kristo aliyesulubiwa kwa ajili ya dhambi zetu, Kristo aliyefufuka kutoka kwa wafu, Kristo aliyepaa juu, Ndiye sayansi ya wokovu ambayo tunapaswa kujifunza na

kuifundisha. {8T 287.2}

"Ambaye Yeye mwanzo alikuwa Yuna namna ya Mungu, Naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." Wafilipi 2: 6-8 {8T 287.3}

"Kristo Yesu Ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, Naye yuko mkono wa kuume wa Mungu" "Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa Yeye; maana Yu hai sikuzote ili awaombee." Warumi 8:34; Waebrania 7:25. {8T 287.4}

"Kwa kuwa hamna kuhani Mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali Yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi." Waebrania 4:15 {8T 287.5}

Hapa kuna hekima isiyo na kikomo, upendo usio na mwisho, haki isiyokoma, rehema isiyo na mwisho – "Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu." Warumi 11:33. {8T 287.6}

Ni kupitia karama ya Kristo ndipo tunapopokea kila baraka. Kupitia karama hiyo huja kwetu siku kwa siku bubujiko lisilokoma la wema wa Yehova. Kila ua, na rangi yake maridadi na harufu nzuri, hutolewa ili kutufurahisha kupitia Karama hiyo moja. Jua na mwezi viliumbwa na Yeye; hakuna nyota inayopamba mbingu ambazo hakuziumba. Hakuna aina ya chakula juu ya meza zetu ambacho hakutupatia kwa ajili ya kuwa riziki yetu. Andiko la Kristo liko juu ya yote hayo. Kila kitu hutolewa kwa wanadamu kupitia kwa Karama/Zawadi moja isiyoelezeka, Mwana wa pekee wa Mungu. Alisulubiwa msalabani ili fadhila hizi zote ziweze kububujika kwa viumbe vya Mungu. {8T 287.7}

Matunda ya mti wa uzima katika Bustani ya Edeni yalikuwa na nguvu isiyo ya kawaida. Kuyala matunda yale ilikuwa ni kuishi milele. Matunda yake yalikuwa dawa ya kifo. Majani yake yalikuwa ni kwa ajili ya kudumisha uhai na kutokufa. Lakini kupitia kutokutii kwa mwanadamu mauti yaliingia ulimwenguni. Adamu alikula kutoka katika mti wa ujuzi wa mema na mabaya, matunda ambayo alikuwa amekatazwa kuyagusa. Uasi wake ulifungua milango ya huzuni katika jamii yetu. {8T 288.1}

Baada ya kuingia kwa dhambi Mkulima wa mbinguni alipandikiza mti wa uzima kwenda Bustani ya Edeni iliyo juu; lakini matawi yake huning'inia juu ya kuta za ulimwengu wa chini. Kupitia ukombozi ulionunuliwa na damu ya Kristo, bado tunaweza kula matunda yake yenye kutoa uzima. {8T 288.2}

Kuhusu Kristo imeandikwa: "Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima

ulikuwa nuru ya watu." Yohana 1: 4. Yeye Ndiye Chemchemi ya uzima. Utii Kwake ni nguvu inayotoa uhai unaofurahisha moyo. {8T 288.3}

Kristo alisema: "Mimi Ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe." Kama vile Baba aliye hai alivyonituma Mimi, Nami ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa Mimi….. Roho Ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima. " Yeye ashindaye, nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu." Yohana 6:35, 57-63; Ufunuo 2:7. {8T 288.4}

"Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu!" 1 Yohana 3:1. {8T 289.1}

## Maarifa Yanayofanya Kazi ya Badiliko

Maarifa ya Mungu kama yanavyofunuliwa katika Kristo ni maarifa ambayo wote ambao wameokolewa lazima wawe nayo. Ni maarifa ambayo hufanya mabadiliko ya tabia. Maarifa haya, yakipokelewa, yataumba upya roho kuwa katika mfano wa Mungu. Yatatoa uwezo wa kiroho ambao ni wa Kiungu kwa kiumbe chote. {8T 289.2}

"Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu." 2 Wakorintho 3:18 {8T 289.3}

Kuhusu maisha Yake mwenyewe Mwokozi alisema: “Kama vile Mimi nilivyozishika amri za Baba yangu.” "Naye aliyenipeleka Yu pamoja Nami, hakuniacha peke Yangu; kwa sababu nafanya sikuzote yale yampendezayo." Yohana 15:10; 8:29. Kama Yesu alivyokuwa katika maumbile ya kibinadamu, ndivyo Mungu anavyomaanisha wafuasi Wake wawe. Katika nguvu zake tunapaswa kuishi maisha ya usafi na heshima ambayo Mwokozi aliyaishi. {8T 289.4}

"Kwa hiyo," Paulo anasema, "nampigia Baba magoti ambaye kwa Jina Lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa, awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho Wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo Wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu." Waefeso 3:14-19 {8T 289.5}

# SURA YA 45

## HATARI KATIKA MAARIFA YA KUKISIA

Sayansi ya uongo ni mojawapo ya wakala wa njia ambazo Shetani alitumia katika nyua za mbinguni, na anaitumia hata leo. Madai ya uwongo aliyowapa malaika, nadharia zake za kisayansi zenye hila, ziliwashawishi wengi wao kutoka kwenye uaminifu wao. {8T 290.1}

Baada ya kupoteza nafasi yake mbinguni, Shetani aliwasilisha majaribu yake kwa wazazi wetu wa kwanza. Adamu na Hawa walijisalimisha kwa adui, na kwa kutokutii kwao ubinadamu ulijitenga na Mungu, na dunia ilitengwa na mbingu. {8T 290.2}

Kama Adamu na Hawa kamwe wasingeligusa ule mti uliokatazwa, Bwana angewapatia maarifa, maarifa ambayo juu yake hakukuwa na laana yoyote ya dhambi, maarifa ambayo yangewaletea furaha ya milele. Yote waliyoyapata kwa kutokutii kwao ni uzoefu wa dhambi na matokeo yake. {8T 290.3}

### Udanganyifu wa Siku -za -Mwisho

Uwanja ambao ndani yake Shetani aliwaongoza wazazi wetu wa kwanza ndio uo huo ambao anawaongoza watu leo kuuingia. Aduii huyu anaujaza ulimwengu na hekaya za kubuni, zinazopendeza. Kwa kila hila iliyo chini ya mamlaka yake anajitahidi kuwazuia watu kupata maarifa ya Mungu ambayo ni wokovu. {8T 290.4}

Tunaishi katika nyakati za nuru kubwa; lakini mengi ambayo yanaitwa kuwa ni nuru yanafungua njia kwa ajili ya hekima na sanaa za udanganyifu wa Shetani. Vitu vingi vitawasilishwa ambavyo vitaonekana kuwa ni vya kweli, lakini bado vitahitaji kuzingatiwa kwa kuchujwa kwa uangalifu na maombi mengi; kwani vinaweza kuwa hila yenye kughilibu ya adui. Njia ya makosa mara nyingi inaonekana kuwa karibu na njia ya Ukweli. Ni vigumu kuitofautisha na njia inayoongoza kwenye utakatifu na mbingu. Lakini akili iliyoelimishwa na Roho Mtakatifu inaweza kutambua kwamba inatoka nje ya njia sahihi. Baada ya muda mfupi njia hizo mbili zitaonekana kuwa zimetengana mbali. {8T 290.5}

### Nadharia ya Kuabudu Miungu Wengi -Pantheisimu

*[Pantheism ni imani ya miungu mingi, kwamba hakuna Mungu wa mbinguni tunayemjua, wala Roho Mtakatifu au nguvu zozote za miujiza, ila kwamba uumbaji una uungu, yaani uumbaji ambao Mungu aliumba una uungu ndani yake. Ni imani kwamba ulimwengu wote na vyote vilivyomo ni mungu. Ni kwamba hakuna Mungu bali kila kitu ni mungu, na hivyo wana miungu mingi, kila kitu ndani yake mungu yupo, iwe ni miti, maua, mimea, milima nk].*

Tayari yamekuja miongoni mwa watu wetu mafundisho ya kiroho ambayo yatadhoofisha imani ya wale wanaoyatilia maanani. Nadharia ya Patheisimu-kwamba Mungu ni hali inayoenea kote katika maumbile ya asili ni mojawapo ya ujanja mkubwa wa hila za Shetani. Inamwakilisha Mungu vibaya na ni fedheha kwa ukuu na utukufu Wake. {8T 291.1}

Nadharia ya Patheisimu- kuabudu miungu wengi-kwamba Mungu Yumo ndani ya kila kitu na kila kitu ni Mungu haikubaliani na Neno la Mungu. Nuru ya Ukweli Wake inaonesha kwamba nadharia hizi ni vyombo vya hila vinavyoangamiza roho. Giza ni sifa yake, kupenda anasa na uchafu wa ngono, kujifurahisha kwa tamaa ni fani yake. Zinafurahisha moyo wa asili na kuruhusu mwelekeo wa kufuatisha tamaa za mwili. Kujitenga na Mungu ni matokeo ya kukubaliana nazo (IMANI YA PATHEIMU NA UZINZI, UASHERATI na DHAMBI NYINGINE ZA ZINAA: Nadharia au imani ya Pantheismu huruhusu hisia na tamaa ya moyo wa asili na chochote anachojisikia vizuri kufanya kwa kuwa Mungu Yuko kila mahali hufanya, kwani husema kuwa ni lazima pia Mungu awepo katika tamaa hizi za mwil). {8T 291.2}

Hali yetu katika dhambi imekuwa si ya kawaida, na nguvu ya kuturejesha lazima iwe ni ile isiyo ya ulimwengu huu, si ya kawaida (supernatural), vinginevyo haitakuwa na thamani. Upo uweza mmoja tu unaoweza kuvunja madaraka ya uovu katika mioyo ya wanadamu, na hiyo ni nguvu ya Mungu katika Yesu Kristo. Ni kupitia kwa damu ya Yule Aliyesulubiwa peke yake tu, ndiyo kuna utakaso kutoka kwenye dhambi. Neema Yake pekee inaweza kutuwezesha kupinga na kutiisha mielekeo yetu ya asili iliyoanguka. Uweza huu nadharia za umizimu humtangua katika macho yake na hivyo kumfanya Mungu aonekane kwamba hayupo au hana uwezo (Mathayo 7:13). Ikiwa Mungu ni nafsi inayoenea katika maumbile yote ya asili, basi Yeye hukaa ndani ya watu wote; na ili kuufikia utakatifu, mwanadamu anapaswa kukuza tu nguvu iliyo ndani yake. {8T 291.3}

Nadharia hizi, zikifuatwa hadi kufikia hitimisho lake la kimantiki, huondoa uwekezaji wote wa historia ya Ukristo -na hivyo Kristo Mwenyewe, na Neno la Mungu kwa jumla. Zinaondoa umuhimu wa upatanisho na kumfanya mwanadamu kuwa mwokozi wake mwenyewe, kwamba anaweza kujiokoa mwenyewe. Nadharia hizi kumhusu Mungu hufanya Neno Lake kuwa bure, na wale wanaozikubali wako katika hatari kubwa ya kuongozwa hatimaye kuiangalia Biblia yote kama hekaya za kubuni-tamthiliya. Wanaweza kutazama fadhila kuwa bora kuliko uovu; lakini Mungu anapoondolewa katika nafasi Yake ya ukuu (Mwenye Enzi), wanaweka utegemezi wao juu ya uwezo wa mwanadamu, ambao, bila Mungu, hauna thamani. Mapenzi na

nia ya mwanadamu yasiyosaidiwa hayana uwezo halisi wa kupinga na kushinda uovu. Ulinzi wa roho unakuwa umevunjika. Mwanadamu hana kizuizi dhidi ya dhambi. Wakati vizuizi vya Neno la Mungu na Roho Wake vimekataliwa, hatujui ni kwa kina cha chini kiasi gani mtu anaweza kuzama. {8T 291.4}

Wale ambao wanaendelea kushikilia nadharia hizi za umizimu hakika wataharibu uzoefu wao wa Kikristo, watakata uhusiano wao na Mungu, na kupoteza uzima wa milele. {8T 292.1}

Madanganyo kumhusu Mungu na asili ambayo yanaijaza dunia na nadharia ya kushuku ni msukumo wa adui yule aliyeanguka, ambaye yeye mwenyewe ni mwanafunzi wa Biblia, ambaye anajua Ukweli ule ambao ni muhimu kwa watu kupokea, na bidii yake ni ya kugeuza akili kutoka kwenye Kweli kuu zilizotolewa kwa ajili ya kuwaandaa wao kwa kile kinachoujia ulimwengu. {8T 292.2}

Nimeona matokeo ya mawazo haya dhanifu ya kufikirika juu ya Mungu, katika ukengeufu, umizimu, na upendo huru (uasherati). Mwelekeo wa upendo huru au usiodhibitika wa mafundisho haya ulifichwa sana kiasi kwamba mwanzoni ilikuwa ni vigumu kuweka wazi tabia yake halisi. Mpaka pale Bwana alipoiwasilisha kwangu, sikujua nitauita kwa jina gani, lakini niliamriwa niuite upendo wa kiroho usio mtakatifu. {8T 292.3}

## Ushupavu wa Kidini Baada ya 1844

Baada ya kupita muda mnamo 1844, tulikuwa na ushupavu wa kidini wa kila aina ambao ungeweza kukutana nao. Nilipewa shuhuda za karipio kwa ajili ya baadhi wanaoshikilia nadharia za umizimu. {8T 292.4}

Walikuwepo wale ambao walijitahidi kufanya kazi ya kusambaza mawazo ya uwongo kuhusu Mungu. Nilipewa nuru kwamba watu hawa walikuwa wakifanya Ukweli kuwa batili kwa mafundisho yao ya uwongo. Niliagizwa kuwa walikuwa wakipotosha roho kwa kuwasilisha nadharia za kufikirika kuhusu Mungu. {8T 292.5}

Nilikwenda mahali walipokuwa na kufungua mbele yao asili ya kazi yao. Bwana alinipa nguvu ya kuweka wazi mbele yao hatari yao. Miongoni mwa maoni mengi walishikilia ni kwamba wale ambao hapo awali walikwishatakaswa hawawezi kutenda dhambi tena. Mafundisho yao ya uwongo yalikuwa yakileta madhara makubwa kwao wenyewe na kwa wengine. Walikuwa wakipata uwezo wa kimizimu juu ya wale ambao hawangeweza kuona ubaya wa nadharia hizi zilizovikwa kwa urembo mwingi. Fundisho kwamba watu wote walikuwa watakatifu lilisababisha imani kwamba mapenzi ya waliotakaswa yasingeweza kupotosha kamwe. Matokeo ya imani hii yalikuwa ni kutimizwa kwa tamaa mbaya/ovu za mioyo ambayo, ingawa

inasemekana ilitakaswa, ilikuwa mbali na usafi wa mawazo na maisha. {8T 293.1}

Mafundisho yasiyo ya utauwa yakifuatiwa na mazoea ya dhambi. Ni chambo chenye sumaku cha yule baba wa uwongo, na husababisha kutokuwa na hatia na kuridhika na uchafu. {8T 293.2}

Huu ni moja tu ya mifano ambayo niliitwa kuwakemea wale ambao walikuwa wanawasilisha fundisho la Mungu ambaye hayupo katika nafsi aliyeenea katika maumbile yote ya asili, na makosa mengine kama hayo. {8T 293.3}

### Uzoefu wa Awali Kurudiwa

Uzoefu wa zamani utarudiwa. Katika siku zijazo, ushirikina wa Shetani utachukua sura mpya. Makosa yatawasilishwa kwa njia ya kupendeza na kubembeleza. Nadharia za uwongo, zilizovikwa mavazi ya nuru, zitawasilishwa kwa watu wa Mungu. Hivyo Shetani atajaribu kuwadanganya, ikiwezekana, walio wateule. Mivuto mingi yenye kupotosha itatumika; akili zitapumbazwa. {8T 293.4}

Ufisadi wa kila aina, sawa na ule uliokuwepo kabla ya gharika, utaletwa ili kuziteka akili. Kuikuza asili kuwa kama Mungu, uhuru usiozuilika wa mapenzi na nia ya mwanadamu, ushauri wa wasiomcha Mungu – haya hutumiwa na Shetani kama mawakala ili kuleta hatima fulani. Atatumia uwezo wa akili juu ya akili ili kutekeleza mipango yake. Wazo la kusikitisha zaidi ya yote ni kwamba chini ya mvuto wake wa udanganyifu, watu watakuwa na mfano wa utauwa, bila kuwa na uhusiano wa kweli na Mungu. Kama Adamu na Hawa, ambao walikula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, wengi hata sasa wanakula vipande vya nadharia zidanganyazo na zenye makosa. {8T 293.5}

Mawakala wa kishetani wanazivika nadharia za uwongo kwa mavazi ya kupendeza, kama ilivyokuwa kwa Shetani katika Bustani ya Edeni alificha utambulisho wake kutoka kwa wazazi wetu wa kwanza kwa kuzungumza kupitia nyoka. Mawakala hawa huingiza ndani ya akili za wanadamu yale ambayo kwa kweli ni makosa ya kutisha na kufisha. Ushawishi wa Shetani wenye kupumbaza utakaa juu ya wale ambao wanageuka kutoka kwenye Neno la wazi la Mungu na kwenda kwenye hekaya za kubuni zenye kupendeza. {8T 294.1}

Ni wale ambao wameipata nuru zaidi ndio ambao Shetani kwa uangalifu hutafuta kuwanasa. Adui anafahamu kuwa kama ataweza kuwadanganya, chini ya utawala wake, wataivalisha dhambi kwa mavazi ya haki, na hivyo wataweza kuwapotosha wengi. {8T 294.2}

Ninawaambia wote: Jihadharini-lindeni vyema katika kituo chenu cha ulinzi! (chunga); kwani kama malaika wa nuru, Shetani anatembea katika kila mkutano wa watendakazi wa Kikristo, na katika kila kanisa, akijaribu kupata washirika kwenda upande wake. Nimeamriwa kuwapa watu wa Mungu onyo: "Msidanganyike; Mungu hadhihakiwi." Wagalatia 6:7. {8T 294.3}

### Jihadharini na Dini ya Msisimko

Wakati huu tunawahitaji katika kusudi la Mungu watu wenye akili za kiroho, watu ambao ni thabiti katika kanuni na ambao wana ufahamu dhahiri wa Ukweli. {8T 294.4} 295

Nimeagizwa kuwa si mafundisho mapya na ya kupendeza ambayo watu huhitaji. Hawahitaji dhana za kibinadamu. Wanahitaji shuhuda za watu wanaoujua na kuutenda Ukweli, watu ambao wanaelewa na kutii agizo alilopewa Timotheo: "Lihubiri Neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo. Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza huduma yako. 2 Timotheo 4:2-5. {8T 295.1}

Tembea imara, kwa kunuia, ukiazimia, bila shaka, miguu yako ikiwa imevikwa utayari wa injili ya amani. Utaweza kuwa na hakika kwamba dini safi na isiyo na mawaa si dini ya msisimko au mori mori. Mungu hajaweka juu ya mtu yeyote mzigo wa kuhamasisha uchu/hamu ya mafundisho na nadharia za kubahatisha/kusadikika/kufikirika. Ndugu zangu, wekeni mambo haya mbali na mafundisho yenu. Msiruhusu yaingie katika uzoefu wenu. Hebu kazi yenu ya maisha isiharibiwe au kunyanguliwa nayo. {8T 295.2}

### Onyo Dhidi ya Mafundisho ya Uwongo

Onyo dhidi ya mafundisho ya uwongo linapatikana katika barua ya Paulo kwa Wakolosai. Mtume anasema kwamba mioyo ya waumini inapaswa "Kuunganishwa pamoja katika upendo, wakapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapate kujua kabisa siri ya Mungu, yaani, Kristo; ambaye ndani Yake Yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika. Nasema neno hili," anaendelea kusema "mtu asije akawadanganya kwa maneno ya kuwashawishi. ……. Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye: wenye shina na wenye kujengwa katika Yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa;

mkizidi kutoa shukrani. Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo. Maana katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika Yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka. Wakolosai 2:2-10. {8T 295.3}

Nimeagizwa kuwaambia watu wetu: Hebu na tumfuate Kristo. Tusisahau kwamba Yeye Ndiye anayepaswa kuwa Kielelezo chetu katika mambo yote. Tunaweza kwa usalama kuachana na mawazo yale ambayo hayapatikani katika mafundisho Yake. Natoa wito kwa wachungaji wetu kuhakikisha kuwa miguu yao imewekwa kwenye jukwaa la Ukweli wa milele. Jihadharini namna mnavyofuata mihemko, na kuiita Roho Mtakatifu. Wengine wako katika hatari katika suala hili. Ninatoa wito kwao wawe kamili katika imani, wenye hekima, waweze kutoa kwa kila mtu anayeuliza sababu ya tumaini lililo ndani yao. {8T 296.1}

**Kupotosha Akili kutoka kwenye Wajibu wa Sasa**

Adui anatafuta kupotosha mawazo ya ndugu na dada zetu kutoka kwenye kazi ya kuwaandaa watu kusimama katika siku hizi za mwisho. Udanganyingu na Ghiliba yake imeundwa kuziongoza akili mbali na hatari na majukumu ya wakati huu. Hukadiria kuwa si kitu nuru ile ambayo Kristo alikuja nayo kutoka mbinguni na kumpa Yohana kwa ajili ya watu Wake. Wanafundisha kwamba matukio yaliyo mbele yetu hayana umuhimu wa kutosha kupewa uangalifu maalumu. Huufanya Ukweli wenye asili ya mbinguni kuonekana kuwa hauna athari yoyote na kuwapora watu wa Mungu uzoefu wao wa zamani, wakiwapa sayansi ya uwongo. {8T 296.2}

"Bwana asema hivi, Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo." Yeremia 6:16. {8T 296.3}
297

Hebu mtu yeyote asijitahidi kubomoa misingi ya imani yetu - misingi ambayo iliwekwa mwanzoni mwa kazi yetu kwa kusoma Neno kwa maombi mengi na kwa mafunuo. Juu ya misingi hii tumekuwa tukijenga kwa miaka hamsini iliyopita. Watu wanaweza kudhani kwamba wamepata njia mpya na kwamba wanaweza kuweka msingi wenye nguvu zaidi ya ule ambao umekwishakuwekwa. Lakini huu ni udanganyifu mkubwa. Hakuna msingi mwingine awezayo mtu kuuweka isipokuwa **Ule uliokwisha kuwekwa**. {8T 297.1}

Hapo awali wengi wamejitolea kujenga imani mpya, uanzishaji wa kanuni mpya. Lakini jengo lao lilisimama kwa muda gani? Lilianguka punde tu, kwa sababu halikujengwa juu ya Mwamba. {8T 297.2}

Je! Wanafunzi wa kwanza hawakukutana na maneno ya wanadamu? Je! Haikuwa lazima kwao kusikiliza nadharia za uwongo, na kisha, baada ya kufanya yote, kusimama imara, wakisema: "Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni Ule uliokwisha kuwekwa.?" 1 Wakorintho 3:11. {8T 297.3}

Hivyo tunapaswa kushikilia mwanzo wa imani yetu imara hadi mwisho. Maneno yenye uweza yametumwa na Mungu na Kristo kwa watu hawa, ili kuwatoa ulimwenguni, hatua kwa hatua, na kuwafikisha kwenye nuru iliyo wazi ya Ukweli wa Sasa. Kwa midomo iliyoguswa na moto mtakatifu, watumishi wa Mungu wametangaza ujumbe huo. Kauli za Mwenyezi Mungu zimeweka muhuri wake juu ya uhalisi wa Ukweli uliotangazwa. {8T 297.4}

### Utoaji Upya wa Ushuhuda Ulionyoka

Bwana anatoa wito wa urejeshwaji wa ushuhuda ulionyoka uliobebwa miaka iliyopita. Yeye Anatoa wito wa kufanywa upya kwa maisha ya kiroho. Nguvu za kiroho za watu Wake zimekuwa legevu kwa muda mrefu, lakini kunapaswa kuwapo na ufufuo kutoka katika kifo dhahiri. {8T 297.5}

Kwa maombi na kuungama dhambi lazima tuiweke wazi barabara kuu ya Mfalme. Tunapofanya hivi, uweza wa Roho utakuja kwetu. Tunahitaji nguvu ya Pentekoste. Hii itakuja, kwa kuwa Bwana aliahidi kumtuma Roho Wake kama uweza wenye ushindi wote. {8T 297.6}

Nyakati za hatari ziko mbele yetu. Kila mtu ambaye ana maarifa ya Ukweli anapaswa kuamka na kujiweka mwenyewe, mwili, nafsi, na roho, chini ya uongozi wa Mungu. Adui anatufuatilia nyayo zetu. Lazima tuwe macho kabisa, tukiwa na tahadhari dhidi yake. Lazima tuvae silaha zote za Mungu. Lazima tufuate maelekezo yaliyotolewa kupitia roho ya unabii. Lazima tuupende na kuutii Ukweli kwa ajili ya wakati huu. Hili litatuokoa kutokana na kuukubali udanganyifu wenye nguvu. Mungu amesema nasi kupitia Neno Lake. Yeye Amesema nasi kupitia Shuhuda kwa Kanisa na kupitia vitabu ambavyo vimesaidia kuweka wazi wajibu wetu wa sasa na msimamo ambao tunapaswa kuwa nao sasa. Maonyo ambayo yametolewa, mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, yanapaswa kuzingatiwa. Ikiwa tutayapuuza, tunaweza kutoa udhuru gani? {8T 298.1}

Ninawasihi wale wanaofanya kazi kwa ajili ya Mungu wasikubali kupokea bandia kuwa ni Ukweli. Hebu sababu za kibinadamu zisiwekwe mahali ambapo Ukweli wa Mwenyezi Mungu, unaotakasa unapaswa kuwa. Kristo anasubiri kuwasha imani na

upendo mioyoni mwa watu Wake. Hebu fikra potofu zisiungwe mkono na watu ambao wanapaswa kusimama imara kwenye jukwaa la Ukweli wa milele. Mungu anatuita tuzishike kabisa kanuni za kimsingi ambazo zimejengwa juu ya mamlaka isiyo na shaka. {8T 298.2}

### Tafuta Upendo Ule wa Kwanza

Katika mioyo ya wengi ambao wamekuwa kwa muda mrefu katika Ukweli kumeingia roho ngumu, ya kuhukumu. Wao ni wakali, wakosoaji, wanaotafuta makosa. Wamepanda juu ya kiti cha hukumu kutamka hukumu juu ya wale ambao hawakubaliani na maoni yao. Mungu anawaita washuke chini ya hicho kiti na kuinama mbele zake kwa toba, wakikiri dhambi zao. Anawaambia: "Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, Naja kwako, Nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu. Ufunuo 2:4, 5. Wanajitahidi kuwa katika nafasi ya kwanza, na kwa maneno na matendo yao wanaumiza na kuipa uchungu mioyo mingi. {8T 298.3}

Dhidi ya roho hii, na dhidi ya dini ya uwongo ya hisia, ambayo ni hatari pia, ninatoa onyo langu. Jihadharini, ndugu na dada. Kiongozi wenu ni nani - Kristo au malaika aliyeanguka kutoka mbinguni? Jichunguze mwenyewe ili ujue ikiwa uko thabiti katika imani. {8T 299.1}

### Neno la Mungu ni Ulinzi Kwetu

Wito wetu na kauli mbiu vinapaswa kuwa: "Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isaya 8:20. Tunayo Biblia iliyojaa Kweli za thamani ya juu. Inabeba Alfa na Omega ya maarifa. Maandiko, yaliyotolewa kwa uvuvio wa Mungu, "Yafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema." 2 Timotheo 3:16, 17. Chukua Biblia kama kitabu chako cha kujifunzia-Kitabu cha Kiada. Wote wanaweza kuelewa mafundisho yake. {8T 299.2}

Natoa wito kwa wachungaji wetu, matabibu, na washiriki wote wa kanisa kujifunza masomo yale aliyoyatoa Kristo kwa wanafunzi Wake mara tu kabla ya kupaa Kwake. Masomo haya yana Mafundisho ambayo watu huhitaji. {8T 299.3}

Uzima wa milele unapatikana tu kwa kuula mwili na kunywa damu ya Mwana wa Mungu. "Amin, amin, nawaambia," Kristo alisema, "Yeye aniaminiye Mimi yuna uzima wa milele…… Mimi Ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele; na chakula nitakachotoa Mimi ni mwili Wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu….. yule Aulaye mwili Wangu, na

kuinywa damu Yangu, anao uzima wa milele; Nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili Wangu ni chakula cha kweli, na damu Yangu ni kinywaji cha Kweli. Aulaye mwili Wangu na kuinywa damu Yangu hukaa ndani Yangu, Nami hukaa ndani yake…. Roho Ndiyo itiayo uzima; mwili haufai kitu; maneno niliyowaambia, ni Roho, tena ni Uzima." Yohana 6:47-63. {8T 299.4}

Kristo anatoa wito kwa watu Wake kuliamini na kulitenda Neno Lake. Wale wanaolipokea na kukubaliana na Neno hili, kulifanya kuwa sehemu ya kila hatua, ya kila sifa ya tabia, watakua na nguvu katika uweza wa Mungu. Itaonekana kuwa imani yao ni yenye asili ya mbinguni. Hawatangatanga katika njia ngeni. Mawazo yao hayatageukia dini ya kupenda hisia na msisimko. Mbele ya malaika na mbele ya wanadamu, watasimama kama wale walio na nguvu, wenye tabia thabiti za Kikristo. {8T 300.1}

Katika chetezo cha dhahabu cha Ukweli, kama ulivyowasilishwa katika mafundisho ya Kristo, tunacho kile ambacho kitasadikisha na kuongoa roho. Wasilisha, katika usahili wa Kristo, Kweli zile ambazo alikuja ulimwenguni kuzitangaza, na nguvu ya ujumbe wako itajidhihirisha yenyewe. Usiwasilishe nadharia au majaribio au mitihani ambayo Kristo hajawahi kuyasema na ambayo hayana msingi wowote katika Biblia. Tunayo Kweli kuu na nzito, ya kuwasilisha. "Imeandikwa" ni kipimo ambacho lazima kifikishwe, nyumbani, kwenye kila moyoni. {8T 300.2}

Watu bado wanaweza kujifunza vitu ambavyo vinahusu amani yao. Sauti ya Rehema bado inaweza kusikika ikiita: "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, na mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu; Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi." Mathayo 11: 28-30. Ni pale tu ambapo maisha ya kiroho yanapotolewa ndipo pumziko hupatikana na mema ya kudumu huhifadhiwa. Ni lazima tuweze kusema, katika dhoruba na tufani: " Nanga yangu inashikilia." {8T 300.3}

Acha tuliendee Neno la Mungu kwa ajili ya uongozi. Hebu tutafute "Bwana asema." Tumekuwa na njia za kibinadamu vya kutosha. Akili iliyofunzwa katika sayansi ya dunia peke yake hushindwa kuelewa mambo ya Mungu; lakini akili ile ile, ikiongoka na kutakaswa, itaona uweza wa Mwenyezi Mungu katika Neno. Ni akili ile tu na moyo uliosafishwa kwa utakaso wa Roho unaweza kutambua mambo ya mbinguni. {8T 301.1}

Ndugu zangu, kwa Jina la Bwana ninawaita mwamke kutenda majukumu yenu. Hebu mioyo yenu na isalimishwe kwa uweza wa Roho Mtakatifu, nayo itawezeshwa kuamini mafundisho ya Neno. Hivyo utaweza kutambua mambo ya kina ya Mungu. {8T 301.2}

Hebu Mungu na awalete watu Wake chini ya uongozi wa kina wa Roho Wake! Hebu

na awaongoze watu kuamka, kuona hatari yao, na kujiandaa kwa kile kinachoujia ulimwengu! {8T 301.3}

## Jifunze Ufunuo

Kwa Yohana, Bwana alifunua masomo ambayo Aliona yangehitajika kwa watu Wake katika siku za mwisho. Maelekezo aliyoyatoa yanapatikana katika kitabu cha Ufunuo. Wale ambao watakuwa washirika katika kazi pamoja na Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo wataonesha kuvutiwa kwa kina na Ukweli unaopatikana katika kitabu hiki. Kwa kalamu na sauti watajitahidi kuweka wazi mambo ya ajabu ambayo Kristo alikuja kutoka mbinguni ili apate kuyadhihirisha. {8T 301.4}

“Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu, awaonyeshe watumwa Wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; Naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa Wake Yohana; aliyeshuhudia Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, mambo yote aliyoyaona. Heri asomaye, na wao wayasikiao Maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu." Ufunuo 1: 1-3. {8T 301.5}

Ujumbe huu mzito ambao umetolewa kwa mpangilio katika Ufunuo unapaswa kuchukua nafasi ya kwanza katika akili za watu wa Mungu. Kisiwepo kingine chochote cha kuruhusiwa kumeza usikivu wetu. {8T 302.1}

Muda wa thamani unapita kwa haraka, na kuna hatari kwamba wengi wataporwa muda ambao ungepaswa kutumika kwa kutangaza ujumbe ambao Mungu ametuma kwa ulimwengu ulioanguka. Shetani anafurahi kuona upotoshwaji wa akili ambazo zilipaswa kujishughulisha katika masomo ya Kweli ambazo huhusiana na mambo ya milele. {8T 302.2}

Ushuhuda wa Kristo, ushuhuda wenye sifa bainifu makini kabisa, unapaswa kutolewa kwa ulimwengu. Kote katika kitabu cha Ufunuo kuna ahadi za thamani ya juu, zinazoinua, na pia yapo maonyo yenye kutisha ya umuhimu mzito sana. Je! haiwapasi wale wanaokiri kuwa na maarifa ya Ukweli kusoma ushuhuda aliopewa Yohana na Kristo? Hapa hakuna kubahatisha, hakuna udanganyifu wa kisayansi. Hapa kuna zile Kweli zinazohusu ustawi wetu wa sasa na wa baadaye. Makapi ni nini ukilinganisha na ngano? {8T302.3}

## Kwa Kanisa Lililoko Sardi

"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye na hizo  Roho saba za Mungu, na zile nyota saba. Nayajua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa. Uwe mwenye kukesha, ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa. Maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu Wangu. Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia; yashike

hayo na kutubu. Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako. {8T 302.4}

"Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja Nami hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili. Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba Yangu, na mbele ya malaika Zake. Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa." Ufunuo 3:1-6. {8T 303.1}

## Ujumbe kwa Kanisa la Filadelfia

"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye mtakatifu, Aliye wa Kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, Yeye Mwenye kufungua wala hapana afungaye, Naye afunga wala hapana afunguaye. Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga, kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza Neno Langu, wala hukulikana Jina Langu. Tazama, nakupa walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, bali wasema uongo. Tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda. Kwa kuwa umelishika Neno la subira Yangu, Mimi Nami nitakulinda, utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi. Naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako. Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu Wangu, wala hatatoka humo tena kabisa, Nami nitaandika juu yake Jina la Mungu Wangu, na jina la mji wa Mungu Wangu, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu Wangu, na Jina Langu Mwenyewe, lile jipya." Aya ya 7-12. {8T 303.2}

## Ujumbe wa Laodikia

"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa Kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu. Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. Nakupa shauri, ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. {8T 304.1}

"Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu.

Tazama, Nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami. Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti chake cha enzi. Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa." Aya ya 14-22. {8T 304.2}

Bwana Yuaja hivi karibuni. Walinzi wa kuta za Sayuni wanaitwa kuamka wapate kutenda majukumu waliyopewa na Mungu. Mungu anatoa wito kwa walinzi ambao, kwa nguvu ya Roho, watatoa kwa ulimwengu ujumbe wa mwisho wa onyo; ambao watatangaza wakati wa usiku. Yeye Anatoa wito kwa walinzi ambao watawaamsha wanaume na wanawake kutoka kwenye uchovu wao, wasije wakalala usingizi wa mauti. {8T 304.3}

## SURA YA 46
## UONGO NA UKWELI KATIKA ELIMU

Mwanzilishi wa njama za uovu hufanya kazi kila wakati kufanya Maneno ya Mungu yasionekane na kuleta katika picha kamili maoni ya wanadamu. Anataka kwamba tusisikie sauti ya Mungu ikisema: "Hii ndiyo njia, tembeeni ndani yake." Kupitia katika michakato ya kielimu anafanya yote kwa uwezo wake kuificha nuru ya mbinguni. {8T 305.1}

Makisio ya Kifalsafa (Falsafa za kufikirika au kusadikika -- uongo)
(Speculation au Dhana ni uundaji wa nadharia au dhana bila ushahidi thabiti.)

Makisio ya kifalsafa na tafiti za kisayansi ambapo Mungu hatambuliwi huwafanya maelfu ya vijana kuwa wenye kushuku. Katika shule za leo mahitimisho ambayo wanadamu wasomi wamefikia kama matokeo ya uchunguzi wao wa kisayansi yamefundishwa kwa uangalifu na kufafanuliwa kikamilifu; wakati wazo linawekwa wazi kuwa ikiwa watu hawa wenye elimu ni sahihi, basi Biblia haiwezi kuwa. Kushuku kunavutia akili ya mwanadamu. Vijana huona ndani yake uhuru ambao unavutia mawazo ya ubunifu, na wanadanganyika. Shetani anashinda; kwa ujumla ndivyo alivyopanga iwe. Anastawisha kila mbegu ya mashaka ambayo hupandwa katika mioyo ya vijana. Anaifanya kukua na kuzaa matunda, na karibuni mavuno mengi ya udanganyifu/ukafiri yatavunwa. {8T 305.2}

Ni kwa sababu moyo wa mwanadamu unaelekea kwenye uovu ndio maana kuna hatari kubwa sana katika kupanda mbegu za mashaka katika akili za vijana. Chochote kinachodhoofisha imani kwa Mungu, kinainyima roho nguvu ya kupinga majaribu. Huondoa kinga pekee ya Kweli dhidi ya dhambi. {8T 305.3}

Hatupaswi kuanzisha shule za falsafa za kisomi au kwa ajili ya kile kinachoitwa "elimu ya juu." Umuhimu wetu umo ndani ya kumheshimu Mungu kwa uzoefu sahili, wa kiutendaji katika maisha ya kila siku. Tunahitajika kutembea pamoja na Mungu, ili kumleta ndani ya mioyo yetu na nyumba zetu. {8T 305.4}

## Waandishi Wakana Mungu

Wengi wanadhani kuwa ili kupata elimu ni lazima kusoma wanachozalisha waandishi ambao hufundisha kumkana Mungu, kwa sababu kazi zao hubeba vito fulani angavu vya fikra. Lakini ni nani aliyekuwa mwanzilishi wa vito hivi vya fikra? Alikuwa ni Mungu, na Mungu peke Yake. Yeye ndiye chanzo cha nuru yote. Kwa nini tupite katika wingi wa makosa yaliyomo katika kazi za wapagani na wakana Mungu, kwa sababu ya kweli chache tu za kisomi, wakati Ukweli wote uko chini ya uwezo wetu? {8T 306.1}

Kuna sababu kwa nini watu hawa wakati mwingine huonesha hekima ya kusifika. Shetani mwenyewe alielimishwa katika nyua za mbinguni, na anao ujuzi wa mema na pia wa maovu. Anachanganya vitu vya thamani na viovu, na hili ndilo humpa uwezo wa kudanganya. Lakini je! kwa sababu Shetani amejivika mavazi ya nuru ya mbinguni, tunaweza kumpokea kama malaika wa nuru? Mjaribu ana mawakala wake, walioelimika kulingana na mbinu zake, wanaotiwa msukumo na roho yake, na kurekebishwa/kuratibiwa kwa ajili ya kazi yake. Je! tutashirikiana nao? Je! tutapokea kazi za mawakala wake kama za muhimu kwa ajili ya kupata elimu? {8T306.2}

"Ni nani awezaye kutoa kitu kilicho safi kitoke katika kitu kichafu? Hapana awezaye." Ayubu14:4. Je! Tunaweza basi kutarajia vijana kudumisha kanuni za Kikristo na kukuza tabia ya Kikristo wakati elimu yao kwa upana huathiriwa na mafundisho ya wapagani, wakana-Mungu, na makafiri? {8T 306.3}

Kama muda na juhudi zilizotumika kutafuta kuyafahamu maoni mazuri ya wakana-Mungu ungetumika katika kusoma mambo ya thamani katika Neno la Mungu, maelfu ambao sasa wanakaa gizani na katika uvuli wa mauti wangekuwa wanashangilia katika utukufu wa Nuru ya uzima. {8T 306.4}

## Maarifa ya Mapokeo ya Kihistoria na Kiteolojia

Wengi wanaotafuta maandalizi kwa kazi ya Bwana wanafikiri ni muhimu kukusanya idadi kubwa ya maandishi/magombo ya kihistoria na ya kiteolojia. Wanadhani kuwa kujifunza kazi hizi kutakuwa kwa manufaa makubwa kwao katika kujifunza jinsi ya kuwafikia watu. Hili ni kosa. Ninavyoona rafu/shelfu zikiwa zimerundikwa na vitabu hivi, baadhi vikiwa hata havisomwi, ninawaza: Kwa nini utumie pesa kwa ambacho si chakula? Sura ya sita ya Yohana inatuambia mengi kuliko vinavyoweza kupatikana katika kazi kama hizo. Kristo anasema: "Mimi Ndimi Chakula cha Uzima." "Maneno hayo niliyowaambia, ni roho, tena ni uzima." Yohana 6:35, 63. {8T 307.1}

Kuna uchunguzi wa historia ambao haupaswi kulaumiwa. Historia takatifu ilikuwa ni moja ya masomo katika shule za manabii. Katika rekodi ya kushughulika Kwake na mataifa nyayo za Yehova zilitambuliwa. Hivyo leo tunapaswa kuzingatia kushughulika kwa Mungu na mataifa ya dunia. Tunapaswa kuona ndani ya historia utimilizaji wa unabii, kujifunza utendaji wa majaliwa katika vuguvugu kuu za matengenezo, na kuelewa maendeleo ya matukio katika kujipanga kwa mataifa kwa ajili ya vita ya mwisho katika Pambano Kuu. {8T 307.2}

Lakini mara nyingi nia ya wale wanaosoma vitabu hivi vingi haiku sana kwa ajili ya kupata chakula cha akili au roho. Ni tamaa ya makuu katika kufahamiana na wanafalsafa na wanateolojia, tamaa ya kuwasilisha Ukristo kwa watu kwa maneno na kauli za kisomi. {8T 307.3}

"Jifunzeni kutoka Kwangu," alisema Mwalimu mkuu kabisa ulimwenguni uliyewahi kumjua. Jitieni nira Yangu, jifunzeni upole Wangu na unyenyekevu." Kiburi chako cha usomi hakitasaidia katika kazi ya kuwasiliana na roho ambazo zinaangamia kwa kukosa chakula cha uzima. Katika kusoma kwako vitabu hivi unaviruhusu kuchukua nafasi, akilini na moyoni, masomo ya kivitendo ambayo unapaswa kujifunza kutoka kwa Yule Mwalimu Mkuu. Matokeo ya kujifunza huku watu hawalishwi. Sehemu kidogo sana ya uchunguzi na utafiti ambao ni unachosha sana akili hutoa kitu chochote ambacho kitamfanya mtu kuwa mtendakazi anayefanikiwa kwa ajili ya roho. {8T 307.4}

Wanaume na wanawake ambao hutumia maisha yao kufanya kazi duni za kimasikini, nyenyekevu, za kawaida huhitaji Maneno sahili kama Kristo aliyoyatoa katika masomo Yake, maneno ambayo yanaeleweka kwa urahisi. Mwokozi alikuja "kuhubiri injili kwa masikini." Na imeandikwa kuwa "watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha." Wale ambao wanafundisha Ukweli wa sasa kwa ajili ya wakati huu wanahitaji ufahamu wa kina juu ya masomo ambayo ameyatoa. {8T 308.1}

Maneno ya Mungu aliye Hai yako juu kabisa ya elimu zote. Misemo iliyodhamiriwa na kukusudiwa kuvutia akili ya wale waliopaswa kutakaswa hukosa kufikia lengo. Wale wanaowahudumia watu wanapaswa kula chakula cha uzima. Hiki kitawapa nguvu za kiroho; Kisha watakuwa tayari kuwahudumia watu wa tabaka zote.

UchaMungu, nguvu ya kiroho ya kanisa hudumishwa kwa kujilisha chakula ambacho kilishuka kutoka mbinguni. Miguuni pa Yesu tunapaswa kujifunza unyenyekevu wa utauwa wa Kweli. {8T 308.2}

### Visasili na Hadithi za Uongo (Myths and Fairytales --Hekaya za mapokeo za watoto kuhusu maajabu au uchawi/magic, mafumbo nk)

Katika elimu ya watoto na vijana, hadithi za uongo, visasili, na visa vya kubuni vinatolewa kwa sehemu kubwa sasa. Vitabu vya jinsi hii hutumiwa shuleni, na vinapatikana katika nyumba nyingi. Inakuwaje wazazi Wakristo wanaruhusu watoto wao kutumia vitabu vilivyojazwa na uwongo? Pale watoto wanapouliza maana ya hekaya ambazo ni kinyume kabisa na mafundisho ya wazazi wao, jibu ni kwamba hadithi hizi si za kweli; lakini hii haiondoi matokeo mabaya ya matumizi yake. Mawazo yanayowasilishwa katika vitabu hivi huwapotosha watoto. Yanaingiza mitazamo ya uongo juu ya maisha na huzaa na kukuza hamu juu ya mambo yasiyo halisi (Mifano ya Fairy tales maarufu ni kama bibi kwingwi, cinderela au bibi majivu, mbilikimo saba na Alice, bibi tarabushi, sungura na mazimwi, alfulela ulela, pinokio nk) . {8T 308.3}

Matumizi yaliyosambaa ya vitabu kama hivyo katika wakati huu ni mojawapo ya hila za werervu za Shetani. Anajitahidi kupotosha mawazo ya wazee na vijana kutoka kwenye kazi kubwa ya maandalizi ya mambo yanayokuja juu ya ulimwengu. Anakusudia kwamba watoto wetu na vijana wapate kusombwa na madanganyo yanaoharibu roho ambayo kwayo anaujaza ulimwengu (mafuriko ya uongo). Kwa hiyo anajitahidi kugeuza mawazo yao kutoka kwenye Neno la Mungu, na hivyo kuwazuia kupata maarifa ya Kweli zile ambazo zingekuwa kinga yao. {8T 309.1}

Kamwe vitabu vyenye upotoshaji wa Ukweli visiwekwe mbele ya watoto au vijana. Na kama hao wenye akili zilizopevuka wasingejihusisha kabisa na vitabu kama hivyo, wangekuwa salama zaidi. {8T 309.2}

### Chemchemi Iliyo Safi Zaidi

Tunavyo vingi ambavyo ni halisi, vile ambavyo ni vitakatifu. Wale wenye kiu ya maarifa hawana haja ya kwenda kwenye chemchemi zilizochafuka. {8T 309.3}

Kristo aliwasilisha kanuni za Ukweli katika injili. Katika mafundisho Yake tunaweza kunywa kutoka kwenye vijito safi vinavyotiririka toka katika kiti cha enzi cha Mungu. {8T 309.4}

Kristo angeweza kuwapa wanadamu maarifa ambayo yangezidi ufunuo wowote wa hapo awali na kuweka katika usuli kila ugunduzi mwingine. Yeye Angeweza kufunua siri baada ya siri, na angeweza kukusanya pamoja kuzunguka mafunuo haya ya

ajabu wazo hai, la dhati katika vizazi vinavyofuatana hadi mwisho wa wakati. Lakini hangeacha hata kidogo kufundisha maarifa ya sayansi ya wokovu. Muda Wake, akili Zake, maisha Yake yenyewe, yalithaminiwa na kutumika tu kama njia ya kufanya kazi ya wokovu wa roho za watu. Yeye Alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea, na Hangegeuzwa kutoka kwenye kusudi hili. Hakuruhusu chochote kumpotosha au kuchukua akili Yake. {8T 309.5}

Kristo alitoa ujuzi ule tu ambao ungeweza kutumika. Mafundisho Yake kwa watu yalifungamanishwa na mahitaji ya hali yao wenyewe katika maisha ya kawaida. Udadisi ambao uliwaongoza kumjia na maswali ya upelelezi, Yeye hakuuridhia (hakuuendekeza). Kwa maswali yote ya namna hiyo alitengeneza kuwa fursa kwa ajili ya wito makini, wa dhati, muhimu wa uzima. Kwa wale ambao walikuwa na hamu kubwa ya kuchuma kutoka kwenye mti wa maarifa, Yeye aliwapa matunda ya mti wa uzima. Walikuta kila njia imefungwa, isipokuwa njia nyembamba inayoongoza kwa Mungu. Kila chemchemi ilifungwa, isipokuwa chemchemi ya uzima wa milele. {8T 310.1} Mwokozi wetu hakumhimiza mtu yeyote kuhudhuria katika shule za marabi za wakati Wake, kwa sababu hiyo akili zao zingeharibiwa kwa kile kilichorudiwa kila wakati, "Wanasema," au, "Imesemwa." Kwa nini basi, sisi tupaswe kukubaliana na maneno ya watu yasiyo thabiti au mashiko, kuwa ni hekima iliyoinuliwa, wakati hekima kubwa zaidi ipo chini ya uwezo wetu? {8T 310.2}

Yale ambayo nimeyaona kuhusu mambo ya milele, na yale ambayo nimeyaona kuhusu uovu wa wanadamu, kama vile Mungu alivyoyasilisha mbele yangu, yameivutia sana akili yangu na kuyashawishi maisha yangu na tabia yangu. Sioni kitu chochote ambacho kwacho mwanadamu anapaswa kuinuliwa au kusifiwa au kutukuzwa. Sioni sababu yoyote kwa nini mwanadamu ainuliwe au asifiwe au atukuzwe. Sioni sababu yoyote kwa nini maoni ya watu wenye hekima ya ulimwengu yaaminiwe na kuinuliwa. Je, inakuwaje wale ambao ni fukara wa elimu ya Kiungu wawe na mawazo sahihi kuhusu mipango na njia za Mungu? {8T 310.3}

Mimi niko tayari kufundishwa na Yeye aliyeziumba mbingu na nchi, na Yeye aliyeweka nyota katika mpangilio wake katika anga na kuagiza jua na mwezi kufanya kazi yao. Sihitaji kwenda kwa waandishi makafiri au wakana-Mungu. Ninachagua kufundishwa na Mungu. {8T 310.4}

## Elimu ya Moyo

Ni sahihi kwa vijana kujisikia kuwa ni lazima wafikie ukuaji wa juu kabisa wa nguvu zao za kiakili. Hatutazuia elimu ambayo Mungu hajaiwekea kikomo. Lakini mafanikio yetu hayatasaidia chochote kama hayatatumika kwa ajili ya kumheshimu Mungu na kwa faida ya wanadamu. Isipokuwa tu pale maarifa yetu ni ngazi ya ufanikishaji wa malengo ya juu kabisa, hayatakuwa na thamani. {8T 311.1}

Tunachohitaji ni maarifa ambayo yataimarisha akili na roho, ambayo yatatufanya tuwe wanaume na wanawake bora. {8T 311.2}

Elimu ya moyoni ni ya muhimu zaidi kuliko elimu inayopatikana katika vitabu. Ni vema, tena muhimu, kupata maarifa ya ulimwengu tunaoishi; lakini ikiwa tutauacha umilele nje ya hesabu zetu, tutashindwa kiasi cha kutoweza kupona kamwe. {8T 311.3}

Si vyema kuijaza akili na jamii ya masomo ambayo huhitaji matumizi ya nguvu nyingi, lakini hayatumiki katika maisha ya kawaida. Elimu ya namna hii itakuwa ni hasara kwa mwanafunzi. Kwa maana masomo haya huondoa hamu yake na mwelekeo wa masomo ambayo yangemwandaa kwa ajili ya kuleta manufaa zaidi na kumwezesha kutekeleza majukumu yake. {8T 311.4}

Kama vijana wangeelewa udhaifu wao, wangetafuta toka kwa Mungu nguvu zao. Kama wakitafuta kufundishwa Naye, watakuwa wenye hekima katika hekima Yake, na maisha yao yatakuwa yenye matunda ya baraka kwa ulimwengu. Lakini ikiwa watasalimisha akili zao kwa elimu ya kidunia na ya kukisia tu, na hivyo kujitenga na Mungu, watapoteza yote yanayositawisha na kurutubisha maisha. {8T 311.5}

## SURA YA 47
## UMUHIMU WA KUTAFUTA MAARIFA YA KWELI

Zaidi sana ya vile tufanyavyo, tunahitaji kuelewa masuala yaliyo hatarini katika pambano ambalo tunahusika. Tunahitaji kuelewa kikamilifu zaidi thamani ya Kweli ambazo Mungu amezitoa kwa ajili ya wakati huu na hatari ya kuruhusu akili zetu kugeuzwa na mdanganyifu mkuu kutoka kwenye Kweli hizo. {8T 312.1}

Thamani kubwa sana ya kafara iliyohitajika kwa ajili ya ukombozi wetu inaonesha ukweli/uhalisia kwamba dhambi ni uovu mkubwa sana. Kupitia dhambi mwili mzima wa kiumbe mwanadamu umeharibika, akili imepotoshwa, imeondolewa katika njia, mawazo yameharibiwa. Dhambi imevuruga welekevu wa roho. Majaribu kutoka nje hupata upatanifu ndani ya moyo, na miguu inaelekea uovu bila kutambua. {8T 312.2}

Kama kafara kwa niaba yetu ilivyokuwa kamili, ndivyo urejeshwaji wetu kutoka katika unajisi wa dhambi unapaswa kuwa kamili. Hakuna tendo la uovu ambalo

sheria italisamehe; hakuna udhalimu wowote ambao utaepuka hukumu Yake. Maisha ya Kristo yalikuwa utimilifu kamili wa kila agizo la sheria. Alisema; "Kama vile Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu." Yohana 15:10. Maisha Yake ndio kiwango chetu cha utii na huduma. {8T 312.3}

Mungu peke Yake Ndiye anayeweza kuufanya upya moyo. "Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema." Lakini tumeambiwa: "utimizeni wokovu wenu wenyewe." Wafilipi 2:13, 12. {8T 312.4}

### Kazi Inayohitaji Mawazo Yetu

Makosa hayawezi kusahihishwa, wala matengenezo ya tabia hayawezi kufanyika, kwa juhudi chache dhaifu, za vipindi vya hapa na pale. Utakaso ni kazi, sio ya siku moja, au ya mwaka moja, bali ni ya maisha yote. Pambano kwa ajili ya ushindi dhidi ya nafsi, kwa ajili ya utakatifu na mbingu, ni pambano la maisha yote. Pasipo juhudi endelevu na kazi ya siku zote hayawezi kutokea maendeleo katika maisha matakatifu, taji ya mshindi haitapatikana. {8T 312.5}

Ushahidi wenye nguvu zaidi wa anguko la mwanadamu kutoka hali ya juu ni Ukweli kwamba inagharimu mno, kurejea. Njia ya kurejea inaweza kupatikana tu kwa mapigano makali, kidogo kidogo, kila saa. Kwa tendo la mara moja la dhamira, mtu anaweza kujiweka chini ya uwezo wa uovu; lakini inahitaji zaidi ya tendo la mara moja la dhamira kuvunja pingu hizi na kufikia maisha ya juu, yaliyo matakatifu. Kusudi linaweza kutengenezwa, kazi ikaanza; lakini ukamilishaji wake utahitaji kazi ngumu, muda, na uvumilivu, subira na kujitoa mhanga. {8T 313.1}
Pamoja na kuzungukwa na kushambuliwa na majaribu yasiyo na idadi, lazima tuyapinge kwa uthabiti la sivyo tushindwe. Kama tutafikia mwisho wa maisha bila kuifanya kazi yetu, itakuwa ni hasara ya milele. {8T 313.2}

Utakaso wa Paulo ulikuwa ni matokeo ya pambano la kila siku na nafsi. Alisema: "Ninakufa kila siku." 1 Wakorintho 15:31. Mapenzi yake na tamaa zake kila siku yalipingana na wajibu na mapenzi ya Mungu. Badala ya kufuata mwelekeo wake, alifanya mapenzi ya Mungu, hata kama ilisulubisha asili yake mwenyewe kiasi gani. {8T 313.3}

Mungu huwaongoza watu Wake hatua kwa hatua. Maisha ya Kikristo ni vita na gwaride la kusonga mbele safari. Katika vita hivi hakuna kuachia; juhudi lazima ziwe endelevu na zenye kuvumilia. Ni kwa jitihada zisizokoma ndipo tutadumisha ushindi

dhidi ya majaribu ya Shetani. Uadilifu wa Kikristo lazima utafutwe kwa nguvu isiyoweza kukinzika na kudumishwa kwa uthabiti wa kusudi ulioamuliwa. {8T 313.4}

Hakuna hata mmoja atakayebebwa juu pasipo kuwa na juhudi isiyo na huruma, yenye kuumilia kwa ajili ya nafsi yake yeye mwenyewe. Wote ni lazima kushiriki katika vita hivi kwa ajili yao wenyewe wakinuia. Kama mtu mmoja mmoja tunawajibika katika suala la pambano; ijapokuwa Nuhu, Ayubu, na Danieli walikuwa katika nchi, wasingeweza kumwokoa mwana au binti kutokana na haki yao. {8T 313.5}

## Sayansi Inayopaswa Kueleweka vyema (Sayansi dhati, Ya kweli)

Ipo sayansi ya Ukristo inayopaswa kufahamika kwa undani, - sayansi iliyo ya kina zaidi, yenye upana, iliyo ya juu kuliko sayansi yoyote ya kibinadamu kama mbingu zilivyo juu kuliko dunia. Akili inapaswa kunidhamishwa, kuelimishwa, kufunzwa; kwa sababu tunapaswa kumtumikia Mungu kwa njia ambazo hazipatani na mwelekeo wa asili. Zipo tabia za kurithi na mazoea yaliyokuzwa katika uovu ambayo ni lazima tuyashinde. Mara nyingi mafunzo na elimu iliyopatikana katika maisha ya mtu lazima iachwe, ili mtu huyo apate kuwa mwanafunzi katika shule ya Kristo. Mioyo yetu inabidi kuelimishwa ili ipate kuwa thabiti ndani ya Mungu. Tunapaswa kutengeneza mazoea ya fikira ambayo yatatuwezesha kupinga majaribu. Ni lazima tujifunze kutazama juu. Kanuni za Neno la Mungu - kanuni zilizo juu kama mbingu, na ambazo huenea kufikia umilele -- tunapaswa kuzielewa kwa jinsi zinavyohusika na maisha yetu ya kila siku. Kila tendo, kila neno, kila wazo, linapaswa kukubaliana na kanuni hizi. {8T 314.1}

Neema za thamani za Roho Mtakatifu hazikuzwi ndani ya muda mfupi. Ujasiri, uvumilivu, upole, imani, tumaini lisiloyumba katika uweza wa Mungu wa kuokoa, hupatikana kwa uzoefu wa miaka mingi. Kwa maisha ya bidii takatifu na uaminifu uthabiti katika Kweli, na usahihi, watoto wa Mungu watapaswa kuwekea muhuri hatima yao. {8T 314.2}

## Hakuna Muda wa Kupoteza

Hatuna wakati wa kupoteza. Hatufahamu ni kwa haraka kiasi gani hukumu yetu ya upelelezi itafungwa (mlango wa rehema utafungwa). Umilele unakaribia mbele yetu. Pazia linakaribia kuinuliwa. Kristo Yu karibu kuja. Malaika wa Mungu wanatafuta namna ya kutuvutia kutoka katika nafsi zetu wenyewe na kutoka kwenye mambo ya dunia. Hebu wasifanye kazi hii bure. {8T 314.3}

Yesu atakapoinuka kutoka Patakatifu pa Patakatifu, na kuyavua mavazi Yake ya upatanisho, na kujivika mavazi ya kisasi, amri itatolewa: “Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa.” "Tazama, Naja upesi, na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.” Ufunuo 22:11, 12. {8T 315.1}

Dhoruba isiyo na huruma inakuja katika ghadhabu yake. Je! Tumejiandaa kukutana nayo? {8T 315.2}

Hatupaswi kusema: Hatari kubwa za siku za mwisho karibu zitakuja juu yetu. Tayari zimekuja. Tunahitaji sasa upanga wa Bwana ukate ndani hasa ya roho na ndani ya tamaa za mwili, hamu, na uchu. {8T 315.3}

Akili ambazo zimesalimishwa kwa mawazo huru zinahitajika kubadilika. "Kwa hiyo vifungeni viuno vya nia zenu, na kuwa na kiasi; mkiitumainia kwa utimilifu ile neema mtakayoletewa katika ufunuo Wake Yesu Kristo. Kama watoto wa kutii msijifananishe na tamaa zenu za kwanza za ujinga wenu; bali kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa Mimi ni mtakatifu." 1 Petro 1:13-16. Mawazo lazima yaelekezwe kwa Mungu. Sasa ndio wakati wa kuweka bidii kushinda mielekeo ya asili ya kimwili. {8T 315.4}

Jitihada zetu, kujikana kwetu nafsi, uvumilivu wetu, lazima ulingane na thamani kubwa ya kitu kile ambacho tunakitafuta. Ni kwa kushinda tu kama vile Kristo alivyoshinda ndipo tutaipata taji ya uzima. {8T 315.5}

**Haja ya Kujikana Nafsi**

Hatari kubwa ya mwanadamu iko katika kujidanganya mwenyewe, kujipa utoshelevu binafsi, na hivyo kujitenga na Mungu, chanzo cha nguvu zake. Mielekeo yetu ya asili, isipokuwa imerekebishwa na Roho wa Mungu, ina mbegu ndani yake za kifo cha maadili. Isipokuwa tumeunganishwa kwa nguvu na Mungu, sisi hatuwezi kuipinga athari mbaya za kujipenda nafsi, anasa, na jaribu la kutenda dhambi. {8T 315.6}

Ili kupokea msaada kutoka kwa Kristo, ni lazima tutambue hitaji letu. Lazima tuwe na maarifa ya kweli kuhusu sisi wenyewe. Ni yule tu ambaye anajifahamu kuwa ni mwenye dhambi ambaye Kristo anaweza kumwokoa. Ni pale tu tutakapoona kutokujiweza kwetu kabisa na kukana kujitumainia nafsi kote, ndipo tutakapoweza kuushikilia uweza wa Mwenyezi Mungu. {8T 316.1}

Si tu mwanzoni mwa maisha ya Kikristo ndipo ukanaji huu wa nafsi unapaswa kufanywa. Katika kila hatua ya mbele kuelekea mbinguni tupaswa kufanya upya ukanaji huu wa nafsi tena. Kazi zetu zote nzuri hutegemea uwezo ulio nje yetu; hivyo kuna haja ya moyo kuendelea kumtafuta Mungu daima, kukiri dhambi mara kwa mara na kwa bidii kuinyenyekesha roho mbele Yake. Hatari kubwa zinatuzunguka; na tuko salama pale tu tunapohisi udhaifu wetu na kumng'ang'ania Mwokozi wetu Mwenye nguvu kwa mkono wa imani. {8T 316.2}

## Masilahi ya Juu Zaidi Huhitaji Umakini

Lazima tugeuke na kuacha mada (topic) maelfu ambazo zinavuta usikivu wetu. Kuna mambo ambayo hutumia muda mwingi na nguvu na kuamsha uchunguzi, lakini huishia kukosa maana. Masilahi ya hali ya juu huhitaji usikivu wa karibu na nguvu ambazo mara nyingi sana hutolewa kwa vitu ambavyo kwa kulinganisha havina maana. {8T 316.3}

Kukubali nadharia mpya hakuleti maisha mapya rohoni. Hata kuwa na maarifa ya mambo ya hakika na nadharia ambazo zina umuhimu ndani yake ni za thamani ndogo isipokuwa tu zimewekwa katika matumizi ya busara. Tunahitajika kuhisi wajibu wetu wa kuzipa roho zetu chakula ambacho kitasitawisha na kuchochea maisha ya kiroho. {8T 316.4}

## Kumjua Kristo Binafsi

"Kila Neno la Mungu limehakikishwa; Yeye ni ngao yao wamwaminio. Usiongeze neno katika Maneno Yake; Asije akakulaumu, ukaonekana u mwongo." Mithali 30:5, 6. {8T 316.5}

Hatufanyi mapenzi ya Mungu pale tunapokisia juu ya mambo ambayo ameona ni vyema kuyazuia kwetu. Swali ambalo tunapaswa kujifunza ni: "Ukweli ni nini, Ukweli kwa ajili ya wakati huu, ambao unapaswa kuhifadhiwa, kupendwa, kuheshimiwa na kutiiwa?" Wafuasi waliojitoa kwa sayansi wameshindwa na kuvunjika moyo katika jitihada zao za kumgundua, kumtafuta au kumpata Mungu. Wanachohitaji kuuliza kwa wakati huu ni: "Je! Ni ukweli upi utakaotuwezesha kuupata wokovu wa roho zetu?" {8T 317.1}

Kristo alimfunua Mungu kwa wanafunzi Wake kwa namna ambayo ilifanya kazi ya pekee mioyoni mwao, kama ile ambayo kwa muda mrefu amekuwa akitusihi tumruhusu apate kuifanya mioyoni mwetu. Wapo wengi ambao, kwa kuzingatia sana nadharia, wameusahau uweza Hai wa mfano wa Mwokozi. Wamemsahau Yeye kama mfanyakazi Mnyenyekevu, Mwenye kujikana nafsi. Wanachohitaji ni kumtazama Yesu. Kila siku tunahitaji udhihirisho mpya wa uwapo Wake. Tunahitaji

kufuata kwa karibu zaidi mfano Wake wa kujikana nafsi na kujitoa. {8T 317.2}

Tunahitaji uzoefu ambao Paulo alikuwa nao alipoandika: "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo Yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, Ambaye alinipenda, akajitoa nafsi Yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2:20. {8T 317.3}

Maarifa kumhusu Mungu na Yesu Kristo yanayooneshwa katika tabia ni utukufu ulio juu ya kila kitu kingine ambacho kinatukuzwa duniani au mbinguni. Ndio elimu hasa ya juu kabisa. Ni ufunguo unaofungua milango ya jiji la mbinguni. Maarifa haya ni kusudi la Mungu kwamba wote wanaomvaa Kristo wapate kuyamiliki. {8T 317.4}

Kwa wachungaji wetu, matabibu, walimu, na wengine wote wanaohusika katika safu yoyote ya huduma kwa Bwana, ninao ujumbe wa kuutoa. Bwana anawaamuru mje juu zaidi, kufikia kiwango kitakatifu zaidi. Lazima mwe na uzoefu wa kina zaidi ya ule ambao hata hamjafikiria kuwa nao. Wengi ambao tayari ni washiriki wa familia kubwa ya Mungu wanajua kidogo tu juu ya maana ya kuona utukufu Wake na kubadilishwa toka utukufu hata utukufu. Wengi wenu mna utambuzi wa utusiutusi juu ya ubora wa Kristo, na mioyo yenu inasisimka kwa furaha. Mnatamani sana kupata hisia kamili zaidi, yenye kina zaidi ya upendo wa Mwokozi. Hamjaridhika. Lakini msikate tamaa. Mpeni Yesu mapenzi bora na matakatifu zaidi ya moyo. Thaminini kila mwale wa nuru. Thaminini kila hamu ya roho kumtafuta Mungu. Jipeni elimu ya mawazo ya kiroho na mazungumzo matakatifu. Mmeona miale ile tu ya kwanza ya alfajiri ya utukufu Wake. Mnapoendelea kumjua Bwana, mtagundua ya kwamba kwenda Kwake mbele ku tayari kama asubuhi. "Bali njia ya wenye haki ni kama nuru ing'aayo, Ikizidi kung'aa hata mchana mkamilifu." Mithali 4:18. Tukiwa tumekwisha kutubu dhambi zetu, na kuziungama, na kupata msamaha, tunapaswa kuendelea kujifunza juu ya Kristo hadi tutakapofikia nuru kamili ya imani kamilifu ya injili. {8T 317.5}

## SURA YA 48
## MAARIFA YANAYOPOKELEWA KUPITIA KWA NENO LA MUNGU

Biblia yote ni ufunuo wa utukufu wa Mungu katika Kristo. Ikipokelewa, na kuaminiwa, na kutiiwa, inakuwa ni wakala mkuu katika kuibadilisha tabia. Na ndio njia pekee ya uhakika ya elimu ya kiakili. {8T 319.1}

Sababu inayowafanya vijana, na hata wale walio na umri wa utu uzima, kuongozwa kwa urahisi katika majaribu na dhambi ni kwamba hawajifunzi Neno la Mungu na kulitafakari kama inavyostahili. Ukosefu wa nguvu thabiti, utashi usioyumba, ambao

hudhihirika katika maisha na tabia, hutokana na kupuuza kwao mafundisho matakatifu ya Neno la Mungu. Hawaelekezi akili zao kwa bidii kwa yale ambayo yangechochea na kuhuisha mawazo safi, matakatifu na kuziondoa kutoka kwenye uchafu na uongo. Kuna wachache wanaochagua sehemu njema, ambao huketi miguuni pa Yesu, kama Mariamu, kujifunza kutoka kwa Mwalimu wa kiungu. Wachache huweka hazina ya Maneno Yake moyoni na kuyatenda maishani. {8T 319.2}

Kweli za Biblia, zilizopokelewa, zitaiinua akili kutoka katika unyonge wake na udhilifu wake. Ikiwa Neno la Mungu lingethaminiwa kama inavyopasa, wote vijana na wazee wangekuwa na uadilifu wa ndani, nguvu ya kanuni, ambayo ingewawezesha kupinga majaribu. {8T 319.3}

Hebu watu wafundishe na kuandika vitu vya thamani vya Maandiko Matakatifu. Hebu mawazo, vipaji, matumizi ya bidii ya akili, yaelekezwe katika kujifunza mawazo/kusudi la Mungu. Usisome falsafa na dhana za wanadamu, lakini jifunze falsafa ya Yeye ambaye ni Kweli. Maandiko mengine ni yenye thamani ndogo yakilinganishwa na hayo. {8T 319.4}

Akili ambayo ni ya kidunia haifurahii kutafakari Neno la Mungu; lakini kwa akili iliyofanywa upya na Roho Mtakatifu, uzuri wa Kiungu na nuru wa mbingu huangaza kutoka katika kurasa takatifu. Ile ambayo kwa akili ya kidunia ilikuwa jangwa lenye ukiwa, kwa akili ya kiroho inakuwa nchi yenye mito hai. {8T 319.5}

### Wapewe Watoto Wetu

Maarifa ya Mungu kama yanavyofunuliwa katika Neno Lake ndio maarifa yanayopaswa kutolewa kwa watoto wetu. Kuanzia mwanzo kabisa wa kufikiri wanapaswa kufahamishwa jina na maisha ya Yesu. Somo la kwanza kabisa wanalopaswa kupewa ni kwamba **Mungu ni Baba yao.** Mafunzo yao ya kwanza kabisa yanapaswa kuwafundisha kutoa utii wa upendo. Kwa kicho na upole hebu Neno la Mungu lisomwe na kurudiwa kwao, katika vipande vinavyowafaa kwa ufahamu wao na kurekebishwa ili kuamsha shauku yao. Zaidi ya yote, hebu wajifunze juu ya upendo Wake uliofunuliwa ndani ya Kristo, na fundisho Lake kuu: {8T 320.1}

"Ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana." 1 Yohana 4:11. {8T 320.2}

Hebu vijana na walifanye Neno la Mungu kuwa chakula cha akili na roho. Hebu msalaba wa Kristo ufanywe kuwa sayansi ya elimu yote, kitovu cha mafundisho yote na masomo yote. Hebu na liletwe katika uzoefu wa kila siku katika maisha ya kiutendaji. Hivyo Mwokozi atakuwa kwa vijana mwenzi na rafiki wa kila siku. Kila wazo litatekwa katika utii wa Kristo. Pamoja na mtume Paulo wataweza kusema: {8T 320.3}

“Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu cho chote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu.” Wagalatia 6:14. {8T 320.4} 321

## Maarifa ya Kiutendaji

Kwa hivyo kupitia imani watamjua Mungu kwa maarifa ya kivitendo. Wamejithibitishia wenyewe uhalisi wa Neno Lake, Ukweli wa ahadi Zake. Wameonja, na wamejua ya kuwa Bwana ni mwema. {8T 321.1}

Yohana mpendwa alikuwa na maarifa yaliyopatikana kupitia uzoefu wake binafsi. Hivyo alishuhudia: {8T 321.2}

"Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tulililoliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la uzima; (na uzima huo ulidhihirika, nasi tumeona, tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu); hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana Wake Yesu Kristo." 1 Yohana 1: 1-3. {8T 321.3}

Hivyo kila mtu anaweza, kupitia kwa uzoefu wake binafsi, "kutia muhuri ya kwamba Mungu ni Kweli." Yohana 3:33. Anaweza kutoa ushuhuda ambao yeye mwenyewe ameuona na kuusikia na kuuhisi juu ya uwezo wa Kristo- Anaweza kutoa ushahidi: {8T 321.4}

"Nilihitaji msaada, na nikaupata kwa Yesu. Kila haja ilitolewa/ilikidhiwa, njaa ya roho yangu ilitoshelezwa; kwangu Biblia ni ufunuo wa Kristo. Ninamwamini Yesu kwa sababu Yeye kwangu ni Mwokozi wa Kiungu. Ninaiamini Biblia kwa sababu nimeiona kuwa ni sauti ya Mungu kwa roho yangu." {8T 321.5}

## Fursa za Ajabu

Ni upendeleo kwetu kufika juu zaidi tena na tena kwa ajili ya mafunuo ya wazi ya tabia ya Mungu. Musa alipoomba, "Nakusihi unionyeshe utukufu Wako." (Kutoka 33:18), Bwana hakumkemea, lakini alimpa ombi lake. Mungu alimwambia mtumishi Wake: "Nitapitisha wema Wangu wote mbele yako, Nami nitalitangaza Jina la Bwana mbele Yako." Aya ya 19. {8T 321.6}

Ni dhambi ndiyo itiayo giza akili zetu na kufifiliza fahamu zetu. Dhambi inaposafishwa/inapokamuliwa kutoka katika mioyo yetu, nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo, inayoangaza Neno Lake na kuakisiwa kutoka

katika uso wa asili, kwa ukamilifu zaidi na zaidi zitamtangaza Yeye "Mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, Mwingi wa rehema na Kweli." Kutoka 34: 6. {8T 322.1}

Katika nuru Yake tutaona nuru, hadi akili na moyo na roho zibadilishwe kuwa katika mfano wa utakatifu Wake. {8T 322.2}

Uwezekano wa ajabu uko wazi kwa wale wanaoshikilia ahadi za Kiungu za Neno la Mungu. Kuna Kweli tukufu zitakazokuja mbele ya watu wa Mungu. Haki, fursa na wajibu ambavyo hata hawajadhani kuwa vipo katika Biblia vitawekwa wazi mbele yao. Wanapoendelea kufuata njia ya utii mnyenyekevu, wakifanya mapenzi Yake, watayafahamu zaidi na zaidi mashauri ya Mungu. {8T 322.3}

Hebu mwanafunzi achukue Biblia kama kiongozi wake na asimame kama mwamba katika kanuni, naye anaweza kuweka lengo la kufikia kimo chochote cha mafanikio. Falsafa zote zenye asili ya kibinadamu zimesababisha ghasia na aibu pale ambapo Mungu hajatambuliwa kama yote katika yote. Lakini imani ya thamani iliyoongozwa na Mungu inatoa nguvu na uadilifu wa tabia. Kadiri wema Wake, huruma Yake, na upendo Wake vinapofikiriwa sana na akili kukita hapo, ndivyo ufahamu wa Ukweli utavyokuwa wazi na wazi zaidi; hamu ya usafi wa moyo na usafi wa mawazo vitakuwa juu zaidi, mtakatifu zaidi. Nafsi inayokaa katika angahewa safi ya fikira takatifu hubadilishwa kwa maingiliano na Mungu kupitia katika kusoma Neno Lake. Ukweli unakuwa mkubwa sana, unaofikia mbali, wenye kina kirefu, mpana sana, kiasi kwamba nafsi inasahauliwa. Moyo unalainishwa na kutiishwa katika unyenyekevu, upole, wema na upendo. {8T 322.4}

Na nguvu za asili zinakuzwa kwa sababu ya utii mtakatifu. Kwa kusoma Maneno ya uzima, wanafunzi wanaweza kuja na akili zilizopanuliwa, zilizoinuliwa, zilizoadilishwa. Kama wakiwa, kama Danieli, wasikilizaji na watendaji wa neno la Mungu, wanaweza kuendelea kama alivyofanya katika matawi yote ya elimu. Wakiwa na nia safi, watakuwa imara. Kila uwezo wa kiakili utahuishwa. Hivyo wataweza kujielimisha na kujiadibisha wao wenyewe ili wote walio ndani ya uwanja wa ushawishi wao waweze kuona vile mwanadamu anavyopaswa kuwa, na kile anachoweza kufanya, pale anapounganishwa na Mungu wa hekima na uweza. {8T 323.1}

### Matokeo ya Kupokea Neno la Mungu

Huu ndio uzoefu ambao mwandishi wa Zaburi aliupata kupitia maarifa ya neno la Mungu. Anasema:
Heri walio kamili njia zao,
Waendao katika sheria ya Bwana.
Heri wazitiio shuhuda Zake,
Wamtafutao kwa moyo wote……. Ningependa

njia zangu ziwe thabiti,   Nizitii amri Zako.
Ndipo mimi sitaaibika,
Nikiyaangalia maagizo Yako yote.”
"Jinsi gani kijana aisafishe njia yake?
Kwa kutii, akilifuata Neno Lako."
"Nimeichagua njia ya uaminifu,
Na kuziweka hukumu Zako mbele yangu."
"Moyoni mwangu nimeliweka Neno Lako,
Nisije nikakutenda dhambi."
"Nami nitakwenda panapo nafasi,
Kwa kuwa nimejifunza mausia Yako."
"Unifumbue macho yangu niyatazame
Maajabu yatokayo katika sheria Yako."
"Shuhuda Zako nazo ndizo furaha yangu,
Na washauri wangu."
"Sheria ya kinywa Chako ni njema kwangu,
Kuliko maelfu ya dhahabu na fedha."
"Sheria Yako naipenda mno ajabu,
Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa."
"Amri Zako zimekuwa nyimbo zangu,
Katika nyumba ya ugeni wangu."
"Shuhuda Zako ni za ajabu,
Ndiyo maana roho yangu imezishika.
Kufafanusha Maneno Yako kwatia nuru,
Na kumfahamisha mjinga.”
“Maagizo Yako hunitia hekima kuliko adui zangu,  Kwa maana ninayo sikuzote.
Ninazo akili kuliko wakufunzi wangu wote,
Maana shuhuda Zako ndizo nizifikirizo.
Ninao ufahamu kuliko wazee,
Kwa kuwa nimeyashika mausia Yako. . . .
Kwa mausia Yako najipatia ufahamu,
Ndiyo maana naichukia kila njia ya uongo."

"Neno Lako limesafika sana,
Kwa hiyo mtumishi Wako amelipenda."
“Jumla ya Neno Lako ni Kweli,
Na kila hukumu ya haki Yako ni ya milele.”
“Wana amani nyingi waipendao sheria Yako,  Wala hawana la kuwakwaza.
Ee Bwana, nimeungojea wokovu Wako, Na maagizo Yako nimeyatenda.
Nafsi yangu imezishika shuhuda Zako,
Nami nazipenda mno."
“Ee Bwana, nimeutamani wokovu Wako,

Na sheria Yako ndiyo furaha yangu.
Nafsi yangu na iishi, ipate kukusifu,
Na hukumu Zako zinisaidie."
"Shuhuda Zako nimezifanya urithi wa milele,
Maana ndizo changamko la moyo wangu."
Zaburi 119: 1-6, 9, 30, 11, 45, 18, 24, 72, 97, 54, 129, 130, 98-104, 140, 160, 165-167, 174, 175, 111 {8T 323.2}

## Msaada katika Kujifunza Asili (Nature- 'Necha!')

Yeye aliye na maarifa ya Mungu na Neno Lake kupitia uzoefu binafsi tayari ameandaliwa kujishughulisha na somo la sayansi ya asili. Kuhusu Kristo imeandikwa: "Ndani Yake Ndimo ulimokuwa uzima, nao ule Uzima ulikuwa Nuru ya watu." Yohana 1:4. Wakati Adamu na Hawa walipopoteza mavazi ya utakatifu pale Edeni, walipoteza nuru iliyokuwa ikiimulika asili. Kamwe hawakuweza tena kuisoma vizuri. Lakini kwa wale wanaopokea nuru ya maisha ya Kristo, asili inamulikwa tena. Kwa nuru inayoangaza kutoka msalabani, tunaweza kutafsiri vyema mafundisho ya asili. {8T 324.1}

Yeye aliye na ufahamu wa Mungu na Neno Lake ana imani thabiti katika Uungu wa Maandiko Matakatifu. Mtu huyu haipimi Biblia kwa mawazo ya mwanadamu ya kisayansi. Analeta mawazo haya kwenye kipimo chenye viwango visivyo na makosa. Anafahamu kwamba Neno la Mungu ni Kweli, na Ukweli hauwezi kujipinga kamwe; Chochote katika mafundisho ya kile kinachoitwa sayansi kinachopingana na Ukweli wa ufunuo wa Mungu ni kazi ya mwanadamu ya kubahatisha tu. {8T 325.1}

Kwa wenye hekima hasa, utafiti wa kisayansi hufungua uwanja mpana wa fikira na taarifa. Njia za Mungu kama zinavyofunuliwa katika ulimwengu wa asili na katika namna anavyoshughulika na mwanadamu hubeba hazina ambayo kutoka humo kila mwanafunzi katika shule ya Kristo anaweza kuchota. {8T 325.2}

Ushahidi wa kweli wa Mungu aliye Hai haupo katika nadharia tu; ni katika usadikisho ambao Mungu ameuandika katika mioyo yetu, ukiangazwa na kuelezewa na Neno Lake. Ni katika uweza ulio hai wa kazi Zake alizoziumbwa, na kuonekana kwa jicho, ambalo Roho Mtakatifu ameliangazia. {8T 325.3}

Wale wanaomwona Mungu kutokana na kazi ya mikono Yake, na wala si kutokana kukisia kwa watu mashuhuri, wanaona uwapo Wake katika kila kitu. Wataona tabasamu Lake kwa mwanadamu katika uwanda wenye uwingi katika msimu wa kupukutisha. Hata mapambo ya dunia, nyasi za kijani kibichi, maua ya kupendeza ya kila rangi, miti mirefu anuwai ya msituni, kijito chenye kuchezacheza, mto mzuri, ziwa lililotulia, hushuhudia utunzaji wa Baba mwema, Mungu wetu na shauku Yake ya kutaka kuwafanya watoto Wake kuwa na furaha. {8T 325.4} 326

## Asili Ufunguo wa Siri za Kiungu (Zaburi 19)

Mwanafunzi anapotafakari hivyo mambo ya asili, mtazamo mpya wa Ukweli humjia. Mafundisho katika kitabu kikuu cha Mungu cha asili hutoa ushuhuda wa Kweli wa Neno lililoandikwa. {8T 326.1}

Katika mpango wa ukombozi kuna siri ambazo akili ya mwanadamu haiwezi kuelewa, mambo mengi ambayo hekima ya mwanadamu haiwezi kuelezea; lakini asili inaweza kutufundisha mengi juu ya siri ya utauwa. Kila kichaka, kila mti unaozaa matunda, mimea yote, ina masomo kwetu ya kujifunza. Katika ukuaji wa mbegu kunapasa kusomwa siri za Ufalme wa Mungu. {8T 326.2}

Kwa moyo uliolainishwa kwa neema ya Mungu, jua, mwezi, nyota, miti, maua ya kondeni, hutamka maneno ya ushauri. Kuotesha mbegu hupeleka akili katika upandaji wa mbegu ya kiroho. Mti unatangaza kwamba mti mzuri hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri. “Mtawatambua kwa matunda yao." Mathayo 7:16. Hata magugu yana somo. Ni pando la Shetani, na, kama yakiachwa bila kudhibitiwa, huiharibu ngano kwa ukuaji wake wa kutoa majani mengi. {8T 326.3}

Akina baba na akina mama, wafundisheni watoto wenu juu ya uweza wa Mungu utendao miujiza. Uweza Wake unaonekana katika kila mmea, katika kila mti ambao huzaa matunda. Wapeleke watoto kwenye bustani na uwaeleze jinsi Yeye anavyosababisha mbegu kukua. Mkulima analima shamba lake na hupanda mbegu, lakini hawezi kuifanya mbegu kukua. Lazima amtegemee Mungu kufanya kile ambacho hakuna uwezo wowote wa mwanadamu unaoweza kukifanya. Bwana huweka Roho Yake Mwenyewe ndani ya mbegu, na kuifanya kuchipua katika uhai. Chini ya uangalizi Wake, mbegu huvunjika kutoka kwenye kasha lake na kuchipuka ili kukua na kuzaa matunda. {8T 326.4}

Watoto wanapojifunza kitabu kikuu cha kiada cha asili, Mungu atavutia na kugusa akili zao. Wanapoambiwa kuhusu kazi ambayo Yeye huifanya kwenye mbegu, wanajifunza siri ya ukuaji katika neema. Kama yakieleweka kwa vyema, masomo haya huongoza kwa Muumbaji, yakifundisha kweli zile sahili, takatifu ambazo zinauleta moyo katika mawasiliano ya karibu na Mungu. (Vitabu vitatu vya Mungu-Biblia, Madhabahu na Asili) {8T 326.5}

## Somo la Utii

Sheria za Mungu kwa ajili ya asili hutiiwa na asili. Mawingu na dhoruba, jua na manyunyu, umande na mvua, vyote viko chini ya usimamizi wa Mungu na hutoa utii kwa amri Yake. Kwa kuitii sheria ya Mungu ncha ya chipukizi la nafaka huchomoza kutoka ardhini, "Kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke." Marko 4:28. Tunda huonekana kwanza kwenye kikonyo, na Bwana hulikuza katika msimu wake unaofaa kwa sababu haliipingi kazi Yake. Kwa hivyo ndege hutimiza kusudi la Mungu wanapohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine mbali wakati wa majira

tofauti, wakiongozwa kupita katika anga lisilo na njia kwa mkono wa uweza usio na kikomo. {8T327.1}

Je inawezekana mtu  kwamba, aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu, na kupewa akili na usemi, peke yake awe mwenye kukosa shukurani kwa karama Zake na kutotii sheria Zake? Je! Wale ambao wangeweza kuinuliwa na kuadilishwa, kuandaliwa wapate kufaa kuwa watenda kazi pamoja Naye, je waridhike kubaki na tabia isiyo kamilifu na kusababisha ghasia katika dunia yetu? Je! Miili na roho zilizonunuliwa na Mungu kuwa urithi izuiwe na tabia zinazowafunga na ulimwengu na mazoea yasiyo matakatifu? Je! Hawataakisi uzuri wa Yeye aliyefanya vitu vyote kuwa vyema, kwamba kwa kupitia neema Yake mtu asiye mkamilifu anaweza mwishowe kusikia Neno la Baraka toka Kwake: "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu.... ingia katika furaha ya Bwana Wako "? Mathayo 25:21. {8T 327.2}

Mungu anataka tujifunze kutoka kwenye asili somo la utii.
"Lakini sasa waulize hao wanyama, nao watakufundisha;  Na
nyuni wa angani, nao watakuambia;
Au nena na nchi, nayo itakufundisha;  Nao samaki wa baharini watakutangazia.
Katika hawa wote ni yupi asiyejua,
Kwamba ni mkono wa Bwana uliofanya haya?" Ayubu 12:7-9, 13

Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria Yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa.
"Heri mtu yule" ambaye "sheria ya Bwana ndiyo impendezayo...
Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji,
Uzaao matunda yake kwa majira yake,
Wala jani lake halinyauki;
Na kila alitendalo litafanikiwa." Zaburi 1:1-3. {8T 327.3}

Kitabu cha asili na Neno lililoandikwa humulika kila moja kwa mwenzake. Vyote viwili hutufanya tumfahamu vizuri Mungu na kwa kutufundisha tabia Yake na sheria ambazo Yeye huzitumia kufanya kazi. {8T 328.1}

## Elimu katika Maisha Yajayo

Elimu iliyoanza hapa duniani, haitakamilishwa katika maisha haya; itakuwa ikiendelea mbele kote katika umilele, daima ikisonga mbele bila  kukamilika kamwe. Siku kwa siku matendo ya ajabu ya Mungu, ushahidi wa uweza Wake wa kimiujiza katika kuumba na kuuhimili ulimwengu, yatafunguka katika akili kwa uzuri mpya. Katika nuru inayoangaza kutoka kwenye Kiti cha Enzi, siri zitatoweka, na roho zitajazwa na mshangao kwa usahili wa mambo ambayo hayakuwahi kufahamika

hapo kabla. {8T 328.2}

Sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana. {8T 328.3}

## SURA YA 49
## HITAJI LETU KUU

Maarifa ya Mungu ambayo hufanya mabadiliko ya tabia ndio hitaji letu kuu. Tukitimiza kusudi Lake, lazima kuwepo ufunuo wa Mungu katika maisha yetu ambao utaendana na mafundisho ya Neno Lake. {8T 329.1}

Uzoefu wa Henoko na wa Yohana Mbatizaji unawakilisha vile wetu unavyopaswa kuwa. Tofauti kabisa na tunavyofanya sasa, tunahitaji kujifunza maisha ya watu hawa - yule ambaye alihamishwa kwenda mbinguni bila kuona mauti, na yeye ambaye, kabla ya ujio wa kwanza wa Kristo, aliitwa kutengeneza njia ya Bwana, kuyanyosha mapito Yake. {8T 329.2}

### Uzoefu wa Henoko

Kuhusu Henoko imeandikwa kwamba aliishi miaka sitini na mitano naye akamzaa mtoto wa kiume; baada ya hapo alitembea na Mungu miaka mia tatu. Katika miaka

hiyo ya awali, Henoko alimpenda Mungu na kuwa na hofu ya Mungu, na alizishika amri Zake. Lakini baada ya kuzaliwa kwa mtoto wake wa kwanza wa kiume alifikia uzoefu wa hali ya juu; alivutwa katika uhusiano wa karibu zaidi na Mungu. Alivyoona upendo wa mtoto kwa baba yake, imani yake sahili kuhusu ulinzi wake; alivyohisi wema wa kina, wenye shauku wa moyo wake kwa mtoto huyo wa kwanza wa kiume, alijifunza somo la thamani la upendo wa ajabu wa Mungu kwa mwanadamu katika karama ya Mwanawe, na imani na ujasiri ambao kwa huo watoto wa Mungu wanaweza kupumzika kwa Baba yao wa mbinguni. Upendo usio na kifani wa Mungu kupitia Kristo ukawa somo la tafakuri yake mchana na usiku. Kwa bidii yote ya roho yake alijitahidi kuufunua upendo huo kwa watu aliokaa miongoni mwao. {8T 329.3}

Kutembea kwa Henoko pamoja na Mungu hakukuwa katika kupagawa au njozi, bali ni katika majukumu yote ya maisha yake ya kila siku. Hakuwa mtu wa kujitenga au utawa, au mwenye kujifungia kabisa mbali na ulimwengu; kwa kuwa katika ulimwengu, alikuwa na kazi ya kufanya kwa ajili ya Mungu. Katika familia na katika maingiliano yake na wanadamu, kama mume na baba, rafiki, raia, alikuwa mtumishi wa Mungu aliye thabiti, asiyeyumba. {8T 329.4}

Imani yake ilizidi kuimarika, upendo wake ukawa motomoto zaidi, kadiri karne zilivyopita. Kwake maombi yalikuwa kama pumzi ya roho. Aliishi katika angahewa ya mbinguni. {8T 330.1}

Wakati matukio ya siku za usoni yalipofunguliwa katika macho yake, Henoko akawa mhubiri wa haki, akiubeba ujumbe wa Mungu kwa wote ambao wangesikiliza maneno ya onyo. Katika nchi ambayo Kaini alijaribu kukimbia kutoka katika uwapo wa Mungu, nabii wa Mungu aliweka wazi matukio mazuri ambayo yalikuwa yamepitishwa katika maono yake. "Angalia," alisema, "Bwana anakuja na watakatifu Wake, maelfu maelfu ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu Yake." Yuda 14, 15. {8T 330.2}

Uweza wa Mungu uliofanya kazi pamoja na mtumishi Wake ulihisiwa na wale waliosikia. Baadhi walitilia maanani maonyo haya na kuziacha dhambi zao, lakini wengi walidhihaki ujumbe huo mzito. Watumishi wa Mungu wanapaswa kuubeba ujumbe kama huo kwa ulimwengu katika siku za mwisho, na utapokelewa pia kwa kutokuuamini na dhihaka. {8T 330.3}

Kadiri mwaka baada ya mwaka ulivyopita, ndivyo kwa kina zaidi na zaidi wimbi la hatia ya mwanadamu lilivyoongezeka, ndivyo mawingu ya hukumu ya Mungu meusi zaidi na zaidi yalivyojikusanya. Lakini bado Henoko, shahidi wa imani, alishikilia njia

yake, akionya, akisihi, na kufundisha, akijitahidi kurudisha nyuma wimbi la hatia na kusimamisha mishale ya kulipiza kisasi. {8T330.4}

Watu wa kizazi kile walidhihaki upuuzi wa yule ambaye hakutafuta kukusanya dhahabu wala fedha, au kujitengenezea mali hapa. Lakini moyo wa Henoko ulikuwa juu ya hazina za milele. Alikuwa akitazamia mji wa mbinguni. Alimwona Mfalme katika utukufu Wake katikati ya Sayuni. Kadiri uovu uliopo ulivyozidi kuwa mkubwa, ndivyo kwa dhati zaidi iliongezeka hamu yake kwa ajili ya maskani ya Mungu. Akiwapo bado duniani, aliishi, kwa imani, katika nyua za nuru. {8T 330.5}

"Heri wenye moyo safi; maana hao watamwona Mungu." Mathayo 5: 8. Kwa miaka mia tatu Henoko alikuwa akitafuta usafi wa moyo, ili aweze kuwa na upatanifu na mbingu. Kwa karne tatu alitembea na Mungu. Siku kwa siku alikuwa akitamani muunganiko wa karibu zaidi; na kwa karibu zaidi alikuza ushirika, mpaka Mungu alipomchukua Kwake Mwenyewe. Alikuwa amesimama katika lango la ulimwengu wa milele, hatua moja tu kati yake na nchi ya wenye heri; na sasa milango ikafunguliwa, kutembea na Mungu, kwa muda mrefu kulikofanywa kwa muda mrefu duniani, kukaendelea, na akapita kuingia katika malango ya mji mtakatifu, mtu wa kwanza kutoka miongoni mwa wanadamu kuingia humo. {8T 331.1}

"Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti; ……. maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu." Waebrania 11:5. {8T 331.2}

"Katika ushirika kama huo ndio Mungu anaotuitia. Kama ulivyokuwa wa Henoko ndivyo lazima uwe utakatifu wao wa tabia wale watakaokombolewa miongoni mwa wanadamu wakati wa ujio wa pili wa Bwana. {8T 331.3}

## Uzoefu wa Yohana Mbatizaji

Yohana Mbatizaji katika maisha yake ya jangwani alifundishwa na Mungu. Alijifunza mafunuo ya Mungu katika asili. Chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, alisoma magombo ya manabii. Mchana na usiku, Kristo Ndiye alikuwa somo lake, tafakuri yake, hadi akili na moyo na roho vilipojazwa kwa maono matukufu. {8T 331.4}

Alimtazama Mfalme katika uzuri Wake, na nafsi ilisahauliwa na kupotea machoni mwake. Alitazama ukuu wa utakatifu na kujiona mwenyewe kuwa mtu asiyeweza kufanya vizuri na asiyestahili. Ilikuwa ni ujumbe wa Mungu ambao alipaswa kuutangaza. Ilikuwa ni kwa uweza wa Mungu na kwa haki Yake ndio alipaswa kusimama. Alikuwa tayari kwenda mbele kama mjumbe wa Mbinguni, bila hofu ya wanadamu, kwa sababu alikuwa amemtazama Mungu. Angeweza kusimama bila woga mbele ya wafalme wa kidunia kwa sababu kwa kutetemeka aliinama mbele ya

Mfalme wa wafalme. {8T 331.5}

Pasipo hoja zilizonakishiwa au nadharia zilizosokotwa vyema Yohana aliutoa ujumbe wake. Yenye kushtusha na kali, lakini bado ikiwa imejaa matumaini, sauti yake ilisikika kutoka nyikani: "Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia." Mathayo 3:2. Na nguvu mpya, ya ajabu, ilisukuma mioyo ya watu. Taifa lote liliamshwa. Umati wa watu ukamiminika kwenda nyikani. {8T 332.1}

Wakulima na wavuvi wasio na elimu kutoka nchi jirani; askari wa Kirumi kutoka Katika ngome za Herode; wakuu wavikosi wakiwa na panga zao pembeni, tayari kuweka chini chochote chenye kuleta harufu ya uasi; watoza ushuru walafi wa mali kutoka kwenye vibanda vyao; na kutoka katika Baraza-Sanhedrini makuhani waliojifunga utepe- wote walisikiliza kana kwamba wameduwazwa; na wote, hata Mafarisayo, na Masadukayo, watu baridi, wenye kudhihaki wasiovutiwa, waliondoka dhihaka zao zikiwa zimenyamazishwa na kuchomwa mioyo kwa hisia ya dhambi zao. Herode katika jumba lake la kifalme alisikia ujumbe huo, na mtawala mwenye kiburi, mwenye moyo uliofanywa kuwa mgumu kwa sababu ya dhambi alitetemeka kwa kusikia wito wa toba. {8T 332.2}

Katika zama hizi, mara tu kabla ya ujio wa pili wa Kristo katika mawingu ya mbinguni, kazi kama ile kama ya Yohana inapaswa kufanywa. Mungu anawaita watu ambao wataawandaa watu kusimama katika siku ile kuu ya Bwana. Ujumbe ulioitangulia huduma ya Kristo ya hadhara ulikuwa: "Tubuni, watoza ushuru na wenye dhambi; tubuni, Mafarisayo na Masadukayo; ‘tubuni: kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.’ Kama watu wanaoamini marejeo ya Kristo hivi karibuni, tunao ujumbe wa kubeba - "Ujiweke tayari kuonana na Mungu wako." Amosi 4:12. Ujumbe wetu lazima uwe wa moja kwa moja kama ulivyokuwa ujumbe wa Yohana. Aliwakemea wafalme kwa uovu wao. Licha ya kwamba maisha yake yalihatarishwa, hakusita kulitangaza Neno la Mungu. Na kazi yetu katika zama hizi lazima ifanyike kwa uaminifu kama huo. {8T 332.3}

Ili kutoa ujumbe kama alioutoa Yohana, ni lazima tuwe na uzoefu wa kiroho kama wake. Kazi ileile lazima ifanyike ndani yetu. Ni lazima tumtazame Mungu, na kwa kumtazama tutaisahau nafsi. {8T333.1}

Kwa asili Yohana alikuwa na makosa na udhaifu wa ulio kawaida ya wanadamu; lakini mguso wa upendo wa Mwenyezi Mungu ulimbadilisha. Pale, baada ya huduma ya Kristo kuanza, wanafunzi wa Yohana walimwendea na malalamiko kwamba watu wote walikuwa wakimfuata Mwalimu mpya, Yohana alionesha jinsi alivyoelewa waziwazi uhusiano wake na Masihi, na jinsi alivyompokea kwa furaha Yule ambaye alikuwa amemtayarishia njia. {8T333.2}

“Hawezi mtu kupokea neno lolote,” alisema “isipokuwa amepewa kutoka mbinguni.

Ninyi wenyewe mwanishuhudia ya kwamba nalisema, Mimi siye Kristo, bali nimetumwa mbele yake. Aliye naye bibi arusi ndiye bwana arusi; lakini rafiki yake bwana arusi, yeye anayesimama na kumsikia, aifurahia sana sauti Yake bwana arusi. Basi hii furaha yangu imetimia. Yeye hana budi kuzidi, bali mimi kupungua.” Yohana 3:27-30. {8T 333.3}

Akimwangalia Mkombozi kwa imani, Yohana aliinuka kufikia kilele cha kujinyima na kujikana nafsi.  Hakutafuta kuwavuta watu kwake, bali kuyainua mawazo yao juu zaidi na zaidi, hadi pale watakapopumzika kwake Mwana-Kondoo wa Mungu. Yeye mwenyewe alikuwa ni sauti tu, kilio nyikani. Sasa kwa furaha alikubali ukimya na kutokuonekana, ili macho ya wote yamgeukie Nuru ya uzima. {8T333.4}

Wale ambao ni waaminifu kwa wito wao kama wajumbe wa Mungu hawatatafuta heshima kwa ajili yao wenyewe. Upendo kwa nafsi utamezwa na upendo kwa Kristo. Watatambua kuwa ni kazi yao kutangaza, kama Yohana Mbatizaji alivyotangaza: "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Watamwinua Yesu, na pamoja Naye ubinadamu utainuliwa. "Maana Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye Jina Lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa Mimi mahali palipoinuka, palipo Patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu." Isaya 57:15. {8T 333.5}

Nafsi ya nabii, ikiwa imekung’utwa ubinafsi wote, ilijazwa na nuru ya Mungu. Kwa maneno ambayo yalikuwa karibu kuwa nakili ya Maneno ya Kristo Mwenyewe, alitoa ushuhuda juu ya utukufu wa Mwokozi. "Yeye ajaye kutoka juu," alisema, "huyo Yu juu ya yote: Yeye aliye wa dunia, asili yake ni ya dunia, naye anena mambo ya duniani. Yeye ajaye kutoka mbinguni Yu juu ya yote . . . Kwa kuwa yeye aliyetumwa na Mungu huyanena Maneno ya Mungu; kwa sababu hamtoi Roho kwa kipimo." Yohana 3: 31-34. {8T 334.1}

Katika utukufu huu wa Kristo wafuasi Wake wote wanapaswa kushiriki. Mwokozi aliweza kusema: "Siyatafuti mapenzi Yangu Mimi, bali mapenzi Yake aliyenipeleka." Yohana 5:30. “Na," Yohana alisema waziwazi, "Baba hamtoi Roho kwa kipimo Kwake." Vivyo hivyo kwa wafuasi wa Kristo. Tunaweza kupokea nuru ya mbinguni iwapo tu tuko tayari kuukung’uta/kuuondoa ubinafsi. Tunaweza kuitambua tabia ya Mungu, na kumpokea Kristo kwa imani, pale tu tunapokubali kila fikira kutekwa kwa utii wa Kristo. Kwa wote ambao hufanya hivi, Roho Mtakatifu anatolewa bila kipimo. Katika Kristo "Unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili." Wakolosai 2:9, 10. {8T 334.2}

## Ahadi za Mungu

Kwa wote walio tayari kuiruhusu nafsi ipate kunyenyekeshwa wanapewa ahadi za

Mungu: {8T 335.1}

"Nitapitisha wema Wangu wote mbele yako, Nami nitalitangaza Jina la Bwana mbele yako." Kutoka 33:19 {8T 335.2}

"Niite, Nami nitakuitikia, Nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua." Yeremia 33: 3. {8T 335.3}

"Basi atukuzwe Yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo," tutapewa, "Roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua Yeye;" ili “mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo Wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu." Waefeso 3:20; 1:17; Waefeso 3:18, 19. {8T 335.4}

Haya ndiyo maarifa ambayo Mungu anatuita tupate kuyapokea, na kando ya hayo mengine yote ni ubatili na utupu. {8T 335.5}